

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Arobaini na Tano – Tarehe 14 Agosti, 2008

(Mkutano Ulianaza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Kwa kuwa Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki kisichopungua miaka 5 au 6 sasa kumekuwa na kilio kikubwa sana cha wananchi katika Sera za Serikali za kuwabomolea maeneo yao waliyojenga kutokana na miundombinu ambayo inajengwa na Serikali na kwa hiyo Serikali mara nyingi inatoa maelezo kwamba kwa kuwa nyumba zilizojengwa ziko karibu na barabara ndiyo maana Serikali imekuwa ikibomoa maeneo hayo.

Kwa kuwa Serikali ilikosa mipango mapema na kuwaeleza wananchi hali ya kujengwa barabara. Je, haoni kwamba hiki kitendo cha kubomoabomoa na hasa pahali panapobomolewa halafu wakakaa kwa muda mrefu hawajajenga ni kuwapa shida wananchi na usumbufu na kuwakosesha rasilimali chache ambazo tayari walishazichuma?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kwa heshima nimjibu Mheshimiwa rafiki yangu sana Hamad swal lake zuri sana kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, anachokisema Mheshimiwa Hamad ni kweli, kwamba inapotokea hivyo ni dhahiri kabisa kwamba mwananchi aliyekuwa amewekeza pale kwanza inakuwa ni bughudha kwa sababu inabidi ahame atafute makazi mapya. Kwa hiyo hilo hatulikatai.

Lakini nadhani ni vizuri nikasisitiza sana maana jambo hili limesemwa na tutaendelea kulisema kwamba ni vizuri wananchi popote pale wanapotaka kujenga nyumba kitu cha kwanza wajiridhishe na taratibu na sheria zinazotawala ujenzi huo. Kwa sababu hilo ni jambo la msingi sana. Mtu ukiamua tu kujenga bila ya kuzingatia hilo matokeo yake siku zote yatakuwa ni yale ambayo yanakuletea matatizo. Sasa mahsus i kwa hilo analoliuliza. Taratibu zinasema kwamba kwa barabara yoyote ile labda nichukue mfano mzuri wa Mwandiga/Manyovu/Ikesa hivi karibuni. Kwa barabara yoyote ile ambapo ujenzi umefanywa kabla taratibu hizi za *Road Reserve* hazijawekwa mtu yoyote tutakayemkuta baada ya utaratibu huo kuanza huyo atastahili kufidiwa.

Kwa hiyo, kwa kesi kama ya Mwandinga - Manyovu barabara ile ambayo umeona imeleta kidogo mkwaruzano ilikuwa ni barabara ya Halmashauri tangu miaka ya nyuma 1987 huko. Lakini mwaka 1989 tukaipandisha ikawa ni *Regional Road* ni dhahiri masharti yake yatakuwa yameongeza eneo ambalo sasa linaingia katika tatizo hili. Ndiyo maana nilipoiona juzi nikasema iko haja sasa kwa Serikali hili kuliweka vizuri kama barabara imemkuta mtu ni dhahiri Serikali lazima ichukue jukumu la kumsaidia kumfidia kwa sababu huyo hakuvunja sheria.

Kwa hiyo, mimi nataka nitoe wito kwa Watanzania wote kwamba msimamo huo tutaendelea nao lakini ni lazima na Watanzania kwa ujumla wake tujue kwamba ni vizuri kuzingatia sheria ili kujiepusha na matatizo kama hayo:-

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu inapotokea kwamba mipango miji yenye ilitoa kibali cha ujenzi na hatimaye wakakuta huo ujenzi uliojengwa basi kulikuwa ni sehemu ya barabara. Je, katika kesi kama hiyo unafanyaje na wakati mamlaka husika wametoa kibali?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba niongeze majibu kwa swali lake Mheshimiwa Hamad kama ifuatavyo:-

Katika mazingira kama haya jibu sahihi ni kwamba haiwezi kusameheka tu kwa sababu Halmashauri ndiyo ilitoa hicho kibali. Tunachoweza kumtia moyo mwananchi wa namna hiyo ni kuishtaki hiyo Halmashauri kwa kuwa ndiyo imesababisha tatizo hilo ambalo sasa linamwingiza gharama na mimi nina hakika katika mazingira ya namna hiyo Mahakama zetu kwa busara zake lazima zitampa haki yake anayostahili. (*Makofî*)

MHE. ALOYCE B. KIMARO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi nami nimwulize Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali ilianzisha Sera ya Uwezeshaji, sera hiyo baada ya kuanzishwa sheria ililetwa Bungeni Sheria Na. 16 ya Mwaka 2004 na ikapitishwa na Bunge letu Tukufu. Baada ya hapo Baraza la Uwezeshaji la Taifa likaanzishwa baada ya hapo Mfuko wa Uwezeshaji ukaanzishwa na ukaitwa jina la

Mwananchi *Empowerment Fund*. Mfuko huo kazi yake ni kuwakopesha Watanzania wazalendo...

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge swalii sio maelezo.

MHE. ALOYCE B. KIMARO: Swali Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa kuwa mfuko huo haujapata fedha mpaka sasa hivi na Serikali inasema inataka kuwawezesha Watanzania wazalendo itawawezeshaje na huku haiweki fedha kwenye mfuko huo?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Aloyce Kimaro, swalii lake kama ifuatavyo:-

Ni kweli yote aliyojasema yana ukweli kwa maana kwamba kwanza tulitunga sera baadaye tukatunga sheria na kwa kweli tukaanzisha mfuko mahsus kwa ajili hiyo.

Lakini suala la mfuko kwa maana ya kwamba Serikali inabidi iweke fedha kwa kazi kubwa kama hii linategemea kwa kiasi kikubwa uwezo wa Serikali. Kwa hiyo, hatua hizo zote alizozieleza ni kuonyesha dhamira ya Serikali yetu, lakini suala la kuwekeza kiwango cha kutosheleza kuanza kufanya hiyo kazi litategemea kwa sehemu kubwa uwezo wa Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme mfuko huo ni sehemu tu ya jitihada pana sana ambazo Serikali inazifanya. Kwa hiyo, tusikodolee macho mfuko huo kana kwamba ndio chanzo kikubwa cha kumwezesha mwananchi. Kubwa hapa ni Serikali kujitahidi kuweka mazingira mazuri ya kumwezesha kila Mtanzania kuweza kijiwezesha kwa namna ambavyo inawezekana, na hiyo ndiyo kazi moja ambayo tunajaribu kuifanya *create environment* ambayo ni *conducive* kwa mambo kama haya.

MHE. ALOYCE B. KIMARO: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mfuko huo upo na wafanyakazi wapo, sasa kama Serikali haiwezi kuweka fedha huko Mheshimiwa Waziri Mkuu hauoni wafanyakazi hao wanaendelea kulipwa bila kuwa na kazi ya kufanya?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, si kweli sana kwamba wanalipwa kwa kutokufanya kazi yoyote. Ukishaanzisha chombo yako mambo mengi ikiwa ni pamoja na kutengeneza kitu ambacho kinasaidia kuwezesha hata mawazo ya Kimaro kuweza kutekelezwa, kwa sababu unahitaji watu pale wawepo kuanza kufanya angalau kazi za awali.

Kwa hiyo, bila hiyo chombo hicho hata mawazo ambayo anayasema Mheshimiwa Kimaro hayatawezekana kwa muda mrefu zaidi kuliko tukifkiria sasa maadamu wako wafanyakazi ambao kazi yao ni kufikiria, maana na wao lazima wafanye kazi. Kwa hiyo

na wao watakuwa wanatoa msukumo na kutoa mawazo kwa Serikali ili tuweze kutoa nguvu za kutosha kuwezesha mfuko huo kuanza.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Spika, nakushukru sana. Mheshimiwa Waziri Mkoo swali langu nalileta kama ombi, ni swali lakini ni ombi.

Kufuatana na Sheria ya Kimataifa ya Bahari nchi ambazo zina bahari zitaruhusiwa kujiongezea mipaka kwa kilomita za bahari 200 na nchi kama Tanzania ikiongezewa mipaka hiyo itasaidia kwa uvuvi, madini, gesi na kwa mipaka yenye. Lakini Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi wakati analeta Bajeti yake amesema zimepatikana dola milioni moja za kufanya kazi hiyo, Serikali ya Norway imetoa dola milioni 4.6. Sasa bado dola milioni 1.6. (*Makofî*)

Sasa Mheshimiwa Waziri Mkoo, wewe kama Kiongozi wa Serikali utawa-*engage* Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi aidha wafanye mapunguzo kwenye mafungu mengine au waongee na *Development Partners* wengine ili fedha hizo zipatikane tufanye upembuzi yakinifu kabla ya *deadline* mwezi Mei, 2009.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Mwambalaswa swali lake kama ifuatavyo:-

Ni kweli anayosema ni dhahiri ndivyo tumekubaliana na mchakato wa mazungumzo kwa maana ya kulenga kuongeza eneo letu la bahari tayari Kiserikali tumeshaanza kuutazama, lakini nikubaliane na wewe kwamba tutajitahidi kwa kadri itakavyowezekana kuhakikisha ile *deadline tunai-meet*. Sasa kuna njia nyingi inaweza ikawa sisi wenye ndani lakini naamini Waziri wa Fedha 1.6 *bilion is not much* kama kweli tunataka kuifanya hiyo kazi. (*Makofî*)

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Waziri Mkoo moja katika majukumu makubwa ya Serikali ni kusimamia utekelezaji wa sheria na maazimio yanayopitishwa na Bunge. Na kwa kuwa lipo azimio ambalo ni muhimu sana kwa umoja na mshikamano wa Taifa letu lakini haionekani kuwa mpaka sasa Serikali imefanya kazi ya kuwaelimisha wananchi juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, naomba univumilie nimsomee Mheshimiwa Waziri Mkoo hili azimio ili aweze kutujibu vizuri. Azimio linasema kama ifuatavyo:- Hoja ya Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, Hoja ya Kufanya Mabadiliko Kwenye Hoja ya Kufuta Azimio la Bunge la tarehe 24 Agosti, 1993 kwamba:-

Hoja ya Kufuta Azimio la Bunge tarehe 24 Agosti, 1993 irekebishwe kwa kufuta maneno yote yaliyomo katika hoja hiyo na badala yake kuweka maneno yafuatayo:-

“Kwa kuwa tarehe 24 Agosti, 1993 Bunge lilipitisha kwa kauli moja Azimio la kutaka iundwe Serikali ya Tanganyika ndani ya Muungano ili kuwa na muundo wenye Serikali tatu”.

Kwa kuwa tarehe 6 Agosti, 1994 Rais wa Jamhuri ya Muungano aliwasilisha kwa Wabunge wakiwa katika kikao rasmi cha Kamati ya Wabunge wote wa CCM Azimio la Halmashauri Kuu ya Taifa kwamba Sera ya Chama cha Mapinduzi ni Muundo wa Muungano wenye Serikali mbili yenye mwelekeo na upeo wa muda mrefu wa Muundo wa Muungano wenye Serikali moja.

Na kwa kuwa Kamati ya Wabunge wote wa CCM ilipokea na kujadili na kulikubali Azimio hilo. Na kwa kuzingatia kwamba Serikali hii

SPIKA: Nenda kwenye swali basi, swali ni nini hapo? Maana ndefu sana hiyo Mheshimiwa Mbunge.

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Nalimaliza Mheshimiwa Spika, nivumilie kidogo nakwenda mwisho.

Hivyo Basi, Bunge katika Mkutano wake wa Bunge huu wa 16 wakati huo uliofanyika Dar es Salaam sasa linaazimia kama ifuatavyo na hapa ndipo kwenye hoja yangu. Linazingatia na kuafiki kwamba sera ya kuwa na Muundo wa Muungano wa Serikali mbili kuelekea kwenye Serikali moja itazingatiwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 1995. Kwamba nasisitiza badala ya kupata idhini ya wananchi katika uchaguzi huo kuhusu Sera ya Muundo ya Muungano wa Serikali mbili na mwelekeo wa Serikali moja, Serikali zote mbili zichukue hatua ya dhati kujenga ridhaa ya pande zote mbili ya Taifa letu kuwa na Muungano wa Serikali tatu na kwa misingi hiyo Bunge linafuta Azimio lake la tarehe 24 Agosti, 1993 linaloelezea Serikali iandae utaratibu wa kuwasilisha Bungeni kabla ya Aprili, 1995 Muundo wa Muafaka wa Muungano ambao unazingatia haja ya kuwepo na Serikali ya Tanganyika ndani ya Muungano.

Hoja yangu ni kuwa je, Serikali inasemaje katika suala hili la Azimio kubwa kama hili kwa wakati huu tulionao wewe Mheshimiwa Waziri Mkuu ukiwa Kiongozi wa Serikali?

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge naitafsiri hii ni njia ya kinyemela kurudi kwenye swali ambalo nilikwishalitolea mwongozo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, lisigestahili kwa wakati huu na ningewasihi hasa wenzetu katika Bunge tujitahidi sana Zanzibar kuna Serikali, kuna Rais, kuna Baraza la Wawakilishi, hivi hii hoja, inavyojirudia rudia hivi kweli ina nia njema au ni kitu gani hiki kinaendelea? Na kuitakia Tanganyika Serikali basi itoke kwa Watanganyika? Leo inakuwa mtu wa Zanzibar ndio ameng'ang'ania kwamba lazima Tanganyika iwe na Serikali, kuna nini? (*Makofi*)

Kwa hiyo, silikubali hilo. Mheshimiwa Mohamed Mnyaa na wewe kama unakwenda huko bora uache tu. (*Makofi*)

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Spika, ni uafanuzi wa Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu mambo ya Muungano kiutawala, kisera yanaamuliwa na Baraza la Mawaziri na Serikali ya Muungano. Zanzibar haiwakilishwi ndani ya Baraza hilo. Rais wa Zanzibar anaingia katika Baraza hilo kwa nafasi yake lakini huwa haiwakilishwi...

SPIKA: Tumsikilize jamani, tumsikilize tipeane fursa.

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Anaingia si kwamba ni chombo kinachowakilisha upande mwingine wa Muungano, sasa swalilangu, kuna chombo gani kinacho julikana, kinachotambulika kisheria ambacho kinawakilisha pande mbili za Muungano?

SPIKA: Waheshimiwa katika utaratibu wetu uwakilishi wa upande mmoja wa Muungano, kama Rais anatoka upande mmoja, Makamu wa Rais anatoka upande wa pili. Sasa ni dhahiri kabisa jibu liko wazi kwamba Makamu wa Rais na kwa sasa hivi ni Dr. Shein ndiyo mwakilishi ambaye anasimamia maslahi ya Zanzibar kwa maana katika Jamhuri ya Muungano na mara nyingine huyo anapokuwa Rais hayupo ye ye ndiyo anakuwa Rais. (*Makofi*)

Looh !!!! naye Katibu leo amewapanga wale wale tu. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. DR. ALI TARAB ALI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano ibara ya 5 kila mwananchi Mtanzania ambaye ametimiza miaka 18 ana haki ya kupiga kura katika chaguzi. Hapa ibara ndogo ya 2 inaonesha tu masharti ya wale ambao hawaruhusiwi kupiga kura na namwomba Mheshimiwa Spika anivumilie kidogo.

WABUNGE FULANI: Aaah!!!!!!

MHE. DR. ALI TARAB ALI Nyie sio Spika, Spika yuko huku.

SPIKA: Endelea endelea wewe unaongea na Spika.

MHE. DR. ALI TARAB ALI: Kuwa na uraia wa nchi mbili. (a) Kuwa na uraia wa nchi nyingine (b) Kuwa na ugonjwa wa akili (c) Kutiwa hatiani kwa makosa fulani ya

jinai (d) Kukosa au kushindwa kuthibitisha au kutoa kitambulisho cha umri, uraia au uandikishaji kama mpiga akura.

Mbali na sababu hizi hakuna sababu nyingine yeyote itakayoweza kumzuia raia asitumie haki ya kupiga kura.

Mheshimiwa Spika,

SPIKA: Mheshimiwa endelea....

MHE. DR. ALI TARAB ALI: Naona kuna Maspika wengi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Waziri Mkoo nikiwa mgombea wa uchaguzi mwaka 2005 kwa nafasi ya ubunge Jimbo la Konde na wapiga kura wengi wa Jimbo langu tuliandikisha katika Daftari la Kudumu na baadaye tukaondolewa katika Daftari la Kudumu hatukupiga kura si ya Rais wa Muungano, si ya Mbunge, si ya mwakilishi si ya Diwani.

Je, utatuhakikishia vipi Mheshimiwa Waziri Mkoo kwamba ukifika uchaguzi wa mwaka 2010 kila raia wa Tanzania atakuwa na haki ya kupiga kura kama ipasavyo. Ahsante.

SPIKA: Swali hilo linahusu taarifa ambazo kwa sasa hivi wote hatuna. Unaposema wewe hukupiga kura na wewe ni Mbunge sasa linaleta utata. Mimi nadhani ebu Dr. Ali Tarab Ali, liweke vizuri liweze kujibiwa wakati mwingine kwa sababu ukilitazama tu wala halilet maana kwamba ni raia una sifa zote za Kikatiba halafu hukuruhusiwa kupiga kura. Inaweza kuwa ni suala la utawala tu na utendaji. Kwa hiyo, liweke vizuri ikiwezekana hata kwa maandishi ili tulijibu tutatue jamani matatizo tusiwe katika hali ya hisia. Tunaendelea, kwa kweli Katibu usirudie mchezo huu wa kuwapanga wale wale tu. (*Makofi*)

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Hivi karibuni kulifanyika Semina ya Wenyeviti wa Tume za Uchaguzi za SADC kule Zanzibar na baada ya Semina kulitolewa kauli mbili tofauti na viongozi wakati alipokuwa anazungumza na Waandishi wa Habari. Kauli ya kwanza ilikuwa ya Mheshimiwa Waziri Kiongozi wa Zanzibar Shamsi Vuai Nahodha ilizitaka Tume za Uchaguzi kufanya wajibu wao wa haki kutoa haki na kuhakikisha kwamba inapunguza vurugu mara baada ya uchaguzi. Kauli ya pili ilitolewa na Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi wa Zanzibar iliyodai kwamba viongozi wa Kisiasa wanaingilia maamuzi ya Tume za Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika ripoti ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar iliyotolewa mara baada ya uchaguzi wa 2005, Mwenyekiti alilalamika kwamba hata Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ilikuwa imeingiliwa katika maamuzi yake. Kwa kuwa Tume ya Uchaguzi ya Taifa (NEC) inapata Wabunge wake kutoka Zanzibar kwa kupitia Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) katika hatua mbalimbali kama ni wakala wao.

Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu anaingaliaje hali hii ya Tume zetu za Uchaguzi za Tanzania jinsi zinavyoelezwa, naomba maelezo yake.

SPIKA: Majibu Mheshimiwa Waziri Mkuu ni maoni tu kuhusu yaliyotokea kwenye semina.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, sina hakika rafiki yangu Salim alitaka kusema nini. Lakini nadhani baada ya Mheshimiwa Spika, kusema sema maneno dhidi ya timu ya leo nadhani kidogo umem-put off, nadhani alikuwa na jambo lingine lakini hakuliweka vizuri sana. (*Makof/Kicheko*)

Kwa sababu ukiniuliza kwa kweli maoni yangu. Je, unazonaonaje Tume hizi zinavyoelekeea elekea kwa kweli inakuwa kidogo taabu maana sipati kitu *tangible* hasa unataka nini. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inayo Tume yake ya Uchaguzi na ndiyo inasimamia chaguzi Zanzibar. Sasa kama Tume hiyo ina matatizo katika usimamizi wa chaguzi ni suala la watu wa Zanzibar pale kusema matatizo gani na tufanye nini? Tume ya Uchaguzi ambayo inasimamia chaguzi zetu nayo vile vile Watanzania kwa ujumla wake kama kuna kasoro watazibainisha na hatua za kurekeblishwa zinaweza zikachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni vigumu sana kwa kweli kujaribu kusaidia kulijibu vizuri kwa sababu limekuwa kidogo kama linataka tu *general opinion* hivi jambo ambalo sio rahisi sana katika mazingira ambayo nadhani alikuwa anayawaza lakini hakuweza kulisema vizuri.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Naomba niseme vizuri sasa.

Kwa kuwa Tume hizi zimekiri kwamba zimekuwa zikiingiliwa katika maamuzi yake. Je, unahisi uchaguzi unaofanyika unakuwa huru na ni wa haki na Wabunge wanaopatikana wanakuwa ni Wabunge halali?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, sina taarifa kwa kweli kuhusiana na haya mambo yote mawili anayoyasema na kwa hiyo siwezi nikatoa kauli nzito hapa juu ya mambo yote mawili ambayo ameyaeleza.

Lakini la pili, sina uhakika sijui nitasema nini Kiswahili safi *context* iliyokuwa imetawala wakati wanatoa maoni hayo sababu Serikali zipo, vyombo viro kama Tume hizi zinaona yako matatizo haya sioni tatizo ya kuyabainisha na kuyawasilisha katika vyombo vinavyohusika kwa lengo la kurekebisha hali ambazo Tume hizo zinahisi kwamba zinaingiliwa.

Sasa kama mimi sijaona hili, sijalionna dhahiri likaletwa kwangu pengine kupitia kwa Rais. Kwa hiyo, inaniwia vigumu sana kusema nini hasa wanachokisema hata kama ni kweli Tume hizo zilitoa maoni hayo.

MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Katika majibu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa anamjibu Mheshimiwa Rashid kwa kweli sikuweza kuyaelewa vizuri, naomba niulize swalii.

Barabara ya Manyovu - Mwandiga sasa hivi inatakiwa iwe ya kiwango cha lami lakini wananchi wameshapewa barua mwezi huu waweze kubomoa nyumba zao na walishaorodheshewa mali zao.

Lakini sasa hivi kilichopo ni kwamba wameshaanza kubomoa nyumba zao na fidia bado hawajalipwa, sasa nilikuwa namwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu. Je, hiyo fidia watalipwa lini?

WAZIRI MKUU: Kwa hili naweza nikalijibu kwa sababu nimelichokoza mimi mwenyewe. Ninachosema ni kwamba barabara hii ya Mwandiga-Manyovu ambayo hivi karibuni nilipokuwa Kigoma nilikwenda nikaweka jiwe la msingi kwenye barabara hiyo. Barabara ile ilikuwa chini ya Halmashauri kwa maana ya Serikali za Mitaa vigezo vinavyotumika kwa maana ya *Road Reserve* lile eneo linaloachiwa kama akiba kwa barabara chini ya Serikali za Mitaa ziko tofauti na vile vigezo vinavyotawala barabara zile ambazo ni za mikoa au ni barabara kuu.

Sasa wananchi wale watakaonekana kwamba wakati barabara ile ipo wale waliokuwa wamejenga nyumba ambazo zilikuwa nje ya eneo lile ambalo tunasema ni *reserve* kwa ajili ya Halmashauri zetu lakini sasa wamepatwa na balaa hili ambalo ni neema kwa upande mwingine kwa kuitangaza barabara ile kuwa ni barabara kuu hawa ndio nimesema Serikali ni lazima tuliangalie kwa sababu tusipowafidia tutakuwa tunawaonea. Ndiyo maana nilisema nilipoiona kwenye televisheni nikasema hili ni vizuri Serikali tukaingilia kati tuweze kupata maelezo bayana na kuchukua hatua zinazostahili isije tukawa tunawaonea jamii kwa sababu ya maamuzi yetu ambayo sisi wenyewe tumekubali kama barabara inamkuta au uamuzi wa Serikali unamkuta mwananchi katika mazingira hayo tunao wajibu wa kuhakikisha tunamfidia. Kwa hiyo nalifuatilia na hakika tutaweza kulifikisha mahali pazuri na likaisha vizuri. (*Makofii*)

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa Tanzania inapakana na nchi zaidi ya saba ambazo hazina bandari na zinategemea bandari zetu. Je, ni lini Serikali itaboresha bandari ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara. Na lini Serikali itaongeza njia za Reli Kusini na Tabora kwenda Burundi na Singida kwenda Mara? (*Makofii*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, nadhani Mzee Msindai anachotafuta ni hilo la mwisho. Hiyo barabara inayotoka Manyoni-Singida anataka iimarishe lakini kwa lengo la kuelekea Musoma kama ambavyo kwa muda mrefu tumekuwa tukilisema.

Mimi naomba niseme tu kwamba dhamira ya Serikali nadhani kwa sasa ni kubwa zaidi kuliko hata ilivyokuwa siku za nyuma kwa maana ya kuimarisha miundombinu ya reli kwa maana ya TAZARA, miundombinu ya reli kwa maana ya Reli ya Kati pamoja na matawi yake. Lakini vile vile kwa maana bandari zetu Mtwara, Dar es Salaam na Tanga.

Nalisema hili kwa sababu ya vuguvugu ambalo nimeliona limejitokeza hivi karibuni. Nia ya Rais wetu na hasa alipofanya ziara China na India na sasa idadi ya watu ambao naona wanaulizia juu ya uwezekano wa kushiriki katika usimamizi na uendeshaji wa shughuli mbalimbali zinazohusiana na miundombinu.

Kwa hiyo, mimi nadhani siwezi nikasema kwa uhakika kwamba lini mambo gani yatafanyika, lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Msindai kwamba dhamira iliyopo sasa hivi na hatu alipokuja yule Gavana wa Benki ya Maendeleo ya China moja ya maeneo ambayo tumemkabidhi ili kuifanyia kazi ni Reli ya TAZARA ambayo Serikali tupo tayari kufanya kazi na Serikali ya China kuweza kuirejesha tena kama ilivyokuwa mwanzoni lakini vilevile tumezungumza naye sana hatu wadau wengine ambao wamekuja ikiwa ni pamoja na Kampuni yetu ya Reli kuboresha hii Reli ya Kati ili iweze kutimiza majukumu yake inavyotakiwa.

Sasa mimi nafikiri kumtendea haki Mheshimiwa Msindai kwa sababu ameuliza jambo kubwa ngoja niombe Wizara ya Miundombinu tujaribu kukaa chini na kuandika maelezo kidogo kwa kina juu ya mipango ambayo Serikali inayo kwa sasa katika kuimarisha reli zetu zote mbili pamoja na matawi haya ya Mpanda na kuelekea Manyoni mpaka Musoma.

MHE. MANJU S. MSAMBYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu. Unapofanya uchaguzi mkuu, Mheshimiwa Rais huteua Mawaziri wake mionganoni mwa Wabunge na inaweza ikatokea kwamba Waziri kateuliwa lakini kwa bahati mbaya na Mungu aepushe mbali Waziri huyo akawa ana kesi ya uchaguzi. Kwa bahati mbaya Mbunge huyu akatenguliwa. Sijawahi kuona katika historia ya Tanzania baada ya utenguzi Rais hata kama anampenda Mbunge huyo viyi atasubiri rufaa ya Mbunge huyo ndiyo amrejeshe kwenye nafasi yake.

Sasa naomba nipate maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu inakuwaje sisi tunalo Bunge la Afrika ambalo tunawakilishwa kule. Mmoja katika Wabunge ambao wanatuwakilisha kule katenguliwa Ubunge wake kwenye kesi ya uchaguzi lakini nafasi hiyo mpaka sasa haijajazwa. Waziri Mkuu anasemaje kwa sababu uwakilishi tulionao kule vilevile tunalipia. Sasa nikinukuu kauli ya Mwanafalsafa mmoja anasema "*No taxation without representation*". Sisi tunalipia kule lakini hatuwakilishwi, uwakilishi wetu haujakamilika. Waziri Mkuu anasemaje juu ya hili.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Msambya anazungumza mambo mawili ambayo kwa upande mmoja unaweza ukaona kama yanafanana lakini hayafanani sana. Hili la Waziri ambaye ameteuliwa na Rais alitokana na Ubunge tumekwenda Mahakamani uamuza ule unaonyesha kwamba uchaguzi wake ulikuwa ni batili lakini amekata rufaa. Utaratibu unataka tusubiri hili la Ubunge wake.

Lakini uteuzi wake kama Waziri si lazima ungoje hilo kwa sababu uteuzi ni uamuza tu wa Rais anaamua akakupa leo, kesho akakuondoa. Havina uhusiano kwa sababu amekuteua basi wewe utaendelea kuwepo pale kwa sababu ni Mbunge mpaka

Bunge litakaposema mwisho, hapana, si kweli. Anaweza kabisa akabadilisha hata kama hiyo *process* bado inaendelea huo ni uamuzi wake kwa sababu kuteua ni *discretion* yake.

Kwa hiyo, kwa hili unaweza kusema kwamba ile sehemu ya pili ya Ubunge ukaihusisha na utaratibu wa Mbunge wa Bunge la Afrika moja kwa moja kwa sababu inawiana na ni kweli kabisa kwamba kama kuna kesi ambayo ni *pending* na amekata rufaa taratibu zinasema ni vizuri mngoje mpaka mwisho.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali kwa Waziri Mkuu umekwishapita. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu yake ya ufasaha katika masuala mbalimbali. Naomba niseme moja, kuna maoni yamekuja kwamba utaratibu wa sasa wa kujiandikisha siku hiyo hiyo una usumbufu. Sasa mimi nasema suala la usumbufu tumezungumza na tukaona kwamba nyakati hizo ambazo tunazungumza na kuitisha jambo hili kwamba haitafaa na inaweza kuleta hali kama ya mizengwe ikionekana kwamba wakati wowote Mbunge anaweza wiki nzima anajiandaa kujiandikisha ili amwulize Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ndiyo maana tukaweka utaratibu kwamba haya ya papo kwa papo yawe siku hiyo hiyo na sijapata sababu ya kutosha nzito za kunifanya nibadili huu uamuzi amba ni wenu. Kwa hiyo, hadi hapo kutakapokuwa na hoja nzito za kutosha, lakini tutaendelea hivi hivi. Saa kumi na mbili sio mapema sana, kuna watu wanaamka saa kumi na moja kwenda kuswali. Kwa hiyo, saa kumi na mbili sio mbaya sana. Kama kweli una haja ya kuuliza swali, kila kitu kina gharama yake duniani hapa. Fursa ya kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu ni fursa nzito. Sasa isiwe inapatikana tu kirahisi unapita tu jioni unamwona Spika unamwambia wiki ijayo nitauliza. Hakuna mambo ya namna hiyo. Katibu kwa shughuli inayofuata.

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, swali namba 392 la Mheshimiwa Mgana Msindai ameliondoa kwa hiyo tunaendelea na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Mohamed Said Sinani wa Mtwara Mjini.

Na. 393

Kuwasadidhia Wavuvi Mkoani Mtwara

MHE. MOHAMED S. SINANI aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi waishio kando kando ya Bahari ya Hindi Mkoani Mtwara wanategemea uvuvi kuijiptaia mahitaji yao; na kwa kuwa wanaendesha shughuli zao kwa matatizo ya ukosefu wa boti na nyavu za kuvulia na kukosa elimu ya kilimo cha mwani;

- (a) Je, Serikali inafanya mpango gani wa kuwapatia mikopo yenyenye masharti nafuu ya zana hizo?

- (b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwapatia mtaalam wa kilimo cha mwani ili nao wanufaika na zao hilo kama wenzao waishio kando kando ya bahari wanavyonufaika?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mohamed Sinani, Mbunge wa Mtwara Mjini, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itatatua tatizo la upatikanaji wa vifaa vya kisasa vya kuvulia samaki kwa sehemu kubwa katika Wilaya zote za Mwambao wa Pwani kuititia mradi wa usimamizi wa mazingira ya Bahari na ukanda wa Pwani (MACEMP). Mradi huu ulianza kutekelezwa kwa majaribio tangu mwaka 2005/2006 katika Wilaya za Kilwa, Mafia na Rufiji.

Kuanzia mwaka huu wa fedha 2008/2009 mradi utaanza kutekelezwa katika Halmashauri zote za ukanda wa Pwana za Mkinga, Muheza, Jiji la Tanga, Pangani, Bagamoyo, Temeke, Ilala, Kinondoni, Mkuranga, Lindi Vijijini, Mji wa Lindi, Mtwara Vijijini na Manispaa ya Mtwara/Mikindani na zile tatu za awali, yaani Halmashauri za Kilwa, Mafia na Rufiji.

Mheshimiwa Spika, kuititia mradi huo, wavuvi waliopo kando ya Bahari ya Hindi wakiwemo wa Mkoa wa Mtwara wataweza kuibua miradi midogo midogo ambayo itafadhiwa na vijiji vya Pwani (*Coastal Village Fund*) na wataweza kununua nyenzo za kisasa na bora za kuvulia samaki pamoja na viambata vyake.

Mfuko umetenga kiasi cha dola za Kimarekani milioni 1.8 kwa ajili ya miradi itakayoibuliwa na wananchi katika Halmashauri hizo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009. Fedha hizi ni ruzuku kwa vikundi ambapo wanakikundi watatakiwa kuchangia kati ya asilimia tano mpaka ishirini ya thamani ya mradi watakaoibua ili wananchi wengi waweze kunufaika na mpango huo. Kama jambo la kuendelea na la kudumu, Wizara yangu kuititia mradi wa MACEMP itahamasisha wavuvi kujiunga katika vikundi mbalimbali ikiwa ni pamoja na vile vya kuweka na kukopa (SACCOS) na pia kukopa kwenye Taasisi za fedha kama mabenki ili waweze kuwijengea uwezo wa kupata zana stahiki za uvuvi pamoja na shughuli nyingine za maendeleo.

- (b) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa zao la Mwani katika kuinua kipato cha wananchi wanaoishi katika mwambao wa pwani ya Bahari ya Hindi wakiwemo wananchi wa Mkoa wa Mtwara, umewapanga wataalam tisa na kati ya hawa wawili katika Halmashauri ya Manispaa Mtwara, Mikindani na saba katika Wilaya ya Mtwara vijijini na fani ya uvuvi ambayo inajumuisha kilimo cha Mwani.

Watalaam hao wamekuwa wakitoa elimu kuhusu jinsi ya kuendeleza zao la Mwani ili kuboresha shughuli za kilimo hicho katika maeneo hayo. Kutohakana na ushauri wa watalaam hao, kwa mwaka 2007/2008 jumla ya tani 18 za Mwani mkavu aina ya *Eucheuma Cottonii* zenye thamani ya shilingi 3,960,000 zimeweza kuzalishwa katika

Wilaya ya Mtwara katika viji vya Mkunga na Naumbu, na wananchi wengi wanaendelea kujifunza na kuzalisha Mwani kama moja ya shughuli mbadala ya uvuvi.

MHE. MOHAMED S. SINANI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swal moja dogo la nyongeza. Nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri. Lakini napenda kufahamu juu ya kiwanda cha kutengeneza Boti za uvuvi cha Mikindani ambacho kimesimama kwa muda mrefu na kiwanda hiki nacho kinaoza na hatujui mwisho wake ni nini.

Kiwanda ambacho kilikuwa kinasaidia kutengeneza boti za kuvulia samaki na wananchi walikuwa wanafaidika na kiwanda kile. Je, kiwanda hiki mwisho wake ni nini?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba fedha zipo kutoka *MACEMP* na kama wananchi wa Mtwara watapenda fedha ambazo zimetengwa ziweze kufufua hicho kiwanda, Wizara yangu haitasita kufanya hivyo na nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Tanzania Bara zipo Dola Milioni 7.2 kwa ajili ya kusaidia vikundi.

Kwa hiyo, tunaweza kumchotea humo na wale ambao wapo Zanzibar napenda kuwaambia kwamba zipo Dola milioni 4.8. Kwa hiyo, kama wananchi wanamatatizo na wanatokea sehemu hiyo hizi Dola milioni 12 zipo mradi tu walete maombi wanawenza kusaidia.

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza swal moja la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri amejitahidi sana kujibu lakini kwa kweli haikutosheleza. Hiki kiwanda cha Mikindani ndio kilikuwa kiwanda pekee kilichokuwa kinatengeneza boti katika ukanda huu wote wa Pwani na kimekufa kabisa.

Je, katika mpango huu wa *MACEMP* wa maendeleo ya uvuvi katika Ukanda wa Pwani, Waziri haoni wa kuwa na Kiwanda kati ya Tanga na Mtwara kiwepo kiwanda cha kutengeneza boti au mpango huu ujikite katika kuagiza boti na nyavy ili tuweze kuongeza suala hili la uvuvi katika nchi hii?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi ni kwamba. Pesa hizi zilizopo ambazo ni milioni 7.2 zipo tayari kufanya shughuli ambazo wananchi wataamua zifanye na kama lengo la upande wa Mtwara ni kufufua hicho kiwanda na wakishakaa na kukubaliana tutatoa pesa kufuatana na maombi.

Lakini kuhusu boti; ni kweli huu mradi unazo fedha za kununua boti, Wilaya ya Kilwa, Rufiji na Wilaya ya Mafia kila moja imenunuliwa boti mbilimbili na tupo tayari kuzinunulia Wilaya zingine zilizobaki ambazo ni 14 kama wakiomba.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. MOHAMMED HABIB MNYAA: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Mwongozo wa Spika, Kanuni ipi?

MHE. MOHAMMED HABIB MNYAA: Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68 (7). Kuna Kanuni ya 46 ambayo Mbunge anapouliza swali na hakuridhika na jibu kuna taratibu za Mbunge huyo kufuata. Lakini mimi sijafahamu Kanuni gani wakati tuna muuliza maswali Waziri Mkuu na Mbunge hajaridhika na jibu alilolipata au amejibiwa na Spika. Je, tufuate utaratibu gani?

SPIKA: Si kazi ya Spika kujibu mnayouliza. Kazi ya msingi ya Spika ni kutoa mwongozo. Kwa hiyo, unapouliza swali ambalo kwa mujibu wa Kanuni halikukaa sawa ama unaendeleza tu usumbufu kwa mambo ambayo yalikwishaamuliwa zamani Spika atakuwa hatekelezi wajibu wake akiachia tu mkondo wa mjadala uchukue hisia za Mbunge yoyote kwa lolote analotaka. Kwa hiyo, kitu ni imara na tutaendelea kulinda, Kanuni, Sheria na Katiba za nchi ahsante sana na naomba wenzangu Mheshimiwa Zubeir, Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mhagama na Mheshimiwa Ndugai wawe na msimamo huu huu ili twende kwa utulivu.

Tunaendelea swali linalofuata linalekezwa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo linaulizwa na Mheshimiwa Benson Mpesya. (*Makofi*)

Na. 394

Ujenzi wa Kiwanja cha Michezo cha Kisasa

MHE. BENSON M. MPESYA aliuliza:-

Kwa kwa, Mbeya ni mionganini mwa Mikoa yenye wapenzi wengi wa michezo ikiwa ni pamoja na riadha na mpira wa miguu, na kwa kuwa Mbeya imetoa wachezaji wengi wa Kitaifa na Kimataifa kama Rwiza John, Makali Kyomo, Mwinga Mwanjala kwa upande wa riadha na Emmanuel Gabriel, Primus Kasonso, Ivo Mapunda, Nsajigwa na Bantu;

Je, lini Serikali itajenga uwanja wa kisasa Jijini Mbeya ili kuzidi kuibua vipaji vingi na vipyta?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mwaigula Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mpesa kwamba Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa Mikoa yenye wapenzi wengi wa michezo. Aidha nakubaliana naye kwamba Mkoa wa Mbeya umetoa wachezaji wengi wa kitaifa na kimataifa hivyo unastahili kuwa na uwanja wa kisasa ili vipaji hivyo viweze kuendelezwa.

Mheshimiwa Spika, historia ya ujenzi wa viwanja vingi hapa nchini hususani viwanja vya mpira wa miguu inaonyesha kuwa viwanja hivyo vilijengwa kwa nguvu za wananchi katika mikoa mbalimbali chini ya usimamizi wa viongozi wao. Uwanja wa kumbukumbu ya Sokoine ulioko Mjini Mbeya ni miongoni mwa viwanja vilivyojengwa kwa njia hiyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa Bajeti ya Serikali, kwa hivi sasa Serikali haina mpango wa kujenga uwanja wa kisasa Jijini Mbeya ili kuzidi kuibua vipaji vingi na vipyta. Hivyo basi, napenda kumshauri Mheshimiwa Mpesa kwa kushirikiana na Wabunge wenzake wa Mkoa wa Mbeya na viongozi wengine wawahamasishé wananchi na taasisi mbalimbali kuchangia fedha au kushiriki kikamilifu katika kukarabati uwanja wa kumbukumbu ya Sokoine uwe wa kisasa zaidi na kuwezesha kuibua wachezaji wengi zaidi chipukizi wa michezo mbalimbali ikiwemo ya riadha na mpira wa miguu kama ambavyo wachezaji wengi waliowataja ambao wamewakilisha nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara yangu ipo tayari wakati wowote kutoa wataalamu watakaoweza kutoa ushauri katika mchakato mzima wa ukarabati au ujenzi wa uwanja wa kisasa Jijini Mbeya.

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nishukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa nguvu nyingi za wananchi sasa hivi katika nchi yetu tumezielekeza katika ujenzi wa shule za sekondari za Kata pamoja na ujenzi wa zahanati; na kwa kuwa wananchi wetu wengi kipato chao ni kidogo.

Je, Serikali haioni sasa ikajielekeza kujenga viwanja vikubwa kama kile kilichopo Dar es Salaam katika Majiji yetu angalau kwa awamu?

La pili, kwa kuwa timu ya *Tanzania Prison* itaiwakilisha nchi katika Kombe la Shirikisho; na kwa kuwa Mbeya iko mbali na Dar es Salaam. Je, Serikali itakuwa tayari kutoa usafiri kwa timu pinzani ili iweze kufika Mbeya na mechi hizo zifanyike Mbeya ambako kuna wapenzi wengi wa *Tanzania Prison*?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, swali la kwanza nikubaliane naye kabisa kwamba nguvu nyingi katika nchi yetu tumezielekeza kwenye ujenzi wa zahanati na ujenzi wa shule za msingi na sekondari. Ni nia ya Serikali kwa kweli katika Wizara yetu tuna mpango na mkaati mzuri tu wa kuboresha ujenzi wa viwanja kikanda.

Suala hili nilishalizungumza hapa Bungeni, tunaanza na Uwanja wa Taifa na wote mnafahamu uwanja huu changamani bado upo kwenye ujenzi tunajenga *phase two* na *phase two* hiyo itagharibu karibu bilioni 60 na ule ambao umeshajengwa tayari umegharimu karibu shilingi bilioni 55.

Kwa hiyo, tutakapomaliza uwanja huu wa kisasa ni nia ya Serikali kufikilia sasa ni sehemu gani tunaweza kuanza kujenga uwanja mwingine wa kisasa ili angalau tuwe na viwanja vinne au vitano vya kisasa na sisi tuweze kupata fursa ya kuwa na uwezo wa kuandaa mashindano ya kimataifa.

Kuhusu swalii lake la pili, napenda nikubaliane naye kabisa kwamba timu yoyote inaposhiriki katika mashindano ya kimataifa ni jukumu la Serikali kusaidia.

Nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mpesa na wananchi wa Mbeya timu ya *Prison* tutaisaidia kwa uwezo wetu wote kuhakikisha kwamba inafanikiwa kufanya vizuri ili kupeperusha vizuri bendara ya nchi yetu.

Na. 395

Tatizo la simba Nyamaume-Kitaraka

MHE. JOHN P. LWANJI aliuliza:-

Kwa kuwa simba nyamaume bado ni tatizo sugu katika maeneo ya Kitaraka ambapo hivi karibuni mtu mmoja aliuawa na kuliwa na simba na kwa kuwa simba hao wamekuwa wakifanya operesheni kila siku na kuua mifugo katika vijiji vya Kata za Sanjaranda, Itigi na Ipande. Kwa kuwa kikosi cha doria cha hifadhi ya wanyamapori Kanda ya Kati wanakiri kuwa wameelemewa na kazi hiyo kutoana na upungufu wa vitendea kazi:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kudumu wa kumaliza tatizo hilo sugu kwenye maeneo husika?
- (b) Je, Serikali haioni kwamba kifo cha mtu aliyeliwa na simba ni cha kusikitisha sana kwa sababu hakuna kinachobaki kuzikwa isipokuwa fuvu la kichwa tu. Je, mrithi wa marehemu huyo hasitahili fidia inayoleweka (*tangible compensation*) badala ya kutoa laki mbili ambayo ni sawa na ubani tu?
- (c) Je, Serikali inafikiria mpango gani wa kuwafidia wafugaji ambao mifugo yao huuawa na simba hao na kusababisha hasara kubwa hasa ikitiliwa maanani kuwa uchumi wao unategemea mifugo kwa asilimia kubwa?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Suala la uhifadhi wa wanyamapori na udhibiti wake ni jukumu la Wizara yangu katika Hifadhi za Taifa (*National Parks*), eneo la Ngorongoro (*Ngorongoro Conservation Area Authority*) na mapori ya akiba (*Game Reserves*). Aidha, uhifadhi wa wanyamapori na udhibiti wake katika maeneo ya Mapori Tengefu (*Game Controlled Areas*) na Maeneo ya wazi (*Open Areas*) hutekelezwa na Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya. Hivyo Halmashauri za Wilaya pia zina jukumu la kuajiri askari wanyamapori kwa ajili ya kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu kwenye maeneo Tengefu na ya wazi katika Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Lwanji, sehemu (a) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na tatizo la wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo ya Wilaya ya Manyoni, Serikali ina mipango ifuatayo:-

1. Wizara yangu kupitia Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (*TAWIRI*) imeanza kufanya utafiti wa kubaini chanzo na ukubwa wa tatizo la migongano kati ya simba na wananchi ili kutafuta ufumbuzi wa kudumu. Aidha, Wizara yangu imeanza kufanya majaribio ya teknolojia ya kutumia sauti ya kuita simba kwenye mitego na kuwakamata kama njia ya muda mfupi ya ufumbuzi wa tatizo hili.
2. Kujumuisha wanyama wakali na waharifu kwenye *quota* ya wanyama wanaowindwa kwa matumizi mbalimbali wakiwemo simba ambalo wanawindwa kitalii.
3. Kuendelea kuimarisha doria za msako wa kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu. Aidha, Wizara itaendelea kuishauri Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni kuajiri askari wanyamapori wa kutosha na kujenga kituo, Itigi kwa ajili ya maeneo ya Kitaraka, Sanjaranda na Muhanga.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu sehemu (b) na (c) ya swali la Mheshimiwa Lwanji kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa uhai wa binadamu hauwezi kuthaminishwa kwa fedha, kwa sasa Serikali hutoa kifuta machozi cha shilingi 200,000/= kwa kila familia ya marehemu anayeuaawa na wanyamapori.

Hata hivyo, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, suala hili pamoja na yale ya uharibifu wa mazao na mifugo inayouwawa na wanyamapori, yatazingatiwa katika Muswada wa Sheria ya Wanyamapori utakaoletwa hapa Bungeni hivi karibuni.

MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu niulize swalii la nyingeza. Kule Rufiji Kata ya Ngorongo, Mloka na Nyaminywili watu zaidi ya 25 waliuliwa na simba.

Je, Serikali inaniambiaje niandike maombi kesho?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kutoa pole sana kwa wananchi wa Rufiji waliofiwa na ndugu zao kwa idadi hiyo kama ni kweli ingawa Wizarani hatuna taarifa hiyo.

Baada ya pole hiyo napenda kumwomba Mheshimiwa Mbunge na kumhakikishia kwamba Wizara yangu ipo tayari kushirikiana na Watanzania wote na mpango wetu upo kitaifa kwamba pale ambapo mwananchi ameuawa na wanyamaporini tunatoa ubani bila kubagua.

Kwa hiyo, tunamkaribisha sana alete taarifa hizo zitahakikiwa na pole zitatolewa kama ambazo tumefanya maeneo mengine.

Na. 396

Madaraka ya Mkuu wa Mkoa na ya Bunge

MHE. GODFREY W. ZAMBI aliuliza:-

Kwa kuwa Ibara ya 61(1) ya Katiba ya nchi inamtaja Mkuu wa Mkoa kama Kiongozi katika Serikali, na Ibara ya ya 61(4) imetaja wajibu wake kuwa ni kusimamia utekelezaji wa kazi na shughuli zote za Serikali katika Mkoa aliopewa kuongoza.

Lakini wakati huo huo katika Ibara ya 63(2) ya Katiba ya nchi inalitaja Bunge kama chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chenye madaraka kwa niaba ya wananchi kuisimamia, kuishauri Serikali na vyombo vyake vyote ikiwa ni pamoja na kutekeleza majukumu yaliyotajwa na kwenye Ibara ya 63(3)(a) – (e):-

(a) Je, Wakuu wa Mikoa ambao ni Wabunge kubaki kwenye Kamati za Bunge sio kwenda kinyume na Katiba ya nchi?

(b) Je, Serikali sasa iko tayari kuwaondoa Wakuu wa Mikoa ambao ni Wabunge kwenye Kamati za Bunge ili kuondoa utata kwamba wao kama sehemu ya Serikali hawapaswi kuwa ndani ya Kamati hizo kama ilivyo kwa Mawaziri ili kulipa Bunge uhuru mkubwa zaidi wa kuisimamia na kuishauri Serikali wakiwemo na Wakuu wa Mikoa?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, lenye sehemu (a) ana (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sio kinyume cha Katiba kwa Wakuu wa Mikoa ambao ni Wabunge kubaki kwenye Kamati za Bunge kwa sababu Mkuu wa Mkoaa ambaye pia ni Mbunge kwa mujibu wa Katiba anazo kofia mbili yaani Mbunge na Mkuu wa Mkoaa. Hakuna sehemu yoyote katika Katiba inayomzuia Mkuu wa Mkoaa kuwa Mbunge au Mbunge kuwa Mkuu wa Mkoaa. Mkuu wa Mkoaa kwa upande mmoja ni mtendaji wa Serikali na upande mwagine ni mwakilishi kwa dhana ya kuwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu si mgeni; kwa mfano, Waziri ni mtendaji wa Serikali, lakini pia ni Mbunge. Hoja zinapokuja kuhusu Wizara yake ndani ya Bunge, hujibu hoja kama mtendaji wa Serikali. Lakini kama kuna hoja inayohusu Jimbo lake anaweza kuuliza au kuomba ufanuzi kwa maandishi kutoka kwa Waziri mwenzake kwa ajili ya maslahi ya wapiga kura wake.

Mheshimiwa Spika, Rais kwa mujibu wa Katiba ya nchi ni Kiongozi na Mtendaji Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 62(1) ingawaje si Mbunge, yeze ni sehemu ya Bunge. Aidha, Waziri Mkuu ni Mbunge, lakini kwa wadhifa wake Serikalini ni mtendaji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mifano hii, dhana ya kuwa na kofia mbili haileti mgongano wa kikatiba. Mkuu wa Mkoaa atakuwa Mbunge akifanya shughuli za kibunge na atakuwa Mkuu wa Mkoaa akifanya shughuli za kiutendaji kama Mkuu wa Mkoaa wake. Kuwepo kwa Wakuu wa Mikoa katika Kamati za Bunge hakuzuii Bunge kuisimamia na kuishauri Serikali. (*Makofi*)

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kuwa na kofia mbili hakuna matatizo.

Lakini je, atakubaliana na mimi kwamba unapokuwa Mkuu wa Mkoaa unakuwa Mbunge huwezi ukazitendea kazi sawasawa nafasi zote mbili na kwa maana hiyo nafasi moja haitatendewa sawasawa.

Je, kuna ulazima wowote wa kuendelea na kofia hizo mbili?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, kwa kuwa Ibara iko wazi kifungu cha 63(2) kwamba kazi ya Bunge ni kuisimamia na kuishauri Serikali; Je, Mkuu wa Mkoaa anapokaa kwenye Kamati ya Bunge hususan nitoe mfano wa Kamati ya Fedha inapojadili taarifa za fedha na Mkuu wa Mkoaa yuko kwenye Kamati hiyo, yeze anasimamia wapi kama siyo utata wa kikatiba? (*Makofi*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, suala la kutendea haki ama kutotendea haki kazi moja kama una kazi mbili, nafikiri ni suala la uwezo tu na nina uhakika, wale ambao wameteuliwa kuwa Wakuu wa Mikoa na pia ni Wabunge, wana uwezo na mpaka sasa wamekuwa wakizitendea haki nafasi zote mbili, wamekuwa wakihudumia Majimbo yao ya Uchaguzi na wamekuwa wakihudumia pia Mikoa ambayo wamepangia kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, suala la pili kwamba inapotokea kwamba wewe ni Mkuu wa Mkoa na uko ndani ya Kamati ya Bunge, basi inapokuja *issue* ambayo inahusu Mkoa wako ni ku-*declare interest* tu kama tunavyofanya hapa ndani ya Bunge. Unapokuwa na *issue* ambayo inakuhusu, basi una-*declare interest* kisha unachangia ama una-*withdraw*, nafikiri huo ndio utaratibu utakaofaa.

SPIKA: Naona nitaruhusu wawili! Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa halafu Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya.

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa dhana ya kutenganisha kofia inatokana na dhana pana zaidi ya *check and balance* yaani mamlaka moja kudhibiti mamlaka nyingine na kwa kuwa Tanzania tunafuata utawala bora na kwa kuwa kutokuwa na *check and balance* ni kigezo kimojawapo cha kutokuwepo utawala bora: Je, Mheshimiwa Waziri anakubaliana kwamba japo Katiba haipingi wala haisemi chochote kuhusu Wakuu wa Mikoa kuwepo kwenye Kamati zetu: Je, anakubaliana kwamba ni kinyume na taratibu za utawala bora?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, *concept* ya *checks and balances* ipo katika mihimili tofauti ya Dola, mhimili mmoja unau-*check* mwengine. Lakini, inapotokea kwamba kazi hizi ziko katika Mhimili mmoja tu, hilo wala haliji wala halihusiani. *Actually* unapokuwa na *Regional Commissioner* ambaye pia ni mtendaji wa Serikali hapo hapo. Kwa hiyo, mimi sina matatizo na hilo kwa sababu *checks and balances* anazozisema Mheshimiwa Slaa zinahusu mhimili kama vile Hakimu au Jaji, ghafla huyu sasa anakuwa tena labda Mkuu wa Mkoa, inakuwa kidogo tofauti. Lakini ndani ya mhimili mmoja, sidhani kama hilo ni tofauti.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa kifungu namba 64(1) cha Katiba kinazungumza kuwa, (samahani sioni vizuri) majukumu yote ya kutunga sheria ya mambo mengine ya Tanzania, majukumu hayo yatakuwa mikononi mwa Bunge na kwa kuwa Bunge linajumuisha Wabunge kutoka Tanzania Bara na Tanzania Visiwani: Je, Kifungu hiki hakileti dosari kwa misingi kwamba wakati wa kujaza akidi, Wabunge kutoka upande mmoja wanaweza kujaza akidi na kusababisha maamuzi yatakayoumiza upande wa Bara?

SPIKA: Nadhani tulisubiri wakati wake hili swali kwa sababu swali la msingi lilihusu Wakuu wa Mikoa, sasa swali hili la nyongeza linakuja kujumuisha tena upigaji kura na akidi kwa uwakilishi wa Zanzibar ama Bara. Kwa hiyo, lina matatizo. Niseme tu kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wengi sana wanataka kuuliza kuhusu masuala haya, nadhani linahitaji mjadala mpana zaidi kwenye Kamati, pengine Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inaweza ikazingatia suala hili, halafu tukapata ushauri amba ni mzuri maana limeulizwa na wengi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, muda wa Maswali umepita na maswali yamekwisha. Sasa niwakaribishe wageni. Mheshimiwa Dr. Mzeru Nibuka ana wageni kutoka

Morogoro Jimboni kwake, Bwana Omari Hassan, Makalla, haikuandikwa Bwana au Bibi, kuna jina tu Makalla. Naomba wasimame! Karibuni sana, karibuni! Ahsante sana.

Wapo wageni 14 wa Mheshimiwa Estherina Kilasi wakiambatana na Kiongozi wa Msafara – Afisa Utamaduni, nadhani atakuwa wa Mbarali, Amos Chiwaya na Edward Musoma – Afisa Utumishi na Lida Lubida – Msaidizi wa Mheshimiwa Mbunge. Ahsante sana!

Wapo wageni 11 wa Waheshimiwa Aloyce Bent Kimaro na Dr. Cyril Chami amba ni Viongozi wa VIKOBA kutoka Kilimanjaro wakiongozwa na Mama Mrema ambaye ndiye kiongozi wao. Naomba wale wa Kilimanjaro wasimame! Ahsante sana. Tena wamevaa sare! (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tu ishara za kupiga makofi kwa wageni haziruhusiwi. Wanatakiwa kusimama tu, kanuni zetu haziruhusu, mnawenza kutabasamu, kupunga mkono lakini msipige makofi. Hata hivyo, karibuni sana. Tunafurahi.

Wapo wageni 29 wa Mheshimiwa Dr. Aisha Omar Kigoda, Naibu Waziri wa Afya, wakiongozwa na Ndugu Joyce Safe – Kiongozi aliyejewa Msajiri wa Baraza la Waaguzi na Wakunga; sasa hii ni Jumuiya ya Wakunga nadhani, Waaguzi na Wakunga. Wale pale, ahsante, karibuni sana. Mama Joyce Safe, Ndugu Alice Usher, Aha, *Alice Usher is from America. You are warmly welcome to Tanzania! We are happy that you are cooperating in the Health Sector. Thanks very much for being here and for all the work that you are doing. Thanks very much.* Karibuni sana Waaguzi na Wakunga, tunashukuru sana. Kazi yenu ngumu, lakini mengine huwa yanalipwa na Mwenyezi Mungu tu, hapa duniani hupati chochote. Ahsante sana.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge wa Wilaya ya Lushoto; Mheshimiwa Sebaru – Diwani na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto, Mheshimiwa Ndege – Diwani na Mheshimiwa Shedafa – Diwani. Karibuni sana Waheshimiwa kutoka kwenye Milima ya Usambara.

Wapo kwenye *Public Gallery* wageni wengine kama ifuatavyo amba wanatoka Chuo Kikuu Dar es Salaam, Law School:- Bwana Alex Luoga, Bi. Josephine Paul, Bwana Allen Mtetemela, Bwana Isdory Joseph Kaaya, Bwana Noel Ndallu na Bi. Beatrice Nsana. Karibuni sana, ni vizuri sana kwa watu mnaojihusisha na sheria kuja kuona mahala ambapo ndio chimbuko hasa la utungaji wa sheria. Karibuni sana.

Wageni saba wa Mheshimiwa Ruth Msafiri wakiambatana na familia yake ni Kijana anayeitwa Imani ambaye ni mwanaye Mheshimiwa. Imani, ooh, mdogo sana, naona ameshikiliwa tu hivi. Karibu sana! Robert Kashemba ambaye ni Mjomba wake. Ahsante sana, Hao ndio wageni wa Mheshimiwa Ruth Msafiri.

Wageni wa Mheshimiwa Manju Msambya ni Shekh Ahmed Zuber – Shekh wa Mkoa wa Dodoma. Yuko wapi Shekh? Aah, ahsante sana! Watu wa Dini kama ninyi mnatuletea baraka humu, tunahitaji muwe mnakuja mara kwa mara. Bwana Yusufu Maulid naye ni rafiki yake Alhaj Msambya. Karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wanafunzi 30 kutoka Shule ya Msingi Santome na Walimu. Ndio wale pale! Lo! Hizi sare nadhifu kweli kweli hizi! Inapendeza sana. Jana tulikuwa na sare za aina ile nyingine, leo ziko za aina hii. Ahsante walimu na wanafunzi, tunawatachia mema katika masomo. Haikaribii sana, lakini ni tofauti kidogo. (*Makofi/Kicheko*)

Wapo wanafunzi 30 kutoka Shule ya Msingi Jomari, nadhani wapo hapo kwenye Ukumbi mwingine. Wanafunzi 40 kutoka *ACT Vocational Centre*. Nadhani nao wapo katika Ukumbi ule mwingine. Aah, ndio wale! Ahsante sana! Ahsante vijana. Tunawatachia mema katika shughuli zenu.

Matangazo ya Kazi zetu, Mheshimiwa Anna Kilango Malecela, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati hiyo ya Miundombinu kwamba leo kutakuwa na Kikao saa 7.00 Mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa, nadhani wanakutana na Wadau wa mambo fulani ya Miundombinu. Ni kikao muhimu sana. Pia Mheshimiwa Gideon Cheyo - Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji anahitaji Wajumbe wote wa Kamati hiyo ya Kilimo, Mifugo na Maji wakutane leo saa 5.30 asubuhi katika Ukumbi Na. 231. Kwa hiyo, Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, saa 5.30 leo ukumbi Na. 231. Kuna tangazo lingine? Mheshimiwa Estherina Kilasi, anauliza, kwa nini wageni wake hawakusimama! Sasa hilo siyo tatizo langu! Wageni wa Mbarali wale. Aah kumbe wapo! Basi nadhani pengine ni mara ya kwanza hawakukumbuka utaratibu. Tunashukuru sana. Mtusalime sana huko Mbarali na mwendeleze sana na kilimo cha mpunga. Dunia inahitaji mchele kwa wingi, kwa hiyo, Mbarali tunakutegemeeni sana na mwendelee kumuunga mkono Mbunge wenu Estherina Kilasi, ni mtu muhimu hapa Bungeni, anafanya mambo mengi kwenye Kamati. Waheshimiwa Wabunge, basi hayo ndiyo matangazo yetu ya leo. (*Makofi/Kicheko*)

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009 Wizara ya Katiba na Sheria

(*Majadiliano yanaendelea*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, bado nina orodha ya Waheshimiwa Wabunge 15 hivi, ni dhahiri hawataweza kupata nafasi wote kwa sababu tunaweza kufikia kama 12 kwa makadiro yangu niliyonayo hapa. Kwa hiyo, tutazingatia hilo. Tutaanza na Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, atafuata Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Shally Raymond na Mheshimiwa Manju Msambya, halafu nitatangaza na wengine kwa utartibu huo.

MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kukubali nichangie leo asubuhi, hivyo kuniwezesha kushiriki kikamilifu kwenye kikao muhimu kilichofanyika jana cha Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mathias Chikawe kwa kuwasilisha bajeti ya Wizara yake kwa ufasaha mkubwa. Vile vile nampongeza kwa kututhibitishia wote hapa kwamba pamoja na kutokuwa na Naibu Waziri, anaweza akafanya kazi barabara na kwa ufanisi mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimefarijika sana na taarifa iliyoko ukurasa 35 wa taarifa ya Mheshimiwa Waziri inayoelezea utekelezaji wa hatua ya kutenganisha shughuli za upelelezi na shughuli za uendeshaji mashitaka, shughuli ambazo kwa muda mrefu sana zimekuwa zikiendeshwa na Polisi. Polisi huyo huyo anakamata, Polisi huyo huyo anapeleleza, Polisi huyo huyo anahoji kwa maana ya *interrogation*, Polisi huyo huyo anaamua nimpeleke huyu Mahakamani, nisimpeleke na Polisi huyo huyo anaendesha mashitaka. Kwa kweli hiyo hali haikuwa nzuri sana na haijawa nzuri mpaka leo kwa sababu madaraka yote hayo kuwa kwenye mikono ya chombo kimoja ni hatari kwa utawala wa sheria na utoaji wa haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini tumechelewa sana kuanza utekelezaji wa zoezi hili hasa ikizingatiwa kwamba pendekezo la kutenganisha shughuli hizi lilitolewa kwa Serikali tarehe 12 Agosti, 1977 (miaka 31 iliyopita) na Tume ya Kupitia Mfumo wa Utoaji Haki (*The Judicial System Review Commission*) iliyokuwa inaongozwa na Mheshimiwa Pius Msekwa, wakati huo akiwa Makamu wa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, nasema tu kwamba hali hii ya kukalia mapendekezo ya msingi kama haya kwa miaka 31 haipendezi. Ni muhimu kwa Serikali kutekeleza bila kuchelewa sana mapendekezo ya Tume ambazo Serikali yenye inaziunda Tume zinatumia muda mwangi na pesa ya walipa kodi.

Mheshimiwa Spika, lakini yaliyopita si ndwele, tugange na yaliyopo na yajayo. Ninachosema tu ni kwamba ili zoezi hili la *Civilianization of Prosecution* liweze kufanikiwa vizuri, basi kuna umuhimu kuboresha mazingira ya kazi ya Mawakili wa Serikali. Kwa kweli hali yao siyo nzuri sana na naweza kudiriki kusema Wizara ya Katiba na Sheria ni moja ya Wizara ambazo kwa kweli wataalam wake wanakimbia kwa urahisi sana kutokana na mazingira ambayo siyo mazuri. Na siyo kosa la Mheshimiwa Waziri au Katibu Mkuu, ni kosa letu sisi wote kwamba kwa kweli *tuna-provide* hela kidogo sana kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, mimi sisemi Wakili wa Serikali alipwe kama Wakili wa Kujitegemea, hapana. Ninachosema ni kwamba, tumeshindwa kuwapa vijana wetu mahitaji ya msingi kabisa kuweza kutekeleza kazi zao. Wakili wa Serikali ambaye tunambebesha mafaili ya kesi za ujambazi, kesi za ufisadi, kesi za aina mbali mbali, hatujui analala wapi. Tunachojua tu sisi ni kumpa Sh. 70,000/= kwa mwezi akatafute chumba. Siku hizi tumeongezea eti 100,000=/. Hata kwa Dodoma hapa, hupati nyumba kwa 100,000/= na Dar es Salaam ndio shida. Kwa hiyo, vijana wetu wametawanyika

hovyo kwa Mfuga Mbwa, sijui Gongolamboto Dar es Salaam na kadhalika. Tunawaweka kwenye vishawishi vikubwa mno!

Mheshimiwa Spika, kwenye nchi za jirani, wenzetu tu hapa hapa, *State Attorneys* wanakaa kwenye *Quarters* za Serikali ambazo ni more *secure* kiusalama. Hapa, siku hizi inakuwa sherehe kwa mwenye nyumba akiona Wakili wa Serikali anakaa nyumbani kwake kwa maana kila asubuhi anakuja kugonga mlango “kijana wangu, hebu nisaidie mtoto wangu wa jirani pale kakamatwa na bangi, kamtoe.” Basi ndio kazi hiyo vijana wetu wanafanya. Tunawapeleka huko.

Wakili wa Serikali hana usafiri. Yeye na daladala, daladala na yeye. Mvua inyeshe, juu kali, akiwa na mafaili ya Serikali. Wakili wa Serikali tunamtegemea awe *smart*; suti nyeusi, kiatu cheusi, soksi nyeusi, shati jeupe na haliwezi kuwa moja tu, litaleta utando wa kutisha, kwa hiyo, mashati ya kutosha meupe, tai nyesi na tai maalum nyeupe. Lakini pesa tunayompa Wakili wa Serikali kununulia vitu hivyo, haitoshi hata kununulia robo ya vitu hivyo. Nafikiri kuna umuhimu sasa hivi kuongeza bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri na uongozi mzima wa Wizara akiwepo rafiki yangu Salula - Katibu Mkuu mwenye uwezo mkubwa sana, walipiganie suala hili ili mwaka ujao wa fedha tuone mabadiliko ya *package* ya *State Attorneys*. Mimi nimefurahia kidogo kusikia kuhusu habari ya Mahakama. Taarifa ya Mheshimiwa Waziri iko ukurasa wa 50 wa kitabu chake inasema kuwa kimsingi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekubali kuanzishwa kwa Mfuko wa Fedha wa Mahakama (*Judiciary Fund*). Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, kwa sababu Rais alikubali mwezi wa Tano, mwezi Oktoba tuone Muswada wa Sheria hiyo hapa, tusichelewe chelewe. Mahakama iko katika hali mbaya, wanahitaji *an Independent Fund*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee suala moja dogo lingine. Jana jioni nilishitushwa na joto lililokuwepo humu ndani kuhusu Mahakama ya Kadhi. Nikapata wasiwasni kidogo kwamba pengine sikusoma vizuri hotuba ya Waziri wa Katiba, kwa hiyo, ikabidi niisome tena ukurasa wa tano mpaka ukurasa wa saba. Lakini ujumbe niliyoupata pale ni mzuri tu. Taarifa inasema, Tume ya Kurekebisha Sheria imekamilisha utafiti wake na taarifa yake imewasilishwa Serikalini na Serikali sasa hivi inatafakari taarifa hiyo na uamuzi wa Serikali utaletwa Bungeni. Sasa hili joto linatoka wapi? *Why are we jumping the gun?*

Mheshimiwa Spika, utadhani kwamba sasa tumepewa Muswada wa Mahakama ya Kadhi uko mbele yetu, sasa tunabishana! Hapana! Mheshimiwa Waziri ameleta habari njema sana kwetu. Baadhi yetu, tunadhani hili suala ni jepesi sana. Wengine wanasesma, hivi mnachelewesha nini? Tungeanza hata jana! Hapana! Wengine walifika hatua jana, nimesikitika kusema eti wengine haliwahu! Eeh, hii hatari! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nadhani hii sio sahihi, wote tunahusika, Mahakama hii ikianza wote sisi Waislam na wasio Waislam, tutachangia uendeshaji wake kuitia kodi zetu. Kwa hiyo, wote tunahusika! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siku ya siku tutalazimika kurudi tena hapa, kubadilisha Ibara ya 19(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inayosema: "Serikali haitajihusisha na uendeshaji wa vyombo vya dini." Itabidi tuibadilishe na kuibadilisha hiyo haitahitaji Waislam peke yao, itahitaji wote hapa. Ibara ya 98 ya Katiba inasema, unahitaji theluthi mbili ya Wabunge wote kuweza kuitisha hilo suala. Kwa hiyo, wote tunahusika! Mimi naomba tuiachie Serikali ifanye kazi yake kwa uangalifu, hili si suala jepesi kama ambavyo wengine wanasema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wengine wanasema, aah, unajua Zanzibar mbona hakuna matatizo. Jamani, Zanzibar ni tofauti. kwani zaidi ya asilimia 99 ya wananchi wake ni Waislam. Kwa hiyo, siyo kitu cha kulinganisha. Ni sawa na Ujerumani. Mimi nimeishi Ujerumani. Ujerumani ukilipwa mshahara, unalipia kitu kinaitwa *Kirchensteur* ambayo ni kodi ya Kanisa, mpaka unajiuliza hivi hawa watu wana akili timamu! Unaambiwa eeh, hapa watu zaidi ya asilimia 90 ni Wakristo. Kwa hiyo, tusitoe mifano ambayo hailingani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kumetolewa mifano ya Uganda. Mimi nimefanya kazi Uganda. Uganda, Mahakama ya Kadhi iko kwenye Katiba, lakini mpaka leo haijaanza kufanya kazi. Kwa hiyo, Serikali ambayo ni *prudent*, lazima iangalie kwa makini kabla ya kuanzisha. Tuipe Serikali muda, tusii-rush. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kadhi Mkuu kwa mfano, inapendekezwa sehemu nyingi na hata hapa itapendekezwa kwamba ateuliwe na Rais. Kwa hiyo, lazima Serikali ianze kuangalia. Je, *what if* Rais anakuwa Mkristo, nani atakubali kwa mfano Kadhi Mkuu ateuliwe na *Kafir*? Kwa hiyo, ni mambo ya kuangalia hayo, tusii-rush Serikali kwenye hayo.

Mheshimiwa Spika, mtu ambaye anaona anacheleweshwa, Katiba haimzuii wala Sheria haizuii kuanzisha utaratibu wa dini wa *dispute settlement*. Tuna mifano mizuri tu. Wakatoriki wanayo *a very elaborated system of dispute settlement* ambayo wanaigharamia wao wenyewe. Utakuta wana *Tribunal of First Instance* kwenye Jimbo, *appeal* zinakwenda kwenye *Tribunal of Second Instance* ambayo ni kwenye Taifa na Majaji pale ni Maaskofu yaani Baraza la Maaskofu na lazima hawa wote wawe wamesoma *Canon Law*. *Appeal* zinakwenda *Rome* na kule wanakaa Majaji watano. Sasa pale ikifika, ndio mwisho. Panaitwa *Signatura Apostolica*, ndio mwisho. Ndio *Supreme Court* hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasema yote haya kusisitiza tu kwamba jamani, hebu tusi-rush suala hili , tusiweke joto lisilo na maana, Serikali imepokea, Waziri amesema. Ametoa tamko zuri, kuwa watalileta Bungeni. Leo tunaongea utadhani kuna hoja hapa ya kadhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee hoja ya Msemaji wa Upinzani jana kwamba suala la Zanzibar ni nchi au sio nchi ni mgogoro wa kikatiba. Mimi siuoni

mgogoro wa Kikatiba hapa, ila ninachokiona zaidi hapa ni utovu wa nidhamu kwa baadhi ya viongozi. Nitaeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kikatiba uwajibikaji wangu, mimi kama Mbunge ni tofauti na uwajibikaji wa Waziri. Mimi nawajibika kwa vitu vitatu; nawajibika kwa Jimbo langu (wananchi walionipigia kura), nawajibika kwa chama changu na nawajibika kwa dhamira yangu kama Mtanzania, kama mzalendo. Lakini Waziri anafungwa na kanuni ya kikatiba ya kwamba yeze lazima awe na msimamo wa pamoja na Serikali nzima wanapokuwa hapa Bungeni. Inaitwa *Collective Ministerial Responsibility*. Wanafungwa na hicho. Sitaki kusoma Ibara ya 53(2) inayosema; Mawaziri wote chini ya Waziri Mkuu, wanawajibika kwa pamoja kwa Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema yote haya kueleza tu kwamba linaloamuliwa na Serikali, Mawaziri hawana *choice*, lazima kuunga mkono. Waziri Mkuu akinyoosha mkono wa kulia, wote lazima wanyooshe kulia. Wasiponyosha kulia watadondoka kwa sababu Waziri Mkuu akiamua tu kujiuzulu, mnajua *Cabinet* yote inakwenda. Waziri Mkuu akikohoa, wote homa hawa! Kwa hiyo, ninachosema tu hapa ni kwamba, kama Waziri au Naibu Waziri hakubaliani na msimamo wowote wa Serikali, hawezi kupinga hadharani. Wana vyombo vyao vyta siri vyta kuyamaliza humo ndani! Akitaka kuongea kama Mwakyembe au kama Mama Anne Kilango Malecela au Selelii au Ole Sendeka, basi ajiuzulu kwanza, huo ndio utaratibu wa *Westminster System*.

Mheshimiwa Spika, nasema haya kwa sababu kilichotokea hivi karibuni, mimi nasema ni fedheha kubwa kwa Serikali yetu. Mimi nasema *as a Constitutional Lawyer*. Waziri Mkuu ametoa tamko hapa Bungeni, tamko sahihi kabisa kwamba kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Zanzibar sio nchi *in the sense of a Sovereign State*. Akasema Wanasheria Wakuu kaeni chini, muangalie kama kuna dosari, basi muishauri Serikali. Kichekesho kinakuja. Mimi siwalaumu Wabunge, siwalaumu wananchi maana wananchi wana uhuru kujadili chochote. Lakini Mawaziri na sijali wa Zanzibar au wa hapa, kusimama kumkosoa Waziri Mkuu na kumkejeli, huko ni kutoka nje ya *Collective Ministerial Responsibility* ya Mawaziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wengine wanafikia mpaka hatua ya kusema, aah, hata hela yetu iko *BOT!* Jamani, mimi nimekuwa naijiliza, Serikali iko wapi? Usiri na heshima ya Serikali yetu umekwenda wapi? Vyombo vyta majadiliano ya Serikali nani amevipeleka likizo? Waziri wa Zanzibar anapomkejeli na kumkosoa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; anajua *constitutional implications* zake? Anaelewa? Sema tu muda hamna, lakini ningependa sana kulieleza kwa nini nasema kwamba lina *serious constitutional implications*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalize tu kwa kusema, sipendi kupigiwa kengele. Kilichotokea kuhusu suala la Zanzibar ni nchi au si nchi na *conduct* ya Mawaziri hasa wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni fedheha kubwa kwa Serikali. Hapa siuoni mgogoro wa kikatiba, ninachokiona hapa ni utovu wa nidhamu wa hali ya juu wa baadhi ya viongozi ndani ya Serikali, utovu ambao lazima uadhibiwe. Ukiacha kutoadhibiwa, mimi sitaona ajabu siku moja Rais akinyoshewa vidole usoni. Naunga mkono hoja! (*Makofi*)

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hii hoja muhimu. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake wote kwa ujumla kwa kazi nzuri waliyofanya kwa kutuletea Muswada huu na maelezo mazuri.

Mheshimiwa Spika, kabla sijasema lolote, niruhusu nitoe pongezi kwa Mkuu wangu wa Mkoa na *DC* wangu wa Singida kwa kazi kubwa waliyofanya ya kumkamata simba wa pili. Simba wa kwanza aliuwawa, Simba wa pili amekamatwa *physically* na sasa wanamsaka simba wa tatu, simba ambao wameua wananchi wapatao 14. Kwa hiyo, naomba nimpongeze Mkuu wa Mkoa, nimpongeze *DC*...

(*Hapa Kengele Ililia*)

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa, hiyo ndiyo ya kwanza? (*Kicheko*)

SPIKA: Haikuhusu kabisa, bahati mbaya tu! Endelea Mheshimiwa! (*Kicheko*)

MHE. MOHAMED H. MISSSANGA: Mheshimiwa *DC* na Kikosi chetu kile cha Wataalam kutoka Arusha, kwa kweli kimesaidia sana pamoja na wananchi kwa ujumla. Pongezi sana, *Inshallah* atapatikana huyu simba wa tatu ili kuondoa hofu kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, labda nianze na hili la Mahakama ya Kadhi. Naheshimu sana mawazo yanayotolewa na wenzetu na hasa ndugu yangu Mheshimiwa Mwakyembe hivi karibuni, wala sina matatizo naye, lakini niseme tu kwamba anaposema subira ifanyike, ninakubali na subira imefanyika muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, suala hili sio la jana wala sio suala la leo, kwa wale ambao wanalifahamu zaidi toka miaka ya 1950, suala la Mahakama ya Kadhi limekuwa likizungumzwa. Mheshimiwa Mwakyembe wakati anamalizia hapa amesema anataka sheria ya nini ije katika Bunge lijalo, alisema ingefaa sheria hiyo ije katika Bunge lijalo na pale Mheshimiwa Waziri anaposema limeshughulikiwa na limepata msaada wa Serikali ingekuwa inasema sasa Muswada unakuja katika Bunge lijalo angalau ingeeleweka, lakini linapokuwa lipo *indefinitely* kwamba limeshughulikiwa, Tume imemaliza, Serikali inakamilisha kwa sababu hayo ndiyo maelezo yametoka huko nyuma mpaka hivi leo linashughulikiwa lipo *indefinitely* hapo ndipo linapokuwa na matatizo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuvumilia kama ambavyo wamevumilia Waislamu kwa ajili ya jambo hili, lakini ningependa tuambiwe ni lini Muswada utakuja kwenye Bunge hili? Hii ya kuwa *indefinitely* ndilo linaleta matatizo. Kwa hiyo, nakubaliana naye kwamba tuwe wastahimilivu, lakini ni lazima tupewe *timeframe*. Haiwezekani ikawa jambo liko hewani tu siku zote kama linavyokwenda.

Mheshimiwa Spika, mimi kama Mbunge wa CCM, moja ya kazi yangu ni kutetea ilani ya Chama cha Mapinduzi na ilani ya CCM inasema wazi kwamba katika kipindi cha

miaka mitano hii suala la Mahakama ya Kadhi litapatiwa ufumbuzi, iko *clear*. Halafu bahati nzuri angalia Mungu anavyoweka mambo, ilani imetengenezwa, Mwenyekiti wa CCM akiwa Mkristo, Katibu Mkuu akiwa Mkristo, Makamu Mwenyekiti akiwa Mkristo, Waziri Mkuu Mkristo angalia mambo yanavyokuwa, lakini walifanya kwa nia safi.

Mheshimiwa Spika, kuna wengine leo wanataka kumpaka matope Mheshimiwa Rais wa awamu ya nne kwa jambo hili, wakati waliolitengeza wote kama nilivyoeleza ni wakristo. Ingekuwa Rais ni Muislam akalifanya hili au kama ndiyo lilikuwa linafanya sasa, kwa sababu Rais ni Muislam walahi sijui kama Ukumbi ungekuwa mkubwa, lakini Mungu ana kheri zake, Wakristo watupu maskini wa Mungu na mimi nawapongeza sana, mpaka Spika alikuwa Mkristo, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, wale ambao wanampaka matope Rais wetu wa awamu ya nne kwa hili, mimi nadhani hawamtendei haki na waache kufanya kitu kama hicho kwa sababu yeze kama Mwenyekiti wa Chama wa Chama cha Mapinduzi anasimamamia ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Mheshimiwa Spika, naomba itofautishwe kati ya Mahakama ya Kadhi na Serikali ya Kiislamu ni vitu viwili tofauti. Kwa sababu wasiiasi mwagine upo hapa watu wanachanganya mambo kwamba ikipatikana Mahakama ya Kadhi ni kama vile ndiyo imeingia Serikali ya Kiislamu, Sharia, hapana. Serikali ya Kiislam ni nyininge, inafanya mambo kwa mujibu wa *Quran* inavyosema, lakini Mahakama ya Kadhi atakuwa anatekeleza mambo ya Mahakama ya Kadhi kama inavyotakiwa wala haiingilii mambo ya kisheria na kadhalika na itakuwa ni *system* ndani ya *system* ya kisheria na itategemea namna itakavyokuwa umeelezwa. Lazima juu kule kutakuwa na Majaji na wengine ambao wanaweza wakapitia haya ambayo yataamuliwa na Mahakama ya Kadhi. Kwa hiyo, wasiiasi wa kusema kwamba eti akiingia Mahakama ya Kadhi atakatwa mkono, Zanzibar amekatwa nani mkono, niambiwe hapa? Mkenya kule kakatwa nani mkono? *For years and years* Mahakama ya Kadhi imekuwepo, nani amekatwa mkono? Nani amepigwa risasi? Nani amekatwa kichwa? Hizo ni *worries* za kuwatisha watu bure bila sababu za msingi.

Mheshimiwa Spika, naomba tutofautishe kati ya Mahakama ya Kadhi ya Serikali ya Kiislam hapa tunachoomba ni Mahakama ya Kadhi, siyo Serikali ya kiislam.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, nataka nieleze kwamba Katiba inaruhusu Waislamu kuabudu au kufanya ibada wanavyoona inafaa. Sasa katika Uislamu chombo hiki kitatekeleza mambo ya ibada, kwa sababu ndoa Kiislamu ni sehemu ya Ibada, talaka Kiislamu ni sehemu ya Ibada, wakfu Kiislamu ni sehemu ya Ibada, mirathi Kiislamu ni ibada, sasa utaniambiaje Ibada niifanye upande mmoja upande wa pili nisifanye ibada? Unasema kwamba Serikali inamruhusu Muislamu au Mkristo kuabudu anavyoona yeze imani yake, lakini sasa unaniambia nenda kasali, nenda Hija, katoe zaka, lakini katika mambo ya ndoa, talaka usifanye; hunipi uhuru wangu!

Mheshimiwa Spika, nataka wenzetu wajue kwamba suala la Mahakama ya Kadhi ni chombo ambacho kitatekeleza ibada kama ambavyo Serikali yenye we imekiri kwenye

katiba kwamba kila mwananchi atapewa fursa ya kuabudu bila kuingiliwa hilo ndiyo jambo lingine ambalo nadhani ningetaka niliseme.

Mheshimiwa Spika, wasiwasi uliopo mimi ningesema hakuna sababu ya kuwepo kwa sababu, hatutaendesha itikadi ya Kiislamu, tunachohitaji hapa ni Mahakama ya Kiislamu ili iweze kuwatendea haki hawa Waislamu kwa sababu baadhi ya ibada hawazifanyi au hazifanyiki sawa sawa.

Mheshimiwa Spika, nchi hii tumekaa katika mkao wa kuvumiliana, wakristo wawavumilie waislamu na waislamu wawavumilie wakristo, kama rafiki zangu wa Vyama Upinzani, ndugu yangu Cheyo pale anivumilie mimi kama mtu wa CCM na mimi nitamvumilia kama mtu wa upinzani, ndiyo maana kuna amani na utulivu kwa sababu tunavumiliana. Mbona yapo mambo Waislamu wanavumilia hapa nchini jamani? Wenzetu nao wajifunze kuvumilia! Hivi nikiambiwa nifanye kazi siku siku ya Ijumaa na ninatakiwa kwenda Msikitini, siku yangu ya kupumzika mbona mimi navumilia? Muislamu gani amelalamika? Lakini mbona wenzetu Jumapili hawafanyi kazi? Wasabato Jumamosi hawafanyi kazi? Hakuna mtu analalamika! Tuvumiliane! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kuwa na Balozi mbili hapa nchini, yaani ubalozi wa Italy na Ubalozi wa Vatican sio wengi wanaelewa, kama nchi ya Italy ina ubalozi, lakini Vatican ipo hapa kwa *interest* ya imani. Nani Mwislamu amelalamika? Hakuna Muislamu aliyelalamika. Nasema tujifunze kuvumiliana, ndiyo maana nchi hii ina utulivu na amani. Tunaweza kупingana bila kupigana, tupingane lakini tusipigane.

Mheshimiwa Spika, katika mambo haya kama iliyopale penye tofauti tupingane.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo mengi tu. Unakumbuka tunesema sana habari ya kupita na magari yetu, mbwa wananza nusa magari, watu wengine siku hizi hawaingii na magari Bungeni kwako hapa, Mbwa anapita kwenye gari ananza nusa wakati kwa mimi Muislamu ni taabu lakini tumevumilia mpaka wengine wameamua kuweka magari yao nje, hilo naomba wakaliangalie, yote haya ni kwa sababu ya uvumilivu tunawavumilia wenzetu na basi watuvumilie na sisi.

Mheshimiwa Spika, baada ya hilo, nataka niseme habari ya Mahakama ya kawaida, kwa maoni yangu iko tofauti kubwa sana kati ya Majaji na Mahakimu *Magistrate* na hawa Mahakimu wa chini ipo tofauti kubwa sana, kana kwamba ukisema Mahakama ya kawaida *impression* iliyopo ni kwamba ni Majaji, kama ni maboresho ni Majaji, kama ni kwenda semina za nje ni Majaji lakini *Magistrate* kwa maana ya *Magistrate* ambayo ndiyo wanafanya *donkey work* mazingira yao ya kazi ni magumu. Mheshimiwa Mwakyembe alikuwa anazungumzia Mawakili, mimi naomba twende *further* kwenye Mahakimu. Mshahara wa Hakimu na Mshahara wa Jaji, *ratial* ni moja kwa sita au moja kwa tano. Kama Hakimu anapata laki moja, Jaji anapata laki tano, kama Hakimu atapata milioni moja, Jaji anapata milioni tano au sita, *the difference is too big*. Hii ni *chain* tu lakini *jurisdiction* ndizo zinawatenganisha hawa, naomba Serikali

iliangalie hili, waangalie na Mahakimu hawana nyumba, hawana gari, hawana ulinzi, anamhukumu kwa mamlaka niliyopewa nakuhukumu jela miaka kumi halafu akitoka hapo anaingia kwenye daladala na ndugu ya huyu aliyehukumiwa miaka kumi, jamani hatulioni hili?

Mheshimiwa Spika, anaingia kwenye daladala pamoja na ndugu hawa ambao umemfunga mtu ndugu yao miaka kumi hana mlinzi hana chochote, hana posho ya nini, naomba sana Mahakimu nao waangaliwe, kwanza mazingira yao ya kazi ni magumu hana usafiri, hana nyumba, anatakiwa tu aje kesho kazini afanye kazi, lakini kalala wapi? Hajulikani! Kaja namna gani? Hajulikani! Kala nini? Hajulikani! Mbaya zaidi hawa wanaandika *Judgment* kwenye majumba yao wanayokaa, anachukua mafaili 20-30. Mimi nimemwona mmoja amebeba mafaili anakwenda nayo nyumbani kwake Mbagala, au Manzese na anajiandikia *judgement* kwa muda wake mwenyewe lakini maslahi yake ni duni. Naiomba Serikali, mimi nilidhani baada ya kukamilisha ile sheria ya Majaji ambayo ililetwa hapa sasa ingefuatwa sasa na mahakimu nao wakaangaliwa ili waweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, wakati mwengine unaweza kusema ndiyo maana tunaongeza Majaji kuwa wengi juu kwa sababu kazi haifanyiki sawa sawa, (sasa kama mimi hinilipi sawa sawa bwana wapo Majaji juu watakwenda kumalizia, mimi kwa hapa niliposema kwa hiki ninachopata mimi nadhani hapa nilichofanya sawasawa) anakata mtu rufaa lakini kama Mahakimu wangelipwa vizuri, Mahakimu wa mwanzo wangelipwa vizuri, nina hakika wangechukua *concern* kubwa sana ya kuifanya kazi yake na *appeals* zingepungua kwa sababu huku chini tumekusahau.

Kwa hiyo, naiomba Serikali sana wawasadie wawaangalie Mahakimu hawa wa chini angalau mambo ya usafiri, malazi na kadhalika ili waweze kuweka mazingira yao mazuri katika kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii adimu na niseme tu kwamba siku njema huonekana asubuhi kwani ametufungulia mwanasheria mwenyewe kuchangia mjadala.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru mwenyezi Mungu kwa kutupa tena afya kuweza kukutana hapa kwa ajili ya kutetea maslahi ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, mjadala huu umekuwa mzuri na niseme kwa hakika ni muhimu sana nimpongeze Waziri wa Katiba na Sheria kwa jinsi ambavyo alivyoweza kuwasilisha hapa vizuri na jinsi ambavyo jana alikuwa na wageni muhimu, naamini bado wapo akiwepo Jaji Mkuu lakini pia niseme watu wamejitlea kuuchangia vizuri sana nami naomba kuungana nao.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea naomba niwapongeze Wanasheria wote wanaoitwa *learned Brothers and Sisters* popote walipo na pia niwapongeze zaidi kwa

jinsi walivyo nadhifu kwa mavazi yao kama alivyoelezea Mwanasheria mwenzao, siku hizi ukivaa suti hasa ikiwa nyeusi unaulizwa: Je, wewe ni Mwanasheria? Tujibu tu kwamba siyo wote wanaovaa suti ni wanasheria. Lakini wao zinawapendeza zaidi kwa sababu zinawaonyesha walivyo na msimamo.

Mheshimiwa Spika, nina mambo manne ambayo ningependa kuzungumzia na kabla sijaendelea ningependa tu niyaseme na yatakuwa kwenye *Legal Sector Reform*. Jambo lingine ambalo nitapenda kuzungumzia ni lile la *Law School* ambayo inatarajiwu kufunguliwa na pia ningependa kuzungumzia elimu ya sheria kwa raia wetu na mwisho kabisa nitapenda nijikite kwenye yale mambo ya wanawake na sheria.

Mheshimiwa Spika, nianzie, hapo kwenye elimu ya sheria kwa wananchi wetu Tanzania, bado naona kwamba wananchi wetu hawajaelimika kwenye eneo hili la sheria na katiba, ni hivi majuzi kwenye viwanja vya sabasaba kule Dar es Salaam watu walikuwa wanadai wapatiwe Katiba, lakini mimi nikajiuliza hivi kupatiwa Katiba bila kuelimishwa kuhusu Katiba inaweza kusaidia chochote?

Mhehsimiwa Spika, nasisitiza kwamba ni vyema Katiba hizi ziweze kutolewa katika ngazi zote tukianzia kwenye Kata zetu hadi Mikoani, lakini pamoja na kupatiwa Katiba hizo ikiwezekana hii Wizara ya Sheria ikutane na izungumze na Wizara ya Elimu ili waweze kufundisha vijana wetu sheria katika umri mdogo.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu haki ya mtu ni muhimu kujua kama ilivyo kwamba mtu akiwa na ufahamu wa yeye mwenyewe anaweza kujitunza na kuweza kuleta maendeleo katika uhai wake.

Mheshimiwa Spika, unakuta kwamba mtu hapendi sana kwenda Mahakamani wala siyo jambo jema kumshtaki mwenzie, lakini pale ambapo hajui afanyaje ili kutetea haki yake. Walio wepesi watachukua mapanga au wale ambao wapo mitaani wakisikia mwizi wanamtundika matairi na kumchoma, sasa mimi najiuliza hivi watu hawa kufanya hivyo ni kiburi au ni kutokujua?

Mheshimiwa Spika, mara nyingi jibu linakuwa kwamba watu hawa hawajui ni jinsi gani wapatiwe haki yao, hivyo basi endapo wananchi wetu wataelimishwa kuhusu namna ya kujipatia haki, naamini kwamba mambo mengine ya uonevu, kuchomwa moto yatapungua na kuleta hali nzuri katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, katika *programme* yote ya *Legal Sector Reform* utakuta kwamba kuna mambo manne yameainishwa. Kuna lile la Mahakama za Watoto, kuna Mahakama za Ardhi na Mahakama za Biashara .

Mheshimiwa Spika, hapa kwenye Mahakama za Watoto naona bado ni changamoto sana. Pale kisutu sijafika, lakini tunaambiwa kuna Mahakama ya watoto, watoto wanaposikilizwa kesi zao huwa wanawekwa mahali ambapo hawapati bugudha. Lakini hili liko kisutu tu na sijui ni kwa jinsi gani linafanyika kwa ufanisi. Wakati mtoto mdogo amefikishwa Mahakamani baada ya kukamatwa na Polisi na labda Polisi huyo

amevaa nguo za kipolisi anafikishwa pale anaanza kuulizwa maswali hata kama jambo lile alikuwa alizungumze kama lilivyo mtoto yule anaingiwa na woga na anashindwa kujitetea.

Mheshimiwa Spika, kama hapo Kisutu inafanyika inavyotakiwa, ningeomba Mahakama hizo za Watoto zipelekwe hata Mikoani ili watoto hawa kesi zao zisikilizwe kwa usiri mkubwa na pia kwa ulinzi kadri ambavyo watoto wangependa, labda zisikilizwe mbele ya mama zao au yule mtu ambaye yule yuko huru naye zaidi.

Mheshimiwa Spika, haitoshi, naomba pia hao ambao wanashughulikia kesi za watoto kama hao wakiwekwa hao *ma-prosecutor* wawe wamepatiwa elimu ya *Counseling*, wawe pia wamefundishwa saikolojia na hapa ningeomba Wizara ya Katiba na Sheria iweze kugharamia elimu kwa wale wote ambao watakuwa wanashughulikia kesi za watoto. Inakuwa ni jambo gumu sana mtu kuzungumzia mtoto kwa vitisho, mtoto yule atakuwa na uwoga na matokeo yake hawezi kusema ukweli.

Mheshimiwa Spika, pale ambako hakuna Mahakama za Watoto, tunaambiwa wajifungie kwenye chumba, ile tu kufunga ile milango na yule mtoto akaona watu wazima wamesimama simama, mtoto yule anaingiwa pia na uwoga. Naomba katika *programme* hiyo Mahakama za watoto zijengwe mapema kwenye Mikoa yote na pia ihakikishwe kwamba zinakuwa katika hali ambayo watoto hawatakuwa na woga kujieleza.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba kuzungumzia hilo la Mahakama ya Ardhi. Ni kweli kwamba kuna wenzetu ambao wanajitahidi, wameweza sana kupita kote kuelezea umuhimu wa watu kufahamu haki zao na namna ambavyo mtu anaweza akawa na eneo lake bila kuingiliwa.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuwapongeza wakiwemo *TAMWA*, *TAWLA*, *KWIECO* na *NGO'S* zote ambazo zimeshughulika, lakini niseme pamoja na juhudhi hizo *NGO'S* zimechukua bado haitoshi, niombe tu *NGO'S* hizo zipewe msaada au zipewe uzito na nguvu zaidi na Wizara yetu ili elimu hii iweze kusambaa hadi vijijini kabisa. Jambo hili ni zuri na limeweza kuleta changamoto na pia limeweza kuleta hamasa na uelewa mkubwa kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika nizungumzie lile la *Commercial court*. *Commercial court* hizi ni muhimu sana na hasa ukizingatia kwamba maeneo mengi kesi za biashara huwa haziishi haraka, huenda basi wataalamu wengi wa kesi hizi hawapo au kesi hizi zina usumbu mkubwa. Hapa nataka nitoe mfano wa nilikotokea, nilikuwa nafanya kazi Benki. Mteja anakuja kukopa lakini huenda anashindwa kuendeleza mkopo au inamtokea kwamba mkopo ule ameshindwa kurejesha, ni lazima mtafikishana Mahakamani, mnapofika Mahakamani, katika Mahakama za kawaida zinapigwa tarehe miaka na miaka, lakini tulikuja kugundua kwamba kwenye *commercial court* jambo hili linachukua muda mfupi, bahati mbaya ni kwamba hizi Mahakama hazijaenea kwenye Mikoa yote. Huko Kigoma hazijafika, Mbeya, hazijafika, Mtwara na kwingine.

Naomba Serikali ione umuhimu wa Mahakama za Biashara kusambaa kwa sababu zina wateja wengi zikiwemo benki ambazo zingependa kesi zake zitatuliwe mara moja ili kazi ziweze kufanyika mapema.

Mheshimiwa Spika, nilizungumzia kuhusu *Law School*, naomba nitoe pongezi kwamba hili ni jambo jema na ninaamini kwa ambao watakuwa wamehitimu sheria baada ya mwaka 2007 itakuwa ni lazima waingie kwenye shule hiyo. Tatizo ninaloliona kwenye *Law School* pamoja na nia njema ni gharama za kujunga na *Law School*.

Katika udadisi wangu, nilielezwa kwamba gharama hazipungui milioni moja, yaani ni zaidi ya milioni moja. Nikajiuliza, maswali mengi sana, kijana huyu amesoma Chuo Kikuu kwa mkopo, amekuja amemaliza sheria anatakiwa kuingia *Law School*, mkopo wa Chuo Kikuu hajamaliza kuurejesha?

Je, ni nani atakayelipia ada yake katika *Law School* na kabla hujaingia *Law School* hujahitimu sheria, kwa nini sasa inavyokwenda na hatapata ajira? Hapa naomba Serikali iangalie endapo hii *Law School* itatafutiwa *Sponsors* ili hata mtoto wa mkulima anayetoka kijijini kama mimi aweze kuhitimu sheria yake vizuri na aweze kupata ajira.

Mheshimiwa Spika, hivi majuzi vijana wetu wengi wamependa kusoma sheria mimi nawapongeza sana kwa sababu hata nikiangalia hapa Bungeni leo Kiti cha Spika, kimekaliwa na mwanasheria, Msimamizi Mkuu wa Shughuli za Serikali hapa ni mwanasheria, Waziri mwenyewe wa hii Wizara ni mwanasheria na mambo yote naona yanakwenda kwa haki. Naomba hawa vijana wetu wa *Law School* wapate watu wa kuwalipia ili wamalize wote kwa pamoja na kuingia kwenye ajira.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa nawaomba hawa wanasheria zile lugha zao wanazozitumia Mahakamani wengi wetu zinatubabisha, zinaitwa *Legal Jargons*, kidogo Kiingereza hakini pigi chenga lakini wanapoingia kile kilatini au sijui ni lugha gani pale Mahakamani huwa inanisumbua, endapo mtu wa *level* yangu anapata taabu: Je, wale kabisa ambao wanakuja kutoka vijijini inakuwaje?

Mheshimiwa Spika, tuelezwe na ikibidi iwe hivyo kwamba lugha ya kutumika Mahakamani iwe ni Kiswahili. Wale walianza hivyo kwa sababu ndiyo ilivyowezekana kwa wakati ule, mkiwa wenye kwenye jopo lenu watumie hizo lugha, lakini tunapoingia sisi basi lugha zile ziweze kuangaliwa ni jinsi gani sisi watu wa kawaida tutanufaika?

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kabla kengele haijagonga ninajua kwamba kwenye mahakama za mwanzo hairuhusiwi kuweka wakili lakini: Je, inakuwaje? Naomba jibu wakati Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha.

Mheshimiwa Spika, mwisho, niseme tu kule nilikotoka Kilimanjaro Mahakama zetu nyingi za mwanzo hazina hadhi, ni chafu na zinaonekana kama *pombe shop*. Naomba Wizara hii itilie mkazo mwaka huu zisionekane kama eneo la vitochi zionekane kama Mahakama kwa kupiga rangi na kukarabati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba niunge mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. MANJU S. MSAMBYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii. Nitazungumzia mambo matatu. La kwanza, ni Idara ya Mahakama, la pili, Mahakama ya Kadhi na la tatu ni *OIC*.

Mheshimiwa Spika, wenzangu wote tangu jana wanalamikia hali ya Mahakama katika maeneo yao na mimi hali kadhalika na pengine niwazungumzie na Wabunge wenzangu wa Mkoa wa Kigoma.

Lakini nianze kwenye Jimbo langu na hasa huduma ya Mahakama ya Mwanzo. Huduma hii ni duni, Jimbo lote la Kigoma Kusini lenye Kata 12 Jimbo lenye ukubwa wa zaidi ya Nchi ya Burundi lina mahakimu wawili wa Mahakama ya mwanzo, sasa na wenzetu ambao tunawaita *learned Brothers and Sisters* wana lugha yao wanasema *justice delayed is justice denied*.

Katika eneo ambalo Hakimu wa Mahakama wa mwanzo atafika kwenye kituo baada ya miezi 12 sijui hapo kama kunakuwa na *justice administered*. Namwomba Mheshimiwa Waziri aangalie kwa makini namna ya kuhudumia eneo hilo na Mkoa wa Kigoma kwa ujumla ambao una uhaba wa mahakimu wa Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Spika, juzi alipokuwa anajibu swalí alinifariji aliposema kwamba sasa Mahakama za Mwanzo watapelekwa vijana wenye elimu ya Chuo Kikuu, basi ningeomba atakapokuwa anawapanga hao waanzie Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, nakwenda sasa kwenye hoja ya Mahakama ya Kadhi. Katika mazingira ambayo wenzangu kama Mheshimiwa Rished Mohamed Abdalah, Mheshimiwa Mudhahir Mohamed Mudhahir, Mheshimiwa Athuman Janguo, mkwe wangu, Mheshimiwa Missanga wameeleza suala hili kwa ufasaha kwa kweli nisingekuwa na sababu ya kwenda kwa undani kuhusu hili.

Mheshimiwa Spika, mimi nimeguswa mahala, kwanza nianze na kauli ya rafiki yangu, ni rafiki yangu mpenzi sana Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe. Dr. Mwakyembe mimi ni Mwanasheria wangu, anakumbuka vizuri alivyonisaidia kwenye kesi ya Uchaguzi ya mwaka 2000. Pamoja na kwamba kesi ile ilichukuliwa na Wakili mwingine. Lakini ile *donkey work* kama alivyosema mwenyewe ambayo inafanya na watu wa huku chini, basi yeye siku ile aliquwa siyo Wakili wa juu bali aliquwa Wakili wa chini. Alifanya kazi kubwa sana ambayo baadaye ilinivusha kwenye kesi hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwakyembe katoa mifano ya Zanzibar, kasema kuna Waislamu asilimia karibuni 98. Kwa hiyo tusichukue mfano wa Zanzibar. Sasa mimi nasema tuchukue mfano wa Kenya. Kenya unaweza ukasema kwa Kiingereza ni *pre-dominantly Christian*, ukitoa *Coastal Strip* ya Mombasa na kwenye miji kama Nairobi ambapo ni

pockets na Nakuru pamoja na Kisumu, mbona hatoi mfano wa Kenya kuhusu suala la Kadhi. (*Makofī*)

Mimi nimewahi kueleza na hasa ninapokuwa kwenye mikutano yangu ya kisiasa, wapo viongozi wa dini wawe ma-Shekh wawe ma-Padri, ma-Kasisi na Wachungaji, akitaka kujenga hoja kwa kutumia aya za vitabu vitakatifu, na hoja hiyo, ikiwa aya hiyo ina mistari minane, anasoma minne, ili ikidhi haja yake. Mingine minne anatia mfukoni. Sasa tunapotoa mifano ya masuala haya, twende wanasema Waingereza *full length* usitoe mfano mdogo ukaacha sehemu nyingine yoyote kubwa. Wapo watu wana hofu na suala la Mahakama ya Kadhi. Lakini kama alivyosema Mheshimiwa Missanga na kwa hoja yoyote ambayo Mbunge anachangia humu Bungeni, Msahafu wake ni huu hapa. Ni Ilani ya Uchaguzi, huzungumzia Mahakama ya Kadhi, huzungumzia kilimo.

Sasa leo kwa Mahakama ya Kadhi, hii ni ahadi ambayo Chama Cha Mapinduzi kimewaahidi Watanzania kitawafanyia nini? Moja ya ahadi zake ni hii. Wachangiaji wamemsifu sana Mheshimiwa Waziri hapa. Lakini mimi kwa bahati jana baada ya Bunge kuahirishwa jioni, nimemwona Mheshimiwa Waziri akihojiwa kwenye *TBC* kauli aliyotoa inapingana na yale aliyoyaandika kwenye kitabu hiki. (*Makofī*)

Pale watu wa *TBC* walipokuwa wanamwuliza anaeleza kwamba suala hili la Mahakama ya Kadhi ni lazima liridhiwe na watu wa upande wa pili kwa maana ya *Christians*. Hivi nchi hii inaongozwa kwamba Wakristo wakikubali jambo ndiyo litekelezwe? Hii ni kauli ambayo Mheshimiwa Waziri ameitoa alipokuwa anahojiwa na Waandishi wa Habari jana. Sasa mimi hii inanipa mashaka pale Mheshimiwa Waziri anaposema kwamba hoja hii ya Mahakama ya Kadhi sasa ameikabidhi kwenye Mamlaka ambayo inaishughulikia. Kumbe inawezekana kuna mamlaka nyingine na yenye vige vige imepewa kwa siri. Hiyo hakuitaja. Lakini jana alipokuwa anahojiwa na *TBC* katuambia mpaka na kundi hilo likubali. (*Makofī*)

Na akaeleza kitu ambacho mimi kilinishtua. Kwa kadri ninavyofahamu mimi Waislamu ndiyo wanaooo wake wengi. Tuna kawaida ya kupotosha mambo na kuchezea takwimu. Anasema katika nchi hii tuko *fifty fifty*. *Fifty fifty* Msambya ana wake wanne. Bwana John ana mke mmoja, ama Msambya huyu ni tasa, ama Msambya huyu watoto wake wote wamekuwa. Au Msambya huyu ametoa talaka kwa wake wote wanne kabla hata hawajapata hii mila. Inakuwaje tuwe *fifty fifty*? Hii ni kutaka kuhalalisha hoja tu kwamba nchi hii tuko sawa kwa sawa. Nani kafanya sensa hii?

Mheshimiwa Spika, twende kwenye kiini cha lini Mahakama ya Kadhi ilivunjwa na sababu ni zippi. Mimi nimekuwa napitia nyaraka. Baada ya hili suala la Mahakama ya Kadhi kuibuka katika uhai wa Bunge hili lilipoibuka Maaskofu wa Kanisa Anglikana walifanya mkutano hapa Dodoma na wakamkabidhi Mheshimiwa Rais matakwa yao. Lakini hata kabla Mheshimiwa Rais hajajajibu wakaanza kumshinikiza. Mnataka ajibu na mnamshinikiza kabla hajatimiza wajibu wake, kwa nini?

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Kadhi, siyo kwamba haikuwepo. Mahakama ya Kadhi imevunjwa mwaka 1963. Sasa tungeelezwa kwanza ni kwa nini ilivunjwa.

Hivi Waislamu wakati huo walionyesha wana matatizo kiasi gani mpaka wakaikataa Mahakama ya Kadhi? Au Serikali iliona kulikuwa kuna tatizo gani ambalo kuendelea kuwa na Mahakama ya Kadhi isingekuwa kwa maslahi ya Taifa. Tuelezwe hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, si suala la kuvunjwa Mahakama ya Kadhi, Watanzania na hasa Waislamu wanafahamu watakaofurahia hili wafurahie. Watakaochukia wachukie. BAKWATA ilianzishwa kwa kubandikizwa kwa Waislaamu Tanzania. Kwa sababu tulikuwanayo *East African Muslim Welfare Society* ambayo ilikuwa inasimamia maslahi ya Waislamu Afrika Mashariki na sisi huko nyuma tumeambiwa kuwa wapigania uhuru wa Tanganyika walikuwa tayari kuchelewesha kupatikana uhuru wa Tanganyika ili upatikanane uhuru wa Afrika Mashariki kwa pamoja. Sasa *East African Muslim Welfare Society* kikiwa chombo ambacho ni moja ya taasisi ambazo zingewaunganisha Wanajumuiya wa Afrika Mashariki kinavunjwa, sababu haielezwi. Hii imekuwa ni kawaida ya kuvunja vyombo hivi bila kuwapa wahusika sababu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kama hiyo haitoshi, hata kwenye Bunge, na uhai wa Bunge hili mimi nikiwa Mwislamu nafahamu. Kofia kama hii hapa ni vazi, kwa sehemu kubwa ni vazi la Kiislamu. Kuna wakati ilitolewa kauli Bungeni humu hii kofia isivaliwe. Sababu hazikutolewa. Halafu baadaye ikarudishwa na ikarudishwa na vile vile ili ihalalishe tuvae na kofia ya tarabushi. Sasa hii pengine ilitolewa kwanza ili baadaye upate uhalali wa kuidhinisha ile kofia ya taratibushi.

Mheshimiwa Spika, tunaambiwa Waislamu tuwe na subira. Ni kweli Waislamu kwa mujibu wa imani yetu tuna subira, na ni subira hiyo ndiyo iliyofanya hata tulinung'unika chini kwa chini kuhusu suala hili. Lakini pengine manung'uniko yaliwafikia wenye mamlaka ya kurudishwa wakaamua kurudishwa. Sasa viko vitu wanafanyiwa Waislamu kwa dhana ya kutegwa waonekane watafanya nini. Sasa nchi hii isiendeshwe kwa kutegeana.

Mheshimiwa Spika, liko suala la *OIC*. Mimi bahati nzuri nimekuwepo Bungeni tangu mwaka 1990 mpaka 2000. Wapiga kura mwaka 2000 wakaniambia sitoshi, nikapumzika. Wamenirudisha 2005. Lakini mwaka 1993 ilikuwepo hoja ya Tanganyika ambayo ilianzishwa na *G55* na niweke wazi kwamba Mheshimiwa Njelu Kasaka wakati ule aliorodhesha watu ambao alitaka kuwatia kwenye G.55 namba moja alikuwa ni Msambya na sababu yake ni kwamba umempa tabu kukwamisha bajeti ya Waziri Mkuu kuhusu soko la Kariakoo. Kwa hiyo, unaonekana wewe ni mtu unayefaa.

Nikawaambia mimi siwezi kukubali hoja ya Tanganyika kwa sababu ninakotoka ni Tanganyika. Sitaki kuwa na Tanganyika mbili. Kitu gani ninachotaka kusema hapa, wakati ule tuliambiwa Zanzibar kuijiunga na *OIC* ilikuwa ni makosa wamevunja Katiba. Mimi sitaki kwenda kwenye utekelezaji kwamba wamevunja au hawakuvunja. Wakaambiwa wasubiri ili utafutwe utaratibu wa kuingia kama Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Miaka 15 imepita na majuzi hapa tumepata jibu chungu bado kiko jikoni kinapikiwa kuni za mawe? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kujiunga na *OIC* kuna faida kwetu sisi kuliko watu wanavyodhani. Mheshimiwa Missanga amezungumzia suala la Ofisi ya Ubalozi wa Vatican hapa. Watu wanachanganya suala la Uislamu na masuala ya imani ya Kiislamu. Leo tunayo nchi ya Iraq. Iraq siyo nchi ya Kiislamu ni nchi ya Kiarabu. Iran siyo nchi ya Kiarabu ni nchi ya Kiislamu. Ndiyo! Wa-Iran ni Waajemi. (*Makofi*)

Sasa suala la *OIC* nchi kama Afrika Kusini ana-*observer status* tu. Nyinyi wote mnajua kwamba Afrika Kusini kwa idadi kubwa ukitoa watu wa Durban idadi kubwa siyo Waislamu. Nenda Uganda, Burkinafaso, Senegal, Gambia, hivi leo Marekani inafanya mpango ijiunge na *OIC* na hili ndiyo taifa kubwa kwa utajiri duniani. (*Makofi*)

Lakini Watanzania mpaka Kanisa likubali ndiyo Tanzania itajunga na *OIC*. Kwa nini? Ningeomba watu waelewe kwamba nchi hii ni yetu wote na wote tuna haki sawa. Sasa katika vite vitu ambavyo vitakuwa ni vya maslahi kwa Watanzania wote bila kujali imani zao. Kwa maana hiyo basi tuhakikishe tunatatua suala la Mahakama ya Kadhi kwa wakati. Tuhakikishe tunaweka utaratibu wa Tanzania ijiunge na *OIC* ili tufaidike kiuchumi. (*Makofi*)

Tukijiunga na *OIC* siyo wanaofaidika ni Waslamu, wanafaidika Watanzania. Lakini kumekuwa na dhana tu kwamba hii sijui wanataka kuifanya nchi kuwa ya Kiislamu. Nani alisema? Hivi kweli kama kwa takwimu tunazoambiwa ndiyo kweli, tuko *fifty fifty* halafu unafanya nchi hii kuwa ya Kiislamu inaanzia wapi.

Mheshimiwa Spika, rai yangu kwa Mheshimiwa Waziri, kwanza atakapokuwa anafanya majumuisho anijibu inakuwaje kauli aliyotoa kwenye vyombo vya habari jana kwamba hoja hii mpaka ikubaliwe na watu wa upande wa pili. Watu wa upande wa pili akina nani? Baada ya kueleza hayo, Mheshimiwa Spika, nakushukuru ahsante.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Msambya. Namwita sasa Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, atafuatiwa na Mheshimiwa Godfrey Zambi, wakati huo ajiandae Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU: Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyoko mbele yetu. Awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuwateua Majaji wengi wanawake. Hii inaonyesha kwamba anaonyesha mfano hai kwamba sisi wanawake tunaweza na kwa misingi hiyo naomba walioteuliwa katika nyadhifa tofauti hasa hao Majaji waonyeshe kwamba wanawake tunaweza kutoa haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wanawake tunaweza kutoa haki kwa sababu tangu tunapoanza kulea watoto, watoto wadogo wakianza kugombana, mara nydingi tunatoa amri pale pale. Kwa hiyo tunatoa haki tukianza kulea watoto wadogo hata akina baba.

Mheshimiwa Spika, naondoka hapo, nakwenda sasa kwenye hoja kamili. Kabla ya kuzungumzia mambo mengine ya kitaifa naomba nijikite kidogo kwenye Wilaya ya

Nzega. Mahakama na Mahakimu wa Wilaya ya Nzega ambao wa Wilaya na Mahakama ya Mwanzo.

Mheshimiwa Spika, pale Nzega ninapozungumza, nikizungumza Nzega ili wengine wanipate vizuri, Wilaya ya Nzega ina majimbo mawili Ina jimbo la Bukene ambalo naliwakilisha mimi na jimbo la Nzega analiwakilisha Mheshimiwa Selelii, ndio Wilaya ya Nzega. Sasa katika Wilaya ya Nzega tuna upungufu wa Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo, tunatakiwa tuwe na Mahakimu 12 wa Mahakama ya Mwanzo. Lakini kwa ujumla tuna Mahakimu watano. Maana yake tuna upungufu wa Mahakimu 7 na Mahakimu wa Wilaya tunao watatu, tunakiwa tuwe nao 8. Kwa hiyo tuna upungufu wa Mahakimu watano.

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo basi namwomba Waziri anapopeleka Mahakimu atukumbuke na sisi watu wa Nzega kutuletea Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo na Mahakimu wa Mahakama ya Wilaya ili tuweze kupata Mahakimu wa kutosha na hivyo kuhakikisha kesi zetu za kule Wilayani zinakwenda vizuri kwa sababu tuna watendaji wanaotenda haki wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie mishahara ya Mahakimu pamoja na nyumba na usafiri. Ukiangalia mishahara ya Mahakimu iko chini sana. Hawa Mahakimu wanafanya kazi kubwa, wanatoa hukumu hata wakati mwengine kwa pesa nyingi sana. Kwa mfano kunakuwa na kesi mtu anakuja pale, ya shilingi milioni 10. Lakini yeche anaotenda kuambiwa kwamba ukifanya hivi tutakupa milioni 1 kwa mfano. Yeye mshahara wake ni 300,000. (laki tatu). Kwa hiyo, anaingia kwenye ushawishi wa kwenda kwenye rushwa.

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo naomba Wizara ihakikishe ione umuhimu wa kupunguza rushwa kwa Mahakimu wetu. Iwapandishe katika kuwapa mshahara wa kutosha ili waweze kupata mahitaji yao na wasiingie katika hatari za kuingia kwenye rushwa. Iwape nyumba zinazostahili. Kwa sababu akienda kukaa kwenye nyumba za kawaida kule kule ndiko anakokutana na watu ambao maisha yake inaweza kuwa matatizo. Leo anahukumu hapa huyu mtu afungwe miaka 10, kesho anakwenda kukaa nyumba moja na ndugu au yule yule aliyemhukumu. Inakuwa siyo sahihi. Maisha yake yanakuwa hatarini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba Wizara ihakikishe kwamba inawapa nyumba Mahakimu wetu na ulinzi wa kutosha ili waweze kuwa na uhakika na maisha yao na familia zao na hivyo vichwa vyao vitulie ili waweze kufanya haki kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, gari vile vile ni muhimu katika usafiri kwa sababu kama walivyotangulia wenzangu wamesema kwamba Hakimu anatoka anakwenda kuingia kwenye daladala. Mle mle ndani ya daladala anakutana na ndugu au rafiki wa wale alio wahukumu. Kwa kweli inakuwa ni matatizo, anaingia katika hatari au pengine anaambiwa tutakutafutia gari, tutakukodi, tutakukodishia gari au tutakupa nini. Kwa hiyo anaingia kwenye mtego wa rushwa.

Mheshimiwa Spika, najua pesa ni chache na mgao ni mwangi. Lakini tuangalie umuhimu wa haki. Ukiangalia haki pale unatakiwa lazima uangalia, unamwangalia huyu Hakimu ili asiingie kwenye matatizo ya kuingia kuomba rushwa au kupewa rushwa hata ikiwa kidogo. Hapo nimemaliza.

Mheshimiwa Spika, naomba niingie katika upungufu wa Maofisi. Pale Nzega Wilayani hatuna Ofisi. Tuna Mahakama yetu ya Wilaya iko katika jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya. Kiutaratibu mimi nafikiri si sahihi. Hawa wanatakiwa wawe na mahali pao binafsi na *private*. Wasiingiliwe na Serikali, wasiingiliwe na nini. Ni Taasisi peke yake katika mafiga matatu, Mahakama ipo peke yake. Serikali ipo peke yake na Bunge lipo peke yake. Kwa hiyo, naomba wapewe Ofisi yao ili wawze kujitegemea, wafanye mambo yao kivyo vyao bila kuangalia ya kwamba wanaingiliwa au wanasumbuliwa na kutegwa tegwa katika kuingia mitego mingine ili watoe haki yao inavyopaswa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba na mimi nizungumzie kuhusu Mahakama ya Kadhi. Kwa kweli ukitazama Mahakama ya Kadhi haraka haraka unafikiria kwamba labda tunakwenda kujigawa kwenye dini. Inaonekana Wakristo wanapata sijui upendeleo zaidi. Waislamu wameonewa. Lakini kwa kweli ukitulia vizuri na naomba Mungu atuongoze sisi wote atupe busara na hekima tuone hilo jambo.

Mheshimiwa Spika, dini zote zinapeleka Katiba kwenye nchi na Katiba ile unasema unataka uwe namna gani katika kuendesha shughuli zao. Katika katiba zile za dini unakuta watu wamesema wanataka kufanya seminari. Seminari ni pale unapowafundisha watu wale ambao watakusaidia wewe kuendeleza dini yako katika hali ya imani ya kwako unavyoona.

Mheshimiwa Spika, huu mwili unavaa roho na yule mtu wa dini anaangalia roho zaidi kuliko mwili huu. Lakini tunapokwenda kwenye seminari ndiyo huko, kila mtu anafundishwa vitu vyake na hapa kwenye katiba huko huko mimi nafikiri na Mahakama ingeenda huko huko kwenye Katiba za dini na siyo katiba ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu Serikali yetu haina dini. Sisi wafuasi wake tuna dini. Lakini bado kuna wafuasi wengine hawana dini. Kwa mfano kule kwetu kwenye jimbo langu mimi kuna wapagani na nikiwaamkia huwa naanza na kuamkia Asalamalekum nikiwaheshimu Waislamu. Kwa sababu ni salamu yao. Halafu nakuja kwenye Wakristo, Tumsifu Yesu Kristu au Bwana Asifiwe nawaheshimu Wakristo. Nakuja kwa Kinyamwezi, *Lekube Lenyangasa*. (*Makofi*)

Lile ni li-Mungu linaogopwa na yule mwenyewe ambaye analijua analiamini anajua nimemheshimu katika imani. Kwa hiyo tusichanganye naomba tusichanganye imani na utaratibu wa katiba na Sheria ya nchi. Serikali yetu tuiache haina dini, sisi ni wafuasi wa dini tunazozitaka na sisi tutafuata Sheria za dini zinazotuambia.

Mheshimiwa Spika, Wakristo wanasema mke mmoja. Lakini Wakristo hao wanaoa wake wengi na sheria ipo, mke mmoja. Lakini wanawake wengi. Waislamu wanasema wanaoa wake wanne. Lakini bado wanaoa wake wengi zaidi ya wanne. Kwa hiyo, Sheria ipo pale kumwangalia mtu kwa imani yake sio mwili huu. Roho ndani yako, wewe unataka kufuata dini unaangalia maisha yako ya baadaye baada ya huu mwili kwishatoka, roho yako katika ulimwengu wa roho. Lakini ukianza kuzungumzia Mwislamu azungumzie alete Mahakama ya Kadhi, Mkristo naye atasema, ambapo Wakristo kwa mfano Wakatoliki wana utaratibu wao katika masuala yao ambayo wala haihitaji kujulikana kwa Waislamu wala kwa mpagani, haina ulazima. (*Makofî*)

Kwa hiyo na Waislamu, mimi ningewaomba ndugu zangu mkae muweke katiba ile muongeze kwamba sisi kwenye katiba yetu tukikwama hapa tunakwenda hivi tunasuluhishwa hivi, kama Wakristo wanavyofanya. Mfano hai, Wakatoliki, hilo naweza kuzungumzia kwa uhakika kwa sababu ninajua ninachozungumza. Nimekuwa kiongozi wa Kanisa Katoliki mpaka kwenye Taifa kabla sijaingia kwenye siasa. Kwa hiyo najua.

Mapadre wale unaweza ukasema tunasuluhisha ndoa wakati hawajaoa. Lakini hawasuluhishi kwa sababu hawaja-*experience* (hawana ujuzi). Wamesomea, wanajua utaratibu kwamba kwa nini unakwenda kuanguka hivi, kufuatana na utaratibu waliojipangia wao na imani yao. Kwa hiyo na Waislamu wangejipangia kwenye Kanuni ya dini kwamba tunasuluhisha hivi kutokana na hivi.

Mheshimiwa Spika, mimi sidhani kwamba tunaendelea. Tuna haja ya kupigiana kelele, Katiba ya nchi haina dini. Nakua kwenye haki za binadamu. Uhuru wako unaishia unapoanza wa mwenzio na sasa hivi dunia nzima inazungumzia haki ya mwanamke. Mwanamke siyo lazima awe Mwislamu au Mkristo ni mwanamke na haki yake.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba Wizara ya Sheria na Katiba ituletee upesi Sheria ya Mirathi, mtuletee upesi Sheria ya Ndoa ili tuweze kuweka kwa wale ambao hawataki kwenda kwenye Kanisa la Roma, hawataki kwenda kwenye Kanisa lingine. Hawataki kwenda kwenye Uislamu, watusaidie kwenda kwenye sheria ya nchi.

Mheshimiwa Spika, huwa sipendi kusema mfano wangu mara nyingi. Lakini inabidi niseme. Mimi mwenyewe nimefunga ndoa ya *DC*. Niko Mkatoliki. Lakini nilifunga ndoa ya *DC*. Lakini kwa sababu sikuweza kupata mwanaume Mkatoliki mwenzangu. Kwa hiyo nikawa nimefutwa kwenye Ukatoliki, wakaniweka upande, siwezi kushiriki katika Meza ya Bwana na mwenzangu na yeye Mwislamu naye akawekwa upande, sikuweza kumpikia futari wakati wa mwezi wa Ramadhani. Yale yalikuwa ni mapenzi yetu sisi na wako wengi wa namna hiyo. Lakini nimekuja kukaa nikatazama nikaangalia hapa duniani ninachohangaikia ni nini? Hili ni mwili tu. Ninachohangaikia ni roho ulimwengu wa roho ndiyo unatakiwa kuuangalia siyo ulimwengu wa mwili huu, kama sisi wote tunaamini kwamba kuna ulimwengu wa roho, kama sisi wote tunahangaikia roho hizo zifike mbinguni kwa hiyo lazima tuangalie. Kila mtu anakwenda kwa staili yake.

Mimi nikaona sina sababu ya kukaa kwenye ndoa na Mwislamu. Nikaona nina mzigo, nikaondoka. Nikaondoka....

SPIKA: Ulipigwa talaka nadhani. (*Kicheko*)

MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU: Sijapigwa, sikupigwa talaka kwa sababu haikuwa ya Kiislamu. Ilikuwa ya DC. Kwa hiyo wale ambao watakwenda mahali apate Muislamu mwinzie au hakubaliani masuala ya Kiislamu anaweza kuwa Muislamu lakini hakubaliani na masuala ya Kiislamu. Kwa hiyo arudi hapa kwenye Serikali.

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea Waheshimiwa. Namwita Mheshimiwa Godfrey Zambi, ajiandae Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja ambayo ipo mbele yetu, hoja ambayo aliiwasilisha Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mathias Chikawe.

Mheshimiwa Spika, lakini pia na mimi kama ilivyo ada naomba nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Chikawe kwa kuwasilisha vizuri sana hoja yake mbele ya Bunge lako Tukufu. Hongera sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, nina mambo machache ya kuchangia na mimi nadhani nitachangia mawili tu. Moja linahusu masuala ya jimbo langu. La pili na naomba tu na mimi niseme ni-*declare interest* kwamba mimi ni Mkristo na kwa sababu suala hili la Mahakama ya Kadhi limenigusa basi na mimi nitalichangia kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri anisaidie kule jimboni kwangu au Wilaya ya Mbozi kwa ujumla tuna upungufu mkubwa sana wa Mahakimu. Lakini pia Mahakama zetu za Mwanzo nydingi sana zimechakaa. Wilaya ya Mbozi ina eneo la takriban kilometra 9,000. Tuna vijiji 175 na Kata 26. Tuna Mahakimu wa Mwanzo katika eneo hilo la ukubwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo chini ya 10. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Waziri na tunajua jitihada anazozifanya atusaidie sana kutuungezea Mahakimu kwa sababu na kama walivyosema wenzangu katika maeneo mbalimbali. Mahakimu hawa wa Mahakama za Mwanzo wanafanya kazi ngumu sana na kwa kweli wakati mwengine kwa sababu ya ugumu wa maeneo zinawapa hata vishawishi vyatupokea rushwa.

Sasa tunaomba tusiwatumbukize Mahakimu wetu katika mambo ambayo wao wenyewe wasingependa kuyafanya. Lakini wanalazimishwa kwa sababu ya mazingira.

Lakini pia nimwombe Mheshimiwa Waziri, atusaidie nilisikia jana kwenye hotuba yake imeandikwa kwamba ana pikipiki karibu 100 na hizi zitasambazwa kwenye Mahakama za Mwanzo, usiisahau Mbozi katika hili Mheshimiwa Waziri. Pengine utakapokuwa unajibu basi wale Mahakimu wa Mbozi na wenyewe wasikie kwamba walau wanapelekewa pikipiki, au tatu ili walau tuweze kupunguza ile ada wanayoipata katika masuala ya usafiri.

Lakini pia Mahakama zetu ni chakavu sana. Naomba katika kukarabati Mahakama zinazoendelea nchini, sijaona kama Mbozi iko kwenye wowote wa ukarabati Mahakama za Mwanzo ambazo nyingi ni chakavu, basi naomba pia utufikirie katika ukarabati wa Mahakama zetu ambazo kama nilivyosema kwa kweli nyingi ni chakavu sana. Nyingi sakafu ni vumbi.

Kwa hiyo, Mahakimu wanafanya kazi katika mazingira magumu. Lakini pia na vitendea kazi vingine kwa mfano makaratasi ni shida. Tunaomba na hili pia utuangalie kama zinavyotazamwa Mahakama nyingine nchini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo ninaomba nichangie hoja ya Mahakama ya Kadhi.

Baada ya kusema Mheshimiwa Mwakyembe, kaka yangu, Mtaalam wa Katiba na Sheria pengine inakuwa vigumu sana wengine kuweza kupata maneno mazuri sana ya kuchangia katika hili.

Mimi naomba Mwenye Mungu anisaidie nizungumzie haya ambayo nataka kuzungumza. Moja nimewasikiliza wazungumzaji wengi wakichangia hoja hii na hususan wa upande mwingine wale ambao wanataka hoja ya Mahakama ya Kadhi ije leo au kesho. Sijui kama ingewezekana kuja jana, lakini wale ambao wanasema ije leo au kesho.

Mheshimiwa Spika, wengi, wametumia Ilani ya Uchaguzi ya CCM, wanasema suala hili imeahidiwa humu na mimi nakubaliana nao kwamba iko kwenye Ilani hii, ukurasa wa 132 na kifungu cha (b) ambacho kinasema:-

“Kulipatia ufumbuzi suala la kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi Tanzania Bara”.

Mheshimiwa Spika, nakubali imezungumzwa lakini ninaomba niwaambie hawa Wabunge wenzangu kwamba hizi ni ahadi ambazo Serikali ya Chama cha Mapinduzi ilizitoa kwa Watanzania, ni ahadi. Sasa ahadi unaweza ukaitekeleza katika kipindi hicho au ukashindwa kuitekeleza kwa sababu ya mazingira ya wakati huo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba wenzetu waelewe kwamba inawezekana kwa sasa mazingira haya bado hayajafika. Hii ni ahadi wala sio sheria hii, ni ahadi iliyotolewa na Chama changu lakini ni lazima tuangalie mazingira ya upande mwingine.

Mheshimiwa Spika, Serikali ambayo iko madarakani na Serikali zote zilizopita, zinaongoza Watanzania wote, hazonozi Waislamu peke yao, hazonozi Wahindi peke yao, wala hazonozi Wabahai peke yao, inaongoza Watanzania wote. Kwa hiyo, ni lazima Serikali hii iwe makini sana kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipokuwa anajibu maswali yanayofanana na haya lakini pia hata Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria kwamba hili suala ni lazima lifanywe kwa umakini. Wenzetu wasisukumwe tu kwamba ni lazima Mahakama ya Kadhi ije leo, hapana! Kwa kufanya hivyo, mimi nadhani pia hawa wenzangu watakuwa wanavunjua hata Katiba yenye kwa nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tulipochaguliwa kuwa Wabunge, tuliapa Kiapo cha Utii na sehemu ya Kiapo hicho cha Utii iko kwenye Kanuni zetu, ukurasa wa nane. Sehemu ya Kiapo cha Utii, kwa ruhusa yako, naomba ninukuu, inasema kwamba:-

“Nitaihifadhi, nitailinda na kuitetea Katiba ya Tanzania kwa mujibu wa Sheria iliyowekwa.”

Mheshimiwa Spika, sasa Katiba yetu tuliyojiwekea ni hii, tunapaswa tuilinde na kuiheshimu hii Katiba.

Mheshimiwa Spika, sasa wenzangu hawa wanasoma Katiba hii, kama alivyosema Mheshimiwa Msambya, ye ye mwenyewe nadhani anaongoza, anasoma kifungu kimoja lakini kifungu kingine anakiacha, hataki kukisoma katika Katiba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nisome kifungu hicho, kwanza, Ibara ya 19, kwa ruhusa yako naomba mimi nisome vifungu vyote ingawa wenzangu wameshvireja. Ibara ya 19(1) inasema:-

“Kila mtu anastahili kuwa na uhuru wa mawazo, imani na uchaguzi katika mambo ya dini, pamoja na uhuru wa mtu kubadilisha dini au imani yake.”

Lakini kifungu kidogo cha (2) kinasema:-

“Kazi ya kutangaza dini, kufanya ibada na kueneza dini itakuwa ni huru na jambo la hiari la mtu binafsi, na shughuli na uendeshaji wa jumuiya ya dini zitakuwa nje ya shughuli za mamlaka ya nchi.” (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tafsiri ya sehemu hii ya Katiba, haihitaji mtu kusoma Sheria, haihitaji mtu kuwa Mwanasheria ndio ajue tafsiri yake! Maana yake ni kwamba masuala ambayo wenzangu wamesema Dini ya Kiislamu inafanya, masuala ya talaka, masuala ya ndoa, sijui masuala ya Wakfu, ni mambo ya dini haya na Katiba imesema katika Kifungu

cha pili, ni mambo ya dini. Sasa, wasiilazimishe Serikali kwamba lazima iingie tu hata kama haijafanya tafakari ya makini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia ninaomba niwarejeshe wenzangu kwenye Katiba hiyo hiyo, Ibara ya 13 ya Katiba, ninaomba kwa ruhusa yako ni *quote* Ibara ndogo (2) na ya (5). Ibara ya 13(2) inasema:-

“Ni marufuku kwa sheria yoyote iliyotungwa na mamlaka yoyote katika Jamhuri ya Muungano kuweka sharti lolote ambalo ni la ubaguzi ama wa dhahiri au kwa taathira yake.”

Sasa Ibara ya 13(5) ambayo inatoa tafsiri ya ubaguzi inasema hivi:-

“Kwa madhumuni ya ufanuzi wa masharti ya ibara hii neno “kubagua” maana yake ni kutimiza haja, haki au mahitaji mengineyo kwa watu mbalimbali kwa kuzingatia utaifa wao, kabilia, pahala walipotokea, maoni ya kisiasa, rangi, dini, jinsia au hali ya maisha kwa namna ambayo watu wa aina fulani wanafanya au kuhesabiwa kuwa dhaifu au duni na kuwekewa vikwazo au masharti ya vipingamizi ambapo watu wa aina nyingine wanatendewa tofauti au wanapewa fursa au faida iliyoko nje ya masharti au sifa za lazima...” naomba niishie hapo.

Mheshimiwa Spika, maana ya maneno haya imetolewa na neno dini hapa limezungumzwa, kama tukiwalazimisha kwamba lazima Wakristo na wenyewe wakubali Mahakama hii kuwepo maana yake tutakuwa tunaanzisha Mahakama ambayo ni ya kibaguzi ambayo itakuwa inahudumia sehemu moja tu ya jamii. Hii itakuwa ni Mahakama ya kibaguzi kwa mujibu wa sheria hii. Sasa kama Wanasheria wana tafsiri tofauti na hizi, basi watupeleke shule tukasome, maana yake mimi sioni ugumu kwamba hivi vifungu ni vigumu sana kuvielewa, mimi sioni kabisa.

Mheshimiwa Spika, kama wenzetu wanafikiri ni lazima tuanzishe Mahakama ya Kadhi basi siku moja Wakristo watadai waanzishiwe Mahakama yao, hatutakuwa na sababu ya kukataa kwa sababu tutakuwa tume-set *precedent* hapa. Lakini pia Wahindu watakuja, wapo Tanzania watasema wanataka Mahakama yao, tutakuwa tume-set *precedent*, Wabahai wapo na wenyewe watataka Mahakama yao, tutakuwa tume-set *precedent*. Katiba yetu ambayo tumeapa kuilinda ni lazima tuiheshimu. Mimi nilifikiri kama wenzetu hawa wanataka Mahakama ya Kadhi basi waje na hoja kwanza ya kubadilisha Katiba hii, lakini wakati Katiba hii hatujaibadilisha, kuendelea kung’ang’ania Mahakama ya Kadhi ni kuidharau Katiba hii ambayo sisi Wabunge tulipa kuilinda tulipokuwa tunaapishwa kuwa Wabunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, watu wamezungumza hapa kwamba kama Mahakama hii ya Kadhi haitaanizishwa maana yake watu wanaweza wakakosa uvumilivu, lakini ni lazima waangalie na sehemu nyingine ya Watanzania na wenyewe pia wanaweza wakakosa uvumilivu, kwa sababu tusizungumzie tu upande mmoja. Pesa zitakazotumika kuendesha Mahakama hii kama itaanizishwa ni za Watanzania wote, lazima wenzetu wajue hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi sidhani kama Mahakama ya Kadhi, ni muhimu sana kuliko kujenga zahanati huko vijijini na sioni kama Mahakama ya Kadhi, kwa Watanzania leo ni muhimu sana kuliko kujenga barabara huko vijijini kwa ajili ya kupidisha mazao yetu. Serikali inakosa pesa kwa ajili ya kuwahudumia Watanzania wote, wenzetu wanataka walazimishe Mahakama ya Kadhi ili Serikali ipeleke pesa za Watanzania wote kwa ajili ya kutatua masuala ya talaka, masuala ya ndoa, masuala ya wakfu na masuala kama hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waislamu hawajazuiliwa kuendesha mambo yao, kama wanataka, wanaweza wakaanzisha utaratibu wao! Wenzangu wamesema hapa, Wakatoliki wana utaratibu wao ndani ya Kanisa lao, Waislamu waanzishe utaratibu wao ndani ya nchi hii, wanaruhusiwa, wako huru, lakini wasiilazimishe Serikali kuendesha suala hili! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimuombe sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri wa Sheria, anasoma haya yanayoendeshwa hapa, kama mkikubali jambo hili lije wakati haya mambo hayajawa makini pamoja na kwamba liko kwenye Ilani kabla halijafanyiwa uchunguzi na tathmini sahihi, mnaweza mkaiweka nchi hii katika wakati mgumu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Waislamu wanapozungumza hivi, ni lazima mjue kwamba kuna watu wengine na sio Wakristo tu, amesema mama Kasela Bantu pale, wako na wapagani pia. Kwa hiyo, naomba tusiingize mambo ya dini fulani likawa ni suala la kitaifa ingawa mimi sina shaka kwamba hili haliwezekani kwa sababu kwa vyovyyote vile ni lazima tuiheshimu Katiba hii na kufanya vinginevyo maana yake ni kwamba tunaivunja Katiba hii na kama nilivyosema, tulipa wote kuilinda na wote watakaokuwa wanazungumza vinginevyo maana yake wanaidharau Katiba hii ambayo wao wenyewe waliapa kuilinda na sitegemei kama kuna Mbunge wa namna hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, watu wanaozungumza kwamba Waislamu watakosa uvumilivu, mtu mmoja alisema kwenye kitabu hiki ambacho Kambi ya Upinzani walileta, wanasema kwamba watu watakosa uvumilivu humu. Wanasema kwamba watu walitembea Tanzania eti kupiga kampeni watu wa *CCM* kwa kuuza neno hili kwamba watarudisha Mahakama ya Kadhi. Mimi kwangu kule Mbozi, Mahakama ya Kadhi, kwanza sio *issue*, Waislamu ndio wapo, lakini walio wengi, zaidi ya 99% ni Wakristo. Kwa hiyo, mkisema kwamba tulipata kura kwa sababu tu Serikali iliahidi kurudisha Mahakama ya Kadhi, tutakuwa pia hatuwatendei haki Watanzania wengine hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, naomba tuzungumzie vitu ambavyo vinawagusa Watanzania wote lakini tukianza leo kimoja kimoja, ninaogopa na ninahofia tutakuwa tunaligeuza Bunge hili sasa kuwa uwanja wa mapambano. Sisi ni Watanzania, mambo haya kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, hebu tuiachie nafasi Serikali ifanye kazi yake na mimi nina hakika hawa wenzetu wa *Law Reform* kama ndio wanafanya kazi hii au Serikali, itatolea maamuzi, nina hakika watafanya maamuzi kwa kuzingatia maslahi ya

Watanzania wote hasa tukizingatia kwamba chombo hiki kitakapoanzishwa kitaendeshwa kwa fedha za Watanzania wote wanaolipa kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi kwa kweli nilitaka tu niyaseme hayo, nikiunga mkono hoja ya Waziri kama alivyoiwasilisha lakini nikitumaini haya mambo hasa hii ya Mahakama ya Kadhi itafanywa kwa uangalifu bila kuathiri upande mwingine. Lakini pia niwaombe wenzangu wasiilazimishe Serikali kuleta Mahakama ya Kadhi hata kama taratibu nyingine bado hazijakamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niseme kwamba naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia kidogo kwenye hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa kazi kubwa anayoifanya kwenye Wizara hii pamoja na wataalamu wake wote, kwa kuandaa hotuba hii na pia kutuletea hapa.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kusema kwamba kuna tatizo kubwa sana la kesi za wananchi kukaa Mahakamani kwa muda mrefu bila kusikilizwa. Hili ni tatizo sugu, Serikali inafahamu na Wabunge wote waliozungumza hapa hakuna ambaye hana tatizo hilo kwenye eneo lake analofanya kazi. Wananchi wameendelea kuteseka kwa muda mrefu, wanatumia gharama kubwa kuhudhuria Mahakamani kila leo wakifutilia kesi zao, wakifutilia haki zao, lakini wameshindwa kuzipata kutokana na kuwepo kwa Mahakimu wachache sana wa kusikiliza kesi za wananchi wetu. Kwenye masuala ya ardhi kesi zinazohusu ardhi hapa Tanzania ndio kabisa ni tatizo kubwa. Ninadhani kama sijakosea wapo Mahakimu wachache sana, sijui kama wanazidi watatu au wanne kwenye masuala ya ardhi. Imekuwa ni tatizo kubwa, wananchi wanafutilia kesi mpaka miaka minne, mitano bila kusikilizwa, kisa kwamba hakuna Hakimu wa kusikiliza kesi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwenye juhudzi za Serikali katika kuhakikisha kwamba tunakuwa na Mahakimu wa kutosha, wahakikishe pia Mahakimu wa masuala ya ardhi wanakuwepo. Nina kesi ambayo ni ya mfano kwa upande wa Wilaya ya Urambo, wananchi wamefutilia kesi yao tangu mwaka 2003 mpaka leo haijawahi kusikilizwa na mbaya zaidi wanapigwa tarehe. Kila wakihudhuria kesi Mahakamani, Hakimu hayupo, ukizingatia kutoka Urambo mpaka kwenda Tabora inabidi walale kule, kwa hiyo, wanatumia gharama za kulala, gharama za kula, gharama nyingine wanazotumia pale mjini lakini pia kwa muda wa miaka yote hiyo hawajasikilizwa. Hili ni tatizo, naomba sana Serikali ihakikishe kwamba wananchi hawa wanapatiwa haki zao kwa sababu imekuwa ni tatizo na wameendelea kukata tamaa kwa kweli. Kwa nchi inayoongozwa kwa Katiba na Sheria kama nchi yetu, mwananchi kukaa miaka minne au mitano anafutilia haki yake bila kuipata, inakatisha tamaa sana.

Mheshimiwa Spika, kuna vitendo vya kusikitisha sana vya unyanyasaji na ukatili wa watoto vinavyoongezeka kila kukicha badala ya kupungua. Sheria zinazolinda watoto wetu hapa Tanzania, niseme tu kwamba zina upungufu mkubwa, tunachotakiwa kufanya ni Serikali kuchukua jukumu la dhati tena la haraka kuhakikisha kwamba Sheria hizi zinabadilishwa.

Mheshimiwa Spika, nina wasiwasi sana pia na hatua za kisheria zinazochukuliwa kwa wale akina baba, wanaume ambao wameshindwa kutumia haki yao ya msingi wanafanya vitendo vya unyama kwa watoto wetu. Ninashindwa kuelewa kabisa, kwanza Tanzania hii wanawake ni wengi sana, kwa sensa iliyopo ni kwamba wanawake tuko wengi zaidi hata ya wanaume, inakuwaje akina baba hawa wanashindwa kwenda kwa wasichana, akina mama wapo wakaenda kwa watoto wetu? Pia kinachosikitisha zaidi ni kwamba sasa hivi wanawabaka watoto hao na wanawauwa ili kuuwa ushahidi, ninadhani adhabu inayochukuliwa haitoshelezi kosa linalofanyika.

Mheshimiwa Spika, mimi nimewahi kutoa pendekeso hapa kwamba ikiwa mtu amepewa haki ya msingi na ameshindwa kutumia haki yake ya msingi, tumnyang'anye hiyo haki ya msingi. Kwa hiyo, ikiwezekana hata tuwa-*castrate* watu hawa kwa sababu wameshindwa kutumia haki yao ya msingi. Ni kwa nini tuendelee kuwanyamazia wakati watoto wetu wanakufa, watoto wetu wananyanyasika, kwa kweli inasikitisha. Kila ukipitia kwenye gazeti, hata leo ukinunua magazeti kati ya magazeti yote, ni lazima utakuta kesi ya mtoto aliyebakwa, mtoto aliyefanywa hivi, mtoto aliyelawitiwa, kwa nini vitendo hivi vinaendelea? Tukae tuijulize ni kwa nini pamoja na kwamba tuna sheria? Inaelekea kwamba adhabu tunayotoa haitoshelezi kwa hiyo haitoi funzo kwa akina baba, haitoi funzo kwa wanaume ambao wameshindwa kutumia haki yao ya msingi.

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye suala la mfumo wa vyama vingi hapa nchini. Nadhani suala la kuwepo kwa Vyama vya Siasa, ni suala la Kikatiba na Kisheria. Mwananchi wa Tanzania ana haki ya kuijunga na chama chochote anachopenda ili mradi asivunje sheria, hilo ni suala la Kikatiba. Lakini inasikitisha kuona kwamba kuna baadhi ya viongozi tena wa Serikali walipewa dhamana ya kusimamia wananchi, wanatumia nafasi zao kwa ajili ya kuwanyanyasa wananchi ambao wapo vyama vya upinzani, inasikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, kuna mifano hai ya kudhihirisha hili ninalolisema lakini hata Serikali inafahamu, viongozi hawa wamekuwa wanachukulia Vyama vya Upinzani kama ni watu wakorofi. Likitokea tatizo lolote kwenye kijiji chochote au kwenye Kata, kwanza wanawa-focus wale wa Vyama vya Upinzani kwamba hawa ndio wakorofi, ndio walioleta tatizo hili. Wapo ambao wamefungwa, wamebambikiwa kesi za ajabu ajabu, mpaka kesi za uhaini, wapo ambao wamefungwa wako Magerezani wanatumikia kesi ambazo ni kinyume na haki, ambazo hawana hatia. Hili ni suala ambalo linasikitisha sana. Ninaombwa Serikali itoe mwongozo na itoe tamko kwa viongozi wote wa Serikali kwamba uwepo wa Vyama vya Upinzani, ni suala la Kikatiba. Kwa hiyo, mwananchi ye yote apewe haki anayostahili kama Mtanzania na sio kama mwananchi wa chama fulani.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wetu wa Urambo Magharibi, kuna viongozi wa Kata, viongozi wa Vijiji, ambao wamewahi kuwanyima hata wananchi kile chakula cha msaada yaani yale mahindi yaliyokuwa yanagawanywa mwaka jana, wanaambiwa kwamba hiki ni chakula cha *CCM* subirini chakula cha *CUF*, tutafika kwa namna hiyo? Imefikia hatua mpaka huduma za kijamii wanatoa kwa upendeleo, kisa ni Vyama vyta Upinzani. Sasa hapo ninapata wasiwasni kwamba ikiwa ni mfumo ulikubalika ndani ya nchi iweje basi kiongozi aliyepewa dhamana atumie nafasi yake kumnyanya sasa mwananchi huyu? Kwa hiyo, wananchi wanakaa kwenye nchi yao bila amani, bila uhuru wakati ni suala la Kikatiba. Ninaomba Mheshimiwa Waziri leo atoe tamko kwamba ni nini kifanyike ili kuhakikisha kwamba haki inatendeka kwa wananchi wote bila kujali itikadi za vyama. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la ukiukwaji wa Katiba na uvunjwaji wa sheria, ni masuala ambayo yanatokea maeneo mengi sana hapa nchini. Mbaya zaidi haya yanafanywa na viongozi waliopewa dhamana katika maeneo mengi. Kuna tukio moja ambalo ni la kusikitisha, ninaomba niliseme wazi na Mheshimiwa Waziri alifanyie kazi na atupe majibu hapa Bungeni. Kuna tukio la kusikitisha sana limetokea kwenye kijiji cha Kisingiri, Kata ya Ilola, Jimbo la Solwa, Wilaya ya Shinyanga Vijiji, ambapo kuna wananchi wa kijiji wametengwa kwa muda karibia wa miezi mitatu sasa kisa wamehoji kwenye mkutano wa hadhara mapato na matumizi ya kijiji. Suala la kuwepo mikutano ndani ya kijiji, ni suala la Kikatiba, tunafahamu ndani ya mwaka mmoja ni lazima vifanyike vikao vinne vyta kijiji kuhakikisha kwamba wananchi wanapewa taarifa zinazoendelea kuhusu maendeleo yao.

Lakini pale ambapo viongozi wanaacha kutimiza hayo na wananchi wakija kuhoji wanaonekana kwamba wamekiuka taratibu matokeo yake wanawekwa kwenye hali ngumu. Kwa hiyo, wapo wananchi wametengwa kuanzia mwezi wa tano kwenye kikao kilichofanyika tarehe 20/05/2008 kilichoitishwa na Diwani, pamoja na viongozi wa vijiji wakiwepo na Sungusungu, walipojitokeza wananchi kuhoji kwamba tunaomba tujue mapato na matumizi kwa miaka miwili iliyopita, wakaonekana kwamba ni wakorofi. Kwa hiyo, viongozi wakakasirika, wakaanza kuwaandika majina wale ambao walikuwa wanashabikia kupata taarifa hizo wakaorodheshwa majina yao wote na likatoka tamko kwamba watu hawa watengwe na huduma zozote na wasiende nje ya kijiji mpaka viongozi watakaporidhia suala hilo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, wananchi hao wameendelea kuteseka kwa muda mrefu. Wakifiwa wanazika wenye, wakitaka huduma nje ya kijiji wananyimwa kwenda, tatizo lolote litakalowapata wakae palepale na kutotoka kijiji hicho wamebekwa Sungusungu ndio wanaofanya hiyo kazi, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba hakuna mwananchi wa kijiji cha jirani anayeingia kuja kutoa huduma yoyote ya msingi ndani ya kijiji hicho.

Mheshimiwa Spika, mbaya zaidi ili watolewe vizuizini, viongozi hawa wa kijiji hiki wametoa masharti kwamba ikiwa mnataka tuwafungue kutoka kizuizini ni lazima mtoe ng'ombe 10 au mbuzi 100. Wananchi hawa baada ya kukaa kwa muda mrefu wakaona kuwa wanateseka wakaamua kutoa mbuzi 100, kwa hivyo, wale waliota mbuzi

100 wakaachiwa wapate huduma wanapoweza kuzipata lakini wapo wengine mpaka sasa hivi wameshindwa kutoa hao mbuzi 100 na ng'ombe wameshindwa, wameendelea kutengwa. Walivyogawana hao mbuzi 100, wamegawana wale viongozi wa vijiji pamoja na Sungusungu kwa sababu ndio wanaofanya hiyo kazi.

Mheshimiwa Spika, nchi hii inaendeshwa Kikatiba na Kisheria, masuala haya yapo na hili ni moja tu kati ya ambayo tumeweza kuya-*identify*. Mimi nadhani kabisa yapo mengine mengi ila wananchi hawana mtu wa kuwasemea. Tunaomba Mheshimiwa Waziri, achukue hatua kwa kijiji hiki na viongozi wake wote na iwe ni mfano kwa vijiji vingine. Mwananchi asinyanyasike kisa kwa sababu kadai haki yake ya msingi, ni haki ya msingi ya Kikatiba mwananchi kujua mapato na matumizi ya fedha za kijiji chao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo sauti yangu sio nzuri sana kwa sababu ya kifua, naomba niseme haya machache. Nakushukuru sana, ahsante. (*Makofi*)

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri ambayo ameileta hapa Bungeni na pia nimpongeze Jaji Mkuu, kwa kazi nzuri ambayo anaifanya. Nikipongeze Chama cha Mawakili, *Tanganyika Law Society*, kwa kufanya kazi nzuri na pia nichukue nafasi hii kuwapongeza watendaji wa Mahakama ya Wilaya ya Karagwe, kuanzia Wilayani na mpaka Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, kwa kazi nzuri wanayoifanya Wilayani kwangu na Jimboni kwangu Karagwe.

Mheshimiwa Spika, nataka kwa leo nizungumzie matatizo mbalimbali ambayo yanaikumba Wizara hii. Tatizo la kwanza ambalo Wizara hii inalipata, ni ufinyu wa bajeti. Kila mwaka tumekuwa tikitenga bajeti ndogo sana kwa Wizara hii na yote yanayozungumzwa humu utakuta karibu 90% yanazunguka kutokana na ufinyu wa bajeti. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba kwa Bunge lijalo au bajeti zijazo, ninaomba Wizara hii iangaliwe kwa umakini sana bajeti yao iweze kuendana na hali halisi, vinginevyo bajeti ya Wizara hii ambayo tunaipitisha leo ni bajeti ya kuwasaidia tu kumudu mambo madogo madogo sio mambo ya msingi ambayo yanaweza yakafanyika.

Mheshimiwa Spika, mengi yamezungumzwa kuhusiana na uchakavu wa majengo. Wilayani kwangu Karagwe, majengo ya Mahakama za Mwanzo, ni mabovu lakini pia tunahitaji majengo mengine mapya kwa sababu idadi ya wananchi imeongezeka.

Mheshimiwa Spika, pia nizungumzie jengo la Mwanasheria Mkuu wa Serikali, *Attorney General Chambers*, ambalo liko pale Kivukoni. Lile jengo nadhani lilijengwa na Mkoloni na ni la siku nyingi sana. Wakati ule nadhani Mawakili wa Serikali walikuwa wachache, lakini sasa hivi Mawakili wa Serikali wameongezeka wamekuwa wengi mpaka imebidi Mawakili wa Serikali waanze kupanga sehemu nyingine utawakuta wako jengo la ATC, wako jengo la Mkapa, kwa kweli haipendezi. Ni kwa nini Serikali isitenge pesa kwa ajili ya kujenga jengo hili na ukizingatia ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na heshima yake yote hiyo lakini haina jengo lake la kudumu.

Mheshimiwa Spika, ukifika mle *Chambers*, nakumbuka na wewe ulikuwa Waziri wetu pale, utashangaa unakuta Mawakili wa Serikali wamelundikana kuanzia watano mpaka 10, hata ile siri ya kusema kwamba Wakili wa Serikali anazungumza na mteja, haipo. Kwa hiyo, napendekeza Serikali itengete fedha ili Mwanasheria Mkuu wa Serikali ajengewe jengo lake.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kuliongelea ni kuhusiana na vyombo vyta usafiri kwa Mawakili wa Serikali, *State Attorneys*. Kwa bahati mbaya, Waheshimiwa Wabunge wengi wanaozungumza humu ndani nadhani ni kama vile hawajui kuna Mawakili wa Serikali. Mambo yote tunayofanya humu, Miswada inayokuja humu na mambo mengine mengi, yanatayarishwa na Idara ya Mwanasheria Mkuu, ambapo wengi ni Mawakili wa Serikali, lakini nataka kukuhakikishia kama kuna Idara imesahaulika, ni Idara hii ya Mawakili wa Serikali. Mawakili wa Serikali ukiwaangalia ni kichekesho kitupu. Mtu anakaa Manzese hana nyumba, hana gari, lakini ndio mtu huyu ambaye ana-*draft Bill* analeta hapa Bungeni! Hawa Mawakili wa Serikali ndio wanasmama Mahakamani kuitetea Serikali, lakini hawa watu wamesahaulika kwa muda mrefu. Nakumbuka wakati ule ukiwa Waziri uli-introduce *Court Attire* na mambo mengine lakini ni vitu vidogo sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimtake Mheshimiwa Waziri, waangalie sana hawa Mawakili wetu wa Serikali, mishahara yao ni midogo. Nimeambiwa wako kwenye kiwango kama cha laki tatu laki nne, ni kichekesho kusikia kwamba Wakili wa Serikali anapata hela ndogo kama hiyo. Lakini pia kwa kuwapa mshahara mdogo, hawa watu wameshindwa kukopesheka, hawakopesheki. Kwa sababu ukimpa mshahara wa shilingi laki nne hawezi hata kwenda benki ya *CRDB* kukopa kagari, sana sana hela atakayokopa *ceiling* yake mwisho wa siku anaambiwa kwamba tutakupa milioni mbili lakini itamsaidia kufanya nini? Hawezi kujenga nyumba, hawezi kulipa karo ya watoto, kwa hiyo kwa kweli anabaki kuwa kama ombaomba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hawa Mawakili wa Serikali ndio watu ambao wanatutengenezea mikataba ya nchi hii. Hapa mtakumbuka *issue* ya *Richmond* ilivyokuja kuna Mawakili wawili wa Serikali walilaumiwa sana, mmojawapo akiwa ndugu Chidowu na mwingine akiwa ndugu Makia, mimi hawa Mawakili nawafahamu vizuri, wengine nimesomanao, walilaumiwa kwamba hawakuishauri Serikali vizuri, mimi niseme kwamba hawa Mawakili tutaendelea kuwalamu sana kwa sababu hatuwapi *exposure* ya kutosha. Kwa sababu wanapotoka Chuo Kikuu wakaingia *Chambers* hawapati angalau hata safari za kwenda nje wakasoma, hawawezi kupewa *attachment* kwenye nchi za wenzetu ambazo zimeendelea wakapata *training* ya kutosha, kwa hiyo, mwisho wa siku yule Wakili anakuwa na uwezo wake aliotokanao Chuo Kikuu. Kwa hiyo, ana-perform to his level of his ability, sasa anapofikia pale anapambana na magwiji, tunasema huyu mtu labda amehongwa, hapana, sio hivyo, hatujaweza kum-train. Kwa hiyo, napendekeza kwamba Waziri wa Sheria, ahakikishe kwamba hawa watu wanapelekwa nje kwa kusoma na sio kwa miezi miwili miwili au mmoja au mitatu, mtu apelekwe abobee akae miaka miwili miaka mitatu, akae kwenye attachment Uingereza au *Canada*, basi akirudi tutajua kwamba mtaalamu wetu ameiva, vinginevyo tutaishia kuwalamu tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata Waheshimiwa Majaji wanapoteuliwa mara nyingi utakuta wanapewa *orientation* ya wiki moja, mtu labda alikuwa Wizara ya Kazi au alikuwa sehemu nyingine, anateuliwa na Mheshimiwa Rais, anakuwa Jaji, *orientation* ya wiki moja haimtoshi. Ujaji ni lazima uendane na *experience*, aangalie wenzake wanafanyaje, aangalie mabadiliko ya duniani yanavyokwenda. Kwa hiyo, napendekeza Majaji wetu baada ya kuteuliwa wapelekwe kwenye nchi nyingine za wenzetu zilizoendelea waangalie *challenges*, wakasome huko, sisemi kwamba hawana uwezo, uwezo wanao lakini wanahitaji ku-*improve*.

Mheshimiwa Spika, lingine ni mikataba ya Serikali. Mara nyingi hapa Bungeni tunazungumzia mikataba ya Serikali kwamba ni mibovu, Mawakili wetu hawakutuwakilisha vizuri, mimi nilitaka nitoe pendekezo moja, kwamba nchi hii bado tunayo *resource* kubwa sana, bado tunao watu ambao wanaweza wakaisaidia Serikali hii. Kwa mfano katika ku-*negotiate* mikataba ya Serikali, napendekeza si lazima watumike Mawakili wa Serikali peke yao lakini tunao watu ambao wamebobe a kwa mfano mtu kama *Professor* Shivji, wa Chuo Kikuu Cha Dar-es-Salaam, *Professor* Kanywanywi, *Professor* Ibrahim Juma, *Professor* Mchome na Majaji wengine wastaa fu kama Jaji Bubesh, Jaji Mapigano, hawa waingizwe katika timu ya kwenda ku-*negotiate* na ikiwezekana yule Jaji ambaye amebobe a au kiongozi ambaye amebobe basi awe ndio *Chairman* wa ile timu, akipewa Mawakili wa Serikali wamsaidie, lakini tunayo *resource* ambayo hatuitumii. Kwa hiyo, nashauri sana kwamba hawa watu waangaliwe. Mheshimiwa Waziri wa Sheria, usiache kuwatumia hata kwa kuwalipa hawa watumishi ambao wamefanya kazi nzuri ya Serikali. Ninaamini kabisa ukimuweka kwenye timu ya ku-*negotiate* *Professor* Shivji, tutatoka na mkataba mzuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilitaka nizungumzie ni kuhusiana na vyeo vya watumishi katika Wizara hii ya Katiba na Sheria. Inasikitisha sana, mimi niliwahi kuwa, labda ni-*declare interest*, niliwahi kuwa *State Attorney* lakini niliondoka kwenda kutafuta maslahi mengine Benki ya *CRDB*. Niliondoka pale kwa sababu ya matatizo, malipo ni madogo sana lakini na sababu nyingine vyeo vinachelewa. Utakuta mtu amekaa pale, nina mfano sitamtaja mtu huyo, amekaa pale miaka sita hajawahi kupandishwa cheo. Sasa anakuja kijana mwagine anatoka Chuo Kikuu, anaajiriwa mwaka wa kwanza, wanapata mshahara unaolingana na wa huyu mtumishi ambaye amekaa pale miaka sita. Tunafahamu kutoka ngazi moja ya Wakili wa Serikali kwenda ngazi nyingine, ni ndani ya miaka mitano. Sasa inakatisha tamaa kumuona mtu amekaa pale miaka sita na cheo chake hakipandi. Hilo ninakuomba Mheshimiwa Waziri uliangalie kwa makini sana.

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumzie habari ya mishahara wa Walimu wetu wa Chuo Kikuu cha Dar – es - Salaam, Kitivo cha Sheria, *Faculty of Law*. Walimu wetu wanafanya kazi nzuri sana lakini kimishahara yao inawakatisha tamaa na matokeo yake inabidi waingie mtaani kufanya *consultancy*. Sasa ule muda ambao anautumia mtaani kufanya *consultancy* angeweza kuutumia kuwafundisha wanafunzi wetu na mwisho wa siku utakuta wanafunzi wanatoka bila kupata elimu ya kutosha na kama hawakupata elimu ya kutosha matokeo ni kwamba wataingia mtaani watakuwa hawajaelimika vizuri na hawa ndiyo watu ambao wanatakiwa kutoa haki. Kwa hiyo, tutaendelea kuwalaumu

kwamba hawatendi haki lakini uwezo wao ni mdogo maana hawakuelimika vizuri. Kwa hiyo, ninaomba suala hilo liangaliwe vizuri.

Mheshimiwa Spika, suala la *Hansard*. Hapa Bungeni tunayo *Hansard*, ni kwa nini *Hansard* isiende Mahakamani hasa kwenye Mahakama Kuu na *Court of Appeal*?

Mheshimiwa Spika, lingine pia ninataka ninapendekeze *website* upande wa *Judiciary*, hii itasaidia wananchi waweze kupata taarifa mbalimbali siku ya *judgement* na kufuutilia mambo yao.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ni kwamba Majaji wetu wanafanya kazi kubwa sana wanahitaji kuwa na Kurugenzi ya Utafiti. Lazima iwepo Kurugenzi ya kuwasaidia kufanya *research* kwa sababu Jaji anasikiliza pande zote mbili sasa wakati mwingine inaweza ikawa rahisi mtu kum-fix au Mawakili ambao ni wajanja wakaweza kum-fix, ni vizuri tukatengeneza Kitengo cha *Research* kwa ajili ya Majaji, Mawakili wa Serikali, *Attorney General* pamoja na wengine.

Mheshimiwa Spika, lingine ni Makarani wa Mahakama Kuu, si wasomi, wengi ni Darasa la Saba na wengine ni *Form Four*, utakuta mambo mengi hawayaelewi. Ninapendekeza kwamba hawa waliopo tuwaache wastaafu lakini kwa wale wanaojiriwa wapya wawe ni watu ambao kwa kweli ni wasomi na ikiwezekana angalau wawe na *Diploma* ya Sheria au hata *Degree*.

Mheshimiwa Spika, lingine ni *retirement benefits*. Mawakili wa Serikali wanapofikia kustaafu, afadhali Majaji, hao tuwaache lakini hasa Mawakili wa Serikali na Mahakimu, mtu anapofikia kustaafu anakuwa amekata tamaa kwa sababu hajui mambo yake ya huko mbeleni na kama huyo mtu hukumwekea mazingira mazuri ya mafao yake ya kustaafu, ndiyo matokeo yake tunaanza kusikia kwamba fulani kachukua rushwa na fulani kafanya nini kwa sababu unamweka katika mazingira ambayo kwa kweli hajui hatma yake itakuwaje.

Mheshimiwa Spika, lingine ninataka kushauri kuhusu Wazee wa Baraza. Yamezungumzwa mengi hapa, mimi nilipokwenda Jimboni kwangu, Wazee wa Baraza walinililia, jamani posho zao. Kwanza ziko chini, ni ndogo, zimepitwa na wakati lakini pili zinachelewa. Kwa hiyo, ninapendekeza kwanza ziongezwe halafu ziwafikie kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri katika *introduction* alivyozungumzia suala la Mahakama ya Kadhi. Wenzangu wamezungumza mengi sana hapa, mimi ni Mkristo na wengine ni Waislamu, yote yaliyozungumzwa ni kwa nia ya kuboresha.

Mheshimiwa Spika, lakini namshukuru Mheshimiwa Waziri alivyozungumza kwamba suala hili tayari liko kwenye Wizara yake na wanalfanyia kazi. Ninachoomba, busara itumike kwa sababu mambo yanavyokwenda humu ndani ndiyo hali halisi ya nchi yetu, sisi ni wawakilishi kwa hiyo tunawakilisha mazungumzo au mawazo ya watu wetu.

Kwa hiyo, katika hilo la Mahakama ya Kadhi, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, ninajua uwezo wako ulivyo mkubwa sana, naomba usome *mood* ya humu ndani halafu hiyo *mood* ndiyo ikuongoze kwa busara na hekima katika kufikia maamuzi kuhusu suala hili la Mahakama ya Kadhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, nataka kurudia kusema kwamba bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria, ni ndogo tena ndogo sana na kwa maana hiyo naishauri Serikali itafute kila mbinu na kila linalowezekana hata kama ni kukopa kama tunakopa kwenye Wizara za Miundombinu kujenga barabara na hata kununua ndege kwa nini tusikope tukaboresha Wizara hii ambayo ni nyeti sana? Safari ijayo mimi sitaunga mkono kama nitaona bajeti hii inaendelea kushuka namna hii. Kwa leo ninaunga mkono hoja hii lakini nikitegemea kwamba bajeti hii itapandishwa katika kikao cha mwaka kesho.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Gosbert Blandes. Namwita sasa Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa na baada ya hapo Mheshimiwa Wilson Masilingi na kwa mchana huu naona tutamalizia na Mhehimiwa George Simbachawene.

MHE. KABWE ZUBERI ZITTO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Wizara hii ambayo ni muhimu sana na ni moja ya Wizara ambazo ni andamizi katika uendeshaji wa Serikali yetu kwa sababu ndiyo Wizara ambayo inasimamia *administration of justice*. Kwa hiyo, nafurahi sana kuzungumza leo hii.

Mheshimiwa Spika, nina kitabu cha *survey* ambayo imefanywa na watu wa REPOA lakini ni kazi ya Serikali na kwa sababu ni kazi ya Serikali, kitabu hicho kinaitwa *Views of the People 2007*. Kitabu hiki ni sehemu ya shughuli za utekelezaji wa kila mwaka wa Mkakati Wa Kupunguza Umaskini na Kukuza Uchumi yaani MKUKUTA. Katika kitabu hiki, inaonyesha kwamba *level* ya kutoaminiana *mistrusts* kati ya Watanzania imefikia 78%, kwa maana ya kwamba katika kila Watanzania 10 ni Watanzania 8 tu ndiyo wanaoaminiana na kuaminika. Kwa hiyo, katika kila Wabunge 10 ndani ya Bunge hili ni Wabunge 2 tu ambao akisimama akizungumza unaweza ukaamini maneno yake, hii ni hali mbaya sana katika taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nimeanza hili kwa sababu ya mjadala ninaouona wa suala la Mahakama ya Kadhi. Mjadala huu ukiangalia tu mtiririko wa watu wanavyochangia, umeligawa Bunge kwa misingi ya dini. Wabunge Waislam wanatoa sababu zao za kwa nini Mahakama ya Kadhi iwepo na Wabunge Wakristo wanatoa sababu zao kwa nini Mahakama ya Kadhi isiwepo na inafikia mpaka kutumia lugha ambazo watu wanaotusikiliza huko nje na wao wanagawanyika.

Mheshimiwa Spika, sasa sisi wengine tumekuta nchi hii ikiwa *united*, nchi ambayo watu wote tunaishi pamoja na kwa kuangalia *level* ya ujana, wengine tunaamini tutaishi muda mrefu zaidi ya wengine, kwa hiyo, tusingependa kuona taifa

linaparaganyika na wengine tusingependa kuona kwa macho yetu wenyewe na kwa kweli wengine tupo tayari kusimama kuona kwamba taifa hili haligawanyiki. Mjadala huu unahitaji *tolerance* ya hali ya juu sana kwa sababu ni mjadala wa imani, mnapoanza kujibizana kwa imani ni kama wengine wanavyosema uvumilivu utaondoka, tunahitaji *tolerance* ya hali ya juu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya sana haujaja Muswada, kuna maelezo, kwa wale ambao wanasema kwamba Mahakama ya Kadhi iwepo, ni haki yao kusema kwamba Mahakama ya Kadhi iwepo, tutakuja kukubali au kukataa tutakapoona kwamba Muswada huu unakidhi haja. Lakini majibizano ambayo yanaendelea sasa hivi siyo *health* hata kidogo kwa sababu akisimama Mbunge Salum akamjibu Mbunge Paul, Paul na Salum ambao si Wabunge wataendelea kujibizana huko nje.

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani tuwe watulivu na tuwe *tolerant*, tusikilize hoja za kila upande kwa sababu hata baadhi ya lugha ambayo inatumika si nzuri, kwa sababu atasimama mtu atasema wenzetu wanasema hivi, Mheshimiwa Spika ukisema wenzetu kwa mfano Mheshimiwa Godfrey Zambi amesimama anasema wenzetu wanasema hivi maana yake ni kwamba tayari kuna makundi kwamba kuna hawa wenzetu na hawa si wenzetu.

Mheshimiwa Spika, mimi nisingependa tufikie katika hali ya namna hiyo ningependa mjadala huu uwe mpana zaidi, uwe mjadala wa hoja zaidi, tusikilizane, tuangalie imani za kila mtu na tuweze kuona na wala sio kwamba mimi niseme tu kwa sababu limekuwa likizungumzwa, hujibu hoja ya kwamba ni lazima Mahakama ya Kadhi iwepo kwa kusema ikiwepo na hao wengine wataanzisha Mahakama yao, inawezekana hao wengine hawana utaratibu wa aina hiyo. Ndiyo maana ni lazima na ni muhimu sana tuweze kuhakikisha kwamba mjadala wa namna hii hautugawi bali unakuwa ni mjadala ambao ni *health* vinginevyo hali ilivyo sasa tumezama Bunge la kuwa Bunge la Vyama Vingi tumekuwa Bunge la dini mbili. Maana tumezoea mjadala ni Kambi hii ya Upinzani inapingana na Kambi ya Chama Tawala lakini toka jana naona mjadala ni kambi ya wanaotaka Mahakama ya Kadhi na kambi ya wasiotaka Mahakama ya Kadhi. Mimi nadhani tusubiri hiyo *report* ambayo Waziri ameizungumzia na ijadiliwe kwa mapana na tusiingie katika lugha ambazo zinaweza zikatufanya kama taifa tuweze kugawanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo nataka kulizungumzia, ni suala la umuhimu wa mabadiliko ya Katiba. Anaweza akaja Kiongozi wa Kisiasa akakaa miaka 20, akamaliza uongozi wake, asikumbukwe kwa chochote, anaweza akaja Kiongozi akakaa mwaka mmoja akakumbwa kwa sababu ameacha *legacy*. Sasa kumejengeka hali ambayo hatufanyi viongozi wetu waweze kutengeneza *legacy* kwa hiyo tumekuwa watu wa *status quo* hali tulioikuta tuiache hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, suala la mabadiliko ya Katiba na baadhi ya watu wamekuwa wakizungumza kwamba hii siyo agenda ya Chama kilichopo madarakani kwa sababu wakati tunagombea hawakusema kwamba watabadilisha Katiba lakini mwaka 1990 Chama cha Mapinduzi kilikuwa na Ilani, hawakuahidi nchi hii kuingia kwenye vyama

vingi lakini mazingira yalilifanya Taifa liingie kwenye vyama vingi. Vivyo hivyo, leo tunavyozungumza kuna matatizo makubwa sana ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, matatizo ambayo ni lazima yaelezwe kwa kufanya mabadiliko ya msingi katika Katiba lakini hii ni bajeti ya tatu tunakwenda hatuoni kabisa hoja ya mabadiliko ya Katiba ikiwa inachukuliwa uzito wake.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1994 ukiwa Waziri wa Sheria na Katiba wakati wa mjadala wa kuhusu kumfanya Makamu wa Rais kuwa mgombea mwenza au kuendelea na utaratibu wa zamani na nina *Hansard* ile ya mjadala mzima, ulisema kwamba Katiba inabadiishwa kutokana na matakwa yaliyopo wakati huo kwa sababu kuna watu ambao walikuwa wanahitaji mabadiliko makubwa sana akina Njelu Kasaka na Ndembwela Ngunangwa yaani Wabunge wa wakati ule, wakati unajumuisha ukasema kwamba kuna mabadiliko ambayo ni lazima yafanyike wakati kwa wakati, sasa wakati huu umefika.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano inawezekana kabisa mwaka 1994, suala la kuwa au na kutokuwa na mgombe binafsi katika viti vya Ubunge, Urais na Udiwani, ni suala ambalo labda lilikuwa ni gumu, haliwezekani lakini baada ya miaka 15 yaani baada ya chaguzi tatu za vyama vingi, hivi sasa, ni suala ambalo linawezeekana na tumefahamishwa kwamba kesi iliyopo Mahakamani hivi sasa ambayo Serikali imekata rufaa siyo ya kupinga kuwepo au kutokuwepo kwa mgombe binafsi bali ni ya kupinga mamlaka ya Mahakama kuhusu suala zima la kubadilisha Katiba.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nafikiri ni muhimu sana Serikali iweze kutufahamisha ni lini italeta Muswada wa Mabadiliko ya Katiba ili kuweza kuongeza huo uhuru wa wananchi kuweza kugombe nyadhifa bila ulazima wa kuwa katika Chama cha Siasa. Ni hali hiyo hiyo kuhusiana na suala la aina gani ya uchaguzi amba tunapaswa kuwa nao, suala la *proportional representation* kwamba aina gani ya Wabunge amba tunao. Leo tunazungumzia masuala ya *fiftyfifty*, lakini lakini ni aina gani ya *fiftyfifty* ambayo tutakuwa nayo? Njia pekee ya kuweza kutuokoa, ni kuwa na mfumo wa uwakilishi wa uwiano katika Bunge amba mimi nilikuwa nafikiria kwamba ni suala la msingi sana tuweze kuliangalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala zima la nafasi ya Waziri Mkuu, wakati aliye kuwa Waziri Mkuu siku alipojiuzulu nilisimama hapa Bungeni nikasema kwamba Waziri Mkuu akijiuzulu basi Serikali nzima imejiuzulu lakini Mawaziri wakaruka kweli, wakasema aaah, inaweze kanaje? Lakini baadaye ikawa ni hivyo.

Mheshimiwa Spika, leo tunavyozungumza, ikitokea uchaguzi wa mwaka 2010 na itatokea kwamba Kambi ya upande wako huu ikawa na Wabunge wengi zaidi kuliko kambi ya upande huu, kambi hii ndiyo itakayopaswa kutoa Waziri Mkuu, Katiba *improve* namna gani? Katiba imesema hivyo kwamba Waziri Mkuu atatoka chama chenye Wabunge wengi lakini kwa utaratibu upi? Rais atateua kwa utaratibu upi? Hayo ni mambo ambayo ni lazima tuyaangalie mbele kama yataweza kutokea ili yasijie yakatuletea mgogoro wa Kikatiba huko tunakokwenda.

Mheshimiwa Spika, la pili, kwanza napenda niipongeze kwa dhati kabisa kazi ambayo inafanywa na yule Wakala wa *RITA*, ni kazi nzuri sana lakini tulikuwa tunashauri na nilishamwambia Mheshimiwa Waziri kwamba kuna umuhimu wa kuangalia uwezekano wa ku-*match* shughuli za usajili za *RITA* na shughuli za Mamlaka ya Vitambulisho vya Kitaifa kwa sababu tukiwa na Mamlaka mbili tutakuwa tunatumia vibaya rasilimali zetu.

Mheshimiwa Spika, la tatu na la mwisho ambalo nataka niungane mkono na Mheshimiwa Gosbert Blandes, ni suala la zima la bajeti ya Mahakama. Kwanza, nampongeza na pongezi hizi zinaanzia kwako, suala la kuwa na *Judiciary Fund*, limeanzia kwako na ilikuwa ngumu sana kuitisha kuwa na Mfuko wa *National Assembly Fund*. Kwa wenzetu wa Idara ya Mahakama wameliona na wenyewe wanalichukua lakini tungependa lije haraka ili Idara ya Mahakama iweze kujitegemea katika bajeti yake, waweze kufanya shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, lakini mtakumbuka kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali alinijibu hapa kuhusu suala la Mahakama kutumia *Hansard* kwa ajili ya kusaidia *recording* ya kesi akasema Serikali inalifanya kazi. Nimeangalia hotuba ya Waziri, sijaona mahali popote ambapo suala hili limezungumziwa. Tuna Majaji wangapi? Tuna Kanda ngapi za Mahakama Kuu kiasi cha Serikali kushindwa kwa haraka iwezekanavyo kuanzisha utaratibu huu wa *Hansard* katika Mahakama ili Majaji wetu nao wafanye kazi zao katika hali ambayo ni nzuri, waweze kuamua kesi zao katika hali ambayo wana taarifa zote badala ya kukaa kama ilivyo sasa hivi, hivi sasa Jaji Mkuu, Jaji Kiongozi, Majaji wa Mahakama ya Rufaa na kadhalika wanakaa wanaandika kesi, unazungumza, Wakili anaandika kwanza ndiyo anaanza kuamua, hii hali haifai!

Mheshimiwa Spika, ninashauri hata kama haijawa *provide for*, hivi hivi tuombe Waziri wa Fedha atakapokuja kwenye *Appropriation Bill*, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Waziri wa Katiba na Sheria, waangalie itagharimu kiasi gani kuweza kuweka kwenye Mahakama Kuu zote za Tanzania na Mahakama ya Rufaa mfumo huu wa *Hansard* ili sisi Wabunge tuweze ku-*reallocate funds*, tutoe maeneo ambayo tunaona kwamba hayana tija zaidi tupeleke Mahakamani ili kuiwezesha Mahakama iweze kufanya kazi zake vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo ambayo nimetaka kuyazungumza kwa leo, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofī*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto. Sasa namwita Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Wilson Masilingi na hatimaye Mheshimiwa George Simbachawene.

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA: Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuzungumza kuhusu bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli tangu jana, nikisikiliza uchangiaji wa humu ndani, ni kwamba tunaelekea kubaya. Naomba suala la Mahakama ya Kadhi tuisitengane, inavyoelekea sasa tunaanza kutokuheshimiana maana tumeanza kujibu upande wa Wakristo na upande wa Waislam, hapa tutanyosheana mikono na baadaye tutafika mahali ambapo si pazuri. Lakini naomba tuheshimu Katiba na ninasititiza Serikali kwamba haina dini, hivyo, naomba Katiba ichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naomba basi nichukue nafasi hii, kumpongeza sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuliona hili katika Idara hii hasa ya Mahakama kuhakikisha anasimamia suala la jinsia na kuhakikisha kwamba sasa tunaelekea kuzuri na ninamshukuru Mheshimiwa Rais kuona kwamba yuko karibu sana na suala letu la kuelekea kwenye 50% kwa 50%, linalelekea katika utaratibu mzuri. Nampongeza baada ya kuteua Majaji kati ya 11, saba ni wanawake, ni hatua nzuri tunakoelekea. Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ukurasa wa 57 ametueleza kwamba kuna Majaji 83, Majaji 28 ni wanawake si haba 55 ni wanaume. Huko tunakoelekea ni kuzuri. Namshukuru sana na kwa hiyo ninaomba tu aendeelee na moyo wake huu wa kujali jinsia zote mbili.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichukue nafasi hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kusema kwamba huko baadaye analeta Marekebisho ya Sheria ambazo zinamgandamiza wanawake na watoto. Mimi kwa kweli huwa najisikia vibaya sana ninapofika kwenye maeneo mengi unakuta kuna watoto wa mtaani, huyu mtoto wa mtaani ni yupi? Ninavyofahamu, mtoto anazaliwa na mwanamke na mwanaume, inakuwaje sasa mzazi anashindwa kutimiza wajibu wake wa kuhakikisha mtoto huyu anapata elimu, mtoto huyu anaheshimika lakini anaachwa katika maeneo ya mtaani hapati chakula. Sasa ninamuomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuja na marekebisho hayo anieleze, je, atakuwa ameyaingiza haya kuhusu huyu mtoto wa mtaani? Suala hili la mtaani litafutika kwa sababu hatuna mtoto wa mtaani kwa kweli.

Mheshimiwa Spika, lingine linalonisononesha sana, ni kuhusu watoto wa kike wanapopata mimba. Kumekuwa na tabia ya wazazi, akiona tu mtoto wa kike ambaye alikuwa anasoma shule amepata mamba, wazazi wanaweka vikao vyao vya makubaliano. Hapa tunamnyima mtoto wa kike haki yake, anapojifungua, haendelei tena na shule lakini mtoto wa kiume anaendelea na shule. Je, katika marekebisho hayo, atakuja sasa atusaidie kumpa haki huyu mtoto wa kike, mtaangalia kama tabia yake ni mbaya basi mtamuacha lakini kuna watoto wengine inakuwa ni bahati mbaya, anaposema kujaribu tu tayari mimba, je, tutamsaidiaje kuhakikisha kwamba sheria hizi tunamlegezea ili angalau huyu mtoto wa kike apate fursa ya kuendelea na masomo kama anavyoendelea na masomo mtoto wa kiume.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kusema katika hotuba yake kwamba hata Mahakimu wa Mahakama za huko wahakikishe kwamba wanasiimamia sana hizi kesi za ujauzito kwa watoto wa kike na nina imani kwamba Mahakimu watatusaidia ili basi hawa wazazi wanaochukua mamlaka ya kuwatolea binti zao maamuzi maana kuna wakati mwinglezea ili angalau huyu mtoto wa kike apate fursa ya kuendelea na masomo kama anavyoendelea na masomo mtoto wa kiume.

hamuhitaji kumbe ilikuwa ni bahati mbaya tu mimba amepata, basi Mahakimu watusaidie ili kumpa haki huyu binti na yeye aweze kutoa maamuzi yake kutokana na haki aliyonayo.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ninalolipata katika kuishi kwangu miaka hii niliyonayo, ni kwa nini watoto wanatupwa sana? Watoto wachanga wanatupwa maeneo mengi sana, wanajifungua baadaye mtoto anatupwa. Hivi Sheria katika marekebisho haya sijui sasa atakuja na Sheria ambayo itambana kwanza huyu mtoto aliyemzaa kwa sababu siamini kabisa kwamba hao wasichana au wengine ni wamama watu wazima lakini wanatupa watoto, wanaishi na jamii na jamii inawazunguka pale, sasa inakuja kwamba eti mtoto ameokotwa hajulikani aliyemzaa, ni kweli? Hili ninaomba Sheria sasa itungwe ya kuhakikisha kwamba tunawabana hata hawa wazazi, tena ninaomba hata jamii ibanwe kwa sababu mimba inachukuliwa kwa miezi tisa, ni mtoto mzima kabisa anayezaliwa halafu anatupwa, je, alipokuwa anaishi huyu binti alikuwa hajulikani? Je, maeneo hata kama ni Wilaya, kijiji au kata hayajulikani? Labda tungejaribu sasa kuja na Sheria ya kuomba hata uongozi ubane mahali fulani na kuhakikisha kwamba tunapunguza tatizo la watoto kutupwa hovyo katika maeneo yetu. Kwanza mtoto anafedheheka hata akija kukua anakuwa hana wazazi wakati alizaliwa na mtoto ametokana na baba na mama.

Mheshimiwa Spika, naomba tena nichukue nafasi hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika Mahakama yake sasa ameweka kitengo maalum cha kutoa elimu katika Mahakama za Mwanzo kwa ajili ya wananchi labda kutafsiri Sheria, lakini naomba hiki kitengo basi kiende mpaka maeneo ya huko vijijini kisiishie tu huko makao makuu kwa sababu wananchi wengi waliopo vijiji huko tunakoishi nao hawajui hata Sheria zinavyokwenda, hawajui hata haki zao. Je, kitengo hiki kinaweza kuwafikia hawa wananchi waliopo vijijini wakatafsiriwa au wakapata tafsiri ya Sheria zetu kwa Kiswahili kizuri na wakaelewa sheria zao?

Mheshimiwa Spika, pia ninamshukuru Mheshimiwa Waziri amesema kwamba Mahakimu wengi watapatiwa usafiri, hilo ninashukuru sana maana Mahakimu wengi maeneo ya kwetu huko vijijini wanapanda daladala za baiskeli. Huyu Hakimu anakwenda kutoa maamuzi ya watu walioleta kesi zao, anapanda baiskeli. Kwanza, anakuwa haheshimiki, unamvutia apokee rushwa kwa sababu mtu mwenye gari anaweza akamchukua na ndiye mwenye kesi ambayo anakwenda kumtolea hukumu kule. Kwa hiyo, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuhakikisha basi hizo nyenzo ambazo anawapelekea Mahakimu zifike mpaka kwenye Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Spika, lingine la kusikitisha sana ni kwamba Mahakimu wengi hawana nyumba za kuishi kwa mfano kuna Hakimu wetu wa Mahakama ya Mwanzo pale Malya anakaa *Guest House*. Kwa Hakimu mnayemtegemea hamna heshima kukaa nyumba ya wageni, haipendezi kwa kweli. Nitaomba sasa Mheshimiwa Waziri pamoja na kwamba bajeti ni ndogo lakini ahakikishe kwamba Mahakimu wao wanapata mahali pa kukaa vizuri kama tunavyozingatia kwamba Walimu wapewe sehemu za kuishi vizuri ili waweze kufundisha basi na Mahakimu na wenyewe tuwaangalie kwa hilo kwa kuona

kwamba wanawekewa mazingira mazuri, atakuwa na usalama zaidi wa maisha yake kuliko kwenye nyumba ya wageni.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri sijaona mahali popote inapoonyesha Sungusungu. Sungusungu ni kikosi kizuri sana ambacho kinaweza kikasimamia amani katika maeneo hayo na ni kikundi ambacho kinaweza kumsaidia sana Mheshimiwa Hakimu maeneo alipo. Lakini sijaona mahali popote Sungusungu watashirikishwa vipi katika kuhakikisha kwamba wanalinda usalama na wanasaidiana na Mahakimu kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, Sungusungu hawa ninaowazungumzia wao ndio wanawajua wahalifu, Sungusungu hawa ndiyo wanajuana wao wenyewe katika maeneo yale, Sungusungu hao hao wanafahamiana wao wenyewe kwamba mhalifu ni fulani na aliyefanya kosa wanawafahamu. Sasa ninaomba Serikali hiki kikosi kizuri ambacho kingeweza kumsaidia Mheshimiwa Hakimu maeneo ya huko waliko vijijini angalau basi mkajaribu kuangalia kama wana kikao chao cha Sungusungu Hakimu akashirikiana nao katika kutoa maamuzi ili kupunguza wingi wa kesi ndogondogo ambazo zimepelekwa Mahakamani zikamalizwa tu kwenye kikundi cha Sungusungu.

Mheshimiwa Spika, mimi sikuwa na mengi sana ya kuzungumza kuhusu hili, ni kumpongeza Waziri kwa kazi nzuri anazozifanya, niombe basi utaifa wetu uwe palepale wa kusimamia haki za binadamu na haki za wanawake na haki za watoto.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofî*)

MHE. WILSON M. MASILINGI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kushiriki katika kujadili hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, nianze kama Waheshimiwa Wabunge wenzangu walionitangulia walivyoanza, kwa kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri na yenye mipango mizuri na nimpongeze pamoja na Katibu Mkuu wake ambaye lazima nieleze maslahi, tumesoma darasa moja na Mheshimiwa Jaji Mkuu. Pia niwapongeze Waheshimiwa Majaji wote na watumishi wote wa Wizara na Mahakama kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na kila mmoja wetu hapa amekiri jinsi ambavyo wanafanya kazi nzuri katika mazingira magumu sana. Napenda kusisitiza magumu sana na kwa hiyo napenda kuwapa hongera sana, Mheshimiwa Waziri endelea kuwapa moyo wote ambao unashirikiana nao katika sekta hii ya haki na utawala wa sheria.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nimpongeze Mheshimiwa Rais na kumshukuru sana kwa dhati kwa sababu amechagua Waheshimiwa Majaji wengi sana hivi karibuni na mionganoni mwao kati ya hao Majaji 34, wanne wakiwa wa Mahakama ya Rufaa na wengine wa Mahakama Kuu, nimesoma nao darasa moja. Darasa letu tuna Waheshimiwa Majaji saba, ni bahati sana na ninafurahi kusema kwamba, ninawapongeza Waheshimiwa

Majaji niliosoma nao na ambao sikusoma nao darasa moja, kazi yao yote ni muhimu sana, shukrani nadhani nimezimaliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatima ya nchi yetu, hatma ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, iko mikononi mwetu sisi Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa mujibu wa Katiba, Bunge lina sehemu mbili, hili limerudiwa mara nyingi. Sehemu ya kwanza Mheshimiwa Rais na sehemu ya pili, ni sisi hapa. Kwa hiyo, amani ya nchi yetu, utawala wa haki na mambo yote kwenda sawa, viko mikononi mwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mjadala ambao nimeusikia tangu jana ndani ya ukumbi huu, unanikumbusha kwamba tuna kila sababu ya kuliombea Taifa letu kwa Mwenyezi Mungu ili amani tuliyonayo ambayo imejengwa kwa kazi ngumu sana na wazazi wetu, wengine wametangulia mbele ya haki, sasa dhamana iko mikononi mwetu, si jambo la mzaha, tukijaribu kuanza kufumua yale ambayo hatuwezi kuziba na bila kutafakari yalizibwa vipi, bila kutafakari hawa baba zetu walioipitisha hii Katiba walizibaje mpaka kufikia muafaka wa masharti magumu ya kupitisha Katiba, tutakuwa hatujawa watu wanaowajibika ipasavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nitachangia katika maeneo machache. La kwanza, Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu kachokozwa na Mbunge mwenzetu akalazimika kuwajibika ipasavyo, akanukuu Katiba ya nchi akasema:-

“Ibara ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema, Tanzania ni nchi moja na ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Akasema Ibara 2(1) ya Katiba inasema, eneo la Jamhuri ya Muungano ni eneo lote la Tanzania Bara na eneo lote la Tanzania Zanzibar na ni pamoja na sehemu yake ya bahari ambayo Tanzania inapakana nayo”.

Mheshimiwa Spika, akamaliza kunukuu akijibu swalii la Mheshimiwa Mbunge mwenzetu. Matokeo yake, kesi imekuwa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mizengo Pinda wala hata si kesi ya Bunge hili! Watu wanaandamana kumpinga Pinda!

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Spika, mwongozo wa Spika.

SPIKA: Mheshimiwa Tahir, Kanuni gani?

MHE. HAFIDHI ALI TAHIR: Mheshimiwa Spika, narudia tena matamshi yako bila kunukuu Kanuni kwamba suala hili limepelekwa mahali na litazungumzwa baadaye. Sasa hii ni mara ya pili unaruhusu linaendelea kuzungumzwa ndani ya Bunge hili wakati umeshatoa tamko kwamba lisizungumzwe, liachwe katika mamlaka inayohusika baadaye litakuja kuzungumzwa. Sasa naomba urudie katika kauli yako ile ile kwamba lisizungumzwe.

SPIKA: Kauli yangu isipotoshwe kwa sababu bado nilikuwa nafuatilia mkondo wa Mheshimiwa Masilingi anaelekea wapi, kuna mambo ya ufafanuzi wa Katiba ambayo

hatuwezi kuyazuia kuzungumzwa na ndiyo maana kwa mfano kwenye hotuba ya Kambi ya Upinzani, suala hili lilijitokeza na sikulizuia kwa sababu lilikuwa linaeleza kwa mwelekeo wa Katiba. Sasa ngoja tumsikilize, bado nasikiliza kwa makini nadhani anakaa kwenye Katiba kwa hiyo hakuna tatizo kwa sasa. Mheshimiwa Masilingi endelea.

MHE. WILSON M. MASILINGI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa uamuzi wako, kama siku zote wa busara. Tunajadili hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, ndiyo hoja iliyoko mbele ya Bunge hili. Tukisema tusizungumzie Katiba hapa itakuwa hatari lakini tusiingie kwenye ubishi.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kusema na nimalizie kwa hilo kwamba, maandamano au lolote lile la kumlaumu Waziri Mkuu wetu kwa kunukuu Katiba likawa tatizo lake binafsi ni kinyume cha sheria, hilo ndilo hitimisho langu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni kinyume cha sheria kwa sababu ameapa kulinda Katiba, ameonyesha kwa ushahidi anavyoitetea Katiba na wenyewe dhamana ya Katiba hii si Waziri Mkuu peke yake, kwa hiyo, tunapaswa kumuunga mkono kwa nguvu zote na kwa gharama yoyote ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naondoka hapo na naingia katika eneo la pili ambalo ni kuhusu bajeti ya Wizara hii na hususan ya Mahakama. Nilikuwa nafutilia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nimesikitika sana, bajeti ya Mahakama yenyewe halisi kuondoa Idara zake ndogo ndogo kama Mahakama ya Ardhi, Mahakama ya Biashara, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, ni Sh.38,548,471,000/=, hapo nimeondoahadi ya fedha za kigeni na hili ndiyo Bunge ambalo kwa mujibu wa Katiba tunatamka kwamba ndiyo tunaidhinisha matumizi ya bajeti, ndiyo sisi tunapitisha bajeti, makusanyo ya nchi yetu kwa wastani, ya mwezi huu sijui lakini niliuliza Kamishna Mkuu wa TRA akaniambia wanacheza kwenye wastani wa 300bn/= kwa mwezi au 320bn/= wanacheza hapo, ni bajeti ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, nguzo ya tatu ya nchi yetu Mahakama na nieleze maslahi kwa sababu haya ni mambo ya Kanuni, nimeanzia kazi Mahakama na nimetoka huko nikiwa Hakimu Mkazi Mfawidhi, Mkoa wa Lindi nilipokuwa Wakili wa Kujitegemea mwaka 1990, kwa hiyo ni Wakili wa Kujitegemea tangu mwaka 1990, kwa hiyo msije kuniingiza huko.

Mheshimiwa Spika, Shirika langu la Sheria sasa hivi halina kesi Mahakamani, tumemaliza kesi zetu, sasa hivi sijaamua wachukue kesi nyingine. Kwa hiyo, sina maslahi ya kifedha huko na kesi yangu inayoshtaki kupitia Mawakili wangu, nimewaruhusu wajadiliane nje ya Mahakama labda wakashindwa ndiyo warudi Mahakamani. Kwa hiyo, hapa ninayozungumza ni kwa maslahi ya nchi, hakuna maslahi binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Ardhi wametengewa Sh.1,234,289,000, ukiondoa za nje Sh.96m/= ni Sh.1.1bn/= na wamepokea kesi ya 5013 za migogoro ya ardhi na wameweza kumaliza 736 tu, kesi za mwaka mmoja mpaka Juni, 4277

zinaendelea, kwa pesa hii! Kwa Majaji hawa, watumishi hawa! Hatujatenda haki kwenye eneo la utoaji wa haki ambalo ni jambo la msingi. Naomba niipongeze Mahakama ya Biashara wanaendelea vizuri, wamejiwekea lengo la asilimia themanini ya idadi ya kesi zitakazofunguliwa ziamuliwe wakaweza kufikia asilimia sabini na saba kwa kuamua kesi tisini kati ya mia kumi na saba na wanalenga asilimia tisini mwaka ujao lakini na wao fedha bado wanapewa kidogo.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Haki za Binadamu hapa ndiyo kuna mambo ya ajabu sana. Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni chombo ambacho katika sura ya nchi yetu ni cha Kikatiba, kimetujengea heshima katika nchi yetu. Hata ukienda nchi za nje, mnaulizwa mna chombo ambacho kinaweza kudhibiti mwenendo wa Serikali na vyombo vyake kuzingatia haki za binadamu na utawala bora, mnasema kipo. Jengo wanaloafanya kazi ni la msaada, tumepewa msaada na Denish. Sasa tunatenga pesa sisi Sh.4bn/= lakini kati ya hizo 1.3bn/= zinapaswa zitoke nje ya nchi lakini ukiangalia mlolongo wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Wizara yake ni tegemezi kwa fedha za nje, yaani kuna fedha za nje, hakuna za ndani za mipango ya maendeleo. Kwa kuwa sina muda wa kutosha kwenda kwenye vifungu naomba niishie hapo.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichangie kuhusu wananchi wa Kata ya Bulungura, Jimbo la Muleba Kusini, walilalamika kwenye Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Wakajibiwa kwa barua, tumepokea malalamiko yetu tutayafuatilia. Nimegundua kwa nini hawajakwenda na mwaka umepita, ni kwa sababu hawana fedha. Siwezi kumlaumu Mheshimiwa Waziri maana ye ye siye anayetoea fedha, tunaotoa ni sisi na umekuja kutuambia tuidhinishe na nakushukuru kwa mahusiano mazuri ya Idara ya Mahakama, kwa mara ya kwanza, umeleta Waheshimiwa Majaji wakiongozwa na Mheshimiwa Jaji Mkuu wakatutembelea hapa, ungekuwa unakorofishana nao, Mheshimiwa Jaji Mkuu asingejuja. Ungekuwa unatamba unasema nami ni Mwanasheria na umri unakuruhusu, Waheshimiwa Majaji hawa wasingejuja, wangekaa kule halafu hawa wakiwa na hasira, wana uwezo wa kutushughulikia. Kati ya Idara ama vyombo vya dola ambavyo vina nguvu sana, ogopa Majeshi na Mahakama. Hawa wana uwezo wa kutushughulikia, wanapuuzwa, wananyamaza, wana nidhamu kama za kijeshi, lakini wakiamua kuleta maasi kimya kimya, tutalia hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pendekezo langu, ili kurekebisha hali hii, tuanze kutafakari, hili Bunge hivi tutaendelea kulialia mpaka lini? Napendekeza utaratibu wa kutunga sheria na kupitisha bajeti ya nchi yetu tuanze kuutafakari. Katika mambo ambayo mtayazingatia kuyarekebisha katika Katiba na hili liwepo. Kwa mfano, kwa mujibu wa Ibara ya 97(4), utaratibu wa kutunga sheria, tukibishanabishana sana na Mheshimiwa Rais, tukampeleke Muswada akaukataa, akaurudisha kabla ya miezi sita tukapata theluthi mbili, tukamrudishia, akiukataa, analivunja Bunge. Hivi katika hali halisi ya uchumi wa nchi yetu, kuitisha uchaguzi mkuu kila mnapobishana baada ya kupeleka Muswada kwa Rais, tuna uwezo huo wa kifedha? Lakini kwa uzoefu wangu, tangu Baba wa Taifa, Rais wa Awamu ya kwanza, Rais wa Awamu ya Pili, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin Mkapa na Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, wana ushirikiano mzuri na Bunge, akitokea Rais ambaye hana ushirikiano na Bunge, migogoro itatokea na nchi haitakwenda.

Mheshimiwa Spika, sasa tumechanganya mambo, ukiangalia Ibara ya 98, imeweka utaratibu mzuri wa namna ya kurekebisha Katiba kwa mambo ambayo yanahusu Muungano, theluthi mbili kwa pande zote, Bara na Visiwani na kwa yale ya kijumla, theluthi mbili zinatosha, mambo mmemaliza. Sasa napendekeza haya yaangaliwe upya kwa sababu hata maeneo ambayo tunaweza kuvunjwa kama mnavyoona Ibara ya 90(2) inasema:-

“Rais hatakuwa na uwezo wa kulivunja Bunge wakati wowote isipokuwa tu:-

(b) Kama Bunge limekataa kupitisha Bajeti iliyopendekezwa na Serikali.”

Mheshimiwa Spika, sasa nani yuko tayari kurudi Jimboni kuomba kura hivi karibuni, akakataa kuunga mkono bajeti hata kama hakubaliani nayo, nani katika hali halisi? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, umekuwa Rais wa *Commonwealth Parliamentary Association*, mwaka kesho tuna mkutano mwezi wa Tisa, tujaribu kurekebisha mambo ambayo wenzetu toka nje watakuja kutuhoji kama vile uwezo wa Bunge, *partnership* kati ya Bunge na Serikali. Bahati nzuri, sisi Bunge letu lina sehemu mbili Rais na sisi. Kwa nini Rais apewe madaraka yote? Mpaka sasa hivi, hapa sina ugomvi na Mheshimiwa Rais wa sasa, ni rafiki yangu sana, nampenda sana, naye ananipenda, ninachosema kwa kweli ni vizuri ikiwa theluthi mbili kwa chini ya miezi sita awajibike kuukubali huo Muswada na akikataa atoe sababu tujadili tena, zikirudi tena theluthi mbili, upite, hiyo ndiyo *partnership* ambayo ina mantiki sio uoga huu ambao tunasema eehee, anawenza akalivunja, hebu piga kura ya ndiyo haraka sana, uchaguzi ni *fatigue*, naujua sana. Bajeti hivyo hivyo, sasa hivi kweli Mheshimiwa Jaji Mkuu amefika hapa sote tunasema bajeti ni ndogo hatuongezi, tunaelekeza bajeti ijayo, ipi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba haya mambo yarekebishwe na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami ili niweze kutoa mchango wangu katika hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, rafiki yangu Zitto hapa amezungumzia habari ya *degree of tolerance* lakini hii *degree of tolerance* inakuja wakati gani? Ni kama watu hawazungumzi mambo yanayowahu su au watu wanapozungumza mambo yanayowahu su? Nadhani *degree of tolerance* nzuri, ni ile inayotokana na watu kujadili kwa uwazi mambo yanayowahu su. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja ya suala la Mahakama ya Kadhi limetawala katika mjadala tangu jana. Niseme tu kwamba, nadhani nianze na hilo ili niweze kuongeza *degree* yangu ya *tolerance*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa ku-declare interest kwamba, ni Mwanasheria mwanafunzi na hapa kuna Mwanasheria Mkuu au wawakilishi wake na Wanasheria wengi waliobobea katika mfumo wa *judicial system* ya nchi yetu. Kwa hiyo, nikizungumza hapa kama mwanafunzi wao, nadhani kama ni mtihani watatia maksi au wataniondoshea.

Mheshimiwa Spika, nchi ya Tanzania ina *sources* ya sheria zake. Hii *legal system* ina *source* ya sheria zake na moja kati ya *source* hizo ni pamoja na sheria zinazotungwa na Bunge, tunaziita *statutory laws*, lakini zipo sheria za kimila tunaziita *customary laws*, pia zipo sheria zinazotokana na maamuzi ya kesi zilizoamuliwa na Mahakama ya Juu ambayo inazibana Mahakama za chini kuamua maamuzi yanayofanana na uamuzi wa Mahakama za Juu tunaziita *the laws of precedent*. Ipo pia *source* nydingine ya sheria katika nchi yetu inayotambulika kisheria ambayo ni *Islamic Laws*. Kwa hiyo, katika maamuzi yanayofanyika katika nchi hii yanatokana na *source* ya sheria hizi.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nije kwenye hoja, matumizi ya sheria za Kiislam hapa nchini yapo na zipo kesi zinazoamuliwa na Mahakama zetu kwa kutumia sheria za Kiislam. Katika Mahakama zetu za kawaida, wapo Wazee wa Baraza amba wanatokana na ufahamu wa sheria aidha za kimila au za kidini na mambo mengine ambayo yanamsaidia Hakimu kuweza kufikia uamuzi ulio mzuri maana mtu ye yeyote atahisi ametendewa haki akiamuliwa kwa sheria inayomhusu na itafsiriwe vile ambavyo anaona inafaa.

Mheshimiwa Spika, sioni tatizo hapa liko wapi lakini sielewi kama hawa wanaodai uwepo, sitaki kusema kwamba wanaodai uwepo wa Mahakama ya Kadhi ni Waislam hapana, wapo watu wanaodai uwepo wa Mahakama ya Kadhi na wengine wanawenza kuwa si Waislamu na tunayo mifano ya kesi ambazo zimeamuliwa na Mahakama za Kiislam hata Zanzibar na baadaye watu waka-*appeal* katika Mahakama ya Rufaa ambayo inatumia sheria za kawaida zilizotungwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, kama kweli lipo tatizo na kama kweli sheria hizo ni muhimu kutumika nataka kusema kwa Tanzania Sheria za Kiislam zinatumika. Tatizo hapa tuelezane, hivi tatizo ni kuwepo kwa matumizi ya sheria za Kiislam au kuanzisha a *parallel system* na *judicial system* yetu? Kama ni kuanzisha *parallel system* yetu, hii ni kinyume na Sheria na Katiba lakini kama ni kuwepo kwa Mahakama ya Kadhi nani amezuia, suala ni kwamba ina-*operate* namna gani?

Mheshimiwa Spika, naomba ninukuu Katiba, Katiba yetu kwenye *preamble*, ukurasa wa 13, naomba ninukuu, ile sehemu ya aya ya mwisho inasema na hii ni *preamble* na *preamble* ni sehemu inayobeba ujumbe mzima wa kitakachokuwepo ndani na utangulizi huu, ni kama kiapo, inasema:-

“Kwa hiyo, basi, Katiba hii imetungwa na Bunge Maalum la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa niaba ya wananchi, kwa madhumuni ya kujenga jamii kama hiyo, na pia kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Tanzania inaongozwa na Serikali

yenye kufuata misingi ya kidemokrasia, ujamaa na isiyokuwa na dini”. Mwisho wa kunukuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama ina-*declare* kwenye *preamble* kwamba Serikali ya Tanzania haina dini lakini tunakubali kwamba Watanzania wana dini, hebu twende Ibara ya 19(2) ya Katiba hii, naomba kunukuu, inasema hivi:-

“Kazi ya kutangaza dini, kufanya ibada na kueneza dini itakuwa ni huru na jambo la hiari la mtu binafsi na shughuli na uendeshaji wa Jumuiya za dini zitakuwa nje ya shughuli za mamlaka ya nchi”. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna yoyote ile, naamini kwamba, kama kuna ulazima wa kuanzishwa kwa Mahakama hii itakuwa ni kinyume cha Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini hakuna mahali palipozuiwa maana shughuli hizi za kidini hazitakiwi kufanywa katika mfumo rasmi wa Serikali lakini hazikatazwi kufanywa kwenye maeneo ya dini hizo.

Mheshimiwa Spika, tuna makabila hapa mia moja na ishirini katika nchi yetu, tuna dini za aina mbalimbali, ninazoweza kuzikumbuka ni hizi zifuatazo:- Hindu, Shia, Wakristo, Waislam, za Kimila na watu wengine hawajui hizo habari nyingine na wapo wasiokuwa na dini yoyote. Sasa kama kila mmoja atataka ku-*legitimize* mfumo wake wa maamuzi ya migogoro yanayotokana na dini yake au anavyoamini katika mfumo wa nchi yenye dini nyingi na dini zenye madhehebu mengi na nchi yenye makabila mengi kama hii, nadhani kutatokea mgogoro.

Mheshimiwa Spika, kwa ilivyo sasa, kwa Katiba hii ya sasa, napenda niseme kwamba, ni vema mambo haya kwa mujibu wa Katiba hii ambayo imeweza kutusaidia kwa kipindi cha miaka zaidi ya arobaini tukawa na amani na utulivu huu tulionao, nadhani inakidhi mahitaji lakini hakuna anayekatazwa kufanya *dispute settlement* kwa namna anavyoamini kwa mfumo wa dini yake. Suluhu nyingi zinafanywa kwenye Makanisa, Misikiti na watu wanakubaliana nazo kwa kadri ya imani zao na zinaendelea kufanyika, kama kuna ulazima huo, nadhani kwa sasa ni kinyume cha Katiba.

Mheshimiwa Spika, yuko Mwanafalsafa mmoja anaitwa Plato aliwahi kusema ‘*the highest thing in life is happiness*’. Kama tuna furaha ya namna hii katika nchi yetu na tumeweza kuishi kwa amani na utulivu kwa miaka zaidi ya arobaini, hatuna haja ya kudodosa dodosa mambo ambayo tunadhani yanaweza kuondoa mshikamano na umoja wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napata shida hata wakati mwingine tunapoitafsiri Katiba yetu ya nchi. Kama mtu tu anaweza kuitafsiri vile anavyotaka kwa wakati huo basi hiyo sio Katiba. Katiba inakulazimisha ujiheshimu na kufuata kwa kadri ya kile ambacho kimekubaliwa na wote. Kwa maneno mengine Katiba ni kama Msahafu maana yake unautaka, huutaki lazima ukubaliane nao.

Mheshimiwa Spika, nadhani utaniruhusu nijadili Katiba kuhusu suala la Muungano. Ibara ya (1) inasema:-

“Tanzania ni nchi moja na ni Jamhuri ya Muungano”.

Ibara ya (2) inasema:-

“Eneo la Jamhuri ya Muungano ni eneo lote la Tanzania Bara na eneo lote la Tanzania Zanzibar na ni pamoja na sehemu yake ya bahari ambayo Tanzania inapakana nayo”.

Mheshimiwa Spika, wapi imesemwa Zanzibar ni nchi au wapi imesemwa Zanzibar si nchio? (*Makofit*)

SPIKA: Mheshimiwa George, sasa ukisema hivyo, ndiyo unaingia kwenye tatizo. (*Kicheko*)

Unataka kujadili kama Zanzibar ni nchi ama siyo nchi, nimekwishazuia humu katika Bunge kwa sababu suala hilo linafanyiwa kazi. Sasa kama unajadili Katiba, ongea tu misingi ya Katiba bila kuliingiza suala hilo kwa sababu linaturudisha nyuma. Nadhani kuna watu ambaao wanajua kwamba kwa miaka mingi tangu 1964, Zanzibar ina Rais wake, ina Serikali yake, ina Baraza lake, wengine wanaona hiyo inatosha, kwa hiyo, ni nchi. Wengine nao wanasema kwamba kwa kuwa Zanzibar haikupewa uwezo wa Kikatiba wa kuingia Mikataba ya Kimataifa na kwa kuwa mambo ya nje na mambo ya ulinzi yanasisimamiwa kwa utaratibu tofauti, basi tafsiri ya nchi hapo haijatimia lakini kama unavyoyaona yote mawili yanaweza kusemwa bila kukosoana na ndivyo imekuwa kwa miaka yote hii. Kwa hiyo, tusubiri agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu hili, Wanasheria watatutolea taarifa ambayo itamaliza tatizo hili. (*Makofit*)

Mheshimiwa George endelea!

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa mwongozo wako.

Mheshimiwa Spika, sasa niendelee kuzungumzia habari ya Idara ya Mahakama. Kama kuna kitu kipyaa ambacho tunakisubiri kutoka kwa Mwanasheria Mkuu, Jaji Mkuu na *system* nzima ya Mahakama hapa nchini, ni kuona utoaji wa haki katika *level* ya chini unakua na kufikia kiwango ambacho kwa kweli angalau kulingana na hali ya makosa yanayotendeka ya madai na jinai yanazidi kuongezeka kadri watu wanavyozidi kuendelea. Jinsi jamii inavyoendelea ndivyo na kesi zinavyokuwa nyingi kwa sababu *conflict za interest* zinaongezeka.

Mheshimiwa Spika, napenda niseme kwamba, huku chini, ni vizuri Wizara ikajua hali si shwari, kesi nyingi zinaamuliwa na watu ambaao si *legal personnel* na mtu ambaye hajasomea sheria, ni vigumu sana kuitafsiri sheria kulingana na mazingira ya wakati huo au mazingira ya kisheria. Nashauri kwamba, Idara ya Mahakama ijaribu kuangalia sana chini pamoja na matatizo yaliyopo lakini angalau idadi ya kesi nyingi zinazotokea ziweze

kutolewa uamuzi na watu ambao wamesomea sheria. Haya Mabaraza ya Kata ya Ardhi ambayo kwa kweli kwa mujibu wa taratibu hayasimamiwi na Wanasheria yanatoa maamuzi ambayo kwa kweli si maamuzi mazuri na ya kisheria bali ni maamuzi ya ukandamizaji.

Mheshimiwa Spika, nikirudi Kibakwe, niseme kwamba pamoja na kuwa na Tarafa mbili katika Jimbo la Kibakwe lakini tuna Mahakama moja tu inayofanya kazi. Naomba Mheshimiwa Waziri kuitia watu wake wa chini, wajaribu kuona ni namna gani wanawenza kutuongezea Hakimu kwenye Mahakama ya Chipogolo ambayo kwa muda wa karibu mwaka sasa Mahakama hiyo haifanyi kazi na watu wanategemea Mahakama moja tu katika Jimbo lenye Tarafa mbili.

Mheshimiwa Spika, pia nizungumzie ombi langu la muda mrefu la Mahakama ya Chipogolo ambayo inafanyika kwenye nyumba ya kupangisha, ni banda tuseme. Hii ni fedheha, tufike mahali kama ambavyo amesema katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri kwamba, sasa tuje kwenye *D by D* tuwashirikishe wananchi katika ujenzi, nadhani uamuzi huu ni mzuri na napenda kuuunga mkono, ni vizuri kwa kweli tukashirikishwa kwa sababu tukiachia peke yake Idara ya Mahakama, si rahisi kuweza kujenga majengo ya Mahakama katika nchi nzima. Tunajua uwezo wa Serikali na tunauona uwezo wa bajeti yao lakini wakitushirikisha na wao wakatuunga mkono na kuzipitisha fedha hizi katika Halmashauri, inaweza kutusaidia sana kwa kiasi cha kila miaka mitano, tunawenza kufikia hatua ya kujenga Mahakama nne au tano ambazo zinaweza kutusaidia katika Mahakama zile za Mwanzo. Haki kule chini bado ni mgogoro, Wizara hii ipokee changamoto hii na ijaribu kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa George Simbachawene.

Waheshimiwa Wabunge, katika orodha yangu, bado wapo wachangiaji wawili Mheshimiwa Susan Lyimo na Mheshimiwa John Cheyo. Sasa Mheshimiwa Susan Lyimo, sijamwona kwa muda kidogo sasa sina hakika, kwa hiyo, jioni saa kumi na moja, tutaanza na Mheshimiwa John Cheyo, kama Mheshimiwa Susan Lyimo atakuwa tayari, basi atafuatia.

WABUNGE FULANI: Hayupo!

SPIKA: Hayupo?

WABUNGE FULANI: Ndiyo amesafiri.

SPIKA: Ohoo! Kumbe amesafiri, nimepata taarifa, basi tutakuwa na msemajji mmoja na baada ya hapo, nitamwita Mheshimiwa Waziri, kuweza kutumia muda wake wa dakika zisizozidi sitini na hiyo itatuchukua hadi saa kumi na mbili na robo. Kwa hiyo, tutakuwa na muda kama wa saa moja na nusu wa Kamati ya Matumizi.

Niwakumbushe Waheshimiwa kwamba, katika Wizara hii, mafungu ni tisa, tutazikuta sehemu tisa ambazo tutapitia, kwa hiyo si eneo fupi sana, naomba mliangalie vizuri kwa sababu wakati wa kuhoji mafungu tutakwenda kwa mujibu wa mafungu.

Baada ya kusema hayo na muda umekaribia bado dakika mbili tu, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja.

(*Saa 6.58 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nataka kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hoja ya Wizara hii muhimu ambayo kazi yake kubwa ni kuweza kutoa haki katika Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna mengi ambayo yamezungumzwa kabla sijafika mahali ambapo ninaona kumeleta utata katika kujadili hoja hii. Nataka kwanza kabisa kueleza Bunge hili kwamba kwa maoni yangu mwenendo wa Wizara kwa sasa katika sehemu kama tatu hivi unaridhisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ile sheria ambayo imetungwa kwa ajili ya kutoa Mwongozo wa Mashtaka na Upelelezi huu ni mwelekeo mzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wewe ni Mbunge na sidhani kama Urambo ni tofauti sana na Bariadi, kila Mheshimiwa Mbunge anakabiliwa na matatizo ya watu kibao ambaowamewekwa mahabusu, wengine sawa sawa kuna ukweli wa kuwekwa mahabusu, lakini wengi kwa visingizio vidogo vidogo. Ni rahisi sana mtu kwenda mahabusu na zaidi Bariadi. Hili kila ninapozungumza hapa kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na mambo kama hayo huwa ninalisema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi sasa ninavyozungumza nina watu zaidi 10 ambaowananiomba mimi Mheshimiwa Mbunge niwasaidie, wameonewa na kwa misingi mbalimbali pamoja na misingi ya kisiasa. Kwa hiyo, ni mwelekeo mzuri tunapoona Serikali sasa inataka kutenganisha Upelelezi na Mashtaka. Huu ni mwelekeo mzuri na mimi ninaunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwelekeo wa pili ambao nataka kuzungumzia pia ni mwelekeo wa Mahakama kuona kwamba Mahakama na yenyewe inafuata nyayo ambayo tunaizingumza katika Bunge wawe na mfuko wao ulio huru. Mimi ninaona ni mwelekeo mzuri wa kuweza kuimarisha namna ya utawala wa kisheria na mfumo huu unafaa uungwe mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna matatizo lukuki ambayo ni pamoja na kwa mfano sasa Shinyanga tumeambiwa jengo la Mahakama Kuu limemalizika, lakini hakuna *furniture*. Sasa mtu unashangaa itakuwaje ujenge jengo bila kujua kwamba utaweka *furniture*. Hapa

nashauri kwamba Serikali mara moja ihakikishe kwamba inaweka fedha inayotosha kuweza kuweka *furniture* ambazo zinastahili ambapo ni pamoja pia na makazi ya Mahakimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo, sasa hivi wanazungumzia Wanasheria wa Wilayani, lakini mpango wenyewe haujawa kamili bila kujua hao Wanasheria wanaokwenda kwa mfano, kama Bariadi wataishi wapi? Kwa hiyo, bado kuna mambo mengi ya kufanywa katika sehemu hii ya utoaji wa haki *both* Mahakamani na pia Wizarani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kama njia ya utangulizi, sasa nataka kuzungumza jambo ambalo nimemwomba Mheshimiwa Spika, anipe nafasi ya kuweza kuzungumza. (*Makofi*)

Kwanza, pamoja na kuwa Mbunge, mimi ni Mwenyekiti wa Chama cha *United Democratic Party*. Kwa hiyo, ni vizuri kwa jambo ambalo linatoka ndani ya Bunge ambalo linaonekana kuwa ni joto sana, vyama vyote tukapata nafasi ya kuweza kulitolea kauli au ushauri. Sisi katika *UDP* na *UDP* maana yake ni *Upendo Daima Pamoja*. Maana ya *UDP* kwa kiingereza *is harmony for all forever*. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ukishazungumzia *harmony for all forever* maana yake kiingereza unakubali kuna tofauti mbalimbali, kuna tofauti za kidini, kuna tofauti za kikabila, kuna tofauti hata za watu za umbo warefu na wafupi, kuna tofauti ya vyama mbalimbali, lakini nchi ili iweze ikatawalika ni lazima pawepo na upendo maana yake *harmony*, vitu vyote viende kwa pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama kundi moja likivuta zaidi ya uwezo wake matokeo yake ni matatizo ambayo ni pamoja na kutokuwa na amani katika Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nataka kuwaambia Waheshimiwa Wabunge kama kuna kitu ambacho hatupaswi kabisa kukiwekea rehani kwa kitu chochote kile ni amani katika Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukiipoteza amani katika Taifa letu kwa sababu yoyote ile wote tutaangamia na zaidi watoto wetu ambao ndiyo tumewazaa, wajukuu wetu watatulaumu hata tutakapokuwa ndani ya makaburi yetu. Tunahitaji kuwaenzi kabisa waasisi wa nchi hii ambao waliona kitu hiki wasikiweke ndani ya sheria, waliona wasichanganye dini na Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo tumesikia kauli za ajabu tena hii ndiyo inanionyesha jinsi gani jambo hili ambalo lina udini ndani yake linahitaji kuangaliwa kwa makini sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tangu jana na leo nimeona hakuna hata u-*CCM*, hakuna u-*UDP* au u-*CUF*, kuna udini. Mtu anasimama kutetea bila hata kujali Chama chake, bila hata kujali Katiba ya Nchi hii, anatetea dini yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi lazima niseme, mimi ni mkristo na ni mkatoliki na ukinipeleka kwenye dini, mimi nataka kuwaambia nitatetea ukatoliki wangu. Kwa hiyo, sishangai kama ni mtu muislam atatetea dini yake. Lakini hapa tumeletwa siyo kwa misingi ya dini. Mimi siwezi nikasema kama tena kwangu kule kwamba nimepigiwa kura na wakatoliki au nimepigiwa kura na wakristu au na waislam, mimi nimepigiwa kura na Watanzania ambapo dini ni kitu chao binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bunge letu tukikaa hapa nikimwangalia ndugu yangu Mheshimiwa Mohamed Missanga simwangalii hata siku moja ana dini gani namwangalia kama Mohamed Missanga, nikiwaangalia Waheshimiwa Wabunge wengine hapa wake kwa waume siwaangalii wana dini gani na nawaangalia kama Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na sasa hivi watoto wetu ndiyo kabisa wanatuacha hoi, wengi ukimwambia oa mkatoliki mwenzako, anasema baba sioi dini unashukia umeletewa Khadija utafanya nini? Watoto wetu hawaoni dini, sasa tunapokuja hapa tunanyoosheana vidole, tunazungumzia nani, kwa sababu wale waliotuleta hapa hawaoni dini kwamba ndiyo jambo ambalo ni la umuhimu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, lakini tatizo hili ni kubwa, ukiangalia tu unasema ni kubwa kwa sababu watu wenyewe ambao tunafikiria kwamba ndiyo ambao tunawasemea, ukisemea wakristu katika Taifa letu leo unasemea takriban asilimia 44 ya watu wote wa Tanzania ambao ni takriban milioni 17, ukileta hisia za kidini hapa, unaleta hisia za kidini za watu milioni 17, ukiwazungumzia waislam ni sawa sawa na asilimia 37, ukileta hisia za kidini hapa maana yake unazungumzia takriban watu milioni 14. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia tuisahau katika hao kuna watu asilimia 19 ambao wao wana dini zao za kila aina tena kama Wasukuma kule kuna akina Malamala, kuna sijui kitu gani na pia kuna dini ya wachawi. Kuna wengine ili apate ibada tumeambiwa hapa ibada yake ni kutafuta albino. Leo hii uniambie hao akina Malamala na wengine wanaotafuta albino na wenyewe waje Bungeni tuwatungie sheria ambayo itaimarisha ibada yao ya kutafuta albino tutafika wapi? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, tumeambiwa Mahakama ya Kadhi inashughulikia ibada, leo tuna dini ya wachawi na mchawi mwenyewe anasema ili awe mchawi kabisa ambaye ni sawa sawa mojawapo ya habari ni kwamba yeze lazima aue mtoto mchanga mmoja. Leo hapa ni watu milioni 17 wanasema tuwatengeneze sheria Bunge la Tanzania ili waimarishe ibada yao, tunataka kusema kwamba tuimarishe ibada ya watu kwenda kuua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika dini zetu hata pia hatuelewani. Mimi ni mkatoliki, lakini ndani ya wakatoliki kuna wakatoliki wa msimamo mkali, hata katika hao wakristu hatuelewani, ndani yake kuna wasabato, ndani yake kuna wengine sijui *African Church*, na wengine sijui kitu gani na wote tuna mitazamo tofauti tofauti, wengine wakikuta unakunywa pombe ukifa hawakuziki na wenyewe wanataka waimarishiwe dini zao, tutafika wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ninatetea Chama changu Upendo Daima Pamoja yaani *harmony for all forever*. Mkitaka tuunguze nchi hii fuatezi wa mambo ya kidini kutawaka moto na ukweli ni kwamba katika siku mbili hizi ndizo zimeonyesha ndani ya Bunge hili tukiwa wachache kama siyo kupiga *balance* hapa wengine hapa walanza kutukanana, hili jambo siyo lako, kama jambo hilo siyo langu kwa nini mimi unataka nilipe kodi ili niimarishe ibada yako wewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukiendelea hivyo tutapigana humu ndani, tupo wachache hapa, sasa kule nje je, milioni 14 ya waislam, milioni 17 ya watu ambao ni wakristu, milioni karibu 7 ya watu ambao hawana dini, tukiwapelekea hisia ambazo zimeonekana katika Bunge hili tutabaki na nchi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hayati Mwalimu Julius Nyerere hakuwa tu yeye ni mkristo alikuwa ni Baba wa Taifa, aliona upeo wa zaidi ya miaka 100 mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na wale wanaosema walikuwa wakristu wametuleta Katiba hii sijui ni kwa nini wamo katika Bunge hili angalau mkristu ambaye alituletea Katiba hii hakusema nchi hii iwe ya dini A, alisema Serikali haina dini, kila mmoja ana uhuru wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuwe waangalifu, na ninaunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda wa kuchangia kwa maneno haukunitosha naomba niendelee kuchangia kwa maandishi, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, katika mchango huu wa maandishi, mengi nitakayouliza ni maswali ya ufahamu na ya utekelezaji kwa idara mbalimbali. Kwanza ni eneo la Mahakama ya Rufaa na Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Spika, ni lini Mahakama ya Rufaa itajenga ofisi kubwa kabisa yenye hadhi na nafasi ya kutosha? Ofisi zake mpya pale walipo Forodhani hapana hadhi na hapatoshi. Kwa kweli pamebanana. Pili ni kuhusu Mahakimu hawatoshi, hasa *Primary Court Magistrates*. Lini chuo cha Lushoto kitapanuliwa ili kukidhi mahitaji ya mahakimu?

Mheshimiwa Spika, tatu ni kuhusu maslahi ya mahakimu katika mahakama za wilaya na hasa kwenye *Primary Courts* (ni kidogo sana), mishahara midogo, hawana nyumba, wanaishi mitaani na hawana usafiri kwa mfano pikipiki.

Kuhusu maslahi ya Majaji ni mazuri na yanaendelea kuwa mazuri, yaani kuboreshwa lakini je, utendaji wao unalingana na fedha wanazolipwa? Ikiwa maslahi yanaendelea kuboreshwa, *they should show that their performance has increased*,

backlog cases bado nyingi katika *level* ya Majaji. Sasa nini tatizo? Waongeze jitihada kusikiliza kesi ili kuepusha msongamano uliopo magerezani.

Mheshimiwa Spika, ofisi ya AG ni muhimu sana, lakini *staff* ni wachache na hawana uzoefu kwani wale wa awali wameondoka kufuata maslahi mazuri. Ni lini basi ofisi hiyo itaboreshwu kwa yote hayo?

Mheshimiwa Spika, baadhi ya matatizo ya ofisi hiyo ni pamoja na haya yafuatayo, *staff* wachache kwani baadhi wamepata *promotion* kuwa Majaji. Hii ni nzuri, lakini wameendelea kudhoofisha ofisi ya AG. *Training programme* haipo au ni *very poor* hasa katika *Business Negotiation*. Matokeo yake ni mikataba mibovu, maslahi ya *State Attorney* *extremely poor, compared with what the Judiciary Staff are earning*. Bila ya AG *staff* kuwa na maslahi mazuri hata *judiciary* haiwezi kufanya kazi zake. Lazima maslahi ya pande zote mbili pawe na uwiano.

Mheshimiwa Spika, mwisho ninampa Waziri pole kwa kazi ngumu sana lakini nzuri mno. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga hoja mkono tena mia kwa mia.

MHE. NURU A. BAFADHILi: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha nichangie hotuba iliyopo mbele yetu kwa maandishi.

Naomba nichangie kuhusu kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi nchini. Mahakama kadhaa zimeanzishwa kama Mahakama ya Ardhi, Mahakama ya Biashara na Mahakama ya Kazi. Waziri atupe maelezo ni vikwazo vipi vinavyosababisha kutungwa kwa sheria ya Mahakama ya Kadhi?

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Kadhi ndicho chombo kitakachosaidia katika masuala ya ndoa, mirathi, talaka katika kesi zinazowahusu waislamu. Sheria ya dini ya kiislam, mtoto wa nje ya ndoa hapaswi kupewa urithi. Itakapoanzishwa Mahakama ya Kadhi itasaidia sana hasa katika suala zima la mirathi kwa watoto/ndugu/mke/mume wa marehemu na uwiano wa mgao unaostahili kwa kila mmoja.

Mheshimiwa Spika, tunamuomba waziri hili alitilie mkazo ili sheria iandaliwe ya uanzishaji wa Mahakama ya Kadhi, ahadi ni deni. Hii ya Mahakama ya Kadhi ilielezwa kipindi cha kampeni za CCM na imo katika Ilani ya Chama Tawala. Je, kigugumizi ni cha nini?

Mheshimiwa Spika, kuhusu chaguzi za Serikali za mitaa, chaguzi hizi husimamiwa na TAMISEMI, kwa kweli hakuna haki inayotendeka. Hii inatokana na watendaji wote hupokea amri toka kwa Wakurugenzi wao. Wakurugenzi hao nao pia wanakuwa wanataka kujiiamarisha kwa hiyo, wanaelemea kwa chama kinachotawala. Tunaiomba Serikali chaguzi hizi zisimamiwe na Tume ya Uchaguzi ya Taifa. Tufuateni Katiba inayotuongoza katika misingi ya demokrasia na utawala wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ufisadi kwa baadhi ya viongozi, kuna matumkio kadhaa ya ufisadi kwa baadhi ya viongozi. Swali la kumuuliza Mheshimiwa Waziri ni kuwa je, hii Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inafanya nini hadi kufikia viongozi kuwa mafisadi kiasi cha kulitia aibu Taifa letu?

Je, viongozi hawa mafisadi wakati viongozi wanaorodhesha mali zao, je, nao waliziorodhesha mali zao? Je, viongozi hao Serikali inawashughulikia vipi? Viongozi kama hawa ni hasara na aibu kwa Taifa letu na je, Serikali inatuambia nini kuhusu mali kadhaa walizohodhi mafisadi hawa?

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuchangia kuhusu mauaji yanayoendelea ya albino, tunaomba Waziri atuambie ni kesi ngapi za mauaji ya albino zimefunguliwa na watuhumiwa wangapi wamefikishwa mahakamani kwa tuhuma za kukutwa na viungo hivyo vyta albino?

Kwa kweli kitendo cha uuaji wa albino kwa imani za kichawi ni kibaya sana. Albino hawa hawakuomba kuwa hivyo ila ni rehema za Mwenyezi Mungu pia nao katika uzazi wao sio kuwa nao wataendelea kuzaa albino laa, watazaa watoto wa kawaida. Kwa hiyo, hawa wauaji wa albino wanapunguza kuzaliana kwa binadamu.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Serikali ifanye juhud zaidi kuwasaka hawa wanaofanya vitendo hivyo na hata akipatikana mmoja akapewa adhabu kali itakuwa fundisho kwa wale wengine.

Mheshimiwa Spika, huenda kuna wananchi wanawajua hawa wauaji wa albino lakini wanaogopa tu kuwataja wahusika. Wananchi wahamasishwe kusaidia kuwafichua wale wote wenye kujihusisha na vitendo hivi vibaya vyta kinyama vinavyolitia Taifa letu dosari.

MHE. JUMA SAID OMAR: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na afya na kuweza kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge, Viongozi wa Kambi ya Upinzani kwa kutuongoza vyema. Pia viongozi wa chama changu pamoja na wananchi wote wa Jimbo langu la Mtambwe kwa ushirikiano wao kwangu.

Mheshimiwa Spika, wakati umefika sasa kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi. Jambo hili limekuwa likiombwa kwa muda mrefu lakini hadi sasa bado Serikali ina kigugumizi juu ya ombi hili. Je, Serikali haioni kwamba hii ni haki ya waislam katika kusimamia mambo yanayohusu dini yao ikiwa ni pamoja na ndoa, talaka, mirathi, haki za yatima na kadhalika? Je, Serikali haioni kwamba kuchelewesha kupatikana kwa Mahakama hii ya Kadhi kunaleta hisia mbaya kwa waislamu jambo ambalo linaweza kuleta mtafaruku hapo baadaye?

Mheshimiwa Spika, wakati umefika sasa kuwa na Katiba mpya itakayoendana na wakati hasa ikizingatiwa kwamba nchi yetu imeingia katika mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Pia kuna madai yaliyojitokeza kama vile Zanzibar ni nchi au si nchi, suala la Rais wa Zanzibar kutokuwa Makamu wa Rais pamoja na kero mbalimbali za Muungano.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa rushwa ni adui wa haki na kwa kuwa Serikali imeahidi kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa kwa kuwachukulia hatua za kisheria, kiutawala na kinidhamu wale wote watakaobainika kuhusika na vitendo vyta rushwa, je, hadi sasa ni rushwa ngapi kubwa kubwa ambazo zimechukuliwa hatua?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utawala bora ni utawala unaofuata sheria na kwa kuwa kuna sheria mbalimbali zinazovunjwa na Serikali haichukui hatua, je, Serikali haioni kwamba hali hii inadhoofisha utawala bora? Kwa mfano mauaji ya albino pamoja na vikongwe kwa imani za uchawi na tamaa za kujipatia utajiri.

Mheshimiwa Spika, dira na malengo ya Wizara kuwa na mahakama nyingi ni jambo zuri ili kuondoa mrundikano wa wafungwa na mahabusu katika magereza. Lakini Serikali imejiandaa viperi ili kuhakikisha kwamba ina mahakimu na watumishi mbalimbali wa mahakama hizo ambaa watatosheleza mahitaji?

Mheshimiwa Spika, Serikali iachane na mikataba mibovu ambayo inaathiri raslimali za nchi yetu pamoja na kuathiri uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, kuwa na sheria ni jambo moja lakini kutekelezwa kwa sheria hizo ni jambo lingine na muhimu zaidi, kwani kutotekelawa kwa sheria ni kuvunja kwa haki za wananchi wengi. Ahsante.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi kumpongeza Mheshimiwa Waziri na wafanyakazi wote wa Wizara kwa taarifa hii katika Bunge lako Tukufu na kwa kazi muhimu Wizara iliyonayo ya kuhifadhi amani katika kuhakikisha haki inatendeka nchini. Naomba kutolea maoni jambo lifuatalo.

Mheshimiwa Spika, kwanza Mahakama ya Kadhi, Serikali inafanya vyema kulifanya utafiti jambo hili kwani kama jambo hili halitatatuliwa kwa makini litaleta utovu wa amani katika Taifa letu kwa misingi ya kidini.

Mheshimiwa Spika, amani imetoweke katika nchi nyingi kwa misingi ya imani. Msimamo wa Serikali, jambo hili lazima kutafakariwa kwa makini ili kulinda amani ya nchi ambayo ina thamani na ni msingi wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, wengi wetu tunaheshimu sana uhuru wa wananchi kuabudu na kufanya ibada. Utaratibu wa kuabudu na kufanya ibada unafanywa kwa utaratibu wa dhehebu linaloeneza hiyo dini na pamoja na maamuzi binafsi namna ya kugharamia ibada na dini inayohusika. Katika historia ya nchi hakuna ulazima wa kisheria kugharamia kuabudu na kufanya ibada.

Aidha, ieleweke Watanzania wanaabudu na kufanya ibada za aina nyingi ambazo ni pamoja na ibada za kimila. Nathubutu kusema waumini wa dini za Kikristo, *Islam*, Hindu na kadhalika ni wachache kama ukilinganisha na watu wenye dini nilizotaja hapo juu. Swali hapa kwa kuwa kinachoombwa hapa siyo kuanzishwa Mahakama ya dini “Kadhi” kwani kama waislam wakitaka kuanzisha kidini kama dini zingine Waislam wanawenza kuanzisha. Kinachoombwa hapa ni sheria itungwe ili Serikali ilipie utaratibu wa mahakama hiyo.

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini mimi nisiye muumini wa dini hiyo nishurutishwe kisheria kuwalipia waislamu waimarishe ibada na imani yao lakini Serikali isilipie wakristo, wasukuma, wahaya, wamasai na kadhalika ambaa ni wengi kuliko waislamu wote nchini? Kinachotafutwa na waislamu wanaotetea jambo hili ni kuifanya Serikali ilipie, basi kama tatizo ni fedha tulete Muswada wa kuchangia fedha kwa madhehebu yote ya dini kama njia ya kuhifadhi maadili mema katika kila dini pamoja na wapagani (*non-believers*). Najua kwa hali halisi jambo hili litakuwa gumu sana. Tuiache Serikali ihudumie mwili na dini zihudumie roho.

Mheshimiwa Spika, hata Ilani ya CCM inasema italitafutia ufumbuzi. Ufumbuzi haina maana kwamba Serikali italeta sheria. Natahadharisha kwa hali halisi jambo hili halitajenga umoja na amani tulioiridhiwa waasisi wa Taifa. Chonde chonde jambo hili lisitungiwe sheria. Naunga mkono hoja.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Spika, pendekezo la kuwa na Katiba mpya, baada ya marekebisho 14 yaliyofanya katika Katiba yetu bado hayatoshelezi, hivyo nashauri Serikali ione umuhimu wa Katiba mpya. Kwa kuwa hakuna aliye juu ya Katiba wote tunaongozwa na Katiba ambayo ndiyo sheria mama, basi ili kutimiza hilo basi Katiba itakapobadilishwa Rais apunguziwe madaraka makubwa yanayofanya dhana ya utawala bora kutoonekana vizuri mfano Rais apewe madaraka ya kuteua watu wengi ambaa hawaletwi kuthibitishwa Bungeni hakuna wa kuhoji maana wao wanawajibika kwa Rais tu. Mfano Mkurugenzi wa TAKUKURU, Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, Mabalozi na wengine wengi.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Kadhi ni maalum kwa ajili ya kesi za waislam kufuatana na mambo yaliyondani ya Quran Tukufu na inashughulikia masuala ya ndoa, mirathi na talaka. Hivyo naamini Mahakama ya Kadhi haitaathiri wala haitaligawa Taifa kwani siku zote tangu tu pale uhuru tumeishi vizuri bila dini kutugawa na nchi yetu inazo dini nyingi na kuu zikiwa dini ya Kikristo na Kiislam.

Hivyo naishawishi Serikali ione umuhimu wa Mahakama hiyo. Kwani kwa sasa kesi hizo zimefanyika katika mfumo wa kusikilizwa mashauri hayo ya ndoa, mirathi, matunzo ya watoto na talaka katika jumuiya ya Bakwata, hivyo si vibaya kukawa na chombo maalum ambacho ni Mahakama ya Kadhi. Tukumbuke Serikali haina dini lakini wananchi tuna dini zetu.

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa umma, chini ya kifungu namba 18 cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma (*The Public Leadership*

Code of Ethics Act Cap. 398), jukumu lake ni kufanya uchunguzi juu ya ukiukwaji wa maadili ya viongozi. Tatizo chombo hiki hakina meno ya kutosha, kwanza hakijawezeshwa vizuri na hakipewi nafasi kufanya kazi yake vizuri kwa ufanisi kwani hakina neno.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na matukio yaliyothibitika ya ufisadi dhidi ya viongozi wakuu hapa nchini lakini Sekretarieti ambao ni wasimamizi wa sheria hii hawaisimamii ipasavyo. Serikali itueleze Sekretarieti inatekeleza vipi usimamizi wa sheria hii?

Kuhusu ucheleweshwaji wa marekebisho ya sheria zinazohusu watoto, wanawake na zote zinazolalamikiwa (Sheria ya Ndoa) mfano Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 inayoruhusu mtoto kuolewa kwa idhini ya wazazi wake na ile ya matunzo ya mtoto kupewa shilingi 100/= ikiwa wazazi wametengana, hii imepitwa na wakati shilingi 100/= haitoshi hata nauli ya daladala. Inashangaza Serikali kusema bado ipo kwenye mchakato kila unapouliza suala hili, je, marekebisho ya sheria hizo yataletwa lini Bungeni?

Mheshimiwa Spika, kutokana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri, hajatuambia ni magari aina gani yamegharimiwa kiasi gani. Pia magari yananunuliwa wakati Mahakama nydingi za Mwanzo hazina Mahakimu na mazingira ya kazi zao ni magumu, hawana nyumba na vile vile bado utaratibu wa kuandika/*Hansard* za Mahakama si wa kiteknolojia ya kisasa, ingekuwa bora vitu hivyo vingeboreshwa kwanza kuliko kukimbilia kununua magari hayo na yakatumika ya zamani baadaye yakanunuliwa mapya.

Vile vile maslahi ya Majaji bado ni duni, yangeboreshwa kwanza kuliko kununua magari. Vile vile Serikali haikusema ugawaji wa magari hayo ukoje yanagaiwa kimkoa au yanagawiwaje?

Mwisho, napongeza Wizara hii kwa kujali uwiano wa kijinsia, angalau namba ya wanawake ni kubwa ambao wameshika nafasi za juu wakiwemo Majaji na Makamishna.

MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI: Mheshimiwa Spika, binafsi naomba nimpongeze sana Waziri na Wizara kwa ujumla kwa hotuba yao ambayo kwa hakika ni nzuri sana na inazingatia kwa asilimia mia moja utekelezaji wa Ilani na malengo ya MKUKUTA kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa sana na namna hotuba iliyochambua matatizo yanayowagusa wananchi na kwa hakika matatizo haya yamekuwa sugu na kuwakera sana wananchi.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili la Ofisi za Kanda za Mahakama Kuu kujengwa katika kila Mkoa, hakika hili litatatua matatizo mengi sana yaliyopo kwenye mikoa yetu ambayo wananchi hugharamia pesa nyingi sana kufuata huduma hiyo kwa mfano, Mara

hufuata huduma hiyo Mwanza. Hii itasaidia pia usikilizwaji wa haraka wa kesi na kupunguza msongamano uliopo kwa sasa pale Mwanza.

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa sana pia na urekebishwaji wa Sheria za Mirathi na Ndoa. Ni ukweli usiofichika kwamba Sheria hizi za Ndoa na Mirathi huwagusa sana wanawake kwani kumekuwepo na vitendo vingi vya dhuluma, uonevu na unyanyasaji wa wanawake utokanao na sheria hizi mbili; hivyo ni matumaini yangu kwamba sheria hizi katika marekebisho yake zitasaidia sana katika kuwaokoa wanawake na unyanyasaji huu.

Mheshimiwa Spika, nimeguswa sana pia na suala la Sheria ya *DNA*. Naipongeza sana Wizara kwa kuliona hili kwani limekuwa pia ni tatizo kubwa sana katika jamii yetu na vile vile jambo hili huwagusa sana wanawake ambao huzalishwa watoto na mara nyingi watoto hao hukataliwa na baba zao hivyo sheria hii ya *DNA* itakuwa ni mkombozi mkubwa wa migogoro ya aina hii.

Mheshimiwa Spika, bado tuna tatizo kubwa sana la ucheleweshwaji wa kesi katika Mahakama zetu na hivyo kupelekeea msongamano mkubwa sana wa kesi katika Mahakama zetu, niiombe Wizara ijaribu kulitizama jambo hili kwa makini na kulitafutia ufumbuzi kwani kwa sasa hii ndiyo kero kubwa sana katika Mahakama zetu. Mfano kesi za jinai kuchukua hadi miaka mitano, hii ni kumdhalilisha mshitakiwa na familia yake kwa ujumla kwa kuwaweka katika *tension* muda mrefu ambapo huwaathiri washitakiwa na familia kisaikolojia.

Mheshimiwa Spika, mwisho narudia tena kuipongeza Wizara kwa hotuba nzuri ambayo inastahili kuwa mfano wa kuigwa na Wizara nyingine kwani imizingatia Ilani na malengo yote ya MKUKUTA.

Mheshimiwa Spika, ninachokiomba ni utekelezaji wa asilimia zote wa kilichoandikwa katika hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Jaji Mkuu, Majaji, Mahakimu na viongozi kwa kazi nzuri inayofanyika katika ujenzi wa nchi yetu. Hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, wakati nikichangia katika Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma, niliomba Wizara ya Katiba na Sheria iangalie uwezekano wa kuwanunulia/kuwakopesha/kuwadhamini Mahakimu hasa wa Mahakama ya Mwanzo vyombo vya usafiri ili kuwasaidia kuwapunguzia adha Mahakimu kutokana na kusafiri umbali mrefu toka kituo kimoja hadi kingine. Nilitoa mfano wa hakimu aliyeleo katika Mahakama ya Nyambiti anayehudumia Mahakama za Nyamikoma, Ngulla na Mahakama ya Koromije iliyoko Wilaya ya Misungwi. Maeneo niliyotaja kama hujayatembelea, au kama huyajui unaweza ukafikiri ni maeneo yanayopakana.

Mheshimiwa Spika, umbali wa kutoka Nyambiti (Mahakamani) kwenda Mahakama ya Nyamikoma ni zaidi ya kilometra 19 hutumia usafiri wa baiskeli iwe kiangazi iwe masika. Umbali kutoka Nyambiti (ambapo ndipo anapoishi) kwenda Mahakama ya Ngulla ni zaidi ya kilometra 15 hutumia usafiri wa baiskeli iwe masika au kiangazi. Umbali wa kutoka Nyambiti (Wilaya ya Kwimba) kwenda Mahakama ya Koromije (Wilaya ya Misungwi) ni zaidi ya kilometra 25 anahudumia Wilaya mbili za Kwimba na Misungwi, napo hutumia baiskeli iwe masika au kiangazi. Ikumbukwe hakimu huyo pamoja na mambo mengine ni mwanamke, naomba nimpongeze sana kwa kujituma na kutekeleza majukumu ya kusikiliza kesi katika maeneo hayo bila kuchoka.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara iangalie, itafakari ione utaratibu wa kuwasaidia usafiri Mahakimu hasa wale walioko katika maedneo hasa ya vijiji. Suala la hakimu huyu, nimeshaliwasilisha kwa Mheshimiwa Waziri hivyo analijua. Ningependa kupatiwa majibu wakati anajumuisha hotoba yake.

Mheshimiwa Spika, pia yapo malalamiko katika Wilaya ya Kwimba na Misungwi Mahakimu wamekosa pesa za usafiri (pikipiki) wakati pikipiki hizo hazijafika. Naomba majibu.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Mathias Chikawe, Mwanasheria Mkuu Mheshimiwa Johnson Mwanyika, Katibu Mkuu na watendaji wote walioshiriki katika kuandaajaa Bajeti hii nzuri iliyoainisha vyema utekelezaji wake pamoja na vipaumbele vyake.

Mheshimiwa Spika, vile vile nitakuwa mchoyo wa shukrani endapo nitashindwa kumpongeza Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, alipokuwa Waziri wa Sheria na Katiba alijitahidi kuweka misingi mizuri pamoja na watendaji wake kazi ambayo imemsaidia Mheshimiwa Mathias Chikawe kuona mzigo mwepesi. Nawaombea Mwenyezi Mungu awape nguvu, afya na mshikamano ili waweze kutekeleza vyema matarajio yao.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Mahakama Kuu mkoani Singida, naipongeza sana Serikali kwa kutekeleza maombi ya Wabunge kwa niaba ya wananchi wao, mfano niliomba Mahakama Kuu ijengwe Singida kuititia swali langu. Kwa vile kesi za mauaji ni nyingi Serikali ilikubali na kutoa ahadi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kazi za maendeleo zinashirikisha nguvu za wananchi na sasa wako tayari kuanza kujenga Mahakama Kuu baada ya kupata kiwanja na kukamilisha taratibu za umiliki, napenda kujua Serikali kuititia Bajeti hii imetenga shilingi za Kitanzania kiasi gani na ujenzi huo utaanza lini?

Mheshimiwa Spika, kukua kwa miji, Manispaa na majiji ni pamoja na kujenga wale waliopata viwanja. Naiomba sana Wizara pamoja na kutegemea Bajeti hii pia wawe na kazi ya ziada ya kutafuta wahisani ili kutekeleza malengo yao. Nategemea sana kupata ufanuzi wenye kutupa matumaini wananchi wa Singida kwani wananchi wengi

wanakosa haki zao kwa kushindwa gharama za kusafiri kwenda Dodoma kuhudhuria kesi.

Kuhusu posho za Wazee wa Mahakama, naamini ni utaratibu mzuri tu wa Serikali kuona umuhimu wa Mahakama zetu kuwepo Wazee wa Mahakama. Kwa taarifa ambazo ninazo Wazee wa Mahakama hupata shilingi 1500/= kwa kesi moja tena hadi imalizike hata kama itachukua miezi mitano ataendelea kuhudhuria hadi iishe hiyo kesi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kwa lengo la kupambana na rushwa kuongeza kiwango hiki angalu kufikia shilingi za Kitanzania 3,000/= au 5,000=/. Endapo Serikali iliridhia ombi hili itasaidia sana kuwapunguzia vishawishi Wazee wa Mahakama kupokea rushwa kwa wenge kesi Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, mishahara ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo hadi Mkoa, naipongeza sana Serikali kwa kuona umuhimu wa kuwa na Mahakimu wenye taaluma ya kutosha kwani hata hakimu wa Mahakama ya Mwanzo wana *diploma*.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kutazama upya mishahara yao kwani wanaoanza huanza na kima cha chini suala ambalo linawafanya wapate kigezo cha kushawishika kupokea rushwa. Naiomba sana Serikali kuwaongeza Mahakimu mishahara yao pamoja na kupata marupurupu yao kwa wakati muafaka.

Kuhusu Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwenda Mikoani, naomba kukiri kuwa Tume hii ni muafaka kabisa kuwepo na majukumu yake ni makubwa sana kwa Taifa hili la Tanzania ukizingatia kuwa wananchi walio wengi hawajui haki zao. Hivyo basi naiomba Serikali kuiwezesha Tume hii ili iweze kwenda mikoani kutoa elimu kwa wadau mbalimbali pamoja na kutoa semina mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba Watanzania wengi wananyanyasika na kupoteza haki zao kwa vile tu hawajui haki zao. Mfano watumishi wengi hunyimwa haki zao na waajiri wao nao hushindwa kuidai na wanawake wengi hunyanyaswa na wanaume zao mfano Morogoro mwanamke alifumania mume wake na shemiji yake lakini mwanamke huyu aliambulia kuchomwa kisu. Hata wanaume wamo wanaonyanyaswa na wake zao na wako wanatumia utajiri wao kuonea wanyonge wasiokuwa na uwezo. Naomba Tume hii sasa isiwe ya Dar es Salaam iende mikoani kutoa elimu.

Mheshimiwa Spika, nategemea Mheshimiwa Waziri atatoa maelezo wakati anafanya majumuisho.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tume ya Kurekebisha Sheria, napenda kuitambua Tume hii, bali napenda sana nielezwe sababu za msingi kwa nini sheria ambazo ni muhimu sana mfano sheria ya matunzo ya watoto ya mwaka 1948 na Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 zinachelewa kuleta hapa Bungeni. Ukweli ni kwamba Tume inafanya kazi taratibu sana tunaomba tupewe sababu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ucheleweshaji wa nakala za hukumu, nachukua fursa hii kuifahamisha Serikali kuwa bado kuna tatizo sugu la upatikanaji wa nakala za hukumu kwa walengwa. Baada ya kufuatilia nimegundua kuwa kuna tatizo la upungufu wa makarani na ukosefu wa miundombinu inayotumika imepitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kuongeza idadi ya makarani ili kufanya kazi yao kikamilifu vile vile kwa kuwa teknolojia inayotumika kupiga chapa, imepitwa na wakati naishauri Serikali kutumia teknolojia mpya kwa maana ya kompyuta ili waweze kutoa nakala za hukumu kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, nyumba za Mahakimu wanaostahili napenda kuikumbusha Serikali juu ya kazi ngumu na ya hatari walionayo Mahakimu ingawa wanaishi mtaani kwa kukosa nyumba. Kwa kuwa ni haki ya hakimu ambaye anastahili kupata nyumba basi ni bora Serikali itekeleze wajibu wake kuwapa Mahakimu nyumba na kuwalipa kodi zake. Hii itasadidua kutokujichanganya mtaani na kuwapunguzia mzigo. Nategemea maelezo ya Waziri wakati wa majumuisho.

Mheshimiwa Spika, Mahakimu kukopeshwa usafiri (pikipiki), ukweli upo pale pale kuwa mtumishi anapata usafiri hupata unafuu wa maisha na kazi yake huiona nyepesi. Hivyo naiomba Serikali kuwakopesha Mahakimu pikipiki hasa wa Mahakama za Mwanzo hadi Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kelele kwenye kumbi za starehe, napenda kuikumbusha Serikali kero inayowapata Watanzania kuitia kumbi za starehe hasa miji mikubwa mfano Dar es Salaam wanamuziki wamekuwa wakipiga muziki bila ya kujali kuwa majengo hayo yapo ndani ya makazi, hospitali, shule na kadhalika na kuathiri wagonjwa, wanafunzi usikivu darasani. Naomba Serikali ikazie nyumba hizi kuwa na *sound proof*.

MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na taasisi za sheria kwa hotuba nzuri. Naomba tamko la Serikali katika maeneo yafuatayo.

Kwanza ni kuhusu marekebisho ya Katiba na Sheria kukidhi malengo ya Ilani kufikia uwiano wa kijinisa wa asilimia hamsini kwa hamsini uchaguzi wa Serikali za mitaa kwa mwaka 2009 na Serikali Kuu kwa mwaka 2010. Je, maandalizi ya marekebisho ya mipaka ya kata na majimbo pamoja na marekebisho ya Katiba na Sheria yamefikia hatua gani na ni lini Miswada hiyo itawasilishwa Bungeni?

Mheshimiwa Spika, pili, Mahakama za Mwanzo kama muhimili muhimu wa utawala bora na maisha bora ya kila Mtanzania, je, lengo la Serikali ni kuwa na Mahakama kila tarafa au kata? Je, lengo ni lipi na litafikiwa lini? Tatu, Mabaraza ya Kata. Hivi ni vyombo vya kutoa haki je, kuna mikakati gani ya kuhakikisha kwamba Mwenyekiti, Katibu na wajumbe wa Mabaraza wana uelewa au wanapatiwa mafunzo ya Sheria?

Mheshimiwa Spika, kuhusu kukiongezea uwezo wa kuendesha kozi nyingi na kuchukua wanafunzi wengi Chuo cha Mahakama (*IJA*) Lushoto. Kuwepo kwa

Mahakama za Mwanzo na za Wilaya na Mahakimu wa kutosha nchi nzima ni kigezo muhimu cha utawala bora. Chuo cha Mahakama Lushoto (*IJA*), ni taasisi muhumu sana inayofundisha na kuandaa Mahakimu wanaohitajika sana pote nchini lakini chuo kinakabiliwa na uhaba wa mabweni kufikia uwezo wa wanafunzi 1,000. Chuo kiliomba mkopo wa shilingi bilioni 6.1 kutoka shirika la *GEPF* na kukubaliwa mkopo wa shilingi bilioni 3.5 kwa kuanzia kujenga mabweni manne, kinachosubiriwa ili mkopo utolewe na ujenzi uanze ni dhamana ya Wizara ya fedha.

Mheshimiwa Spika, mkopo utalipwa ndani ya miaka kumi, hauna *risk* kwa vile chuo kina uwezo wa uhakika wa kurejesha mkopo huo kutokana na makusanyo ya ada za wanafunzi. Namwomba Mheshimiwa Waziri na au Waziri wa Fedha alihakikishie Bunge kwamba *guarantee* hiyo itatolewa mwaka huu wa 2008 kuwezesha ujenzi wa mabweni uanze.

Kwa heri mikataba ya umma mibovu. Mwisho naiomba ofisi ya *Attorney General* na watendaji wote wa umma wajidhatiti ili Tanzania iwe nchi ya mikataba safi inayozingatia maslahi ya Taifa kwa ukamilifu kabisa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, wakati sheria ya kuanzishwa *Law School* iliyokuwa inajadiliwa ilizuka hoja ya nani hasa atakuwa na jukumu la kuwalipia wanafunzi husika, hasa ikizingatiwa kwamba wengi wanatoka *direct from Universities* hivyo hawana kipato cha kujilipia, majibu yaliyotolewa yalionyesha uwezekano wa *Loan Board* kuendelea kuwakopesha wanafunzi husika.

Mheshmimiwa Spika, ningependa kufahamu mchakato huo umefikia wapi na nani atakayekuwa na jukumu la kutoa mikopo kwa wanafunzi hawa kuwawezesha kukamilisha shahada yao ya sheria?

Mheshimiwa Spika, kuhusu maslahi ya Majaji na Mahakimu mwaka jana katika uchangiaji wa hotuba ya Wizara ya Sheria na Katiba kulikuwa na malalamiko juu ya maslahi finyu ya Majaji, Mahakimu na watumishi wengine wa Mahakama hali ambayo kwa kiasi kikubwa inatoa ushawishi wa kupokea rushwa. Ningependa kufahamu ni kwa kiasi gani maslahi ya Majaji na Mahakimu yameongezwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Human Rights Commission*, taarifa zilizopo zinaonyesha kwamba *Commission* ya Haki za Binadamu inakwama kufanya kazi kutokana na kukosa meno. Kuna mkakati wa kufanya mabadiliko ya sheria, ili kuiwezesha Tume hii kutekeleza majukumu yake.

MHE. SIJAPATA F. NKYAMBA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa niwapongeze viongozi wote wa Wizara hii pamoja na Waziri na Naibu wake, baada ya kusema hayo naunga kwanza hoja mkono asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kuna wastaafu katika Wizara hii ya Sheria ambao walishatuma maombi yao ya kustaafu lakini hadi sasa hivi hawajapata mafao yao.

Mheshimiwa Spika, kuna mstaaafu mmoja jina lake ni Aloyce V. Toyi aliyejkuwa akifanya kazi Kigoma Vijijini na mpaka sasa amestaafu tangu mwaka 1998 huu ni mwaka wa 11 bado hajalipwa mafao yake na sasa hivi ni mzee kabisa hata nauli ya kuja Dar es Salaam kufuata mafao hayo hana uwezo wa kufika, baada ya hapo mwaka 2007 nilichukua jukumu la kuleta vyeti vyake vya mafao ambayo nilimkabidhi Mheshimiwa Dr. Mary Nagu mpaka anahama Wizara bado hakuna jibu lolote, je, wengine wanaokufa bila kupata mafao yao kwa ajili ya kucheleweshwa.

Mheshimiwa Spika, ni lini huyu Mzee atalipwa mafao yake?

MHE. KHERI KHATIB AMEIR: Mheshimiwa Spika, kati ya mihimili mitatu muhimu ndio hii mhimiili mmoja muhimu sana unashikiliwa na Wizara hii yaani Mahakama. Mhimili huu ndio kila kitu nchini kwenda utawala bora, kusimama kwa Serikali na kuendesha mambo yake sawa sawa tunategemea sana Mahakama utulivu wa wananchi na nchi yenye ni uadilifu wa Mahakama kwa kutekeleza sheria za nchi ipasavyo. Nchi huingia kwenye vurugu, mauaji, mtafaruku wa chuki kama sheria zinazotungwa za Bunge wahusika Mahakama kama hawazitekelezi.

Kwa hiyo, Bunge halisimami kama mhimiili kwa niaba ya watu, kama Mahakama na Majaji wakiwa wanazipinda sheria za nchi na kuzichezea Serikali kwa maana ya mhimiili mkubwa kwa nafasi yake haitasimama kama Mahakama inazembea kuwajibika, ila kwa vile *transalation* ya sheria zenye wao ndio wanaozijua na kuzitekeleza na kutowajibika kwao ni vurugu katika nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa lugha nyepesi Mahakama ni kila kitu ni Bunge, ni Serikali na ndio utulivu kwenye nchi yenye utawala bora na wa haki. Tumeziomba Mahakama na Majaji wawe waadilifu, uwezo waliopewa uwe dhamana kubwa kwao binafsi, duniani na akhera tuendako.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Kadhi, tunajua suala hili linaleta msuguano mkubwa kwenye nchi na hasa kutokana na *translation* ya Sheria za Kiislam, mtazamo wa labda watu wakatwe mikono (wezi), walevi kupigwa hadharani, wazinifu wapigwe mawe, hiyo sio dhana sahihi kwa nchi ya Tanzania, na wala hapatakuwa na utawala wa kisheria kwa maana ya uislam, katika hili kuna mambo mahususi ambayo Mahakama hizo zitakuwa zinayashughulikia mfano, Sheria za Ndoa za Kiislam, mirathi, haki za watoto, mke/mume na kadhalika na kwa wale ambao hawataki wataendelea kukuhumiwa na Mahakama wanazozitaka. Lakini kwa waislamu kuachwa (talaka) ni lazima Kadhi ahushishwe na wala sio Mahakama nytingine. Hivi sasa linafanywa mitaani na masheikh kufuata Sheria hizi, lakini haziko Kikatiba na wakati mwingine hao hao masheikh huwa wanakosea. Mfano Zanzibar ilivyo au Kenya na kadhalika, kama wahusika hawakukubaliana na hukumu kesi hiyo hupelekwa Mahakama Kuu.

Kuhusu haki za mirathi kwa waislam si sheria iliyotungwa ni sheria iliyomo kwenye kitabu kitukufu cha *Quran* na si vinginevyo, hukumu yoyote inayotolewa dhidi ya aya za *Quran* ni makosa na dhima wanachukua Mahakama na Serikali kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, kuhusu Mahakama ya Katiba, kuna umuhimu wa Serikali kutamka wazi namna bora ya kushughulikia matatizo ya Muungano kwa kuyapeleka kwenye Mahakama ya Katiba, hivyo nashauri kuwa Mahakama hii iwe ya kudumu hivyo Waziri alete Sheria mwezi wa Oktoba, 2008 ya kuundwa kwa Mahakama ya Katiba, kwani katika kipindi cha miaka 46 sasa matatizo ya mfumo wa Muungano yanashindwa kutatauliwa pamoja na Mahakama ya Rufaa kushauri wanasiwa wakae wamalize matatizo haya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mahakama ya Kadhi, mimi sitaki niamini kuwa CCM ilipoweka katika muongozo wake suala la kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi ilikuwa ni kuwalaghai waumini wa Kiislam, sielewi kwa nini Serikali ya CCM nayo inapata kigugumizi katika uanzishaji wa Mahakama hii. Ni vyema Waziri akatueleza je, CCM haikuwa na dhamira ya kweli juu ya uanzishaji wa Mahakama hii?

Mheshimiwa Spika, suala la Watanzania kuhukumiwa nje ya nchi, baada ya Septemba 11 Watanzania wengi waliofuhumiwa kwa ugaidi wamepelekwa Marekani kuhukumiwa, wakati Tanzania tunazo sheria na Mahakama kukabiliana na uhalifu huu. Waziri atueleze kwa nini raia wetu wakahukumiwe nje ya nchi yetu? Je, Wamarekani wakikosa Marekani wanaweza kuleta Tanzania?

Mheshimiwa Spika, kuhusu msongamano wa kesi, katika Jedwali Na. 1(d) Mahakama ya Wilaya/mkazi inaongezeka, wakati pamoja na maboresho ya Mahakama Waziri atueleze je, haya maboresho yanasaadid au tatizo ni nini?

Aidha, Mahakama kuu ni 83% wakati Majaji wa Mahakama Kuu wameongezwa maradufu, wakati Mahakama Kuu za *division* ni asilimia 96 tatizo ni nini wakati Majaji wameongezwa na upelelezi umeboreshwa?

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya *DPP* izidi kuimashwa, lakini pia kuna malalamiko ya kucheleweshwa kuzipeleka Mahakamani kesi zinazohusu ufisadi, tatizo ni nini? Kesi ngapi zimefikishwa Mahakamani zilizopelekwa kwa *DPP* kutoka TAKUKURU?

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maamuzi ya Mahakama, kumekuwa na mtindo wa baadhi ya taasisi au uongozi kupuuza maamuzi ya Mahakama. Yapo malalamiko mengi kwa wafanyakazi waliopeleka malalamiko yao Mahakamani na wahusika kupuuzia maamuzi ya Mahakama kuna haja ya Jaji Mkuu kuitia maamuzi ya Mahakama husika ambao wamekataa kuchukua hatua za utekelezaji wa maamuzi ya Mahakamani.

MHE. FELIX N. KIJKO: Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa mchango wangu kuhusu mafanikio ya Wizara ya Katiba na Sheria, napenda kusema kuwa naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wakati wa kuwasilisha Makadirio ya Wizara yake. Shukrani zangu ziwafikie wataalam wote na

hasa kwa kuonyesha ushirikiano mzuri wa kuandaa hotuba ambayo imejieleza kitaalamu na kuonyesha maeneo yote ambayo yameonekana kuwa na kasoro kwa Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu haya, naomba kuchangia kwa maana ya kuboresha katika vipengele vifuatavyo, kuhusu nyumba za watumishi, lipo tatizo kubwa la nyumba za watumishi wa Wizara hiyo na hasa wale walioko chini ya Mahakama mikoani. Tatizo hilo linachangia kwa kiasi kikubwa kuhatarisha maisha ya watumishi na hasa inapofikia hatua ya watumishi hao kwenda kupanga kwenye nyumba za uraiani. Ni dhahiri kazi ya kutoa hukumu ni kazi nzito ambayo kwa asilimia kubwa inafanya mtoa hukumu kuwa katika maisha ya utata. Ninamwomba Waziri alione hili wakati akiandaa Bajeti nyingine ili suala la kujenga nyumba za watumishi hawa lipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, tatizo la usafiri kwa watumishi wa Mahakama lipo. Magari madogo yanayotumika katika Wilaya kwa kutumiwa na Mahakimu wa Wilaya hayaendani na hali ya miundombinu ya barabara zetu. Nashauri pia hili litizamwe upya kwa kuongeza Bajeti ambayo itaboresha hali ya usafiri kwa ofisi za Mahakama na idara zake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchache wa watumishi, kumekuwepo na hali isiyoridhisha ya mrundikano wa kesi, hali ambayo inasababisha msongamano wa mahabusu kwenye Magereza. Kwa kipengele hiki ambacho kimekuwa kikiwakera hata wale watuhumiwa, nashauri yafanyike mafunzo yatakayopunguza tatizo hili ambalo ni kero kwa watuhumiwa wanaojikuta wakutumikia rumande kwa muda mrefu badala ya kukitumikia kifungo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu dawa za kulevya, matukio ya Watanzania kukamatwa kwa kuhusika na kuingiza dawa za kulevya/dawa haramu yanazidi kuongezeka siku hadi siku, yapo maoni tofauti kutoka kwa wasamaria wema kuwa sheria ya kudhibiti hili haitoshelezi kuwabana. Nashauri sheria ibadilishwe na itungwe na kuwa hukumu kutumikia kifungo kwa muda mrefu ili kuwapa fundisho. Nimewashuhudia watu wa aina hiyo wakikamatwa na kuachiwa huru baada ya muda mfupi na hiyo ndiyo sababu kubwa inayojitokeza kwamba wahusika wa kosa hilo wamekuwa ni hao hao kila wakati.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa nchi imeshavamiwa na wageni haramu na hasa katika miji mikuu pamoja na miji ya mkoa ambayo iko mipakani. Wageni hawa haramu wakajihushisha sasa na biashara zisizofuata taratibu kwa wageni. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inayotakiwa kudhibiti hili na hasa Idara ya Uhamiaji inajikuta ikihangai na ukamataji unaokwenda kinyume na sheria. Hatimaye ni watu wa aina hii kuachiwa huru. Ninao ushauri kuwepo na sheria ya kuwabana watu aina hii na hasa kuwahukumu kifungo kikubwa na kutopendelea kuwapa uhuru wa kuzurura katika nchi yetu.

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Spika, kuhusu Mahakama ya Kadhi, jambo hili limekuwa likizungumzwa kwa muda mrefu hivi sasa ndani ya Bunge na ndani ya Tanzania kwa mtizamo tofauti na huku Serikali yenyewe ikionyesha mwelekeo wa kuvunja Katiba.

Mheshimiwa Spika, Kifungu 19(2) cha Katiba kinazungumza kuhusu “Uhuru wa kuabudu dini uitakayao.” Serikali imekuwa ikitaka kujiunga katika mambo isiyoyahusu yaliyo nje ya uwezo wake kwa mujibu wa Katiba, suala la Mahakama ya Kadhi ni suala la Kidini, kwa nini Serikali inataka kujiingiza katika kuendesha shughuli za kidini.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Kadhi ni taasisi inayoshughulikia mambo yaliandika ndani ya Kitabu Kitukufu cha Waislam cha *Quran*. Mahakama ya Kadhi na viongozi hawalipwi na Serikali na wala watumishi wake hawastahili kulipwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, vipi Serikali inataka kujiingiza katika kuilipa Mahakama ya Kadhi wakati haimo kwenye mamlaka yake? Mbona Serikali haiwalipi mapadri, maaskofu, makanisani na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapotaka kujiingiza katika mambo ya dini inataka kuleta mzozo mkubwa wa kidini ndani ya Jamhuri yetu jambo ambalo ni hatari sana kwa jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ya Jamhuri yetu Mahakama ya Kadhi ipo na inaendesha kazi zake kwa mujibu wa dini inavyosema, pindi Mtanzania au Mzanzibar asiporidhika na matamshi yaliyomo ndani ya vitabu vya dini mtu huyo anaweza kuiomba Katiba inayohusika kusaidia na hapo kwa mujibu wa *Quran* muumini huyo mwisho wa siku atakwenda motoni kwa kukhalifu amri za *Quran* je, Serikali inataka kujiingiza huko?

Mheshimiwa Spika, Serikali ijitoe na wala isijishughulishe na mambo ya kidini kwa sababu Tanzania haina dini lakini Watanzania wana dini.

Mheshimiwa Spika, hukumu ya kifo si jambo la busara hata kidogo hukumu hii ikaondoshwa, kwa sababu italeta mfarakano kubwa ndani ya jamii, lakini pia itawaondolea haki yao wananchi wanyonge na mara nyingine wasiokuwa na uwezo fulani.

Mheshimiwa Spika, leo hukumu hiyo ipo tunao na jinsi baadhi ya watu wanavyojichukulia sheria mkononi mwao kwa kuwaa wananchi wengine kwa sababu wanazozijua wao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Marais kusindwa kuthibitisha kupitishwa hukumu hii ni kitendo cha woga na uvunjaji wa Katiba na maamuzi ya Mahakama yetu. Haiwezekani mtu mmoja amuuve mwengine kwa sababu ya vivu au mwizi ameua mwenye mali kwa makusudi lakini yeze asife ni dhambi kubwa na wala hakuna uhalali wowote kwa mtu mmoja kupewa uhalali wa kumuua mwengine na yeze asife. Hukumu ya kifo ibakie.

MHE. SAVELINA S. MWIJAGE: Mheshimiwa Spika, kama leo nilivyouliza swalı langu la Wizara hii Mkoa wa Kagera kuna matatizo mengi sana tena sana ya kupata haki zao kisheria hasa inafikia mahali pa kuuliza hivi sisi tuko Tanzania. Hapa napenda nikuorodheshee matatizo tuliyonayo makubwa sana napenda kujua sheria ya kukamata baiskeli za wananchi na kurundikwa kituo cha polisi bila kuwa na huruma ya kuweka chombo hilo ambacho hakina mdomo.

Mheshimiwa Spika, kama sisi wananchi wa Mkoa huo usafiri wetu kuanzia kwa baba zetu mtu anabebea mzigo wake kwenda sehemu yoyote mpaka sasa wananchi wanashindwa kutumia chombo hilo kwenye shughuli binafsi wanakamatwa na ni lini sheria hii italetwa hapa Bungeni ili wananchi wawe huru na vyombo vyao, pili na kuwapatia kipato na naomba Wizara hii itoe tamko baiskeli zilizorundikwa kituo cha polisi warudishiwe haraka na hiyo sheria ina kigugumizi gani, hizi kesi inakuwa tatizo Bukoba, ni jambo la kusikitisha.

Mheshimiwa Spika, baiskeli hizo hizo sehemu za Geita, Sengerema, Mwanza yote ndiyo *taxi* zao je, Bukoba ina tatizo gani? Naomba Waziri ukiwa unajibu naomba tamko hata wananchi wa Kagera wakusike. Unawajali kimaisha ni tatizo kubwa, tatuatizo.

Naomba Wizara yako isimamie suala la miradi ya wajane na yatima Mahakamani wasipende kuwaliza mara mbili ni tatizo gani linalofanya wasumbuliwe. Wanaadhirika hao watu napenda kupata ufanuzi kwa hayo niliyoweka kwenye maandishi yangu ningependa kusimama. Lakini kama unavyojuu matatizo niliyonayo siwezi kusimama ni muda mfupi sana naomba njibewe kwa ufasaha. Nakutakia Bajeti njema.

Mwisho, je, sheria ya baiskeli na pikipiki na baiskeli kubeba abiria narudia tena wananchi warudishiwe mali zao naona maduka yanauza baiskeli Bukoba haina haja.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, kuna Mahakama za Mgandu na Mwamagemebe Wilayani Manyoni ambazo hazina kabisa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo. Mahakama hizi zilikuwepo tokeaa enzi za mkoloni.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa Mahakimu kunawalazimisha wananchi kusafiri kilometra 70 na kilometra 130 *respective* kufuata Mahakama ya Itigi ili kupata haki. Kutoka Rungwe hadi Itigi ni kilometra 220, hakimu akiwepo Mwanagemebe, wananchi wa Rungwa na Kintanula watasafiri umbali wa kilometra 60 kuja Mahakama ya Mwanagemebe. Naiomba Wizara hii (Serikali) itupati Mahakama mbili kukidhi adha hii inayowapata wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sheria ya kutoruhusu kesi iliyoko Mahakamani kutojadiliwa nje ya Mahakama, sheria zetu tumeiga mfumo wa Sheria za *Commonwealth*. Lakini mazingira ya nchi zetu (*third world countries*) ni tofauti kabisa na nchi zilizoendelea kama Uingereza, tofauti hii haiweki uwanja sawa kwenye kutumia sheria hizi katika kutafuta haki.

Mheshimiwa Spika, kuna upungufu mkubwa wa Mahakimu waendesha mashtaka, wapelelezi, polisi, magereza mengi ni finyu na kadhalika, hali hii ya mapungufu

makubwa inaifanya sheria hii ya kutozungumza kesi iliyo Mahakamani kuwa ndiyo sera ya ukandamizaji wa wananchi hasa maskini. Kesi nyingi za kubambikiza *root cause* yake ni sheria hii. Mwananchi anafunguliwa kesi haraka na kufikishwa Mahakamani haraka lakini kuendeshwa kwa kesi huchukua miaka kwa visingizio mbalimbali nya mapungufu na wakati huo huo mtuhumiwa anasota rumande au kama ni mtumishi basi anasota nyumbani baada ya kusimamishwa kazi.

Napendekeza kipengele hiki cha kutozungumzia kesi nje ya Mahakama kifanyiwe marekebisho, watu na vyombo nya habarai (nchi maskini) viruhusiwe kujadili kesi zote isipokuwa ile ya jinai na kuuwa (kifo). Kama kesi zitajadiliwa kwa mwezi kwanza ita-speed up utekelezaji na pia hakimu atakuwa na *information* ya kutosha kumsaidia kuamua ingawa hawezi kuwa *bound* kutumia mawazo ya watu wa nje ya Mahakama. Ushahidi utaendelea kuwa msingi wa maamuzi yake katika kutoa hukumu ya haki.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi kipengele hiki cha kanuni ya kutozungumzia kesi iliyoko Mahakamani, ni kichaka cha rushwa na kabati la kufungia haki za wanyonge. Ni muda huo ambaa matajiri hupata nafasi nzuri ya kununua haki kwa kificho na mara nyingi hukumu huwa imeshatayarishwa katika mazingira ya wasiwasi na woga kwa wananchi wasiokuwa na uwezo.

Napendekeza tuache kuwa watumwa wa sheria za nchi nyingine. Tutafute mfumo wetu kulingana na mazingira yetu kwa mfano, *GACACA* za Rwanda.

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia ifuatavyo, kwa vile watu wengi sana, ikiwemo vyombo mbalimbali nya Serikali wanalamikia mapungufu mbalimbali katika Katiba yetu, ni lini Serikali itafanya mabadiliko makubwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kukidhi mahitaji haya ya mabadiliko kuendana na mabadiliko ya kiuchumi, kisayansi na kisiasa yanayoendelea nchini kwetu na hata duniani kote.

Kwa miaka kadhaa sasa, nimekuwa nikitaka Majaji wetu wapatiwe msaada wa vyombo nya kisasa mfano wa *Hansard* au vinyofanana na hivyo kwa lengo la kuwawezesha kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Majaji wetu na hata Mahakimu wanaumia sana kusikiliza, kutafakari, kufanya marejeo ya sheria na kuandika yote kwa wakati moja. Hii ni kazi nzito sana. Leo naitaka Wizara iniambie na kulijulisha Bunge lako Tukufu mpango mikakati wenye ratiba kamili wa kuwatekelezea Waheshimiwa Majaji hitaji hili muhimu. Tunawaumiza sana kuwachosha/zeesha Majaji wetu bila sababu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Karatu tangu imeanzishwa haina wala Mahakama ya Wilaya na wala hakimu wa Wilaya. Lini Wilaya ya Karatu sasa itapata Mahakama ya Wilaya na hasa baada ya mpango wa awali wa *quick wins* kushindikana? Ni kwa nini angalau kwa sasa jengo jipyla ya Mahakama ya Mwanzo ambalo liko kwenye hatua ya kukamilika lisitumike angalau kwa muda kama Mahakaka ya Wilaya kuwapunguzia wananchi wa Karatu adha ya kusafiri hadi Monduli, jambo ambalo ni gumu kwani mji wa Monduli uko pembeni, hakuna usafiri wa moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini angalau hakimu wa Wilaya ateuliwe ili kuweza kushirikiana na wenzake, wapange utaratibu mzuri wa kutumia majengo mapya ya zamani ili angalau wananchi ambao sasa hawapati haki zao kutokana na umbali wa Monduli, wapate haki zao Wilayani? Lini Hakimu wa Wilaya atateuliwa na kupelekwa Karatu?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha nikitegemea majibu ya kina.

Mheshimiwa Spika, pia naomba kuchangia kama ifuatavyo, kuhusu *Law School of Tanzania*, ninaona matatizo makubwa kama ifuatavyo:-

Kwanza, kwa sheria ilivyokuwa sasa itakuwa vigumu sana vijana wetu kupata ajira bila kupitia “*Law School*” na kwa hali ilivyo “*capacity*” ya kuwaingiza *Law School* ni ndogo sana. Serikali inatoa kauli gani kunusuru vijana hawa, wamehitimu, wana sifa stahiki lakini wala si Serikali wala si sekta binafsi inayoweza kumwaajiri kwa vile tu hawajapitia *Law School*.

Pili, kwa vile *Law School*, ni *mandatory* na wanaotakiwa kuingia *Law School* ni vijana wadogo waliomaliza tu Chuo Kikuu, hawana ajira bado, wala hawana mapato yoyote, bado sheria “inawanyima” haki ya mkopo toka Bodi ya Mikopo! Kwa hali hii, ni mtoto gani wa mkulima ataweza kuingia “*Law School*”? Nashauri Serikali ilete Bungeni haraka iwezekanavyo marekebisho sheria husika ili kipengele hicho kiondolewe na kuruhusu vijana hao wapate haki yao ya mikopo.

Tatu, siku za hivi karibuni, kumezuka utata kuhusu ni hati gani wahitimu wa *Law School* watapewa baada ya kuhitimu. Wako wanaosema ni *Certificate* wako wanaosema ni “*Advanced Diploma* kwa vile masomo yenye ni *Post Graduate Studies*. Ningependa Waziri alitangazie Bunge hili ni cheti gani watapata wahitimu hawa ili kuepuka migogoro ya baadaye kama ilivyotokea kwa taasisi zingine.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

MHE. ALOYCE B. KIMARO: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nampongeza Waziri wa Sheria na Katiba, Mheshimiwa Mathias Chikawe pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa hotuba iliyoandaliwa vizuri. Kwa mantiki hiyo naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ipo kama haipo. Mojawapo ya majukumu ya Tume ni kuhamasisha nchini hifadhi ya haki za binadamu na wajibu kwa jamii. Pia tume hii inatakiwa kutoa elimu ya haki za binadamu kwa jamii.

Majukumu haya ni mazito yanahitaji tume kuwezeshewa kifedha ili iweze kufanya kazi, magari ya tume ni machakavu sana. Ofisi za Tume ni chache sana ziko nne tu nchi nzima. Wananchi wenye malalamiko wanapata taabu sana kufika kwenye ofisi hizo ili

kutoa kero zao. Ili kufanya utafiti wa fedha zinahitajika na pia nashauri *staff capacity building* iwepo ili wananchi wafikishiwe kilicho bora. Serikali pia lazima iheshimu maamuzi ya Tume.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ni kero kubwa ni mishahara ya Mahakimu na Wanasheria wa Serikali. Wanasheria wa Serikali na mahakimu wanakutana na vishawishi vingi vya rushwa hasa wakati huu wa utandawazi. Kama hawa hawalipwi vizuri wataendelea kusaini mikataba mibovu na hata mkiwafukuza kazi wataajiriwa na hayo makampuni waliosimamia. Tafadhali Mheshimiwa Waziri hawa wapewe mishahara na maslahi mazuri ili wapate uchungu wakiachishwa kazi wasipate vishawishi vya fedha.

La mwisho napenda kujua ni maamuzi gani mazito ambayo tume imeamua na kuishauri Serikali na yakatekelezwa? Pia ni mashauri mangapi ambayo yalishaamuliwa na Tume lakini Serikali inashindwa kutekeleza kwa wakati huku ikielewa kucheleweshwa kwa haki ni sawa sawa na kunyimwa haki kabisa?

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria na watendaji wote, kwa jitihada wanazofanya kuboresha ufanisi katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Majaji na Mahakimu wanafanya kazi katika mazingira magumu na hatarishi. Ipo haja ya kufanya jitihada za makusudi kuboresha maslahi ya watumishi kama usafiri, makazi na vitendea kazi muhimu ikiwa ni pamoja na kujenga Mahakama ndogo ndani ya Wilaya zetu kupunguza umbali wa huduma za Mahakama kwa wananchi. Mabaraza ya kata yawe sehemu ya mpango mzima wa maboresho hayo kwa majengo mazuri na watendaji wenye uwezo wa fani za Sheria.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo sasa nitoe maoni yangu juu ya mchango wa Wizara hii katika mfumo wa uchumi wa Tanzania. Swali la msingi ni je, Wizara ya Katiba na Sheria inasaidia vipi Serikali na taasisi zake katika kusimamia, kushauri kabla na baada ya kuingia katika mikataba ya biashara, uzalishaji, huduma, uwekezaji? Maswali ya ziada ni kama ifuatavyo, je, malalamiko ya udhaifu wa mikataba katika sekta za madini, nishati, fedha, usafirishaji (miundombinu) yanatolewa maelezo gani na Wizara ya Katiba na Sheria?

Mheshimiwa Spika, je, Wizara haioni ina wajibu wa kusimamia na kushauri Watanzania, Serikali na taasisi za umma kujenga tabia na msingi wa kuwa na mikataba bora inayosaidia kulinda maslahi ya Taifa letu la Tanzania? Je, ofisi ya Mwanasheria Mkoo inaposhiriki katika majadiliano ya mikataba kama mshauri wa Serikali na bado ikatokea mlolongo wa mikataba dhaifu inatoa picha gani kwa uwajibikaji wa Wizara hii ya Katiba ha Sheria?

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa majibu ya maswali niliyotoa hapo juu iwapo Mheshimiwa Waziri ataona umuhimu wa kuyajibu unaweza ukatoa mwanga wa kasoro zilizopo katika mfumo wa wajibu wa ofisi ya Mwanasheria Mkoo katika kushiriki na kushauri Serikali wakati wa majadiliano ya mambo ya msingi ya mikataba kati ya Serikali, taasisi za Serikali na upande wa pili wa mikataba katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, iwapo zipo dosari za msingi basi ni vyema dosari hizo zikafanyiwa marekebisho ili Tanzania iweze kunufaika ipasavyo katika majadiliano na mikataba ya uwekezaji biashara hasa huduma muhimu. Leo Tanzania inachekwa kwa kukosa umakini katika mikataba mingi katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ili Wizara ya Katiba na Sheria iendelee kutoa huduma pia Wizara itasimama imara katika kuikomboa Tanzania katika janga la mikataba dhaifu kisheria.

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Spika, Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo hasa maeneo ya Wilaya, tarafani, vijijini uhudumia zaidi ya Mahakama moja kitu kinachosababisha kesi kuchukua muda mrefu sana katika Mahakama za Mwanzo bila kusikilizwa na pia wakati huu ni muda muafaka wa kuongeza idadi ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo.

Kuhusu sheria hii inaruhusu kwa watoto kuwapo gerezani kwa kutoa tafsiri ya mfungwa kijana kuwa ni mtu yeyote aliye na umri wa miaka 16 hadi 21 na mfungwa mtu mzima ni mtu yeyote aliye na umri wa zaidi ya miaka 18. Kwa kuzingatia tafsiri zilizotolewa hapo juu mtoto aliye chini ya miaka 18 ila amezidi miaka 16 anastahili kufungwa gerezani.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina shule moja tu ya mafunzo (*approved school*) ambapo watoto wanaopatikana na hatia katika makosa ya jinai wanapaswa kupelekwa. Hii shule ya mafunzo haitoshi na hivyo kwa njia moja au nyingine inasabasiha kuwepo kwa watoto magerezani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 inahurusu msichana mdogo wa umri wa miaka 14 kuolewa kwa idhini ya Mahakama au akiwa na miaka 15 kwa ridhaa ya wazazi au walezi. Kifungu hiki kinakinzana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na sheria zingine kama sheria ya mikataba kwa kuwaruhusu kuolewa katika umri huo. Mtoto anakosa haki ya kuijendeleza kielimu na kuathiri haki yake ya kuwa na afya njema.

MHE. AME PANDU AME: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Spika, Sheria ni Silaha muhimu na kubwa sana ya ulinzi na kuendesha na kusimamia mambo yote ya Serikali na ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, Sheria wameletewa wanadamu na Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kuendesha mambo yote yahusuyo wanadamu na wasio wanadamu.

Mheshimiwa Spika, Mwenyezi Mungu ndiye aliyetuletea hii kitu inayoitwa Sheria hata kama hiyo aliyotuletea yeye kuna wengi hawaifiati na yeye ametuletea jambo hilo la sheria kwa sababu ya vituko vya mwanadamu.

Mheshimiwa Spika, mwanadamu ndiye kiumbe wa mwisho kabisa kuumbwa kuliko viumbe wote lakini ni kiumbe aliyeletewa sheria kwa vituko vyake. Kwa hiyo, sheria ni kitu cha kufuatwa na cha kutekelezwa sana na sio kuwekwa tu kwa maandishi vitabuni bila ya kufuatwa na kutekeleza na kama yatekelezwa kwa yule mnyonge tu. Sheria ni msumeno itumie kwa wote.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni vema iongezewe Bajeti kwa mwaka mwininge ili iweze kumudu shughuli zake. Naunga mkono hoja.

MHE. VUAI ABDALLA KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakupongeza wewe jioni hii kwa kuwa Mwenyekiti na kuongoza Bunge hili la Jamhuri ya Muungano, pia napongeza Wizara ya Katiba na Sheria kwa kazi nzuri chini ya usimamizi wa Waziri Mheshimiwa Mathias Chikawe, na wasaidizi wake pamoja na watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii ni nzuri lakini mahitaji ya fedha ni makubwa na fedha hizi ni ndogo. Naiomba kwa Bajeti ya mwaka mwininge fedha iongezwe.

Mheshimiwa Spika, sheria ni msumeno huenda nyuma na mbele kwa hiyo, naiomba Serikali chini ya Wizara hii kusimamia vyema na kuona haki inatendeka katika nchi kwa kila mwananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *OIC*, Umoja wa Shirika la Waislamu Tanzania hadi leo kwa nini tusijiunge na suala hili limezungumzwa siku nyingi na hata Zanzibar mwanzoni ilitaka kujiunga na ikawekewa vizingiti kuwa haiwezi kujiunga ila Tanzania au Serikali ya Muungano ndio inaweza kujiunga, basi taratibu hizi zitakamilika lini? Naiomba Serikali kutimiza ahadi hii kwa maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na kero za Muungano zinazohusu Sheria na Katiba, naiomba Serikali kuziona na kuzitatu hasa zile zinazohusu Zanzibar na kama Muungano wa nchi mbili Zanzibar na Tanganyika kuwa na Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Tanzania. Kwa nini kusiwe na usawa wa haki kisheria. Naiomba Serikali kama bado kuna tatizo basi sheria itazamwe upya ili kusiwe na tatizo na wanasheria walione sio kulipalilia.

Mheshimiwa Spika, Mahakama Kuu ya Rufaa, kwani Tanzania tuna Mahakimu wawili na Tanzania Bara, Mahakimu wengi kusiwe sawa. Naomba vile vile iwe sawa kwa sawa.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magogoni na mimi mwenyewe naunga mkono hoja.

MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI: Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora hapa nchini, kuliwapa imani

Watanzania kwamba sasa kuna chombo ambacho kitaweza kuwasaidia kupata haki zao na kudumisha utawala bora hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa sana Tume hii inaonekana kama ni chombo cha kisiasa zaidi kuliko matarajio ya walio wengi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kipengele cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano ukurasa wa 111, kifungu cha 130 (5), Tume hii inaonekana kubanwa katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kati ya malalamiko ambayo Tume hiyo inaweza kuyapokea ni pamoja na malalamiko ya matumizi au matendo ya watu wenye madaraka katika utumishi wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na kuhusu matumizi mabaya ya madaraka, kutotenda haki au kuonea.

Mheshimiwa Spika, kuna malalamiko mengi ya wananchi dhidi ya viongozi wa Serikali au watendaji wa Serikali, mfano *DC* anapoamuru kuchomwa nyumba za wananchi na kadhalika, hivi ni kweli Tume hii ambayo hata ikimwita *DC* kufika ofisini kwao kwa mazungumzo, *DC* anaweza kudharau wito huo na hapo Tume haina uwezo wa kumlazimisha. Kwa ufupi Tume hii haina meno katika utendaji wa shughuli zake. Je, Serikali haioni kwamba ipo haja ya kuipa uwezo zaidi Tume hii kutekeleza wajibu wake?

Mheshimiwa Spika, Tume hii pia inabidi iwezeshwe kifedha ili iweze kufanikisha majukumu yake vizuri.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Kurekebisha Sheria inafanya kazi nzuri na mimi nawapongeza, lakini Tume hiyo baada ya kupitia Sheria hizo, huwasilisha ripoti za mapendekezo yao kwa Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria na kwa sasa ripoti hizo bado nydingi hazijafanyiwa kazi.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba ipo haja ya Wizara ya Katiba na Sheria baada ya kupokea ripoti hizo kutoka Tume ya Kurekebisha Sheria, basi pia ripoti hizo ziwasilishwe Bungeni, ili Waheshimiwa Wabunge ambaa ndio wanaopitisha sheria, waweze kufahamu mapendekezo ya wanasheria ili kuweza kuhimiza utekelezaji wa mapendekezo hayo?

Mheshimiwa Spika, naomba kufahamu nini msimamo wa Serikali kuhusiana na Mahakama ya Kadhi?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Wizara hii kwa kujali jinsia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hukumu ya kifo, adhabu ya kifo ni uvunjaji wa haki za binadamu. Tukumbuke anayetoa hukumu ni binadamu anayehukumiwa na binadamu na hukumu inaweza kutolewa kimakosa kama anayejieleza hakujieleza vizuri. Tumeona

sehemu nyingi duniani kuna wafungwa waliokuwa wanasubiri adhabu ya kifo baadaye ikagundulika hawakutenda kosa lile. Pia kwa wale wafungwa walio gerezani wakisubiri adhabu hiyo *ki-psychology* ni mbaya sana hawajui wakati wala saa mlango wa gereza ukifunguliwa wanafikiri wakati umefika.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu adhabu hii ifutwe, anaweza kuhukumiwa mtu kimakosa na akishakufa harudi tena na pia akiwa anapata adhabu kifungoni ndio itakuwa fundisho kwa wengine na atajuta wakati wote.

Kuhusu Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, kitu cha kwanza sheria hii imepitwa na wakati katika sheria za Kimataifa mtoto si chini ya miaka 18 na hata hapa Tanzania sheria yetu inasema watoto hawaruhusiwi kupiga kura mpaka watimize miaka 18. Swali iweje sheria hii itoe tafsiri tofauti kwa mtoto? Sheria hii ya ndoa ya mwaka 1971 inaruhusu watoto miaka 15 kuolewa na kama sikosei Sheria hii ilishapelekwa katika *Law Reform* siku nyingi kwa nini hailetwi Bungeni?

Mheshimiwa Spika, swali, hivi watalaam (*consultant*) wangapi walitumika kupitia sheria hii, je, ilipitiwa hii na *Legal Reform Commission*? Kama ilipitiwa inachukua muda gani kupitiwa au kuletwa Bungeni?

Mheshimiwa Spika, waathirika wakuu ni watoto wa kike na kwa kuwa tunakataka kuendeleza Taifa kufikia malengo ya milenia (*millennium*) Serikali itamke rasmi itamaliza mchakato huu hili? Je, sheria hii inakinzana imani ya dini yoyote? Sheria ya Matunzo ya motto, mfano mpaka leo hii mtoto anatunza kwa shilingi 100/= imepitwa na wakati inabidi matunzo yaendane na mishahara ya sasa na wasioajiriwa yakadiriwe kwa busara za Hakimu au Jaji. Kama ndoa ikivunjika basi matunzo yaanze kutoka ujauzito (mimba). Tatizo kubwa lingine ni matatizo ya mirathi na waathirika ni wanawake tunajua kuna sheria za mila, dini na Serikali kuhusu mirathi.

Ushauri wangu, kuna haja ya kuwa na sheria moja ya mirathi ili kuondokana na unyanyasaji. Kuhusu upungufu wa vitendea kazi na wafanyakazi kuna upungufu wa watendaji katika Wizara hii hasa katika Mahakama za Mwanzo (*Primary Court*) ikiwa ni uchache wa Mahakama hizi za mwanzo katika vijiji ni vizuri Mahakama hizi zikawepo kule vijijini ili kusogeza huduma za Mahakama kwa wananchi, je, Serikali ina mikakati gani ya kuweka Mahakama za Mwanzo katika kila kata? Kwa mfano, Moshi Magharibi kesi za Mahakama ya Mwanzo zote lazima waje Mjini Moshi ukizingatia vijijini ndiko kwenye watu wengi wanashindwa kufuata haki zao sababu ya umbali.

Mheshimiwa Spika, kwa vile suala la rushwa lipo katika sekta mbalimbali Serikali na Wizara hii ni mojawapo, kuna haja ya kutengeneza mazingira mazuri ya kazi, wawe na vitendea kazi (*stationery*), ofisi nzuri, mishahara mizuri (*dissent salary*) waishi kwa raha na pia waipende kazi ili wasipate vishawishi vyta rushwa. Baadhi ya Mahakama za Mwanzo hata sheria zilizokuwa *amended* hazipo kule, Wizara iangalie ni jinsi gani ya kila mkoa kuna *library* ambayo Mahakimu wanaweza kutumia.

Mheshimiwa Spika, sheria ya Magereza 34(1967). Sheria hii inawanyima watu kwenda katika maeneo ya Magereza hivyo basi inakizana na Katiba sababu inaingilia uhuru wa vyombo vya habari ambao wangeweza kufika pale na kuandikia umma ili wajue hali halisi ya magereza yetu. Tukumbuke Sheria nyingi tuli-inherits kutoka kwa wakoloni na kwa mtazamo wao sheria zao zilikuwa za kutugandamiza.

Mheshimiwa Spika, swal, katika mapendekezo ya marekebisho ya sheria mbalimbali katika zile sheria 40 za Tume ya Jaji Nyalali ni sheria ngapi zimefutwa mpaka leo?

Mheshimiwa spika, kuhusu Zanzibar nchi au siyo nchi, je, Serikali ipo tayari kurejea mawazo yaliyotolewa na Tume ya Jaji Kisanga na Jaji Bomani badala ya kuunda tume mpya na kutumia kodi zetu bure?

Kuhusu sheria 13 (1995) Maadili ya Viongozi wa Umma, pamoja na mengine sheria inatamka kuwa kiongozi wa umma lazima aainishe mali zake kati ya siku 30 kuingia au kila mwisho wa mwaka na baada ya kazi mali zake zote. Pia sheria hii *section (1)* inaainisha mali ambazo zinakuja kutolewa taarifa lakini katika *section 32* mtu yejote akitaka kuangalia fomu za maadili kwa ajili ya kufuatilia *section 21*, hairuhusu mpaka sekretarieti ya maadili ikupe taratibu zinazotaka kufuatwa ambazo ni (3)(i) upeleke kwa maandishi malalamishi kwa Kamishna dhidi ya kiongozi anayetaka kuangalia mali zake; (ii) huyu Kamishna lazima kwanza akubaliane na malalamiko yako kama ni *geniun (and was made in faith)* na (iii) lazima ulipe pesa za ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, swal *and was made in good faith* tafsiri yake ni nini na ni kwa nani? Hata hivyo ukiweza kutimiza yote matatu hairuhusiwi kutumia *information* hiyo kwenye vyombo vya habari, inatajwa ni kosa na matokeo yake taarifa kama kweli zina makosa haziwezi kufikia umma kama vile ni kosa lakini hapo hapo katika kifungu cha 18(b) anayo haki ya kutafuta, kupokea na kutoa habari bila kujali mipaka ya nchi. (d) anayo haki ya kupewa taarifa wakati wowote kuhusu matukio mbalimbali muhimu, maisha na shughuli za wananchi na pia kuhusu masuala muhimu kwa jamii. Hivyo basi hatuoni sheria hii inakinzana na \katiba?

MHE. HAJI JUMA SEREWEJI: Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia nikushukuru wewe kwa kuniruhusu kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, nianze kuunga mkono hoja hii mia kwa mia. Pia niipongeze hotuba ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia kuhusu ubomoaji nyumba za wananchi kiholela wakati wa kutaka kuitisha barabara sehemu hiyo. Wananchi hupata taabu kubwa sana kwa kukosa malipo, kwa kukosa kujikimu kwa makazi mengine na kuhangaika ovyo kwa hiyo, ni vyema Serikali ianze kulipa fidia, baadaye ubomoaji uendelee ili wananchi wasiwe na shida ya kupata makazi mengine.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa wakati umefika kwa madhehebu ya dini kuwa na uwezo kufuata madhehebu yao na kuhukumiana kwa sheria zao hasa za ndoa na mirathi, isipokuwa Serikali isimamie tu.

Mheshimimiwa Spika, ni vigumu kama matatizo ya wanandoa wa kiislam kuwa na matatizo hayo yasikilizwe na mtu ambaye si muislam wakati sheria za kiislam zipo, hata mirathi hivyo hivyo. Kwa hiyo, wakati umefika hivi sasa kuwe na Kadhi hapa Tanzania Bara, wakati Mufti yupo kwa nini Kadhi asiwepo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu ulimbikizaji wa kesi, ulimbikizaji wa kesi ni jambo ambalo linawaweka pabaya wenye kesi kwa sababu wanachukua siku nyingi kuhangaika. Mambo haya hata wananchi wema huwa wanaogopa kabisa kuwa mashahidi kwa kuogopa kuhangaishwa kwa muda mrefu.

Kuhusu Mahakimu, uhaba wa Mahakimu unaleta matatizo kwa sababu unafikia wakati hakimu asukume kesi bila kutenda haki kwa hivyo ni vizuri Serikali iongeze Mahakimu ili kesi ziende haraka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ubakaji, kuna kesi hazina sababu kuwekwa muda mrefu kama hii ya ubakaji kwa sababu ushahidi ukishakamilika tu ilivyokuwa ni mambo yanayopigwa vita sana haya ya ubakaji. Kwa hiyo, kesi hizi ziendeshwe haraka sana ili wahusika wapewe adhabu inayostahili ili iwe somo kwa wengine.

Mheshimiwa Spika, nazidi kukushukuru kwa kuniruhusu kuchangia. Nazidi kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia.

MHE. MERCY M. EMMANUEL: Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Waziri wa Katiba na Sheria kwa kuwasilisha hotuba hii nzuri na yenye matumaini, niwapongeze wataalamu wote wa Wizara hii muhimu. Nimpongeze pia Katibu Mkuu wa Wizara, naomba nichangie kuhusu kesi zinazochukua muda mrefu bila kupata maamuzi tukiachana na kesi za mada, kuna kesi nyingi za kawaida zinachukua muda mrefu zaidi ya miaka miwili bila sababu maalum na wakati mwengine mlalamikaji hahudhurii ipasavyo hivyo mshitakiwa kunyanyasika sana na huudhuria kila wakati mahakamani kulingana na tarehe yake na kesi hizi huvutwa tu na kuchukua muda mrefu. Sasa kwa kuwa jambo hili ni wazi kuwa lipo na nimelishuhudia mwenyewe. Serikali inasema nini kuhusu tatizo sugu hili? Je, Wizara haioni kuwa kurefusha kesi hizi ni kuhurusu mwanya wa rushwa?

Mheshimiwa Spika, naomba wakati unatoa maelezo unisaidie ni jinsi gani utatatua tatizo hili au unaiagiza nini mahakama.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kuhusu vifaa vya Mahakimu, zaidi karatasi. Ni kweli kwamba Mahakama nyingi hazina vitendea kazi hii nayo inachangia kuzorota kwa kesi naomba Wizara, ishughulikie tatizo hili ambalo ndio limekuwa la muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kuhusu uhaba wa watumishi (makakimu) ni kweli kuwa Mahakimu hawatoshi kabisa na hii husababisha Mahakimu kufanya kazi kupita kiasi kwani huwajibika kuzunguka Mahakama zaidi ya tatu. Naiomba Wizara ijitahidi kuongeza watumishi katika Wizara hii au eneo hili muhimu.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie tena eneo la Wazee wa Baraza. Wazee wa Baraza wana tatizo juu ya malipo yao. Kwa kweli pesa wanayopata ni kidogo sana hivyo inasababisha wazee hawa kuomba rushwa kutokana na kipato kidogo wanachokipata.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie eneo la wanasheria wa Serikali. Wanasheria hawa ni tofauti kabisa na wanasheria wa kujitegemea. Hawa kipato chao kikubwa na wengi wao au karibu wote wana magari binafsi na ni kweli kuwa wako *smart* kabisa kimavazi. Sasa Wizara haioni kuwa kutowajali Mawakili wetu wa Serikali ni kusababisha watawanyike na kutafuta ajira mahali pengine au hata kujitegemea kabisa. Lakini pia usalama wao unakuwa ni mdogo kabisa kutokana na mazingira wanayoishi na pengine kuleta tamaa ya rushwa. Naomba Serikali iangalie kwa upya kabisa Bajeti ya Wizara hii muhimu pesa wanatengewa kidogo kabisa haitoshi kwa ujumla.

MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja. Pia napongeza kazi nzuri inayofanywa na viongozi mbalimbali katika Wizara na sekta.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la baadhi ya majaji kukosa uadilifu. Makarani wa Mahakama baadhi yao sio waadilifu, wana *collide* na baadhi ya washtakiwa kuiba nyaraka. Baadhi wanatumia nafasi kupata chochote mahakamani na kuwasaidia wastaki/washtakiwa katika kuwapatia taarifa za kesi za watu kitu kinachopunguza sifa za Mahakama zetu.

Mheshimiwa Spika, Majaji wana kazi nyingi na mazingira ya kazi zao sio mazuri, wafikiriwe, likiwemo suala la maslahi yao ili wasiwe *easily corrupted*. Upo uwezekano sasa wa kuwapigia kura wale Majaji wala rushwa (sio wote ni wachache). Nawapongeza Majaji waadilifu wanaotenda haki katika majukumu yao ya kazi, Mwenyezi Mungu atawabariki kwani wanaloofanya ni lile Mwenyezi Mungu analotaka waje wake wawafanyie wenzao. Hongera hongera na Mola awe nanyi.

Mheshimiwa Spika, kwa wale waliokosa uadilifu tutasali na kuwaombea dumu daima, labda iko siku Mola atawadilisha. Askari wanao simamia kesi, baadhi waelewe sasa utaratibu utabadilika, tuwaombe wawe waadilifu, wasiuze kesi za wanyonge.

MHE. SHOKA KHAMIS JUMA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuongelea suala la Mahakama ya Kadhi ambalo nimeshaliongelea kwa muda mrefu, sasa leo naomba nipate majibu yake ambayo nimeshayaongelea siku za nyuma hasa kwenye hotuba ya Waziri Mkuu ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu Katiba mpya ninaiomba Serikali mara hii isitujibu kama inavyokuwa ikitujibu kuwa haina mpango wa kuandika Katiba mpya. Sote tunafahamu kuwa Katiba yetu ina mapungufu na ni ya chama kimoja hivyo irekebishwe ili iendane na vyama vingi na iwe ya kisasa inayokidhi haja ya kisasa. Je, ni lini Serikali itakuwa tayari kurekebisha Katiba hii?

Mheshimiwa Spika, tatu suala la takrima nashukuru kwa hili Serikali kukubali kuondoa takrima lakini tusiondoe takrima ya kupika wali, ugali na pombe lakini tusiendelee kutoa vibahasha vya wapigakura. Je, Mheshimiwa Waziri ni lini atalaeta Sheria ya Uchaguzi Bungeni ili tufanyie mabadiliko ili tuzibe mianya ya rushwa?

Mheshimiwa Spika, nne kuhusu Tume ya Haki za Binadamu inafanya kazi nyingi lakini ina upungufu wa vifaa vya kufanya kazi pamoja na Bajeti ndogo, je, Serikali inaongezaje Bajeti hii?

Mheshimiwa Spika, tano, kuhusu Tume ya Kurekebisha Sheria ina kazi ya kufanya utafiti na uchambuzi na kuhuisha sheria je, ni sheria ngapi zimeshafanyiwa kazi hii? Na kwa kuwa Sheria ya Mirathi imeshafanyiwa kazi hiyo je, ni lini italetwa hapa Bungeni?

Mheshimiwa Spika, sita na mwisho, kwa kuwa mara nyingi nimekuwa nikiulizia kwa Serikali kuhusu kuridhia Mkataba wa Mataifa wa Kutokuwatesa Wafungwa na Mahabusu lakini napata ahadi hewa, je, kuna sababu gani za msingi za kutokuridhiwa mkataba huu wakati Tanzania tunajigamba kuwa tunafuata haki na utawala bora?

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii pamoja na watendaji wake wote kuandaa hotuba hii na kuleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa sana la kesi za wananchi kukaa miaka mingi Mahakamani bila kusikilizwa, wananchi wameendelea kuteseka na kutumia gharama kubwa kwa miaka mingi wakifuatilia haki zao bila kuzipata na bila hata kusikilizwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kesi zinazohusu ardhi ndio kabisa usiseme, hakuna Mahakimu wa kusikiliza kesi za ardhi Tanzania kama sikosei kwa nchi nzima wapo wawili au watatu kwa eneo hilo tajwa. Kwa kuangalia jinsi tulivyo na matatizo mengi na kesi nyingi za ardhi hapa nchini kuwa na mahakamu wachache kiasi hiki ni kuongeza matatizo kwani wanaosababisha kesi hizo ndio hao wanaolalamikiwa na wanaendelea kutenda makosa mengine.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana kwa nchi inayoongozwa kwa Katiba na Sheria mwananchi anafuatilia haki yake ya msingi kwa muda wa miaka mingi hadi anafariki bila kupata na watoto wake wanaendelea kufuatilia kwa miaka kadhaa bila hata

kusikilizwa. Serikali iangalie jinsi gani ya kundoa tatizo hili sugu kwani wananchi wamekuwa wavumilivu kwa muda mrefu, tusije kusababisha uvunjaji wa amani yetu kwa sababu ya watu huishiwa na uvumilivu kwa kukosa haki zao kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, suala ya uvunjaji wa sheria na ukiukwaji wa Katiba yamekuwa ni masuala yanayotokea kila leo maeneo mbalimbali hapa nchini. Mbaya zaidi viongozi waliopewa dhamana ya kuwahudumia wananchi kwa makusudi kamili wanatumia nafasi zao kuwanyanya wananchi wanaowaongoza na haswa pale mwananchi anapojitokeza kuhoji masuala ya ukiukwaji wa taratibu au kanuni na miongozo iliyowekwa.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa la kusikitisha sana, kuna wananchi wa Kijiji cha Kasingiri, Kata ya Ilola, Jimbo la Solwa Wilaya ya Shinyanga, vijiji ambavyo wametengwa tangu mwezi 5, 2008 kwa sababu ya kuhoji mapato na matumizi kwa miaka miwili iliyopita. Wananchi hao walitengwa kutokana na kuhoji mapato na matumizi kwenye mkutano wa kijiji uliofanyika tarhe 20/5/2008 ulioitishwa na Diwani wa Kata hiyo. Viongozi waliokuwa wanaendesha kikao hicho ni Ndugu John Kanza, Afisa Mtendaji Kata, Kashinje Castory Masasi, Mwenyekiti wa Kijiji, Joel Iseme, Kaimu Mtendaji wa Kijiji, Buga Buga Debele, Mwenyekiti Kata na Hamisi Makoye , Katibu Kata Sungusungu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuuliza maswali waliorodheshwa majina na hivyo kuwekwa chini ya *quarantine* kwa zaidi ya mwezi mmoja hakuna kutoka. Viongozi hao pia wametoa masharti kuwa ili wafunguliwe, waweze kuwa huru itolewe ng'ombe 20 au mbuzi 100 ndiyo waondolewe kizuizini.

Mheshimiwa Spika, baada ya wananchi kuwa wanateseka walichanga wakatoa mbuzi 100 kwa viongozi hao. Hadi sasa wapo wananchi ambao bado wametengwa kisa wameshindwa kutoa mbuzi au ng'ombe.

Mheshimiwa Spika, huu ni ukiukwaji wa Katiba na uvunjaji wa sheria na zaidi wananyimwa kupata huduma za kijamii za msingi kutoka kwa vijiji vya jirani mfano hospitali na shule. Hata wakifiwa wanazika wenyewe. Sungusungu ndio wapo mipakani wakilinda mpaka watu wasitoke. Hii ni Tanzania au Somalia/Burundi?

Mheshimiwa Spika, suala la kuwepo vyama vingi vya siasa ni suala la Kikatiba na imeridhiwa na Taifa. Hapa nchini mwananchi ye yeyote anaruhusiwa kujiunga na chama chochote anachokitaka ili mradi asivunje sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, viongozi wa Serikali wanatumia nafasi zao kunyanya wananchi wa vyama vya upinzani, likitokea tatizo lolote huko kijijini au kwenye kata wa kwanza kuhisiwa ni mwananchi wa chama cha upinzani. Wanawabambikiza kesi mbalimbali za ajabu ajabu na wengine wanafungwa bila hatia.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya maeneo wananchi kuwa chama cha upinzani ni kosa kubwa, anaonekana ni mhalifu kwa sababu ameamua kujiunga na chama cha upinzani.

Mheshimiwa Spika, tunapenda Waziri atoe tamko hapa Bungeni wananchi wa vyama vya upinzani wana kosa gani?

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuona umuhimu mkubwa wa kuzingatia jinsia katika nafasi nyingi ndani ya Mamlaka ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, nimelisema hili kwa sababu Rais hivi karibuni ameteua Majaji kati ya Majaji 11, saba ni wanawake. Ahsanteni sana Rais wetu. Ukurasa wa 57, kati ya majaji 83, wanawake 28, wanaume 55 si haba, bado Rais ataendelea kuteua ili azma ya Ilani ya CCM ya mwaka 2005 ifikie 50/50.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hatua nzuri ya kuliarifu Bunge kuwa kuna marekebisho yanaletwa kwa sheria ambazo zinamgandamiza mwanamke na watoto pia, naomba sheria hizi ziletwe haraka.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa kuwataka Mahakimu wamalize kesi hasa za watoto wanaopewa mimba.

Mheshimiwa Spika, nataka kumuuliza Waziri mambo yafuatayo, kwa nini wazazi wanafanya makubaliano juu ya mtoto wa kike anapopewa mimba analazimishwa kukaa kimya, mtoto wa kiume anaendelea na masomo lakini mtoto wa kike anakatizwa masomo na anaachwa anahangaika? Je, marekebisho anayofanya Waziri hii sheria itasemaje?

Mheshimiwa Spika, kwa nini watoto wengi wanazaliwa na kutupwa ovyo, huyu aliyetenda kosa hili anakaa katika jamii, kuna uongozi kamili katika eneo hilo huyu mwanamke ameibeba mimba hiyo miezi tisa, kwa nini mwanamke huyu asijulikane? Uongozi hawatambui wananchi wanaoishi nao? Mzazi anayeishi naye hajui?

Mheshimiwa Spika, haki ya mtoto huyu atasimamiwa na sheria ipi? Naomba ufanuzi!

Mheshimiwa Spika, naomwomba Waziri, anieleze ni sheria zipi zinasema nchi hii itakuwa na watoto wa mtaani? Mtoto huyu ananyimwa haki zifuatazo, anakosa elimu, anakosa mapenzi ya wazazi wake na haheshimiwi na jamii. Je, Waziri atanieleza hakuna sheria ambayo itamlinda mtoto huyo ili wazazi wabanwe wasiachie watoto kukaa mitaani bila kupata elimu na iletwe sheria ya kila mtu awajibike kwa watoto wanaowazaa.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa kuhakikisha Mahakimu wanapewa usafiri, hii itasaidia sana na haki itatendeka vizuri.

Mheshimiwa Spika, mwisho namwomba Mheshimiwa Waziri awatambue sungusungu ni jeshi zuri sana katika jamii wepewe motisha. Namwomba Mheshimiwa

Waziri awatake Mahakimu washirikiane na sungusungu katika ulinzi na usalama katika maeneo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Waziri aepuke sana hili suala la Mahakama ya Kadhi sisi wakristo hatukubali hili neno, lipelekwe kwa wananchi walitolee maamuzi na hii Ilani kipengele hiki kitatufikisha pabaya.

MHE. TEDDY LOUISE KASELLA-BANTU: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nampongeza Rais Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuteua Majaji wengi wanawake, kweli inaonyesha kwamba Mheshimiwa Rais anatuthamini na anaamini kwamba sisi wanawake tunaweza, nasi wanawake lazima tujitahidi na tuonyeshe kuwa tunaweza kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuwasemea wananchi wa Nzega na Nzega maana yake ni Jimbo la Bukene na Jimbo la Nzega.

Mheshimiwa Spika, tunaomba kuongezewa Mahakimu wa Wilaya na Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo. Tunahitaji tuwe na Mahakimu nane, lakini tuna watatu tu. Hivyo tuna upungufu wa Mahakimu wa Wilaya watano.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo kumi na mbili lakini tuna watano tu, hivyo tuna upungufu wa Mahakimu saba. Kwa misingi hiyo tunaomba tupatiwe hawa Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo na ya Wilaya ili waweze kutenda kazi yao ipasavyo kwa haki wakiwa hawajachoka sana.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia mishahara yao iko chini sana na wanatoa hukumu ya pengine ya mamilioni ya fedha, kwa mfano shilingi milioni 10 wakati mshahara wao ni shilingi 300,000/= tu. Kwa msingi hiyo naomba waongezewe mishahara na posho ili kupunguza rushwa.

Mheshimiwa Spika, usafiri ni muhimu pamoja na nyumba zao, kwani hawa wanatoa hukumu na baadaye hawana usafiri na hawana nyumba, wanakaa uswahilini. Mimi nafikiri wanatakiwa kuwa na usafiri na nyumba ili wasidhurike na ndugu/jamaa waliowahukumu. Naomba wapatiwe usafiri na nyumba kwa ujumla wao hasa wale wa Wilaya ya Nzega.

Mheshimiwa Spika, Mahakama zetu za Nzega zote ni mbovu basi naomba ukarabati wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, ofisi ya Mahakama ya Wilaya hawana. Ofisi yao iko kwenye ofisi ya *DC* (Mkuu wa Wilaya). Hii si sahihi, Mahakama inatakiwa kuwe na ofisi yake na uhuru wake, hivyo naomba ofisi ya Mahakama ya Wilaya ya Nzega iondoke kwenye ofisi ya *DC*.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Kadhi, mimi naomba kusisitiza kwamba Serikali yetu haina dini na naomba tubaki hapo hapo. Kila dini ni imani na kila dini ina Katiba yake, na ina seminari zake ili kuweka mambo sawa ya kiroho, ili kuhakikisha watu hawa baada ya uhai huu wa mwili, katika ulimwengu wa roho, tupone roho zetu.

Mheshimiwa Spika, Wakatoliki wana ngazi za usuluhishi na hata Waprotestanti naamini wana utaratibu wao. Hivyo vyote tuache dini katika Katiba zao waende *ki-style* yao ili mradi hawadhuru wengine, kwani mwisho wa uhuru wako ndio mwanzo wa uhuru wa mwingine. Uhuru bila mpaka basi ni vurugu, naomba tuheshimu mipaka.

Mheshimiwa Spika, mimi naamimi tukileta sheria ya mirathi, ndoa, ardhi na kadhalika, naamimi wote tutapata haki. Tukipitisha Mahakama ya Kadhi, basi Wakristo nao, halafu tutakuwa hatutoi kero, tutaunda kero nyininge.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. FUYA G. KIMBITA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wangu wa Hai, ninaanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wengine wote Wizarani, hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, awali kabisa, nipongeze jinsi ambavyo mnakuwa waangalifu sana kuhusu swala la Mahakama ya Kadhi ambapo hili suala ni la muda mrefu sana lakini lengo ni kuhitaji umakini mkubwa. Ni vizuri masuala ya itikadi za kidini yakaachwa kwenye dini na Serikali isijiingize katika masuala hayo kwani sasa kila dhehebu/dini watataka wawe/kuwepo na Mahakama yao jambo ambalo badala ya kuboresha ustawi wa jamii itakuwa ni vurugu na kuondoa hali ya utulivu iliyopo hapa nchini kwetu kiasi kwamba hata mataifa mengine ya nje yamekuwa yakijiliza hivi Tanzania pamoja na kuwepo na makabila mengi sana na tofauti za kidini kwa kila raia kuabudu anavyoamini hakuna matatizo yoyote ya kuheshimiana na kupendana.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze pia kwa kuanzisha Kanda mpya za Mahakama Kuu katika maeneo mbalimbali hapa nchini kwani hii itaongeza tija na utolewaji wa haki kuwa wa mapema/haraka zaidi na hivyo kuondoa malalamiko yaliyokuwepo.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze pia kwa kuundwa kwa Tume ya Kurekebisha Sheria mbalimbali haswa zile kandamizi, pamoja na mabadiliko mengine yote yanayoendelea kwa maana ya kuboresha masuala ya sheria zetu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze kwa ujenzi wa Mahakama za Wilaya ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Mahakama ya Wilaya yetu ya Hai na kukamilika, ninatumaini kazi ndogo ndogo zilizobakia zitakamilishwa na hivyo jengo liweze kutumika kama ambavyo imekusudiwa.

Mheshimiwa Spika, nishauri mambo machache yanayohitajika kufanyiwa kazi au kuboreshwa zaidi ili ustawi wa nchi yetu uwe endelevu zaidi na kuwa mahali pazuri pa kuishi kwa kuzingatia utawala wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni rushwa. Tuongeze vita dhidi ya rushwa ikiwa ni pamoja na kuangalia uwezekano wa kuboresha zaidi maslahi ya watumishi wa Wizara na Idara zinazohusika lakini pamoja na kuwachukulia hatua za kinidhamu wale wote wasiofufata maadili ya kazi zao.

Mheshimiwa Spika, pili, ni vitendea kazi. Kuwapatia vitendea kazi ikiwa ni pamoja na vyombo vya usafiri ambapo niwapongeze kwa hatua za mwanzo mlizochukua.

Mheshimiwa Spika, tatu, bajeti. Bajeti ya Wizara ni ndogo, ni muhimu bajeti iongezwe na hivyo kusaidia kuboresha huduma zitolewazo na Wizara hii ikizingatiwa kuwa ni Wizara nyeti inayosimamia utawala wa sheria.

Mheshimiwa Spika, nne, vituo vya kazi. Ni vema wale watumishi waliokaa kwa muda mrefu katika eneo moja la kazi wapelekwe maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MGENI JADI KADIKA: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na kuniwezesha kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Waziri na Naibu Waziri pamoja na wale wote walishiriki kuiandaa hotuba hii ambayo ina mambo muhimu ndani yake.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Kadhi. Mahakama ya Kadhi, ni chombo cha sheria kinachosimamia haki za ndoa, talaka, mirathi, wakfu na mambo ya unyanyasaji wa mtoto. Sheria hii ya Mahakama ya Kadhi, ni ya dini ya Kiislam, Muislam anataka kufuata maneno yanayotoka kwenye Kitabu cha *Quran* na kama hakufuata sheria hizo basi anakosea na anapata dhambi.

Mheshimiwa Spika, nchi nyingi duniani zina Mahakama ya Kadhi na nchi hizo zina dini tofauti kwa mfano Zanzibar, Kenya na nchi nyingi tu na zinaendesha mambo yao vizuri tu hakuna ugomvi wala mashaka yoyote. Kwa nini Serikali haianzishi Mahakama hii ya Kadhi? Ina kigugumizi gani mpaka leo haijanzisha? Nakuomba Waziri ukifanya majumuisho unijibu.

Mheshimiwa Spika, Hakimu ana kazi nzito sana kwa hiyo tuwaangalie kwa kuwaboreshea maslahi yao kwa sababu ni madogo mno. Hakimu huyo kama hatutamboreshea maslahi, usafiri, makazi yao ili asiweze kuchukua rushwa, kwa hiyo tumwezeshe na vile vile Mahakama zetu za Mikoa na za Wilaya ziboreshwani maana ni mbovu, ni mbaya mno, na nyingine zijengwe.

Mheshimiwa Spika, sheria ya mtoto ni lazima irekebishwe kwa mfano, sheria kuwa mtoto aolewe kwa amri ya Mahakama au rizaa ya mzazi au mlezi anapofikia umri wa miaka 15 hii ni kumkosesha mtoto wa kike masomo.

Mheshimiwa Spika, watoto wengi wanabakwa kwa ushahidi kamili lakini la kushangaza utamuona mshtakiwa anapelekwa Mahakamani baadaye kesi ile inakufa kama hakuna kilichofanyika sijui rushwa au ni nini kilichofanyika pale.

Mheshimiwa Spika, tunaomba sheria ichukue mkono wake hata pale mzazi anapompa mtoto wake adhabu kubwa kwa kukosa makosa madogo madogo, kama kumtesa au kumpiga mpaka kumfanya mlemau au kumpiga mpaka kupoteza maisha.

Mheshimiwa Spika, kuna tabia za kimila kuwa mwanamake akifiwa na mumewe anatakaswa na shemeji yake yaani kuingiliwa kimwili, hii ni unyanyasaji na pengine kuambukizwa Ukimwi, hii ni mila potofu. Sheria hii iwekwe wazi ili kukomesha mila potofu kwa kupewa adhabu.

Mheshimiwa Spika, namuombea Waziri na Naibu wake, afya njema na awape maisha marefu ili aweze kulitumikia vizuri taifa hili. Amina.

MHE. MAULIDAH ANNA KOMU: Mheshimiwa Spika, naomba kuwapa pole wale wote wanaofanya kazi ya kutoa hukumu, kwani kazi hii ni ngumu inayohitaji uwe mkweli na mwaminifu na usijali yule unayemhukumu ni nani kwako au ametangulia kukupa nini kwani hukumu ya duniani haishi, hapo hata Mwenyenzi Mungu anakuangalia unapota hukumu kwa mtu na ni hukumu ya adhabu kali wakati unajua fika hakutenda hilo kosa – wanaotoa hukumu wajue wanafanya kazi ngumu.

Mheshimiwa Spika, Katiba ni mkataba wa anayeongozwa na kuongoza. Ni lazima yule ambaye amekuteua kumwongoza ujue unamwongozaje na aridhie kwani yeze ndiye aliyekuweka hapo ulipo, kakukabidhi nchi na mali yake uiangalie na umsaidie yeze mwenyewe, hayo yote yamo katika Katiba.

Mheshimiwa Spika, Katiba hazipatikani kabisa, nilimuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu na alinijibu vizuri kwamba hizo Katiba hupatikana kwenye maduka yanayouza vitabu, lakini cha kusikitisha kuna wananchi hawajapata hata kuiona hiyo Katiba mpaka leo miaka 40 na ushee ya kujitawala, naomba sana Katiba zisambae na sio kugawa bure zisambae na ziuzwe ili wananchi waweze kuzipata na wajisomee wajue haki zao za msingi, Serikali ni nini kwao na anahitaji nini kutoka kwenye Serikali yake na yeze afanye nini kwa Serikali yake.

Mheshimiwa Spika, sheria ni kitu muhimu na bila kuweka sheria hakuna utawala, lakini unapoona sheria inapindishwa kwa ajili fulani inasikitisha, nimeshaongea huko mwanzo.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ndipo panapota haki na anayetoa haki hiyo ni binadamu na kama tunataka Mahakama itoe haki basi muhimu kuhakikisha maslahi mazuri kwa Mahakimu toka wale wa Mahakama ya Mwanzo mpaka wale wa Mahakama Kuu. Maslahi mabovu, upungufu wa vitendea kazi na upungufu wa usafiri wa kuwawezesha kufika mahali pa kazi, yote haya ni muhimu, Hakimu anatembea kwa miguu kwenda kutoa hukumu, ni aibu.

Mheshimiwa Spika, kuna Mahakama mbalimbali kwa mfano Mahakama ya Biashara, Mahakama ya Ardhi na Mahakama ya Kazi, Mahakama hizi zote, zinatoa hukumu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naomba sana kuwepo na Mahakama itakayoshughulikia kesi za ndoa na mirathi kwani mpaka sasa wanandoa wanapotalikiana, Mahakama huwa zinachelewa kutoa hukumu ya nani atunze watoto na kwa vyovoyote mama ndiye huachiwa kazi ya kutunza hao watoto mpaka hukumu inapotolewa na hapo basi nani anagharimia matunzo hayo? Ni mama!

Mheshimiwa Spika, mirathi, baba anapofariki kuna kukaa siku 90 kabla kesi hazijaanza kusikilizwa, mali ya marehemu nani arithi na hapo hapo yule anayeteuliwa na ukoo kuwa msimamizi kama si mama mwenyewe huanza vituko na kuchelewesha uamuza.

Mheshimiwa Spika, sheria zinazohusu wanawake na watoto, sheria hizi zimekuwa zikipigwa chenga mpaka inatia huzuni, hivi kuna nini? Naomba nijulishwe kuna nini mpaka leo ndio tunaanza kusema kwamba kunaandaliwa waraka wa kuwashirikisha wananchi walio wengi zaidi kutoa maoni yao kuhusu sheria zinazohusu wanawake na watoto? Hiyo ni janja tu wanawake wanaendelea kuteseka, watoto wadogo wa chini ya miaka 18 wanaolewa kwa idhini ya mzazi au mlezi, kitu ambacho sio kizuri. Ndoa ni mkataba inakuaje leo mtoto wa miaka 15 alazimishwe kukubali kwenye mkataba wa ndoa na kupewa waraka aweke saini yake kwamba amekubali?

Mheshimiwa Spika, sheria za nchi zinasema, naomba ninukuu; “Mtu ye yeyote ambaye hajafikia umri wa miaka 18 haruhusiwi kuweka saini mkataba wowote ule.” Mheshimiwa Spika, je, leo inakuaje mtoto wa umri wa chini ya miaka 18 anaweka saini mkata wa ndoa?

Mheshimiwa Spika, leo tunasema tunataka maoni, yapi wakati watoto wadogo wanaozeshwa, wanapata mimba, wanashindwa kuzaa wanakufa wao na watoto wenzao waliowazaa!

Mheshimiwa Spika, tufanye bidii sheria hizi zije Bungeni ziridhiwe ili ziwe sheria kamili, mateso ni mengi sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. JOEL N. BENDERA: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Mathias M. Chikawe, Waziri wa Wizara hii, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wataalam mbalimbali wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba hii na kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara pamoja na matatizo mbalimbali yanayowakabili.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu nitauelekeza kwenye mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni upungufu wa Mahakimu nchini hususan Wilaya ya Korogwe. Wilaya ya Korogwe ina Tarafa nne, Bungu, Mombo, Magoma na Korogwe. Katika Tarafa hizo, kuna Mahakama za Mwanzo katika maeneo mengi kama vile Mashewa, Magoma, Makuyuni, Mnyuzi na kadhalika. Hizo Mahakama nilizozitaja, hazina kabisa Mahakimu. Katika Tarafa zetu hizo pia hakuna Mahakimu. Jambo hili linasikitisha sana. Ombi langu, ninaomba sana nipatiwe Mahakimu katika Mahakama hizo ili wananchi wapate haki yao wanayostahili.

Mheshimiwa Spika, pili, Mahakama ya *Old Korogwe*. Mahakama hii ni mpya lakini hadi leo hii haijafunguliwa. Hivi tatizo ni nini? Naomba kupata maelezo. Mahakama hii ndio inayotegemewa sana kwa sababu ipo mjini toka wakati wa ukoloni. *Old Korogwe* kulikuwa na Mahakama na ndio maana Serikali yetu ya Awamu ya Nne ikaona umuhimu wa kujenga Mahakama mpya na ya kisasa Old Korogwe. Tunaomba Mahakama hii ifunguliwe na tupatiwe Mahakimu. Kwa kuwa majengo yamekwisha ni lini sasa itafunguliwa?

Mheshimiwa Spika, tatu, Mahakama ya Hale kupatiwa Hakimu. Hii ni Mahakama mpya na ya kisasa lakini hadi leo hii huu ni mwaka wa tano haina Hakimu. Hii ndio Mahakama inayotegemewa na Wilaya ya Korogwe na Wilaya ya Muheza kwa kuhudumia zaidi ya Kata nne ikiwemo na Kata ya Michungwani Wilaya ya Handeni. Kinachofanyika ni kuletwa Hakimu toka Korogwe kwa zamu. Jambo hilo ni kero kwa wananchi wa maeneo hayo. Ninaomba ufumbuzi wa kero hii sugu.

Mheshimiwa Spika, nne, matatizo ya upatikanaji wa mirathi. Hili ni tatizo sugu sana, upatikanaji wa mirathi baada ya wazazi au wahusika kufa, inachukua muda mrefu sana. Mlolongo wa kupata hundi, ni mrefu sana. Ninapenda kufahamu ni sababu zipi za msingi hundi zinachelewa sana kupatikana? Hali hii imefanya sana wananchi kukata tamaa ya kupata mirathi yao. Mimi nina mfano wa watoto ambao wamefiwa na baba yao alikuwa Mwalimu, pamoja na mimi mwenyewe kuwasaidia wamechukua zaidi ya miaka mitatu kupata mirathi yao ya kwanza hadi leo hii hundi ya pili ambayo ndio yenye malipo mengi hawajaipata. Ninaomba sana suala hili litafutiwe ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, tano, vitendea kazi. Mahakimu na wafanya kazi wa Mahakama wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Jambo hili linatamanisha rushwa. Ninaomba sana jambo hili lirekebishwe kwa kuwa haipendezi Hakimu wa Wilaya anakosa usafiri ni hatari.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuunga mkono hoja.

MHE. MCHUNGAJI DR. GETRUDE P. RWAKATARE: Mheshimiwa Spika, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri na watendaji wake wote kwa hotubu nzuri ambayo imekidhi mahitaji ya Watanzania wengi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba na mimi nichangie yafuatayo. Kwanza, ni Mahakama ya Kadhi. Serikali haina dini. Serikali ni watu wote na dini zote, Waislam na wakristo. Tusilazimishe sheria za dini zetu ziingizwe kwenye Serikali. Wakristo

wamalize matatizo yao Kikristo na Waislam wamalize matatizo yao Kiislam. Serikali, ishirikishwe tu kwenye yale yanayoshindikana kwenye dini zetu. Serikali isibebeshwe mzigo wa dini zetu.

Mheshimiwa Spika, pili, sheria kali zichukuliwe kwa wanaume wanaowapa mimba watoto wa shule. Kwa sababu ni waharibifu, wanaharibu maisha ya wanawake na wanaua matarajio ya wazazi na wasichana na kadhalika, wafungwe/wakamatwe.

Mheshimiwa Spika, tatu, sheria za unyanyasaji wa wanawake za mwaka 1971 zibadilishwe maana zimepitwa na wakati na zinazidi kugandamiza wanawake. Wanaume wengi wanaona ni haki yao kuwadharau na kuwatumiwananawake na baadaye kuwatelekeza na watoto wao wahangaike. Wanaume wanaotelekeza watoto na wake zao wafungwe na wapigwe viboko.

Mheshimiwa Spika, nne, Wazee wa Baraza, wapewe *uniform*, hali zao ni mbaya na kazi wanazofanya katika Mahakama zetu, tuuheshimu mchango wao.

Mheshimiwa Spika, Mahakama nyingi za Mwanzo zinahitaji ukarabati. Nyingi ni magofu au *pombe shop*, hali yake hailingani na kazi kubwa ya Mahakama.

MHE. SIRAJU JUMA KABOYONGA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote katika Wizara kwa matayarisho mazuri ya bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, maslahi ya wafanyakazi (Wanasheria). Wanasheria wa Serikali wanalipwa mishahara midogo kwa kulinganisha na Wanasheria katika maeneo mengine wenye viwango vinavyofanana kitaaluma. Ndiyo maana Wanasheria wengi wa Serikali wanahama kwenye mashirika mengine.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali irekebishe maslahi ya Wanasheria wa Serikali kuanzia mishahara, hadhi ya ofisi, vitendea kazi kama vile magari, *computer, uniforms* na kadhalika. Ni hatari kwa Wanasheria wetu kutumia *public transport* na kuishi katika maeneo ya watu wengi bila kujali hatari zinazowakabili toka kwa baadhi ya wahalifu wanaowashughulikia Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, jengo la Mahakama Tabora. Jengo hili halitoshi kwa shughuli za Mahakama Kuu ya Kanda ya Tabora. Kwanza, ujenzi wake haukidhi mahitaji ya Mahakama. Hili ni jengo ambalo lilikuwa ni ofisi ya Manispaa ya Tabora. Lilipochukuliwa na Mahakama ndipo lilipofanyiwa marekebisho ili kukidhi mahitaji ya Mahakama. Kadri shughuli za Mahakama zinavyoongezeka, jengo hili sasa limeelemewa. Naishauri Serikali itenye fedha za kuanza ujenzi wa jengo la Mahakama ya kisasa Mjini Tabora. Aidha, naipongeza Serikali kwa kuongeza idadi ya Majaji. Lakini uteuzi huu wa Majaji sasa umezaa tatizo la uhaba wa nyumba za Majaji na Mahakimu. Naishauri Serikali itafute ufumbuzi wa tatizo la nyumba za Majaji na Mahakimu.

Mheshimiwa Spika, mishahara ya Mahakimu na Wanasheria wa Serikali. Hivi karibuni Serikali ilipandisha mishahara ya Majaji, naipongeza Serikali kwa uamuzi huu.

Lakini naikumbusha Serikali kwamba kazi nyingi za kisheria zinafanywa na Mahakimu pamoja Wanasheria wa Serikali. Bila ya utendaji mzuri wa Mahakimu na Wanasheria wa Serikali, kazi za Majaji zitakuwa ngumu sana. Kwa hiyo, naishauri Serikali iharakishe marekebisho ya mishahara ya Mahakimu na Wanasheria wa Serikali kwa kuzingatia umuhimu wa ugumu wa kazi wanazozifanya.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Kadhi. Naishauri Serikali ikamilishe uchambuzi wa mawazo mbalimbali yaliyokwisha kusanya kuhusiana na suala la Mahakama ya Kadhi na kulitolea uamuzi wa namna moja au nyingine kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

MHE. DR. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na Wizara yake kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii muhimu ya kutenda haki na kulinda amani na maisha ya mwanadamu.

Mheshimiwa Spika, kuna uhitaji mkubwa sana wa Wanasheria na Mahakimu kwenye Mahakama zetu huko Mikoani. Bahati nzuri, vijana wengi kwa sasa wanachukua masomo ya sheria kwenye vyuo mbalimbali hapa Tanzania. Ombi langu ni kuwa kwa sababu ya uhitaji mkubwa wa Wanasheria hawa, vijana au Wanasheria wanaohitimu vyuoni, waajiriwe mara moja kama Walimu wanavyoajiriwa mara moja wanavyomaliza masomo yao huko vyuoni.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kesi huko Mahakamani zinakaa sana bila ya hukumu au kushughulikiwa. Kwa hiyo, ombi langu, kesi hizi ziangaliwe na ziishe haraka bila kukaa muda mrefu. Mahakimu hao wachache tulionao wajitahidi kumaliza kesi hizi kwa muda mfupi. Hii pia inasababishwa na mlundikano wa mahabusu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Wizara iangalie sana nyumba/makazi ya wafanyakazi wake kwa ujumla. Najua bajeti ni ndogo, lakini tufanye kazi za kuboresha nyumba au makazi ya wafanyakazi hawa kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru Mheshimiwa Waziri kwa kazi anayoifanya, utendaji wake mzuri wa kazi, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba utuangalie Mkoa wetu wa Morogoro na Pwani kwa kutuungezea Mahakimu na ukarabati wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, *Law School*, vijana wengi sasa wanavutiwa na Wizara hii na kuamua kuchukua masomo ya sheria. Ni kweli ghamra (*fees*) za *Law School* ni kubwa sana. Naomba tuone tutafanyaje ili vijana hawa wapatiwe mikopo ili wamalizie vizuri masomo yao na kuajiriwa mara moja.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia.

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Spika, hoja inayotaka kuleta Mahakama ya Kadhi, ninaipinga. Sababu zangu ni hizi zifuatazo:-

Kwanza, inapingana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Serikali haina dini;

Pili, Ilani ya CCM haisemi tulete Muswada wa kuleta Mahakama ya Kadhi, inasema italipatia ufumbuzi;

Tatu, wapagani ndio wengi nchini, Wakristo na Waislam ni *minority* tu. Kwa nini tufanye ubaguzi kinyume cha Katiba?; na

Nne, kama Serikali iko *serious* na hoja hii basi tufanye *referendum*.

Mheshimiwa Spika, baada ya haya, naomba kuunga hoja ya Waziri wa Katiba na Sheria.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, suala la *Law School* liangaliwe kwa makini sana. *The School* iruhusu wanafunzi wajisajili kabla ya kulipa ili waweze kudahiliwa. Hivi sasa wanazuiwa kudahiliwa mpaka walipe shilingi 500,000/=. Hebu tuwasaidie hawa vijana ili waweze kusoma bila vikwazo. Tafadhali suala la *Law School* liangaliwe kwa kina kabisa.

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria na Katibu Mkuu wake, kwa kazi nzuri sana ya kuandaa hoja hii.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichangie machache kuhusu Mahakama ya Kadhi. Mimi sioni ugomvi uko wapi wa kuwa na Mahakama hizi kama kitaruhusiwa kuendesha mambo yao bila kutumia mfumo wa Serikali, waendeshe mambo yao bila kuingiza Serikali. Katiba ya nchi lazima iheshimiwe. Sipendi kutoa vifungu vyta Katiba, maana Waziri anavielewa. Naomba niitake Serikali ilete Bungeni maoni ya Serikali ili tujadili kwa undani athari za kuwa na chombo hicho katika sheria zetu.

Mheshimiwa Spika, suala la adhabu ya kifo, nililileta miaka miwili iliyopita ndani ya Bunge hili. Bado ninaamini kuwa Tume ya Kurekebisha Sheria italeta utafiti wake humu Bungeni ili tuijadili na tutoe ushauri wetu na kushirikisha Wabunge wote kwa niaba ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa sasa nimuombe Mheshimiwa Waziri, aone namna ya kusaidia uimarishaji wa maslahi ya watumishi wote wa Mahakama. Tuanzie na Mahakimu wa ngazi zote kuanzia Mahakama za Mwanzo hadi Mahakama Kuu. Hili ni jukumu letu sote ili kuleta utawala bora nchini, lazima mishahara yao na posho zao ziweze kuwapunguzia adha ya kuwa omboomba na wapokea rushwa ili shida zao ziweze kuangaliwa kwa mapana yao.

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru Waziri kwa kutupatia Mahakama Kuu mjini Sumbawanga. Mafanikio ya kazi katika Mahakama hizi, yatatokana na motisha za ziada kwa watumishi wanaoletwa Mikoa yetu ya pembezoni. Posho, fedha za *OC* na zana za

kazi, ni budi vikapewa upendeleo maalum kwa kila hali ili wasiwe wanaonekana wametumwa huko kama adhabu.

Mheshimiwa Spika, mlundikano wa mahabusu Magerezani, unaweba kupunguzwa iwapo kutakuwa na utaratibu wa kuzitembelea mahabusu hizi kwa Wabunge ili kwenda kusikia malalamiko yanayotolewa ili kwa yale yanayoweza kutatuliwa kwa njia rahisi na hivyo kupunguza mlundikano wa wafungwa na mahabusu wengi ambao wengine hubambikizwa kesi zao, bila hata kupata nafasi ya kujieleza vizuri mbele ya vyombo nya dola.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Spika, uhamisho wa Mahakimu. Uhamisho wa watumishi wa Serikali, ni jambo la kawaida. Kwa mujibu wa taratibu za Serikali, mtumishi wa Serikali anapaswa kukaa katika kituo kimoja cha kazi sio zaidi ya miaka mitano na sio chini ya miaka mitatu. Utaratibu huu hautekelezwi sehemu nyingi kwa sababu ya ukosefu wa fedha za uhamisho. Lakini utaratibu huu ulikuwa na maana yake. Hakimu kwa mfano kukaa katika kituo kimoja miaka 10 – 15, ina matatizo yake kama ifuatavyo:-

- Hakimu atazoeleka kiasi cha hukumu zake kutodhaminiwa;
- Hana tofauti na mwanakijiji kama hajaenda shule (kozi) kupigwa msasa;
- Matajiri na watu mashuhuri watamtumia vibaya; na
- Atashawishika kupokea rushwa hususan kwa watu wasiojua haki zao kiraia na kisheria.

Mheshimiwa Spika, kesi za mimba kwa watoto wa shule na ubakaji. Hili limenikuta. Mtoto wa dada yangu baada ya kumaliza elimu ya msingi mwaka 2005, alirubuniwa na mwanamume mmoja kwamba atamtafutia shule ya sekondari. Alimpeleka mjini na kulala naye *guest!* Baada ya matokeo ya mtihani wa *STD VII* kutoka, binti yule mdogo (miaka 14) alifaulu na kupangiwa *Kinampanda Secondary School, Form I*. Mimba ile ilizidi kukua na hatimaye alizaa lakini kiumbe kile kilifariki!

Mheshimiwa Spika, nilifungua kesi *RM Court Arusha* na mhalifu kupatikana na hatia na kufungwa kwa kosa la ubakaji miaka 30! Mheshimiwa Waziri, cha kushangaza ni kuwa mhalifu yule alikaa ndani miezi miwili na nusu tu katika Gereza Kuu la Arusha akaachiwa huru na Mahakama hiyo kwa vyovyote rushwa ilitumika kumnyima haki binti yule lakini yote tulimwachia Hakimu wa Kujitegemea (*Mwenyezi Mungu*) ambaye kwa wakati muafaka kwake atatoa hukumu yake ama kwa mtoe rushwa au kwa mpokea rushwa ama kwa wote wawili kwa jinsi anavyoona inafaa!

MHE. SUSAN A.J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, ucheleweshaji wa kesi Mahakamani. Ni ukweli ulio wazi kwamba wafungwa wengi au watuhumiwa, wamekuwa wakisota kwa muda mrefu sana bila kupatiwa hukumu zao. Kwa kiasi kikubwa, ni kwa sababu ya ukosefu wa Mahakimu na Majaji. Ninaamini baada ya kupata Chuo cha Sheria cha Lushoto na uwepo wa Vyuo Vikuu vyta Umma na Binafsi vinavyotoa Shahada na Stashahada za Sheria kutapunguza sana tatizo hili kwa kuwa watuhumiwa wengi wanabambikizwa kesi na hivyo kukaa kwa muda mrefu bila hukumu ni kukiuka haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu. Kumekuwa na tatizo kubwa sana la wananchi kutokujua haki zao na hivyo hata wanapodalilishwa au kufanyiwa maovu yoyote yale, wanashindwa kujua waende wapi na wengine kujichukulia sheria mkononi. Pamoja na kuwa na Tume ya Haki za Binadamu bado haijasaidia sana wala haijelimisha vyta kutosha. Tunaomba Tume hii itoe elimu ili wananchi wajue haki zao na hivyo waweze kujitetea pale wanapooneewa.

Mheshimiwa Spika, sheria zinazokinzana. Kuna tatizo kubwa sana la Sheria hasa ile ya Ndoa kwamba mtoto anaweza kuolewa akiwa na miaka 15 ambapo ile Sheria ya SOSPA (*Sexual Offences Act ya 1998*), inamtambua mtoto kama mwenye umri wa 18 kwenda chini. Kwa maana hiyo binti akiolewa na miaka 15 – 18 ni mtoto!! Lakini miaka 15 ni mtoto wa ‘O’ level kwa hali yoyote ile. Ni kutokana na ukinzani wa sheria hiyo ndio maana wanaendelea kuoa watoto hawa.

Mheshimiwa Spika, kuna hawa wazee wa Mahakama ambaa ni muhimu sana lakini posho wanazopata ni ndogo mno. Wazee hawa wanapati Sh.1,500/= lakini unakuta anasimamia kesi ya milioni kumi na kuendelea. Hivi hawa wenye kesi wataancha kuhonga hawa wazee?

Mheshimiwa Spika, makazi ya Mawakili/Mahakimu. Ni wazi kuwa watu hawa wanaishi ndani ya makazi ya jamii na hivyo ni rahisi sana kuhongwa. Mfano unakuta amepanga kwenye nyumba ya mtuhumiwa. Ni rahisi sana kupindisha maamuzi ili asifukuzwe kwenye nyumba.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ni *uniforms* zao (*Suits*). Wakili anapaswa kuwa na *uniform* safi na walau tatu na ili aweze kubadili *suit* hizi ni zaidi ya Sh.200,000/= lakini kutokana na mshahara mdogo, wengi wao huishia kuva mitumba, hii ni hatari sana.

Mheshimiwa Spika, ubakaji. Ubakaji ni tendo si tu la kudhalilisha lakini ni la kiuaji kwa maana ya kuua kisaikolojia (utu wa mtu) lakini pia kuua kimwili kwa maana ya kupoteza uhai lakini pia kuambukiza maradhi ya Ukimwi na hatimaye kifo.

Mheshimiwa Spika, ubakaji umekuwa ukiongezeka kwa kasi kubwa pamoja na sheria iliyopo ya mbakaji kufungwa miaka 30. Kibaya ni kwamba sasa hivi wabakaji wamekuwa wakishirikiana na familia za wabakwaji hususan wazazi na kuwapa fedha ili

wamalizie mambo hayo nyumbani. Hii yote ni kwa sababu ya wazazi kutokuwa na elimu ya kutosha na umaskini. Tunaomba Tume ya Haki za Binadamu itembelee vijijini ili kutoa elimu juu ya haki zao.

Mheshimiwa Spika, vinginevyo wananchi wachukue hatua ikiwa ni pamoja na kukata sehemu za siri za wanaume hawa kwani wameamua kutumia sehemu zao za siri kama silaha za maangamizi dhidi ya wanawake, basi ni wakati muafaka kwa wanawake hawa kujibu mapigo kwa kuteketeza silaha hizo za maangamizi. Wanaume lazima waelewe umuhimu wa wanawake na hivyo wajue thamani yao na kwamba miili yao (wanawake) si kwa ajili ya kuingiliwa au *disposable* kama *toilet papers*.

MHE. BENITO W. MALANGALILA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nichangie yafuatayo:-

Kwanza, kuhusu Sheria ya Mirathi, ni ya muda mrefu sana sasa, wanawake wajane, watoto yatima, wamekuwa wakidhulumiwa na ndugu wa marehemu. Baada ya marehemu kuzikwa, hujitokeza ndugu ambao hujifanya wakarimu, ni watu ambao wangkuwa msaada sana kwa mjane au wajane pamoja na watoto kumbe mara nyingi watu wa namna hiyo huwa matapeli na wengine husingizia sheria za mila, dini kukandamiza wajane na yatima. Hivyo, nashauri itungwe sheria moja tu ya kitaifa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni Mahakama ya Kadhi, kama Waislam wanataka kuanzisha wao wenyewe wakae na waamue lakini si kazi ya Bunge hili kuwatungia sheria, gherama za uendeshaji wa Mahakama hii bila shaka itakuwa mabegani mwao lakini haitawezekana zibebwe na watu wengine ambao hawahusiani na dini hiyo, hata hivyo taifa hili halina dini. Tumefungua *box* lenye mambo mengi magumu, zipo dini na madhehebu yenze sheria zao. Kwa hiyo, tunakoelekea ni pabaya sana. Mimi binafsi hoja hii siiungi mkono.

MHE. MWAJUMA HASSAN KHAMIS: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ni kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijaalia kwamba niko mzima. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake ambayo ina mwelekeo wa kumpatia haki zake mwananchi kwa misingi ya sheria.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hayo, sasa naomba nitoe mchango wangu katika hotuba husika. Kwanza, kuhusu mikataba. Hivi karibuni nchi yetu ilisaini Mikataba ya Kimataifa kuhusu haki za binadamu kwa ujumla na haki za makundi maalum zikiwemo sheria za watoto. Tanzania imesaini na kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto wa mwaka 1989. Kwa kuzingatia mikataba yetu ya kibinadamu sio sahihi jinsi Mtanzania wa leo anavyofanyiwa.

Mheshimiwa Spika, kumejitokeza mauaji ya kinyama katika nchi yetu. Kuna wanaouliwa kwa misingi ya uchawi, hawa ni Malbino na wazee wakongwe. Pia kumejitokeza tabia ya watu kuwaa wenzao na kuwatia moto, eti kwa sababu ameiba. Kama mikataba yenyewe ni hivyo basi bado haki za binadamu hazijapatikana. Naiomba Serikali itueleze ni jinsi gani inajiandaa kuzuia mauaji hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sheria. Kwa kuzingatia hali ya Watanzania walivyo, inaonesha wazi sheria za nchi yetu kwa misingi ya haki yake hazijulikani. Je, kupitia bajeti hii isiyokidhi hoja, Wizara itafanya maajabu gani ya kuwawezesha Watanzania kujua sheria ya nchi yao?

Mheshimiwa Spika, kuhusu rushwa, watendaji wakuu Wizarani kuna udhaifu wa kutoa huduma kwa sababu ya rushwa hasa katika maeneo ya Mahakama ngazi za Mahakama za Mwanzo na Wilaya. Kwa kuwa neno rushwa limezagaa nchini na kuzaa mtoto mwingine ajulikanae ujisadi, je, Serikali inajиandaa vipi kutokomeza neno rushwa pamoja na ujisadi?

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hayo, sasa naomba nimalizie kwa kumpungeza Mheshimiwa Waziri na kumuombea kwa Mungu ili ampe uwezo wa kufanikisha azma yake katika Wizara yake. Ahsante.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Spika, leo katika nchi yetu, kuna malalamiko makubwa ya wajane, kukoseshwa mali zao na watoto kukoseshwa mirathi zao badala yake mirathi hizo huchukuliwa na watu wasiostahili.

Mheshimiwa Spika, jamii ya kiislamu itakapokuwepo Mahakama ya Kadhi suala la ndoa, talaka, mirathi na mizozo misikitini, litakuwa limeshapata ufumbuzi unaostahili.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani kabisa kwa Muislam yejote suala la ndoa, talaka, mirathi kuhukumiwa kwa Mahakama hizi tulizonazo, kufanya hivyo kutasababisha hukumu hizo ziende kinyume na kitabu cha Mwenyezi Mungu, *Quran*. Iteleweke Mahakama ya Kadhi itawahudumia Waislam tu.

Mheshimiwa Spika, Kiswahili ndio lugha yetu ya Taifa lakini bado sheria zetu zinaandikwa kwa Kiingereza. Kwa kufanya hivyo, ninajiuliza na pia ninawauliza sheria hizo zipo kwa ajili ya nani? Ni dhahiri wanaolewa Kiingereza, tena sheria, ni wachache mno hapa nchini. Inavyotakiwa sheria zieleweke ili wanandhi wajue wajibu na haki zao.

Mheshimiwa Spika, nadhani umefika wakati sheria zote zitafsiriwe kwa Kiswahili na sheria zote mpya zitungwazo ziwe kwa Kiswahili. Ipo haja kwenda kusoma kwa wenzetu wa Zanzibar ambapo sheria zote zinazotungwa na Baraza la Wawakilishi ni za Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia runinga na kusoma magazeti, utagundua kuwa uvunjwaji wa haki za binadamu katika baadhi ya matukio. Wananchi wakati mwingine wanabakia kulalamika tu licha ya kuwepo Tume ya Haki za Binadamu. Kwa mazingira hayo, inadhihirisha kuwa uelewa wa wananchi juu ya kuwepo Tume hiyo ni mdogo. Kwa hivyo, ipo haja ya Tume wenye kutoa elimu ya kutosha ili ueleweke kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. MARIAM R. KASEMBE: Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii, kuwashukuru na kumpongeza Waziri pamoja na viongozi wote katika Wizara hii kwa maandalizi mazuri ya hotuba ya bajeti ya mwaka 2008 – 2009 ambayo imelenga katika kuzingatia utawala bora na kutatua kero zilizopo katika Ilani ya uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo mengi ya nchi yetu hususan Mkoa wa Mtwara, wananchi wamekuwa wakipata shida sana katika kupata haki za kisheria kwa kuwa Kata nyingi zipo mbali sana na Mahakama za Mwanzo au za Wilaya na hata sehemu zilizopo hali ya watumishi haitoshelezi, vitendea kazi vichache na hata nyumba za watumishi katika Mahakama hizo za Mwanzo hakuna hivyo kupelekea Mahakimu kukaa mbali na vituo vyao vya kazi. Kwa kutambua tatizo hili, wananchi hawa wameamua kujenga Mahakama na nyumba za watumishi hususan katika Wilaya ya Masasi kata ya Lukuledi. Ombi langu kubwa kwa Wizara hii, ni kutambua jitihada hizi za wananchi ambao wanapenda kuwa na vyombo vya haki kwa kuwasaidia au kuwawezesha vifaa vya ujenzi ili kufanikisha ujenzi huo wapate kujenga nyumba bora na zenye hadhi ya kisasa. Ni matumaini yangu kuwa Wizara itazingatia ombi hili katika utekekezaji.

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu hadi sasa akina mama wengi na jamii kwa ujumla, wamekuwa wakipata shida sana katika kufuatilia mirathi mara wanapopatwa na tatizo la kufiwa na ndugu kwani kumekuwa na usumbufu mkubwa na kuchukua muda mrefu katika kufanikisha kupata haki zao na kutumia gharama kubwa katika ufuatiliaji. Je, ni nini kinachosababisha usumbufu mkubwa huo? Je, Serikali haioni ni wakati muafaka wa kuangalia dosari zilizopo ili zirekebishwe ili wananchi hawa ambao hupata shida waondokane na usumbufu huo?

Mheshimiwa Spika, hadi hivi sasa kumekuwa na mwendelezo mkubwa kwa akina baba kuwanyanya akina mama na kupelekea akina mama hao kutelekezwa wakiwa na watoto, hivyo watoto hawa kukosa haki zao za kupata huduma muhimu za kimsingi na mwisho kuishia kuwa na mazingira magumu na kuishia kuwa watoto wa mitaani.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika ubakaji umekuwa ukiendelea kwa kasi hali ambayo imekuwa wakifanyiwa watoto, vikongwe na wanawake kwa ujumla, je, ni kwa nini hali hii inakua kwa kasi kubwa na wakati sheria ipo? Je, sheria ina upungufu? Kama yapo, Serikali itarekebisha lini sheria hii ili iweze kuwabana wahalifu hawa ili kupunguza hali ya unyanyasaji na ubakaji unaoendelea?

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ucheleweshaji sana wa kesi nyingi katika Mahakama zote jambo ambalo huleta kero kubwa kwa wananchi na wengine hupelekea kufuta kesi zao au kutohudhuria siku za kesi zao zinapotajwa, hivyo kupoteza haki zao za kisheria. Je, Serikali haioni hali hii hupelekea mianya ya rushwa? Ni lini Serikali itaweza kusimamia chombo hiki ili kuondoa kabisa tatizo hili na kazi zitekelezwe kama inavyotakiwa?

Mheshimiwa Spika, mwisho nirudie kuipongeza Wizara hasa Waziri anayeongoza Wizara hii kwa umakini na mipango mizuri ambayo ninaamini sana kama ikitekelezwa, haki zitatendeka na matatizo mengi yataisha.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, nikiwatakia kheri na ufanisi katika utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA: Mheshimiwa Spika, nauga mkono hoja. Pongezi kwa kusimamia Wizara hii nyeti.

Kwanza, ukarabati wa Mahakama ya Magamba, Nzundu na Mazingwa Wilaya ya Handeni pamoja na nyumba za Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, ufanyike.

Pili, uharakishaji wa kusikiliza kesi; na tatu, suala la watumishi lipewe kipaumbele.

MHE. MARGRETH AGNESS MKANGA: Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Jaji Mkuu, Majaji, Mahakimu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba nzuri inayoleweka na yenye mwelekeo wa kuweza kutekelezeka.

Mheshimiwa Spika, naipongezwa Wizara kwa kutoa maelekezo thabiti (uk. 43), kuhusu umuhimu wa kumaliza haraka kesi zote zinazohusiana na kupewa mimba kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari. Hii itasaidia kujua hatma ya wahalifu husika na labda kusaidia ukomeshaji wa tabia hii mbaya.

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa sana kusikia kuwa sheria mbalimbali za kulinda maslahi na haki za mtoto zimepitwa upya na Serikali na kwamba marekebisho yake yanatarajiwa kuletwa Bungeni katika mwaka huu wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nimetatanishwa sana na maelezo kuwa kuna sheria kadhaa ambazo bado tafiti zake zinaendelea kufanyika ikiwemo ile Sheria ya Kutetea Haki za Watu wenye Ulemavu (*Disability Law*).

Mheshimiwa Spika, wakati Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Waziri mhusika alipokuwa akijibu hoja za Waheshimiwa Wabunge mbalimbali, alitoa taarifa kuwa Rasimu ya Sheria tajwa hapo juu iko karibu kukamilika na italetwa hapa Bungeni katika mwaka huu wa fedha. Sasa nimechanganyikiwa kipi ndiyo kipi? Bado utafiti unaendelea au imekaribia kukamilika ili kuwezesha Muswada kuwasilishwa Bungeni kwa maamuzi?

Naomba ufanuzi kwa sababu vinginevyo jamii ya watu wenye ulemavu hawataelewa kwa vile wengi wao walitegemea kusikia ni lini hasa Muswada huu italetwa Bungeni kama Wizara mama ya masuala ya watu wenye ulemavu ilivyotoa matumaini juu ya sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba ufanuzi kuhusu *Law School* kama itatoa pia Mafunzo ya Diploma baada ya mhusika kuwa amemaliza Digrii ya Kwanza na endapo pia mafunzo ya Cheti yanaweza kutolewa na chuo hicho.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja, ahsante sana.

MHE. ANIA SAID CHAUREMBO: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika hoja ya Wizara ya Sheria na Katiba ya mwaka 2008/2009 na pongozi kwa Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu kumekuwa na suala la kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi bila ya mafanikio. Je, tatizo ni nini? Maana hivi sasa kuna mambo mengi ya Kiislam, sheria na maagizo ya kitabu cha Kiislam, *Quran* zinatakiwa zifuatwe na sioni sababu ya jambo hili kutopatiwa ufumbuzi maana kuna ukiukwaji mkubwa katika Mahakama zetu kuhusu Sheria za Ndoa na Ardhi za Kiislam.

Mheshimiwa Spika, sjui kwa nini Tanzania inakuwa na kigugumizi katika suala hilo, wakati nchi jirani kama Kenya na Uganda na upande mmoja wa Muungano Zanzibar zipo Mahakama za Kadhi na hakuna tatizo lolote na ni muda mrefu sasa.

Mheshimiwa Spika, matumizi mabaya ya sheria na kutotumia sheria zilizopo. Kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa baadhi ya sheria, mfano tunashuhudia wafanyabiashara ndogo ndogo wakinyang'anywa bidhaa zao au kuchukuliwa mali zao bila ya wao wenyewe kufikishwa katika vyombo vya sheria.

Mheshimiwa Spika, chaguzi za Serikali za mitaa, kumekuwepo na ukiukwaji mkubwa wa sheria. Katika Halmashauri, Wakurugenzi wamekuwa wanasasa na kuvunja sheria zilizopo lakini hili zaidi linatokana na utaratibu huu wa TAMISEMI kuendelea kusimamia chaguzi za Serikali za Mitaa. Naomba, wakati umefika sasa wa chaguzi za Serikali za Mitaa zisimamiwe na Tume ya Uchaguzi ya Taifa ili kuondoa ukiritimba na uvunjaji wa sheria.

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa bajeti yake hii nzuri na ya kwanza toka kuteuliwa kwake kushika wadhifu. Nimpongeze pia Katibu Mkuu, Jaji Mkuu na watendaji wote walio katika Wizara hii. Wanafanya kazi kubwa, zipo kasoro ndogo na hisia nyingi juu ya rushwa. Ni jukumu la Wizara na taasisi zake kuwahakikisha Watanzania kwamba wao si kama wanavyofikiriwa. Ni kweli zipo hisia hizo zinazosababishwa na watendaji wachache na hii ipo katika ngazi zote ingawaje vijijini kunaathirika zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala la Mahakama ya Kadhi, naona ni suala zito na linaongelewa kwa nguvu sana. Maombi yangu ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, yako madhehebu mengi sana katika nchi yetu, ikiwa kila dhehebu linataka kuanzisha *legal system* yake, iwe kimila au dini yoyote Serikali itafanyaje?

Pili, ni sababu zipi zilizofanya cheo cha Kadhi kuondolewa baada ya uhuru? Je, sababu hizo zimeisha?

Tatu, kama dhehebu linazo sheria zake, kuna sheria ipi inakataza madhehebu hayo kutekeleza sheria zao?

Nne, kwa mfano madhehebu ya *Roman Catholic* wanayo *legal system* na wanatekeleza. Wapo waumini wake wanaofanya uamuzi wa kwenda Mahakama ya Serikali kwa hiari yao. Kwa nini basi jambo hili liwe *mainstreamed* katika Serikali?

Mheshimiwa Spika, naona pengine mtu mwenyewe ndio tatizo, anapoona atafaidika zaidi kwa kwenda kwenye Mahakama za kawaida ataenda huko hata kama kidini hatakiwi kufanya hivyo au kwenda kwenye dini yake ikiwa ataona huko anapata maslahi zaidi.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Serikali kwamba jambo hili linyumbuliwe kwa makini zaidi ili mwisho wa siku tupate maamuzi yenye maslahi ya taifa na kutuacha wamoja zaidi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Serikali na namtakia Waziri na watendaji wake heri tu.

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Spika, katika kuwasilisha Hotuba ya Wizara hii ya Katiba na Sheria, awali ya yote, nachukua nafasi kumpongeza sana Waziri mwenye dhamana na Wizara hii, Mheshimiwa Mathias Chikawe na Mheshimiwa Johnson Mwanyika, Wanasheria Mikuu wa Serikali, kwa kazi nzuri ya usimamizi wa Wizara hii, inayogusa haki za msingi za kila mtu na katiba kwa ujumla.

Nachukua nafasi hii pia kumpongeza Jaji Mikuu, Mheshimiwa Augustino Ramadhani na Majaji wote wa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa, kwa utendaji wao mzuri. Vilevile nawashukuru Mahakimu, Wanasheria na Watumishi wote wa Wizara hii, kwa uendeshaji wao wa shughuli hii ya sheria.

Mheshimiwa Spika, misingi mikubwa ya maisha ya binadamu mbali na haki ya kuwa na uhai wa pumzi aliyopewa na Mwenyezi Mungu, pia wanadamu tumejiwekea mamlaka zetu za kutusimamia ili kwa njia moja ama nyingine, asitokee mmoja wenu akavunja sheria kwa matakwa yake ye ye binafsi. Kwa maana hiyo, ndio maana tukawa na mihimili mikuu mitatu ya nchi, ambayo ni Bunge, Mahakama na Utawala.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri hata sisi Wabunge tukaelewa mtiririko huu na sio kujiendea ovyo kwa kuitaja bila mpangilio, kila chombo kina wajibu wake. Bunge ndilo lenye wajibu wa kutunga sheria ambayo ni pamoja na katiba ya nchi kwa niaba ya wananchi. Katiba ndio msingi wa yote kama ilivyotamka yenyewe kwamba, wananchi ndio msingi wa yote, hapa utaona wananchi kwanza halalfu katiba inayotokana na watu.

Kinachofuatia ni Mahakama, ambayo ina jukumu kubwa la kufanya tafsiri juu ya sheria iliyotungwa na Bunge na baadaye ni Utawala ambao una kazi ya kutekeleza yale yaliyotungwa na Bunge na kufanyiwa tafsiri na Mahakama. Utawala unakuwa mhimili wa mwisho kiutekelezaji. Nimelazimika kusema masuala haya awali ili kujenga misingi ya hoja yangu ninayokusudia kuiwasilisha hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, kimsingi katika tamaduni za maamuzi ya mashauri, zipo aina mbili za kesi; zipo kesi za jinai (*criminal*) na madai (*civil nature*), hii mara nyingi inakuwa katika *personal law* (sheria binafsi). Katika mgawanyiko huu, inategemea sana hasa katika sheria juu ya muamuzi ni lazima awe ni mjuzi wa suala linaloletwa mbele yake, kwa maana ya *professional*, yawezekhana utaalamu wake ukawa umejikita katika masuala ya sheria ya biashara, basi huyu anastahili kuamua kesi za biashara, kadhalika mambo mbalimbali na ndio maana zipo mahakama za aina mbalimbali kama vile Mahakama ya Biashara, Kazi, Ardhi, Vyombo vyta Usafiri na kadhalika. Huu ndio utaratibu mzuri katika maamuzi, haiwezekani kesi ya *traffic* ukaipeleka kwa Hakimu wa Biashara na vivyo hivyo kesi ya inayohusu mirathi, ndoa, talaka, wosia na hata migogoro ya ibada misikitini, huwezi kupeleka katika mahakama ambazo mahakimu ama majaji hawana *knowledge* ya masuala ya kiislamu.

Nikizungumza hilo, wanasheria wanafahamu, japo sheria yenyewe haikatazi kupokea kesi yoyote, lakini bado imesisitiza juu ya misingi ya kesi zenyewe hasa kufuata haki ya asili katika maamuzi. Hili linazingatia pale hakimu ama jaji anapotoa maamuzi ama hukumu, lazima awe amejiridhisha pasipo shaka (*prove reason beyond doubt*), haiwezi kutokea hakimu ama jaji kutoa hukumu bila kuzingatia hili. Ukiona yupo hakimu anayetoa hukumu bila kuzingatia haki ya mashauri kwa mujibu wa sheria, basi elewa huyu ana upungufu. Kwa maana hiyo ni wajibu wa nchi kupitia chombo chake cha kutunga sheria, kuelewa ndani ya nchi yake kinao watu wa aina tofauti kwa makabila na dini na kwa kuwa ni wajibu wa watawala kuwatendea haki watu wote bila kujali rangi, dini, wala kabilo. Serikali inawajibika kuheshimu tamaduni za watu wake, kwa kutengeneza mazingira ambayo yataonekana wao wananchi wameyaridhia kwa kuyaamini wala si vinginevyo. Kwa hili naamini ili watawala waweze kutenda haki, wanaelewa lazima pawepo na msingi ambao umeridhiwa na vyombo vilivyo juu yake kama nilivyovitaja; Bunge na Mahakama, ambavyo kila kimoja kina wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia taratibu hizi nilizozitaja, tutakuwa na nchi ya ajabu sana kama nchi yetu isiyokuwa na dini, lakini inayoheshimu tamaduni za wananchi wake juu ya kuabudu, pale ambapo panatokea jambo mahususi linalohitaji kwa mwenye kulijua ndio aweze kulitatua, hili sio jingine ni juu ya tamaduni za Dini ya Kiislamu. Naomba nichukue nafasi hii ili nieleze kidogo juu ya kitu kiinachoitwa Mahakama ya Kadhi.

Mheshimiwa Spika, neno Kadhi ni la Kiarabu lenye maana ya Jaji kwa Kiswahili. *AlKadhi* ikiwa na maana ya sheria na neno *Hakeem* sawa na mahakama. Hivyo, kinachoombwa hapa sio kuanzisha mahakama itakayokuwa *separate* na mahakama zetu, bali ni kitengo kitakachokuwa chini ya Mahakama Kuu, kama ilivyo kwa Mahakama za Kazi, Ardhi, Biashara na kadhalika ambazo zina waamuzi ambao ni wataalamu wa eneo

hilo. Hivyo, suala kwamba Mahakama ya Kadhi itatengeneza utaratibu wake; hilo halipo. Bado mtiririko wa kesi utakwenda kama unavyotakiwa, isipokuwa kwa kufuata Sheria ya Dini ya Kiislamu inavyosema katika maamuzi, kwani atakuwepo Msajili wa Mahakama na taratibu nyingine. Wanasheria wenyе taaluma ya *Islamic Law* watawatetea watu watakopeleka mashauri katika mahakama hii, kwa kuzingatia katiba ya nchi yetu inavyosema juu ya uhuru wa kuabudu. Hapa hakuna shaka juu Waislamu kuhimiza kuwepo kwa Mahakama ya Kadhi. Sijui sababu zilizopelekea kuifuta mahakama hii baada ya uhuru wa nchi yetu? Katika kuzingatia misingi ya haki, ndio maana wageni waliotutawala tena wasio Waislamu, waliona umuhimu wa kuwa na Mahakama hii.

Mheshimiwa Spika, nakishukuru sana chama changu CCM kuona hilo na hata kuliingiza katika Ilani ya Uchaguzi 2005 - 2010 kwamba, kitahakikisha suala la Mahakama ya Kadhi limetatuliwa kwa maana ya kuwepo.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri mwenye dhamana sasa alete Muswada ndani ya Bunge hili Tukufu, ambao utaananza Mahakama hii ya Kadhi. Kwa kufanya hivyo, itakuwa ni kutii katiba ya nchi juu ya uhuru wa kuabudu na pia tutakuwa tumetimiza ahadi kupitia Ilani ya CCM 2005 – 2010, juu ya uanzishwaji wa Mahakama hii ya Kadhi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nimalizie juu ya kuziimarisha mahakama kiutendaji. Nashukuru kwamba, juzi juzi Wizara imetuletea Hakimu wa Mahakama ya Wilaya ya Iramba, baada ya kuwa na malalamiko ya muda mrefu juu ya mlundikano wa majalada katika usikilizaji wa kesi. Inasikitisha kwamba, hakimu aliyeletwa Iramba umri wake wa kustaafu umefika na hivyo tayari ameshastaafu na sasa anachongoja ni kukabidhi ili aondoke, hivyo tunaendelea na lile tatizo la awali. Namwomba Waziri, kabla huyu hajaondoka basi taratibu za kutupatia hakimu mwingine zifanyike haraka. Naomba tujengewe Mahakama ya Wilaya ili kesi za Mahakama ya Wilaya zitenganishwe kutoka kwenye Jengo la Mahakama ya Mwanzo.

Mheshimiwa Spika, kadhalika kuhusu Mahakama za Mwanzo za Kaselya, Ndago, Urughu, Shelui, Ntwike, Kisiriri na Kinampanda, naomba Mahakimu wa Mahakama hizi wapewe vitendea kazi zikiwemo pipipiki kwa ajili ya ufanisi katika utekelezaji wa majukumu na hata usalama kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, sina sababu ya kuipinga hoja iliyowasilishwa na Waziri, lakini sitamuunga mkono hadi pale atakaponipa maelezo ya kutosheleza juu ya mchakato wa kuanzisha kwa Mahakama ya Kadhi.

MHE. JANET B. KAHAMA: Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja. Napenda pia kutoa hongera zangu kwa Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Viongozi wote, kwa kazi nzuri.

Napenda kuungana na Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, katika kuona umuhimu wa kutafsiri sheria kwa Lugha ya Kiswahili, ili kuwezesha wananchi wengi kuelewa sheria na hivyo kuwaepusha wananchi kutovunja sheria.

Bado kuna umuhimu wa Wizara hii kuangalia kwa makini eneo la mila na desturi potovu zilizopitwa na wakati. Tangu kipindi cha Bunge kilichopita (2000 – 2005), niliwahi kuuliza swali katika Bunge kuhusu mila na desturi za baadhi ya makabila ya Mkoa wa Mara ya Nyumba Ntobo.

Mheshimiwa Spika, aina ya ndoa ya nyumba ntobo ya mwanamke anamuoa mwanamke kwa maana ya mama mtu mzima anamchukua msichana na kumtafutia mwanaume atakaezaa nae. Mtindo huu huendelea baada ya msichana huyu kuzaa mtoto, hupatiwa tena mwanaume mwingine mbali na yule wa kwanza na huzaa tena.

Faida anayopata mama mwenye nyumba kwa mhifadhi msichana huyu (au kumuo) ni yeye kupata watoto na nguvu kazi. Kwangu mimi, naona kuwa huu ni utumwa wa aina yake, unamnyima uhuru msichana huyu, kuamua na kuchagua maisha yake mwenye.

Kwa njia nyingine, mtindo huu unachangia sana katika kusambaza UKIMWI na maradhi mengine ya zinaa. Jibu nililopewa nilipouliza Bungeni kipindi kile ni kuwa, hakuna sheria inayohusu kudhibiti mfumo huo wa nyumba ntobo. Lini sasa Wizara hii itaona umuhimu wa kutunga sheria ya kudhibiti tabia hii kabisa, ili kupunguza Maradhi ya UKIMWI na kumpa uhuru wake mwanamke ya kuchagua na kuzaa na mwanaume amtakae na kuendesha maisha yake kwa uhuru wake. Ahsante sana.

MHE. ATHUMANI S. JANGUO: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, pamoja na kuwapongeza wasaidizi wake, kwa hotuba nzuri na kufanya kazi nzuri katika mazingira magumu. Nawapongeza sana Majaji na Mahakimu kwa matatizo wanayoyapata, mishahara finyu, majengo ya ofisi na makazi yasiyotosheleza na upungufu wa zana za usafiri.

Upungufu huo ni mkubwa zaidi katika ngazi za Mahakama za Wilaya na za Mwanzo. Kwa mfano, hali katika Wilaya ya Kisarawe ni kama ifuatavyo: Wilaya ina Mahakama ya Wilaya na za Mwanzo tano. Mahakama ya Wilaya na moja ya Mwanzo haina majengo ya ofisi bali wao na Idara ya Polisi zinahifadhiwa katika Jengo la Mkuu wa Wilaya. Kati ya Mahakama nne zilizobaki za mwanzo; mbili katika Kata za Sungwi na Chole Samvula, zina ofisi mbovu sana. Kuna upungufu mkubwa wa wafanyakazi; Mahakama ya Wilaya haina Mahakimu baada ya Hakimu Kiongozi kustaafu. Amebaki msaidizi mmoja tu ambaye analazimika pia kuhudumia Mahakama mbili za Mwanzo. Mahakama ya Tarafa ya Sungwi haina hakimu wala karani wa mahakama; inahudumiwa na Hakimu mmoja wa Wilaya.

Pamoja na kuzingatia taarifa yako katika hotuba yako, nalazimika kusema kuwa suala la Mahakama ya Kadhi limecheleweshwa sana na serikali. Kama ulivyosema mwenywewe, suala hili liletwa Bungeni tangu mwaka 1958.

Mheshimiwa Mikidadi, alikuwa anawasilisha kero ya Waislam ambayo inafungamana na ibada. Mheshimiwa Mrema, Mheshimiwa Baruti na Mheshimiwa

Ngawaiya, walileta hoja hii kati ya mwaka 1995 – 2000, kwa sababu Waislam walikuwa wanakereketwa na suala hili.

Mwaka wa jana ulikuwepo kwenye chakula cha mchana kwa Mheshimiwa Mary Nagu, tukaahidiwa kuwa, suala hili lilikabidhiwa Tume ya Uchunguzi wa Sheria; lakini ndiyo kwanza leo unatueleza eti sasa taarifa ya Tume ndiyo imepelekwa Serikalini.

Nakubalina nawe kuwa, baada ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kulitolea maelezo suala hili katika mkutano huu, si vizuri kwako wewe Waziri kulirejea. Sisi wawakilishi wengine wa wananchi, lazima tuendelee kutoa mawazo yao. Kwa hivyo naishauri serikali kuzingatia yafuatayo:-

(a) Mahakama ya Kadhi, kama zilivyo mahakama nyingine maalum, haitashughulikia kesi zote bali binafsi, yaani masuala ya ndoa za kiislam, mirathi kwa waislam, malezi ya watoto, talaka za kiislam na migogoro misikitini.

(b) Kama hizi zilikuwepo kabla ya 1963, zipo Kenya kwenye Waislam wachache na Zanzibar kwenye Waislam wengi. Hapakuwepo na migogoro yoyote.

(c) CCM iliahidi katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005, ibara 99(g) na 108(b) zimeahidi kulipatia ufumbuzi suala hili.

Sikubaliani na rai iliyomo kwenye hotuba kuwa serikali inachukua tahadhari eti ili tusiligawe taifa. Sikubali kwani kuachia sehemu fulani ya umma iendelee kunung'unika, tutaligawa taifa. Mheshimiwa Jaji Mkuu Agustino Ramadhani anasema: “...Again there is a feeling that nationalism is forged better by acknowledging ethnic or tribal origins rather than surprising them.” The same can be said about religions. The more conscious we are of varying faiths and willing to respect or even incur some expense to enable their observance, the more harmonious we are going to be.” Maneno haya ni *Loud and Clear*.

Mheshimiwa Spika, kwa kutegemea kuwa sasa serikali haitachukua muda zaidi kulitolea uamuzi suala hili, pamoja na kutatua matatizo ya Mahakama za Wilaya ya Kisarawe, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana.

MHE. GIDEON A. CHEYO: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Chikawe, kwa kuteuliwa kuiongoza Wizara hii muhimu. Namtakia mafanikio mema.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri na Watendaji wote wa Sekta ya Katiba na Sheria, kwa jitihada zao za kuboresha huduma kwa umma katika sekta hii.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuongezeka kwa uelewa wa wananchi kuhusu haki zao za kimsingi, mashauri mengi yanajitokeza katika ngazi mbalimbali. Mwamko huu wa uelewa na ongezeko la mashauri, haviendani sambamba na ongezeko la wanasheria wa kuwashudumia wananchi katika ngazi mbalimbali. Bado kuna upungufu mkubwa wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na kusababisha mlundikano wa mashauri katika Mahakama za Mwanzo. Hali hiyo inajitokeza katika ngazi ya Wilaya mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, ipo haja kwa serikali kuendelea kuiwezesha Wizara hii kibajeti ili iweze kuwafunza wataalam zaidi wa sheria na kuwasambaza katika ngazi mbalimbali za mahakama, hususan ngazi ya Wilaya na Kata.

Napenda kutumia nafasi hii, kumwomba Mheshimiwa Waziri, azingatie ombi la Wilaya ya Ileje kupatiwa Hakimu wa Wilaya. Mpaka sasa Hakimu wa Wilaya ya Mbozi ndiye anaihudumia pia Wilaya ya Ileje. Hali hii husababisha kesi/mashauri kuchukua muda mrefu kushughulikiwa na inakuwa kero kwa wahusika. Ombi ni kupatiwa Hakimu wa Wilaya ambaye atakuwa na makazi ya kudumu Wilayani Ileje.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuanzisha mfumo mpya wa kushughulikia mashauri ya migogoro ya ardhi nchini, umekuwepo mgongano wa utoaji haki kati ya Mahakama za Mwanzo na Mabaraza ya Ardhi, hususan katika ngazi ya vijiji. Ipo haja kwa Wizara kuhakikisha kwamba, Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wanapata sheria zote zinazohusu mfumo mpya wa kushughulikia migogoro ya ardhi ili kuepuka migongano kati ya Mahakimu hao na Mabaraza ya Ardhi husika. Aidha, uelewa wa sheria hizi utatoa fursa kwa wananchi kutendewa haki kwa mujibu wa sheria husika. Nalisema hili kwa sababu limejitokeza katika Wilaya yangu ya Ileje.

Mheshimiwa spika, naipongeza Wizara kwa jitihada za kutoa vitendea kazi kwa Mahakimu. Naomba Wizara izingatie mazingira magumu ya kijiografia, kama vile Ileje na kutoa kipaumbele katika kugawa vyombo vyaa usafiri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii.

MHE. KHADIJA SALUM ALLY AL-QASSMY: Mheshimiwa Spika, kwanza, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwangi wa rehema, kwa kuniwezesha kufika hapa leo na kuweza kuchangia au kutoa maoni yangu kuhusu hoja hii iliyoko mbele yetu leo.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kukupongeza wewe kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa CPA na kuiwezesha nchi yetu kuwa Mwenyeji wa Mkutano wa Mabunge yote ya Commonwealth.

Mheshimiwa Spika, sina budi kumshukuru Msemaji wetu wa Upinzani, kwa jinsi alivyoweza kuwasilisha hotuba na maoni ya Upinzani kuhusu Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, vile vile nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitampongeza Waziri, Naibu Waziri na timu yake yote, kwa jinsi walivyoweza kuwasilisha hotuba yao.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kuhusu katiba ya nchi hii. Nadhani Waziri atakubaliana na nami kwamba, katiba ya nchi sasa imeshapitwa na wakati hasa ukizingatia nchi hii ni ya vyama vingi; katiba haikidhi mahitaji na upungufu makubwa. Kwa hiyo, naiomba serikali ikubali kuandika upya katiba ya nchi ambayo inaendana na wakati tulionao sasa, hasa ukizingatia wananchi wengi wanapiga kelele. Hebu tuijulize; kwani serikali ina kigugumizi cha nini kuwardhisha wananchi wake kama ina nia njema?

Mheshimiwa Spika, wananchi wanalalamikia sheria ya mgombea binafsi, ambayo mahakama imeshatoa uamuzi. Kwa nini serikali inakuwa ya kwanza katika kuvunja sheria zake? Je, wananchi wa kawaida watafanya vipi?

Mheshimiwa Spika, nchi hii ina zaidi ya watu 38,000,000 na watu wanaojiandikisha hawazidi 12,000,000; je, kutokana na hali hii; serikali haioni kwamba inawanyima haki watu wengi zaidi ya kupiga kura kutokana na sheria iliyoko hivi sasa?

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa Sheria ya Mahakama ya Kadhi, hata Ilani ya Uchaguzi ya CCM imeona umuhimu wake. Kweli serikali haina dini, lakini wananchi wake wanazo dini zao; sasa serikali kwa nini hawatilii maanani suala hili mpaka leo wanalipiga danadana? Nadhani jambo lolote unaloliweka katika Ilani, unakuwa tayari ushalifanya utafiti; sasa iweje sasa hivi mpaka zipigwe kura za maoni hasa ukizingatia serikali yetu hivi sasa haina fedha za kutosha na mambo kama haya yanataka fedha nyingi; hatuoni hicho ndio kitakuwa kikwazo kikubwa cha kuweza kuleta sheria hii mapema ambayo ni muhimu sana kwa wananchi walio wengi?

Mheshimiwa Spika, tunashangaa sana kuona wanasheria wetu wanatuingiza katika mikataba mibovu, kiasi kuitia nchi hii katika gharama kubwa ambayo mwisho inawa-cost wananchi ambao hawana hatia. Je, wanasheria kama hawa wanawapa adhabu gani?

Mheshimiwa Spika, naamini maoni yangu haya Mheshimiwa Waziri atayatilia maanani, hasa ukizingati sasa hivi kumejitokeza sakata la Zanzibar nchi au si nchi. Kwa hiyo, tunaomba serikali suala hili walitilie maanani, hasa ukizingatia kuwa, kumetolewa ushauri wa wanasheria kukaa pamoja ili kulishughulikia. Naomba Wizara ichukue jitihada za makusudi ili usije Muungano wetu ukaingia ufa. Sisi sote ni ndugu, tumeshazaar na kukaa pamoja kwa upendo mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Wafanyakazi wote wa Wizara, inayoongozwa na Katibu Mkuu. Nampongeza Jaji Mkuu, Majaji na Wafanyakazi wote nchini, kwa kazi ngumu wanayoifanya katika kutoa, kulinda na kusimamia haki za nchi na mali zao. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, naomba nichangie/nitoe ushauri kuhusu Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kabati, Sheria na Utawala Bora.

Wilaya mpya ya Rarya ilianzishwa Aprili, 2007, kabla ya kuanzishwa ilikuwa Jimbo la Rarya, Wilaya ya Tarime. Wilaya ya Rarya ina tarafa nne, kata 21, vijiji 81 na vitongoji 17. Idadi ya watu ni 250,000 kutokana na sensa ya 2002. Wilaya ya Rarya haina Mahakama ya Wilaya.

Baada ya kutangaza Makao Makuu ya Wilaya, Wizara inaombwa kuanzisha Mahakama ya Wilaya kwa kutumia majengo ya muda. Wilaya ya Rarya inakabiliwa na matukio ya wizi wa mifugo, ujambazi na magendo. Hivyo, kuna kesi nydingi ambazo zimekuwa zikingojea kutolewa hukumu kwa kuwa mahakama inayotegemewa ni ya Wilaya ya Tarime.

Mahakama za Mwanzo zilizopo Wilaya ya Rarya ni nne tu nazo ni Mahakama ya Tarafa ya Girango; Mahakama ya Tarafa ya Nyancha; Mahakama ya Tarafa ya Suba; na Mahakama ya Tarafa ya Luo-Imbo.

Mahakama hizi zilijengwa na wakoloni (Waingereza) miaka 70 iliyopita wakati idadi ya watu ilikuwa ndogo sana ikilinganishwa na ilivyo sasa.

Majengo ya Mahakama nilizozitaja hapo juu ni chakavu, hayana nafasi ya kutosha mahabusu, nyumba za wafanyakazi na vitendea kazi, hivyo kudhoofisha huduma zitolewazo.

Mahakama hizi zifanyiwe ukarabati mkubwa na zipatiwe watumishi wa kutosha na vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, Jaji Mkuu Mstaafu Barbanas Samatta, alipotembelea Rarya mwaka 2005 alishuhudia tatizo hili na alinihakikishia kuwa, ofisi yake kwa kushirikiana na Wizara; ukarabati, uboreshaji na upanuzi wa Mahakama ya Kinesi, Ryagoro, Shirati na Nyathango zitafanyiwa kazi. Hadi sasa, ahadi ya Jaji Mstaafu Samatta hajatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Rarya inahitaji kuwa na Mahakama za Mwanzo zaidi ya nne zilizopo sasa, kuna kata 21 ambazo hazina Mahakama hizo. Tarafa ya Nyancha ina kata nane na vijiji 34, lakini hakuna Mahakama ya Mwanzo. Tarafa ya Girango ina kata saba na vijiji 22, nako pia hakuna Mahakama ya Mwanzo ya Kata. Tarafa ya Suba ina kata nne na vijiji 16; hakuna Mahakama ya Mwanzo ya Kata; na Tarafa ya Luo-Imbo yenye kata mbili na vijiji tisa vilevile haina Mahakama ya Mwanzo.

Kutokana na kukosekana kwa Mahakama za Mwanzo katika kata 21 Wilayani Rarya, imesababisha malalamiko mengi kutoka kwa wananchi dhidi ya serikali kutokuwatendea haki yao ya kikatiba. Mchakato wa kuanzishwa kwa Mahakama za Mwanzo na Mahakama ya Wilaya upate msukumo wa haraka. Naomba tamko la Serikali.

Mheshimiwa Spika, nampongeza tena Mheshimiwa Waziri na timu yake, kwa hotuba yenye matumaini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI: Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 71, ukurasa wa 43, kuna magari yanayotolewa kwa Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo. Ingawa utaratibu wa kununua pikipiki hizi utaendelea, nadhani ni busara pikipiki hizi 100 zisambazwe kwanza kwenye maeneo yenye mazingira magumu, hususan maeneo ya pembezoni pamoja na Wilaya ya Ludewa. Naomba nithibitishiwe kama nitapata pikipiki kwenye mgao huo.

MHE. JACOB D. SHIBILITI: Mheshimiwa spika, nakushukuru kutoa ruhusa ya kuchangia katika hotuba hii. Nimpongeze Waziri kwa juhudzi wanazofanya, kwa kusaidiana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Jaji Mkuu, katika majukumu ya kuwapatia haki zao wananchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inaongoza mhimili kamili kama ilivyo Bunge na Utawala; hivyo mhimili huu unapaswa kuvutiwa kwani uko nyuma sana na mihimili miwili.

Mheshimiwa Spika, tutahitaji Waziri alihakikishie Bunge juu ya kupunguza matatizo yafuatayo:-

(i)Idadi ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo haitoshi na pia majengo yamechakaa, yanahitajika majengo mapya na pia vitendea kazi kama gari au pikipiki kwa kuanzia. Mfano, Wilaya ya Misungwi haina Hakimu wa Wilaya kwa sasa, Hakimu wa Kwimba hupanga ratiba ya kutembelea mara moja au mbili kwa wiki, jambo ambalo linawanyima haki wananchi.

(ii)Mahakama ya Mwanzo ya Inonelwa ni kati ya Mahakama iliyo na mazingira mabaya sana. Ipo ahadi toka kwa Hakimu wa Wilaya ya Kwimba kuwa, ingejengwa lakini dalili hazionekani. Naomba serikali iliambie Bunge; je, juhudzi hizo zimefikia wapi; ikiwemo Mahakama ya Mbarika iliyoezuliwa miaka mingi na haijakarabatiwa; Waziri anasemaji kwa hilo?

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Mahakama Lushoto ni muhimu sana kwa nchi yetu; kinahitaji bajeti ya kutosha na ni chuo tunachokitegemea kuandaa mahakimu wengi wa kutosha kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, taasisi ya waendesha mashtaka imejipanga kutekeleza majukumu yaliyokuwa yanatekelezwa na polisi; ipo mikoa itakayoanza kutekeleza kazi hiyo ikiwemo Mwanza. Tunaipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Misungwi iliombwa itengete eneo la kujenga taasisi ya waendesha mashtaka sehemu ya Usagara na pia Wilaya ya Misungwi imetenga eneo la ujenzi wa Mahakama ya Wilaya na nyumba za watumishi, ikiwemo nyumba na Ofisi ya Wanasheria (Mwanasheria Mkuu). Je, serikali inafahamu hayo yote na ni nini mkakati wa kuyatekeleza hayo, ili wananchi waliota ardhi yao waone inatumika kwa waliyoyategemea.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Misungwi kutokuwa na Hakimu wa Wilaya hii ni kero. Hii ni ahadi ya viongozi mbalimbali. Wilaya hii ilianzishwa mwaka 1997, idara zote nyingine zimekamilika kama vile *District Commissioner* yupo, *District Executive Director* yupo, *OCD* yupo, *DMO – District Medical Officer* yupo, *TRA* ipo na *PCCB* ipo. Hivi upande wa Hakimu wa Wilaya kuna ugumu gani? Tunaishauri serikali itupangie Hakimu wa Wilaya ili wilaya ijitosheleze kama zilivyo nyingine.

Mheshimiwa Spika, mwisho, malipo ya wazee wa Mahakama za Mwanzo yaongezwe kutoka shilingi 1,500 na taratibu ziwe wazi, kwani zipo sehemu wazee wanacheleweshewa malipo yao hadi miezi mitatu; hii si haki.

Mheshimiwa Spika, nirudie kumpongeza Waziri, Katibu Mkuu, ambaye ni Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, pamoja na Uongozi wote wa Mahakama chini ya Jaji Mkuu. Nina imani watayapatia ufumbuzi matatizo ya Wilaya ya Misungwi. Naomba Jaji Mkuu apatapo nafasi, aitembelee wilaya hii ambayo alahirisha ziara yake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri na Wataalamu wake wote, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii.

Mahakama ya Kadhi ina umuhimu wa pekee hivi sasa kuliko wakati wowote, kutokana na Waislam kuhukumiwa na mahakimu wasio Waislam katika mambo ya mirathi, ndoa na takala. Hii ni kinyume na maadili ya Waislam wote na uvunjwaji mkubwa wa haki za binadamu. Kwa kuwa Tume ya Kurekebisha Sheria imeshamaliza utafiti wake na kulipeleka suala hili serikalini, basi serikali ilitolee maamuzi ya haraka. Aidha, Serikali ikutane na Viongozi wa Dini ya Kiislam, kujiridhisha ni kwa vipi serikali inaweza kuanzisha mahakama hizi bila kuathiri shughuli za Serikali.

Sheria ya Maadili ya Viongozi ama ina upungufu mkubwa au haitekelezwi ipasavyo. Itakuwaje viongozi wanatangaza mali zao wakati wanapoanza kazi, lakini hawatangazi mali zao baada ya muda Fulani; mathalani Rais au Mbunge wanapomaliza vipindi vyao vya kazi. Aidha ni kwa nini suala hili liwe ni siri kati ya mfanyakazi na serikali? Mambo haya yanafanya zoezi hili lisiwe na maana yoyote na haliwezi kamwe kuondoa tatizo la kujilimbikizia mali kinyume na sheria.

Mheshimiwa Spika, katiba mpya ni jambo lisiloweza kuepukika kwa sasa. Marekebisho ya mara kwa mara ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yanaonyesha kuwa mabadiliko ni jambo la lazima. Hata hivyo, kuweka viraka katika katiba yetu ya sasa, ililenga hasa katika mfumo wa chama kimoja. Kuendelea na katiba ya sasa ni kutoukubali ukweli kwamba, jamii inahitaji katiba mpya; ni kujidanganya na ni upotofu.

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Tanzania ya mwaka 1977, imeruhusu Mfumo wa Vyama Vingi na chaguzi huru na za haki. Kikatiba, chombo kinachosimamia chaguzi ni

Tume ya Taifa ya Uchaguzi, lakini cha ajabu ni kuwa, chaguzi za Serikali za Mitaa hazisimamiwi na Tume ya Taifa ya Uchaguzi; bali zinachaguliwa chini ya usimamizi wa TAMISEMI. Hili ni jambo la hatari na la aibu kubwa kwa nchi yetu, inayoimba demokrasia na utawala bora. Kinachofanyika ni kwa viongozi wa serikali kutoa maagizo kwa walio chini yao, kuhakikisha kuwa Chama Tawala kinashinda vinginevyo kiongozi, huyo hana kazi.

Mheshimiwa Spika, wakati umefika sasa wa chaguzi zote zisimamiwe na chombo kilichopo kisheria, ambacho ni Tume ya Uchaguzi ya Taifa. Naomba sheria ichukue mkondo wake ili kufanikisha hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hukumu ya kifo, mimi naiunga mkono sana; ni haki na tena ni halali kabisa, kila aliyeua naye auliwe. Thamani ya roho ya mwanadamu ni kubwa sana, haiwezi kufidiwa kwa thamani yoyote. Kubadilisha hukumu ya kifo kuwa kifungo ni kutothamini roho ya mwanadamu na hivyo kutoa mwanya kwa binadamu kuuwana ovyo ovyo. Ikiwa mtu hawezi kujifunza kwa kumuona yule aliyeua naye anauliwa; atajifunzaje kwa kuona aliyeua hauliwi bali anafungwa jela tu?

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Jaji Mkuu, Mwanasheria Mkuu na Watendaji wote wa Wizara yake, kwa kazi nzuri wanayofanya kuhakikisha Watanzania wanapata haki na wanakuwa huru kuishi ndani ya nchi yao kwa amani na usalama.

Mheshimiwa Spika, hapa nchini tuna upungufu mkubwa wa mahakimu wa ngazi zote, hasa wa Mahakama za Mwanzo, hilo linaendana sambamba na upungufu na nyumba za kuishi na hizo chache zilizopo zipo kwenye hali mbaya sana, yaani zimechakaa. Majengo ya mahakama nayo ni machache sana tena yamechakaa. Mahakimu hawana vitenda kazi, usafiri na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, umefika wakati sasa, kuangalia na kushughulikia matatizo makubwa yanayokikibili Chuo cha Mahakama Lushoto. Hiki ndio chuo pekee kinachotoa mahakimu kada ya kati na mwanzo. Naomba sana serikali itoe msaada mkubwa kwa chuo hiki, kuanzia wakufunzi, nyumba za wakufunzi na wanafunzi, vitenda kazi vyote magari, vitabu, vyakula, mavazi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana kuona Wizara yake ina makaimu wengi sana. Hivyo, haipendezi kwa sababu nyadhifa zinazokaimiwa ni kubwa na nyeti. Kawaida mtumishi anatakiwa akaimu miezi sita tu halafu anathibitishwa au kama hana sifa anaondolewa. Sasa kwa hili, nataka maelezo kwa nini linafanyika?

Mheshimiwa Spika, kuna jambo bayaa sana limetokea jimboni kwangu (Iramba Mashariki), ambalo naomba uamuza wako wakati ukihitimisha hotuba yako. Ndugu Kiliauginge Kiula, amekuwa kero kijiji cha Lyelyembo, Kata ya Kinyangiri; amekuwa anavunja amani kwa kuwatishia wananchi. Tarehe 30 Julai, 2008 alipelekwa Polisi Iguguno na Polisi wakampeleka Mahakama ya Mwanzo Iguguno, akafunguliwa kesi

Namba 112 ya mwaka 2008. Cha kushangaza, kesi ilipopelekwa Mahakamani, Hakimu aliifuta kesi hiyo kwa kisingizio kwamba, mhusika hakutishiwa kwa silaha bali kwa maneno. Inasemekana mshtakiwa alipotoka, aliendelea kuwatishia kwa sababu eti yeze na hakimu wanafahamiana.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kesi ilishafunguliwa; si ingekuwa haki isikilizwe ndipo uamuza utolewe badala ya kusimamia upande mmoja tu? Mahakama za Mwanzo za Kirumi, Iambi na Kinyangiri, hazina Mahakimu kwa muda mrefu sasa; naomba mahakimu wapya wakiajiriwa wapelekwe huko.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Jaji Mkuu, kwa kutujengea Mahakama mpya ya Wilaya na pia kutujengea Mahakama mpya ya Mwanzo Iguguno. Wananchi wameridhishwa sana na kazi hii. Tunaomba Mahakama za Ibaga, Nduguti, Iambi, Kirumi na Kinyangiri zikarabatiwe. Mheshimiwa Waziri, nawapongeza naona muanze kuwakumbuka kuwapatia baadhi ya Mahakimu usafiri. Tunaomba mpango huo ufike mpaka kwa Mahakimu wa Mwanzo.

Mheshimiwa Spika, wazee wa mahakama ni muhimu sana kwenye kutoa haki, naomba waendelee kukumbukwa kulipwa posho zao.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hatua wanazochukua kupambana na rushwa, pamoja na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

MHE. RITA L. MLAKI: Mheshimiwa Spika, kwanza, natoa pongezi kwa Waziri wa Sheria, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hiyo, kwa hotuba nzuri ya bajeti yao. Naomba kuchangia kuhusu mazingira ya Mahakama zetu za Mwanzo hasa ya Kawe.

Kwa vile sheria ya *Judiciary* kuwa na bajeti yenu imepitishwa; ni matumaini yangu mtaweza kukarabati Mahakama za Mwanzo kwa awamu.

Nashauri Wizara iunde *Task Force* lya kuandaa mikakati ya kufuatilia maamuzi ya kesi imbalimbali za mahakama na kutazama kama haki ilitendeka. Hii itasaidia katika kudhibiti rushwa na haki kutolewa. Wananchi wengi wakikosa haki zao, hawasubiri rufaa ila wanakata tamaa. Nawapongeza kwa marekebisho ya sheria mbalimbali hasa za wanawake na mirathi.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache, naunga mkono hoja.

MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY: Mheshimiwa Spika, lengo la serikali kwa kupitia Wizara hii ni kujaribu kuondoa au kumaliza kesi zote zinazofikishwa Mahakamani ili kuwaondolea wananchi dhiki za kwenda na kurudi Mahakamani kwa siku au miaka mingi. Lakini zaidi, shida huwa kubwa pale ambapo mshtakiwa katika kesi ya jinai (*criminal*), amewekwa mahabusu; anaweza kukaa miaka mingi gerezani kabla kesi yake haijasikilizwa. Hii ni kuwatesa wananchi.

Je, kwa nini hatuanzishi mfumo wa *sentence bargaining*, kama wanavyofanya baadhi ya nchi nyingine kwa mfano, baadhi ya States za Marekani, ambapo kwa kiasi kikubwa, inapunguza mlundikano wa kesi na hivyo, kuwapunguzia raia wetu shida za kukaa sana rumande?

Suala la pili ni kuhusu makosa yanayofanywa na utawala (*Administrative Officers*). Hivi sasa kuna maeneo mengi yanayoshughulikia kesi kama wizi, kwa mfano, Maadili ya Viongozi wa Umma, Tume ya Haki za Binadamu na kadhalika. Nchi nyingi siku hizi wanazi-*consolidate* sheria za aina hii na kuifanya sheria moja tu yenye maudhui hayo. Nchi nyingi za West Indies, kwa mfano, Barbados, Antigua, Trinidad and Tobago, pamoja na Australia, U.K. na kadhlika, wana sheria inayojulikana kama *Administrative Justice (Decisions) Act*. E.U. wana sheria inayoitwa *The European Code of Good Administrative Behaviour*, ambazo zote zinahusu matendo mabaya yanayofanywa na mtawala (*maladministration*).

Je, utaratibu huu hatuuoni kuwa ni mzuri na wa busara na hivyo na sisi tujaribu kuufuata kwa kuwa na sheria moja inayohusu matendo mabaya yanayofanywa na utawala; pengine tuiite *Administrative Justice Act*, ambayo inaweka sababu za maamuzi, muda wa kesi na kadhalika?

Tatu, ninavyohisi mimi, Sheria ya Maadili ya Viongozi ina upungufu kidogo (No.13/95). Sheria ilivyo na fomu zinazotolewa kujazwa na mhusika ni tofauti na zinagongana (Ibara ya 90) na (2). Ibara ya sita (6) hakuna *mainstreamed* chini ya sehemu nyingine za sheria, ambapo inazidi kuleta utata. Sheria inazungumzia sana juu ya mambo ya utawala na wala siyo *substantive issues* zinazohusu masuala ya maadili. Ninachotaka kusema ni kuwa, sheria hii inahitaji marekebisho makubwa ili azma iliyokusudiwa ifikiwe.

Nashauri tutajaribu kuifanya mapitio sheria hii, kwa kutazama wenzetu walivyofanya. Kwa mfano, *the European and Code of Good Ethics Act, Code of Conduct and Ethical Standards for Public Officials and Employees of Republic of Phillipines*. Naamini sheria hizi na nyinginezmo nyingi, zinaweza kutusaidia kwa kuwa na sheria yetu nzuri zaidi.

Mambo muhimu yanayoshawishi kuwa na Katiba mpya katika nchi ni pamoja na kutokea kwa mapinduzi, kubadilika mfumo wa serikali kutoka chama kimoja kuwa na vyama vingi, kuunganishwa kwa nchi na kuwa na mfumo wa muungano uliokubalika, mabadiliko ya hali ya siasa na kiuchumi na kadhalika. Tanzania imepita katika baadhi ya mambo niliyoyaeleza hapo juu. Katiba yetu tulionayo ni mirathi ya katiba tuliyokuwa nayo zamani, pamoja viraka vingi vilivyoitiwa kwa kukidhi haja ya mabadiliko tuliyonayo. Hata hivyo, bado kuna upungufu mkubwa ndani ya katiba hii tuliyonayo; ni katiba ambayo kwa sasa haiendi na wakati. Kuondokana na upungufu huo, kuna haja kubwa ya kuwa na katiba mpya ya Tanzania. Tuanze kuwaelimisha wananchi kuhusu suala hili na mchakato wa kuwa na katiba mpya kwa maslahi ya nchi yetu na watu wake uanze haraka iwezekanavyo.

Katika uendeshaji wa kesi, kipindi kirefu tulikuwa tukiwatumia polisi ambao ujuzi wao ni mdogo. Zaidi *DPP* (mwendesha mashtaka) na *AG*. (Mwanasheria Mkuu), walikuwa ni Idara moja. Nakubaliana na mpango wa sasa wa kutenganisha vitengo hivi viwili; *AG* na *DPP* na kwamba, *DPP* iwe *independent* na kuwa ile kazi ya kuendesha kesi iondolewe kutoka polisi na wabaki na uchunguzi wa kesi tu, wakati kazi ya kuendesha kesi iende kwa *DPP*. Hivi sasa umeanza mgawo kwa hatua ndogo ukilinganisha na mahitaji makubwa ya nchi yetu.

Nashauri *Law School of Tanzania* ipanuliwe ili wanafunzi wote wanaotoka kujiunga kila mwaka waweze kuingia chuoni hapo ili baadae tupate wahitimu wengi, waweze kusambazwa mikoani. Hii ni kwa sababu sheria iliyopo sasa mtu hawezi ku-practice mpaka apitie *Law School*, wakati chuo chenyewe ni kidogo.

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Spika, naomba nichangie hoja hii; kwanza, kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa juhudhi kubwa wanazofanya ili kuboresha shughuli za Wizara hii muhimu katika Taifa.

Mheshimiwa Spika, katiba ndiyo sheria mama na asilimia kubwa ya Watanzania hawaijui katiba ya nchi yao, hata kwa kuiona kwa sura. Maoni yangu ni kwamba, serikali iandae mkakati madhubuti wa kutoa mafunzo juu ya katiba ya nchi ili wananchi waondokane na usumbufu unaowapata katika kusimamia ama kudai haki zao kama raia wa nchi hii na pia kujuwa wajibu wao; bila ya hivyo, Watanzania wataendelea kudhalilishwa kwa kutokujua sheria, haki na wajibu wao. Ikiwezekana basi ni busara kuingizwa katika *syllabus* mashulenii ili watoto wetu waanze mapema kuwa na uelewa wa sheria na katiba ya nchi yao.

Mheshimiwa Spika, inashangaza nchi yetu kurejeshwa kwa Mahakama ya Kadhi kumelazimisha kufanywa utafiti wa muda mrefu. Jambo hili lilikuwepo, liangaliwe tu liliondolewa kwa msingi upi, kwani Tanzania ni kweli haina dini lakini Watanzania wenyewe wana dini. Kwa kuwa kila mmoja ana uhuru wa kuabudu dini aitakayo, kuna ubaya gani Waislam kuwarejeshea Mahakama ya Kadhi, ambayo itasimamia ndoa, mirathi na talaka kwa mujibu wa sheria ya dini yao kama inavyowaelekeza?

Mheshimiwa Spika, niipongeze Wizara kwa kuamua kuwapatia vitendea kazi mahakimu ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Naomba zoezi hilo liendeshwe kwa haraka bila kusua sua, kwani mlundikano wa kesi umekithiri. Jambo hili linapelekea wananchi kupata usumbufu mkubwa, kwani kesi nyingine zinachukua hata miaka miwili.

Mheshimiwa Spika, naomba kupata taarifa juu ya kesi ya mwanamke aliyebakwa kule Pemba Kaskazini, Wilaya ya Wete, kwani taarifa ambazo zijazithibitisha ni kwamba, kesi hiyo ilionekana kuendeshwa kisiasa. Sina hakika, naomba Mheshimiwa Waziri aifuutilie kwa karibu sana. Nakushukuru.

MHE. YONO S. KEVELA: Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Hotuba ya Waziri wa Sheria, Katiba na Utawala. Nawapongeza sana katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara hii, ikiwa ni pamoja na Majaji, Mahakimu na Wasajili wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, Waziri au Serikali ifanye marekebisho haraka katika Sheria ya Ndoa, upande wa fedha ya matunzo ya watoto ambayo ni ndogo sana. Sheria ya Mirathi; wajane bado wanateseka sana kupata mirathi kwani inachelewa sana. Sheria ya Mtoto; watoto bado lipo tatizo kubwa la watoto wa mitaani; sheria iangalie jinsi ya kuwalinda kisheria.

Katika Jimbo langu la Njombe Magharibi, lenye Tarafa ya Wanging'ombe Imalinyi na Mdandu, tuna Mahakama ya Mwanzo ya Wanging'ombe ambayo hakuna nyumba ya hakimu, wala usafiri wa gari au pikipiki. Hakimu anakaa mbali kule Makambako, tunaomba sana ajengewe nyumba pale Wanging'ombe na ikiwezekana apewe usafiri.

Kwa vile pale Illembula ni mji mdogo, tunaomba Mahakama ya Wilaya ijengwe pale kwa vile hata kituo cha polisi kipo pale Illembula. Idadi ya watu ni kubwa na wananchi wanapata shida sana ya kupata haki. Kesi nyingi zinapelekwa Makambako; hivyo, wananchi wajengewe Mahakama ya Wilaya au ya Mwanzo pale Illembula.

Mwisho, nawapongeza sana Mahakimu wa Njombe na pale Makambako wanajitahidi sana. Naomba wapewe nafasi za kusoma zaidi katika viwango vyta shahada na kupewa motisha za kazi.

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Mathias Chikawe, Waziri wa Katiba na Sheria, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Jaji Mkuu, Watendaji wa Wizara na Mahakama, kwa uwakilishi wa kutosha katika kuleta hotuba yao ya bajeti. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, changamoto niliyotaka kuchangia katika Wizara hii ni hii ambayo Waziri mwenyewe katika ufanuzi wake ameisemea, nayo inahu Mahakama ya Kadhi. Nilikuwa nimejiandaa kuchangia mambo mengi kuhusu suala hili, lakini sasa nimeridhika kuwa tuisubiri Ripoti ya Tume ya Kurekebisha Sheria, ambayo imemaliza kazi yake na sasa tunasubiri maamuzi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, naomba kutoa rai kwamba, suala hili liamuliwe kwa umakini mkubwa, *emotions* ziwekwe pembeni kwani tusipoangalia hili ni eneo linaloweza kuleta mpasuko mkubwa zaidi kuliko Muafaka wa Zanzibar. Kuna kila dalili kwa wenzetu wa Kambi ya Upinzani kutaka kuchukua suala hili kuwa ni lao na iwe ni ajenda yao. Tusiwaachie kutafuta umaarufu kupitia hoja hii, matokeo yake yatakuwa kuiangamiza Tanzania.

Mheshimiwa Spika, suala la dini moja kutambuliwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano katika hali ya sasa ya Tanzania ni kuleta mtafaruku mkubwa kwa dini nyingine nazo kudai aina fulani ya utambulisho na hata uanzishwaji wa mahakama zao.

Ikumbukwe Sheria ya Mahakama ya Kadhi ilifutwa miaka 45 iliyopita na wananchi wengi (*new generation*), hawaelewi dhana yake. Kwa hiyo, taifa litaingia gharama kubwa kufundisha mashulenii mpaka vyuoni na hivyo ubaguzi wake kuwa dhahiri.

Mheshimiwa Spika, masuala ya ubaguzi hayatakuwepo tu katika dini husika, bali hata katika utekelezaji wake kwani itabidi mahakimu wawe Waislam pekee na kwa upande wa jinsia matatizo yatakuwepo tu, kwani mshitaki au mshitakiwa anaweza kumkataa hakimu mwanamke kwa misingi ya kuwa mwanamke na kutokana na imani yake, anaona hastahili kuwa hakimu wa kesi yake. Ubaguzi wa aina hii utaturudisha nyuma na hata pale Watanzania watakapoomba wakiwa wa dini nyingine, kimsingi wanawenza kukosa kazi kwa kuwa sio Waislam.

Mheshimiwa Spika, nimetahadharisha vya kutosha, tuwe waangalifu sana, suala hili lisilete mpasuko. Naunga mkono hoja.

MHE. RAJAB HAMAD JUMA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri aliyoiwasilisha katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, uchache wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo: Nchi yetu ni kubwa sana kieneo na ina idadi ya watu ambao hivi sasa wanafikia 35 milioni. Waswahili wanasesma, penye wenye pana mengi. Kadiri idadi ya watu inavyokua ndivyo uhalifu au makosa yanavyotokea katika jamii. Ili nchi yetu iendelee kuwa na utawala bora ni lazima iimarishe vitengo vya kutoa haki, kwa kuwa na mahakama za kutosha na mahakimu wake. Aidha, maslahi yaani mishahara, posho na fursa nyingine ziimarishe.

Tume ya Haki za Binadamu ipo na inafanya kazi vizuri lakini ina upungufu ufuataao:-

(i) Wafanyakazi wake ni wachache; hali hii inasababisha malalamiko mengi kuchelewa kupatiwa ufumbuzi wake.

(ii) Uelimishaji wa elimu ya haki za binadamu na utawala bora bado haujatosheleza. Bado kuna maeneo mengi nchini, Makamishna wa Tume ya Haki za Binadamu hawajayafikia kwa kuyapa elimu juu ya haki za binadamu na utawala bora.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa Tanzania Bara kuanzisha Mahakama ya Kadhi upo kwa sababu nyingi, mionganii mwa sababu hizo ni kama ifuatavyo:-

(a) Sehemu moja ya Jamhuri ya Muungano, yaani Zanzibar ipo Mahakama ya Kadhi bila ya kuivunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(b) Nchi jirani ya Kenya ambayo nayo ina watu wa madhehebu tofauti ya dini ndiyo mfano wa hoja hii.

(c) Zipo Mahakama Maalum kama vile Mahakama za Ardhi, Nyumba, Kazi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, je, mpaka sasa ni sheria ngapi kati ya sheria mbaya zilizoainishwa na Tume ya Jaji Nyalali; zimerekebishwa na Tume ya Kurekebisha Sheria?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. PROF. IDRIS ALI MTULIA: Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Mheshimiwa Jaji Mkuu na Watumishi wote wa Wizara hii, kwa kutuletea hotuba nzuri, iliyojaa maudhui yanayotia imani kwa wananchi wote juu ya mahakama zake. Kwa hiyo, ninaunga mkono hoja mia kwa mia lakini kuna hoja:-

Mheshimiwa Spika, Serikali iongeze Bajeti ya Wizara hii, kwani ni mhimili muhimu wa kusimamia utawala wa sheria wa nchi yetu. Aidha, kuna kesi nyingi zimerundikana zinasubiri kusikilizwa lakini hazisikilizwi kwa upungufu wa nyenzo na mahakimu wachache. Ili tufanikiwe kudumisha amani ya nchi yetu, serikali lazima iongeze Bajeti ya Wizara ili tuweze kuonekana tunatoa haki kwa wakati (*Justice delayed is justice denied*).

Mheshimiwa Spika, tunaomba serikali iwaenzi Majaji, Mahakimu, pamoja na Watumishi wa Mahakama zetu kwa kuwapa mishahara mizuri zaidi na vivutio vingine. Hatua hii itazidisha motisha yao na kuondoa vishawishi vya kuomba na kupokea rushwa. Aidha, wazee wa baraza katika mahakama ndogo wapewe posho nzuri ya kujikimu ili waone fahari na kuipenda kazi yao.

Mheshimiwa Spika, nyumba za mahakimu zijengwe na ziwe na hadhi. Kuwe na chumba maalum katika nyumba hizo ili mahakimu wapate sehemu ya kufanya kazi zao wakati wakiwa nyumbani. Hakimu yupo kama analala nyumba ya kupanga mtaani, naye anatakiwa atoe hukumu juu ya hao hao watu anaoishi nao mitaani. Hili si jambo la busara.

Usafiri wa mahakimu uwe wa uhakika. Mahakimu wetu wasigombee usafiri wa daladala na kupata bughudha na misukosuko.

(a) Upungufu wa Mahakimu ni tatizo kubwa sana Wilayani Rufiji; tunaiomba serikali (Wizara) iongeze Mahakimu kwa Wilaya ya Rufiji.

(b) Tunaomba ujenzi wa Mahakama za Mwanzo katika Wilaya ya Rufiji. Naomba kuwepo na *time table* itakayoonyesha sisi Rufiji tutafikiwa lini.

(c) Tunaomba sambamba na ujenzi wa mahakama, kujengwe nyumba za mahakimu huko Rufiji ili kuwapa mahakimu wetu heshima na motisha ya kupenda kufanya kazi katika mazingira magumu ya Wilaya yetu ya Rufiji.

Mwisho, Serikali isiwe na kigugumizi katika suala la Mahakama ya Kadhi. Hakuna hoja ya msingi ya ucheleweshaji wa kutoa maamuzi hayo, Waislam wanahitaji Mahakama ya Kadhi. Mfano, Uganda Wakristo ni 90% wana Mahakama ya Kadhi; Kenya Wakristo ni 80 – 90% wanayo Mahakama ya Kadhi; Zanzibar Waislam 98% wanayo Mahakama ya Kadhi. Tanzania Bara Waislam zaidi ya 50% wanaonekana kucheleweshewa uamuzi wa kuanzisha Mahakama ya Kadhi.

Mheshimiwa Spika, hakuna hoja yoyote ya msingi ya kuchelewesha uamuzi wa kutoa haki hiyo kwa Waislam.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Katiba, pamoja na Watendaji wa Wizara, kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Nkenge, Wilaya ya Missenyi, tuna upungufu mkubwa wa Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo.

Naomba Wizara itupatie Mahakimu wa Makahama za Mwanzo zifuatazo: Kayanga, Kanyigo, Gera, Minziro na Ndwaniro iliyoko Kata Buyango. Mahakama hizo zipo Tarafa za Kiziba na Missenyi. Mahakama zote hizo zina majengo ya mahakimu na mahakama, tatizo hakuna mahakimu. Kutokuwepo kwa mahakimu kunasababisha wananchi kutegemea mahakama moja tu ya Kyaka na hivyo kuingia gharama kubwa za kusafiri umbali mrefu ili kupata huduma ya Mahakama ya Mwanzo.

Aidha, Wilaya ya Missenyi ni mpya. Naomba Wizara itambue uwepo wa Wilaya na Wilaya ya Missenyi iwekwe kwenye mipango ya Wizara, ikiwa ni pamoja na kujenga Mahakama ya Wilaya na kutupatia Mahakimu wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

MHE. HEMED MOHAMAED HEMED: Mheshimiwa spika, ni vyema nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniamsha hali nikiwa mzima. *Alhamdulillah*. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa maelezo yake yanayotoa sura ya mwelekeo wa kufanikisha utawala bora kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hayo, sasa naomba nielekee kutoa mchango wangu katika hotuba husika.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya serikali ni kuimarisha utawala bora kwa kuhakikisha nchi inaendeshwa kwa misingi ya sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa za kidemokrasia. Vilevile kutoa mafunzo juu ya utawala bora kwa watendaji katika ngazi

zote na kuhakikisha kwamba matokeo ya mafunzo hayo yanaiweka serikali kwenye utendaji ulio wazi na kuzingatia kwa ukamilifu, haki za binadamu katika utendaji wa vyombo vyanya dola.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Wizara ni kufanikisha mafunzo ya utawala bora kwa watumishi wake wote katika ngazi zote, pia kumuwezesha mwananchi kuzijua haki zake. Ni wazi bajeti ya Wizara ni ndogo sana; kufanikisha elimu hii katika mipaka yote ya nchi yetu ni vigumu kutokana na ufinyu wa bajeti hiyo.

Mheshimiwa Spika, dira na malengo ya Wizara ni kuweka mahakama nyingi, pamoja na mahakimu ili kuondoa msongamano wa kesi.

Mheshimiwa Spika, bado nasema azma ya Wizara itabaki kuwa ndoto kutokana na uhaba huu wa bajeti yao. Je; ni kweli serikali ina nia ya kuiwezesha Wizara kufanikisha azma yake au utendaji ubaki kuwa andiko badala ya matendo?

Mheshimiwa Spika, ni muda murefu nchi yetu inakosa dhana ya usimamizi wa pato la nchi yetu kiuchumi kutokana na kuwepo mikataba mibovu. Wizara inatupa jibu gani kutokana na dosari hizi zinazopelekea nchi maskini. Je, Wizara inaelewa hili na kama ni kweli ina mpango gani wa dhati kuondoa tatizo hili ambalo ndio palipo na milango ya ufisadi?

Mheshimiwa Spika, ongezeko la biashara ya rushwa katika nchi yetu limekuwa likizaa fedha haramu siku hadi siku. Yapo baadhi ya maeneo katika Wizara hii ndio chimbuko la rushwa kwa mfano, mahakamani. Mtazamo wa wengi juu ya rushwa hapa nchini, inatokana na mambo mawili tofauti; huduma iliyio na maumbile ya urasimu mkubwa; na kujitoa katika kosa ililolitenda. Hili ni mahakamani.

Mheshimiwa Spika, ili Serikali kutokomeza rushwa, iandae mikakati ya makusudi ya kuhakikisha maeneo ya huduma yawe yameenea katika ngazi zote za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ndoa, mirathi na pia wosia kwa Watanzania ni somo kubwa linalohitaji muda na pia fedha, ikiwezekana na wataalamu walio wengi.

Mheshimiwa Spika, Wantanzania walio wengi wapo vijijini, ambao mara nyingi haki zao kimsingi zinakosekana kwao. Serikali ingepaswa itoe elimu kwa Watanzania wote ili wajue haki zao.

Mheshimiwa Spika, kupatikana kwa Mahakama ya Kadhi nchini, itawenza kusukuma mbele taarifa kwa watu wetu. Pamoja na azma ya Wizara kuwa na nia njema juu ya kuwepo kwa Mahakama ya Kadhi nchini, bado kumebaki kitendawili. Kwa kuzingatia serikali yetu imetua uhuru wa kuabudu, hapana sababu ya dhana juu ya kuwepo kwa Mahakama hii. Ni vyema Wizara iwe mkweli kuruhusu Mahakama ya Kadhi kuwepo nchini. Dhana ya kidini haina sura, mradi haki ya kuabudu ni tamko la serikali.

Mheshimiwa Spika, bado serikali ipo nyuma sana katika kusimamia haki za binadamu. Naiomba serikali itueleze ni jinsi gani watu wanajichukulia hukumu mikononi mwao; wapo watu wanauliwa kwa misingi ya ushirikina kama vile mauaji ya wakongwe na maalbino; kwa nini serikali isilinde dosari hizi? Wapo watu wanaouliwa na kutiwa moto kwa madai kuwa ni wezi; eti wameuliwa na watu walio na hasira; kuna haki gani ya kuua na kutia moto? Matendo haya serikali imejiandaa viperi kuyapinga?

Mheshimiwa Spika, narejea tena kusema Bajeti ya Wizara hii ni ndogo sana, ukizingatia kuwa Wizara imelazimika kutoa elimu kwa watu wapatao milioni 38. Baada ya maelezo yangu hayo, namtakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri katika kazi zake. Ahsante.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wote, kwa kuandaa na kuwasilisha Bajeti ya Wizara mbele ya Bunge lako Tukufu. Hata hivyo, nina mambo machache ya kuchangia:-

Mheshimiwa Spika, nimesoma kwa makini sana, Hotuba ya Kambi ya Upinzani kuhusu uanzishwaji wa Mahakama ya Kadhi. Msemaji wa Kambi hiyo anasema kwamba, tafsiri ya vifungu fulani kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hasa kifungu cha 19 si sahihi.

Mheshimiwa Spika, Msemaji wa Kambi ya Upinzani analeta tafsiri yake. Ifahamike kwamba, Wabunge wote tuliapa kiapo cha utii. Sehemu ya kiapo hicho inasema; nitaifadhi, nitailinda na kuitetea Katiba ya Tanzania kwa mujibu wa sheria iliyowekwa. Hii ni kwa mujibu wa ibara ya 20 ya Kanuni za Bunge (Toleo la 2007), ukurasa wa nane.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 19(1), kinatoa uhuru wa mawazo na Ilani ya Uchaguzi katika mambo ya dini. Aidha, kifungu kidogo cha 19(2) kinaweka bayana kwamba, kazi ya kutangaza dini, kufanya ibada na kueneza dini, itakuwa ni uhuru na jambo la hiari la watu binafsi. Shughuli na uendeshaji wa jumuiya za dini, zitakuwa nje ya shughuli za mamlaka ya nchi.

Mheshimiwa Spika, tafsiri ya kifungu hicho wala haihitaji mtu aliyesoma sheria; mtu ye yeyote ataaelewa kwamba, shughuli za dini zitafanywa nje ya serikali, pamoja na ukweli kwamba, watu wenyewe wana dini zao na imani zao.

Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge tulioapa kuilinda na kuitetea Katiba ya Tanzania ni vizuri tusiidharau. Kama kifungu hicho kina upungufu usio na tafsiri, zipo taratibu za kurekebisha sheria. Si busara Wabunge wakawa wavunja sheria kwa kusukumwa na imani zao za dini.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mbozi yenye eneo la kilomita za mraba zaidi kidogo ya 9000, kata 26 na tarafa sita; ina Mahakimu wa Mahakama za Mwanza wasiozidi kumi na huwalazimisha kufanya kazi katika mahakama za maeneo zaidi ya

mawili tofauti na wakati huo huo hawana nyenzo za usafiri. Hakimu mmoja hulazimika kusafiri kati ya km. 10 hadi km. 60 kwenda kuendesha kesi! Badala ya kufurahia kazi, mahakimu huichukia kwa sababu tu ya mazingira. Hii inaeleza nini? Moja kubwa ni kucheleweshwa kwa kesi za wananchi. Sote tunajua kwamba, mtu anayecheleweshewa kesi yake ni sawa kwamba amenyimwa haki yake.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii, kumshauri Waziri afanye jitihada za makusudi, atuongezee mahakimu walau watano kwa dharura. Aidha, mahakimu hao wapatiwe vifaa vyta usafiri hasa pikipiki ili waweze kusafiri kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

MHE. WILLIAM V. LUKUVI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo kwa Mahakama za Tarafa ya Idodi.

Naomba posho za mavazi kwa Mawakili wa Serikali ziongezwe. Kiasi kinachotolewa hivi sasa, hakitoshi hata kwa pair za mwaka mmoja. Si ajabu hivi sasa kuona Mawakili wa Serikali kutokuwa nadhifu. Naomba iongezwe.

Mheshimiwa Spika, naomba ukarabati ufanywe katika Mahakama za Mwanzo za Kata za Kimande, Ismani, Tarefeni, Idodi na Migoli.

Mheshimiwa Spika, naomba Mahakama mpya zijengwe katika Kata za Nduli, Malengamekali, Izazi, Mahuninga, Mlowa, Ilolo Mpya na Nyang'oro. Ujenzi ukianza, nami nitakuwa tayari kuchangia bati 200 endapo ofisi yako itaamua kujenga hizo Mahakama kwenye Kata hizo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DAMAS P. NAKEI: Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, kwa hotuba yake nzuri. Pia naunga mkono hoja yake kama ilivyowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu, tangu mwaka 2002 nimekuwa nikiomba serikali ilete Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo katika Mahakama za Mwanzo za Dareda, Bashanet na Ufana. Leo napenda kuishukuru serikali kwa kutupatia Mahakimu wa Mahakama hizo na sasa huduma za kimahakama zinapatikana kwa karibu na hiyo kero sasa imeondoka. Hata hivyo, naomba serikali katika Programu yake ya Maboresho ya Sekta ya Sheria, izifanyie ukarabati Mahakama muhimu za Bashanet, Dareda na Ufana.

Mheshimiwa Spika, katika suala zima la ufanisi wa kutoa haki mahakamani, Wazee wa Baraza ni sehemu muhimu. Kinachosikitisha ni kwamba, wazee hawa

wanalipwa ujira mdogo sana. Wanlipwa Sh. 1,500 tu. Nashauri serikali iboreshe hali ya wazee hawa muhimu, kwa kuangalia hali halisi ya maisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Mahakama ya Kadhi, nina ushauri kwamba, masuala ya dini ni nyeti; ni mambo matakatifu (*sacrosanct*), kwa hiyo, haya yafanyike ndani ya mamlaka ya dini zinazohusika siyo Serikali. Naunga mkono hoja.

MHE. DR. LUKA J. SIYAME: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi, napenda awali ya yote, nichukue fursa hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, kwa hotuba yake nzuri, yenye upeo mpana wa masuala ya Wizara yake. Napenda pia nimpongeze Katibu Mkuu, Viongozi, Watendaji Wakuu na Watumishi wa Wizara ya Katiba na Sheria, kwa kazi kubwa waliyofanya katika kutayarisha hotuba ya Bajeti hii na pia kwa shughuli zao za kila siku.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira ya uchache wa watumishi na vitendea kazi, unaowakabili watumishi wa Wizara hii, napenda kuwapongeza sana watumishi hao kwa kufanya kazi kwa moyo wa kujitua. Watumishi wa ngazi mbalimbali, kuanzia za kati kwa maana ya mahakimu hadi ngazi ya chini kwa maana ya wasaidizi wa mahakimu na watumishi wengine, wanapaswa kuboreshewa mazingira ya kazi.

Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo hususan wale wa Wilaya ya Mbozi, ambao husafiri umbali wa zaidi ya kilomita 120 kutoka sehemu moja hadi nyngine, kwa baiskeli ama kwa kudandia magari ya mizigo ili kuendesha kesi. Hali hii inafanya utendaji kazi wa mahakimu hawa kuwa mgumu na pengine kusababisha maamuzi yao kutokuwa sahih, na pia kusababisha mlundikano wa kesi.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mbozi yenye ukubwa wa kilomita za mraba 9,750 ina Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo wasiozidi 10, ambao hulazimika kuhudumia kata 26 na vijiji 200. Katika hali hiyo, kutokuwepo Mahakimu wa kutosha na pia upungufu mkubwa ya Mahakama za Mwanzo, suala la utawala bora na utendaji wa haki linakuwa gumu sana kutekelezwa. Katika hali hii, maonezi na ulaji rushwa vinakuwa mfumo wa kila siku katika jamii ya Wilaya yetu.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Mbozi Magharibi kuna majengo ya Mahakama za Mwanzo yaliyojengwa toka mwaka 1997 na kuahidiwa kufunguliwa, lakini hadi hii leo hayajafunguliwa na hivyo kusababisha mangung'uniko makubwa mionganoni mwa wananchi, ambao walitumia mali zao na nguvu zao kujenga Mahakama hizo. Mfano hai wa jambo hili ni pale Msangano, ambapo tarehe 7 Desemba, 2008, Mheshimiwa Frederick Sumaye, Waziri Mkuu Mstaafu, alipoweka Jiwe la Msingi la Mahakama ya Mwanzo ya Kata ya Msangano. Hivi sasa kati ya Kata 11 zilizopo Jimboni; Kata mbili zina Mahakama za Mwanzo; Tunduma na Kamsamba.

Mheshimiwa Spika, suala la Mahakama ya Kadhi ni suala la ndani ya Dini ya Kiislam, ambalo ni vyema wakaachiwa Waislam wenyewe ndani ya dini yao, walishugulikie bila kuibebesha serikali mizigo wa aina yoyote, kwani serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haina dini bali watu wake ndio wenye dini zao, ambazo mbele ya serikali zina haki sawa ilimradi hazivunji Katiba ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nina maoni kama ifuatavyo: Jeshi la Sungusungu ambalo linafanya kazi kama ya Polisi, litambuliwe kwa kulinda usalama wa raia na mali zao. Kuna ahadi ya kutunga sheria kuwawezesha wananchi wanaotumia vyombo kama baiskeli na pikipiki. Je; ni lini serikali italeta sheria ya kutambua usafiri muhimu kwa wananchi wa kipato cha chini?

Naomba Wizara iondoe upungufu wa Mahakimu katika Wilaya ya Nzega. Ni muda mrefu mno Mahakama za Mwanzo za Puge na Ndala, hazina Mahakimu na majengo yake yamechakaa sana.

MHE. USSI AME PANDU: Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nichukue nafasi kuipongeza Wizara hii chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Waziri, pamoja na Watendaji wote wa Wizara, kwa kuweza kuleta bajeti nzuri na ambayo inaleta matumaini kwa Watanzani, lakini pia ni bajeti ambayo inatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005.

Pamoja na kuwepo kwa Wanasheria wa Serikali wa kufungua mikataba ya mashirika na makampuni, inaonekana kwamba, wanasheria hao hawana taaluma au wanajihuisha na mambo ya ujisadi na kulisababishia taifa kupata hasara kubwa, kutohuna na uzembe huo wa baadhi ya watu wasioitakia mema nchi hii; mfano mdogo ni Mkataba wa RICHMOND. Je, Waziri haoni kwamba sasa kuna haja mikataba yote ya serikali ni vyema ikaletwa Bungeni na kupata ridhaa ya Bunge? Naomba jibu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mazungumzo mengi ambayo yanazungumzia Mahakama ya Kadhi, Ilani ya Uchaguzi ya CCM inazungumzia hilo na imeahidi wananchi kwamba utekelezaji wake utafuata.

Je, Mheshimiwa Waziri anaeleza ni lini Sheria hii italetwa Bungeni ili kutimiza Ilani ya CCM kama ilivyoahidi?

MHE. COL. FETEH SAAD MGENI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, sina budi kumpongeza Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wake wote wa Wizara, kwa kuandaa na kuwasilisha mbele ya Bunge hili, hotuba nzuri iliyogusa maeneo yote muhimu katika kuleta maendeleo ya Kikatiba na Kisheria katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wangu, ningependa kuchangia maeneo machache yafuatayo:-

Mahakama zetu nyingi hapa nchini hasa zile za Mwanzo si za kuridhisha sana. Aidha, majengo ni makongwe na mengine ni mabovu; hivyo yanavunja hadhi ya Mahakama ya Wananchi hasa kama Taifa hili la Tanzania ambalo limejitawala muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, suala la mlundikano wa mahabusu magerezani mara nyingi linasababishwa na kucheleweshwa hukumu za kesi. Kesi nyingi zinacheleweshwa kwa kukosa kupatikana ushahidi wa kutosha au upungufu wa kumalizwa hukumu kwa haraka. Ninashauri juhudzi za kuongezwa Mahakimu na Majaji ziendelezwe. Aidha, watunzwe vizuri Mahakimu na Majaji kwa kulipwa mshahara na stahili zao vizuri.

Mheshimiwa Spika, fursa *Parole* bado haijaeleweka vizuri kwa wananchi wengi vijijini na baadhi katika baadhi ya miji. Wanajaa hofu pale mfungwa anapoachiliwa na kupelekwa kijijini kwao kwa kazi za kumaliza kifungo chake; mara nyingi wananchi wana kuwa na hofu, ninashauri elimu ya fursa ya *Parole* ielimishwe zaidi. Tukiitumia vyema fursa hii, itasaidia sana kupunguza mlundikano wa wafungwa magerezani.

Mheshimiwa Spika, ipo haja kubwa ya kuendeleza Mahakama za Watoto. Aidha, sio busara hata kidogo watoto kuonekana ndani ya gereza la watu wazima. Nionavyo, tunaliharibu taifa la kesho, lazima zitenganishwe.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu huu mdogo, kwa heshima kubwa sasa, ninaomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

MHE. ANNE K. MALECELÀ: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, Nchi ya Tanzania inaheshimika sana kwa sababu ya utulivu wake na amani. Ni vyema sisi Wabunge ambao ni sehemu ya Serikali, tuijepushe na mambo yoyote yale ambayo yatakuwa ndio chanzo cha migogoro na uvunjaji wa amani. Hapa naongelea suala la Kadhi. Mahakama ya Kadhi, lakini jambo ambalo sio sahihi na hatutawafanya haki Watanzania wasio Waislam, kutumia kodi zao walizozitolea jasho na wakawa ni maskini kwa kuendesha Mahakama ya dini moja tu, ambayo ni ya Kiislam. Naishauri serikali kuititia mahakama hizi hizi za kawaida, kwa sababu kuna wanasheria waliosomea *Islamic Law*, hao wanaweza wakatumika kuendesha kesi za Kiislamu. Nirudie waliyoyasema wenzangu kwamba, Waislam wanaweza wakawa na taratibu zao za mahakama kama wanavyofanya Wakatoliki, bila ya kuihusisha serikali na bila ya kugusa kodi za Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kinachohitajika sasa hivi ni Waislam wajipange vizuri sana na kuweza kutatua matatizo yao kwa kutumia sheria zao, bila ya kuihusisha Serikali.

Nirudi kwenye Ilani ya Uchaguzi: Ilani ya Uchaguzi haijasema itafanya bidii kuanzisha Mahakama ya Kadhi. Imesema itaendelea kutafakari; maana ya kutafakari ni kuangalia uwezekano ambao hautaleta madhara. Serikali kuititia Ilani yake, inatafakari faida na hasara za kuanzisha Mahakama ya Kadhi. Ilani inazungumza kutafakari; sio vyema kupotosha maana ya yaliyoandikwa kwenye Ilani ya Uchaguzi. Baada ya kutafakari, serikali ikiona hasara ni nyingi, inaweza ikaamua kuacha. Mahakama ya Kadhi inaweza ikaanzishwa, lakini si busara kutumia kodi za Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Spika, naipongeza hotuba na kuiunga mkono asilimia mia.

Mheshimiwa Spika, Sh. 100 chini ya Sheria ya Mwaka 1949; ni miaka mingi sana takriban 60 sasa. Sheria hii haijabadilishwa na inawatesa sana wanawake. Hii ni pamoja na Sheria ya Fidia. Naomba kumuuliza Waziri; je, hivi sheria hizi zitabadilishwa au kufutwa kabisa na kutunga sheria mpya? Naunga mkono hoja.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, pamoja na wadau wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kuwepo kwa Mheshimiwa Waziri pekee, hakumaanishi udogo au kutokuwa na unyeti wa Wizara hii, bali naamini una wataalam wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, sheria hizi kandamizi, zinazonyanyasa watu kama za ndoa, mirathi na matunzo ya watoto zinaletwa lini Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikataba mibovu, Waziri ameizungumza na nimefurahi kwa jitihada zinazochukuliwa.

Suala la Mahakama ya Kadhi, litazamwe kiundani, ili sheria hizo zitakapoletwa zizingatie imani zote. Ni vyema kupata maoni kwa kina, kwani katika ufanuzi uliotolewa na baadhi ya Wabunge waliozungumzia suala hilo, wamenitisha hasa niliposikia kuwa mwanamke wa imani nyingine, haruhusiwi kurithi. Sasa kwa nini sheria hiyo ianze kufanya kazi baada ya kifo? Kimsingi tuangalie vizuri zaidi.

MHE. CLEMENCE B. LYAMBA: Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumpongeza sana, Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria na Watendaji wote wa Wizara yake, kwa kufanikisha uandaaji wa hotuba nzuri sana aliyoiwasilisha.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuiwezesha Tume ya Kurekebisha Sheria kukamilisha taarifa inayohusu uanzishwaji au kutoanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi.

Mheshimiwa Spika, kuna dalili za wazi kuwa, suala zima la Mahakama ya Kadhi, kwa maana ya mfumo wake, namna ya kuiendesha, muundo wake katika ngazi mbalimbali za vijiji, Tarafa, Wilaya, Mkoa na Taifa, halieleweki mionganoni mwa wananchi wengi na hata mionganoni mwa baadhi ya Wabunge. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri au Serikali, itoe elimu ya kina kwa lugha nyepesi ili kutusaidia wengi kulielewa jambo hili.

Mheshimiwa Spika, napenda Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge lako Tukufu kuwa, Mahakama ya Kadhi itakuwa ni mhimili mwingine pembeni mwa Mahakama ya nchi yetu? Je, ni jukumu la serikali kugharimia uendeshaji wa Mahakama ya Kadhi? Kama jibu ni ndiyo kwa nini?

Mheshimiwa Spika, napenda Mheshimiwa Waziri afafanue; je, endapo Wakristo wataiomba serikali igharimie vyombo vyake vya kidini vinavyoshughulika na masuala ya ndoa, mirathi na kadhalika, kuhusiana na maadili ya jamii; serikali itakuwa tayari kugharimia?

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza ombi langu kuwa, wakati tukisubiri uamuzi wa serikali kuhusiana na Ripoti ya Tume ya Kurekebisha Sheria juu ya Mahakama ya Kadhi, serikali itoe chapisho linaloeleza kwa ufupi kazi za Mahakama ya Kadhi, muundo wake na kadhalika ili itakapofika wakati wa kujadili suala hili, tuwe tumekwisheselewa ipasavyo na tutoe ushauri na uamuzi wa busara kwa manufaa ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Mheshimiwa Jaji Mkuu, Waheshimiwa Majaji wote na Watendaji wote wa Wizara hii na taasisi zake, kwa kazi nzuri sana wanazozifanya. Hivyo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia.

Naishukuru sna Wizara na Mahakama Kuu kwa ujenzi wa Mahakama Kuu Tawi la Shinyanga Mjini. Matumaini yangu ni kuwa ujenzi huo utaenda kwa kasi ili kazi hiyo ikamilike mapema; na ujenzi mzima utaambatana na nyumba stahili za Majaji.

Mheshimiwa Spika, nionavyo mimi, hoja ya kuwepo Mahakama ya Kadhi inapasha kuwa nyepesi ikiwa wanaohitaji wangeamua kuanzisha wao bila ya kuihusisha serikali na umma wote wa Watanzania. Nasema hivyo kwa sababu Waislam ndiyo inawagusa, hivyo hakuna kizuizi ilimradi wataigharimia na kuendesha kwa mujibu wa imani na taratibu za imani yao.

Kuhusu Dini/Madhehebu kuwa na Mahakama zao kwa gharama zao ipo hata kwa wenzetu Wakristo wa Madhehebu ya Katoliki, ambapo Mapadri, Maaskofu na Papa, kwa nafasi na masuala husika ni Majaji kwa mujibu wa taratibu za maisha ya waumini wao katika masuala yanayogusa imani ya Kanisa.

Kwa mfano, Mkatoliki hawezi kufunga ndoa na mtu asiyeye Mkatoliki bila ya kibali cha Askofu mhusika. Hapa Askofu ni hakimu. Ndoa halali ya Mkatoliki ni ile iliyofungwa kanisani kwa mamlaka ya Padri. Ndoa za kiserikali hazitambuliwi na Kanisa la Katoliki kwa waumini wake. Hapa Kanisa ni Mahakama ya Wakatoliki wote, kwa maisha yao yote yanayogusa imani ya Kanisa.

Mifano hii na mingine mingi, inadhihirisha kanisa kuwa na Mahakama yake ikiwagusa waumini wake tu. Mahakama hii inaendeshwa na Kanisa, kwa gharama ya Kanisa na bila kuzungumzwa nje ya Kanisa. Hivyo, Mahakama ya Kadhi na Mahakama nyingine kwa mujibu wa imani ya kidini, zinapaswa kugharimiwa na kuendeshwa na wanaimani husika, bila kuingilia imani na maisha ya waumini wa dini/madhehebu

mengine. Tanzania haina dini, bali Watanzania wana dini zao mbalimbali. Hii iheshimiwe.

MHE. SAID J. NKUMBA: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kukupongeza kwa hotuba yako. Baada ya pongezi hizi, napenda kukuomba mambo mawili kwa ufupi:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Sikunge haina Mahakama kama zilivyo Wilaya nyingine. Kukosekana kwa Mahakama ya Wilaya Sikunge, kunawakosesha haki Wananchi wa Sikunge wasio na uwezo, baada ya Mahakama moja tu ya Mwanzo iliyopo Sikunge Mjini kutoa uamuzi na kama mlalamikaji anaona hakutendewa haki. Hali inayosababisha gharama na umbali kuja Tabora Mjini kufuatilia haki yake. Hivyo, ninaomba Wizara ione umuhimu wa kuweka kipaumbele kuhakikisha kila Wilaya ikiwepo Sikunge, inakuwa na Mahakama ya Wilaya ili kuondoa kero hii.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Sikunge mpaka sasa ina Mahakama moja tu ya Mwanzo; hivyo naiomba serikali angalau ione umuhimu wa kuweka Mahakama za Mwanzo mbili eneo la Tutuo na Tarafa ya Kiwera na moja eneo la Kipiri au Kitunda.

Mwisho, nawatakia kila la kheri na ninaunga mkono hoja.

MHE. JANETH M. MASSABURI: Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumpongeza Waziri wa Katiba na Sheria, Katibu Mkuu na Watendaji wote, kwa kazi kubwa na nzuri sana wanayoifanya na kwa kuandaa taarifa hii. Pamoja na pongezi, nina maoni yafuatayo:-

Kwa kuwa Mahakimu wengi mara nyingi hutoa adhabu ya kifungo kwa makosa madogo madogo, hali ambayo husababisha mlundikano wa wafungwa magerezani na pia huisababishia serikali gharama kubwa ya kuwatunza kama chakula, matibabu na gharama nyinginezo. Ningependa kuishauri serikali itafute uwezekano wa kutumia adhabu za kifungo cha nje kwa makosa madogo madogo, kama kutumikia kwa kufanya kazi za usafi wa mazingira, kupanda miti na kuitunza hata kwa miaka miwili ili nguvu kazi hii ya wafungwa isaidie kutunza mazingira ya nchi yetu. Nchi ya China, imepiga hatua kubwa kwa kuwatumia wafungwa. Kesi ya kuiba kuku au kutukanana na makosa mengine madogo madogo, hukumu zao ziwe kwa kuisaidia serikali kupunguza gharama zake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. DR. SAMSON F. MPANDA: Mheshimiwa Spika, kutokana na umbali wa mahakama uliopo katika Tarafa ya Kipatimu kwenda Kilwa Masoko, hasa nyakati za masika, tunaiomba serikali itupatie mahakama, ili tuweze kutatua matatizo ya Kisheria na hukumu.

Mheshimiwa Spika, Tarafa ya Kipatimu ina vijiji sana kama vile Nandete, Nandembo, Kibata, Mt-kimwaga na uhalifu unaongezeka siku hadi siku kutokana na hali ya maisha inavyokuwa. Aidha, watuhumu wanalazimika kuwasafirisha watuhumiwa

kwenda kwenye mahakama ya karibu kwa gharama zao wenyewe; mfano, mahakama iliyopo karibu ipo Kilwa Masoko – umbali wa kilometra 80.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kilwa Kaskazini wanashindwa kuelewa Mgombea binafsi wa Urais, Ubunge na Udiwani atatumikia chama gani, sera gani na atawezaje kuunda Baraza la Mawaziri na Utawala Bora? Wananchi wa Kilwa, wanapendekeza kuwa, Rais atoke kwenye Chama cha Siasa kilichosajiliwa na kupigwa kura na wananchi walio wengi na kiwe cha utaifa zaidi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Watendaji wa Wizara, kwa maandalizi ya hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Wilaya ya Makete ilianzishwa mwaka 1979. Miaka 28 imepita, Wilaya hii haina Mahakama ya Wilaya. Jengo la Mahakama ya Wilaya lilikwishaanza kujengwa, lakini mpaka sasa halijamalizika na huo msingi sasa umeanza kuharibika baada ya kukaa muda mrefu. Naomba serikali ifafanue ni lini Wilaya ya Makete itakuwa na Mahakama ya Wilaya?

Mheshimiwa Spika, kuhusu watoto wanaopata mimba mashulen; serikali ilete sheria inayoruhusu mtoto baada ya kujifungua, aruhusiwe kurudi sheleni ili apate elimu kwa sababu elimu ni haki ya msingi ya mtoto.

Mheshimiwa Spika, Serikali iharakishe kuleta sheria zinazokandamiza wanawake na watoto. Zipo sheria ambazo zinakandamiza wanawake na watoto kama vile Sheria ya Ndoa ya 1971; Sheria ya Watoto na Vijana ya 1937; Sheria ya Elimu ya 1978; Sheria ya Makosa ya Kujamiihana ya 1998; na Sheria ya Mila ya 1963.

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua muda mrefu kufanya marekebisho na hivyo, kufanya wanawake na watoto kuendelea kukandamizwa. Serikali ileze ni lini italeta sheria hizi?

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ahsante. Hapo ndiyo mwisho wa orodha yangu ya wachangiaji. Kwa hiyo, sasa namwita mtoa hoja ambaye ni Waziri wetu wa Katiba na Sheria. Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kufika wakati huu. Pia ninakushukuru wewe kwa kunipa fursa hii ili nihitimishe hoja nilioitoa jana asubuhi kwa kutoa maelezo kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza na yaliyozungumziwa na Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa Waheshimiwa Wabunge ni wawakilishi wa wananchi ni wazi kuwa wanayoyasema ni mawazo ya wananchi na wameyasema kwa

niaba ya wananchi. Hivyo basi, nafasi hii niliyoipata ni sawa na nafasi ya kutoa majibu kwa hoja za wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa majibu katika maeneo mbalimbali, naomba nianze kwa kutambua wote waliochangia amba wapo katika makundi makubwa matatu, kwanza, wapo wale ambao walitoa michango inayohusu masuala ya Katiba na Sheria wakati wakichangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na pili, wapo wale waliochangia kwa kuzungumza humu ndani ya Bunge na mwisho ingawa si mwisho kwa umuhimu wapo wale waliochangia kwa maandishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza humu Bungeni ni wafuatao, Mheshimiwa Ramadhani Maneno, Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbiri, Mheshimiwa Dr. Omar Nibuka, Mheshimiwa Florence Kyendesya, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Fred Tungu, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Athuman Janguo, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa George Simbachawene na hatimaye Mheshimiwa John Cheyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia masuala ya Katiba na Sheria ya Wizara yangu wakati wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni hawa wafuatao, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Juma N'hunga, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Athuman Janguo na Mheshimiwa Mohammed Abdulaziz. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi na hili ndiyo kundi la tatu ni wengi walikuwa 88 amba ni Mheshimiwa Rita Mlaki, Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Janet Kahama, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Khadija Salim Ally Al-Qassmy, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya na Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Athuman Janguo, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Dr. Omar Nibuka, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mheshimiwa Vua Abdallah Khamis, Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Jacob Shibili, Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa Aloyce Kimaro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mheshimiwa Nuru Awadh Bafadhili, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Meryce Emmanuel, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Mchungaji Dr. Getrude Rwakatare, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Kanali Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Margreth Mkanga, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Ludovick Mwananza, Mheshimiwa Kabwe Zitto na Mheshimiwa Juma Said Omar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia wametoa michango vizuri sana yenye lengo la kuimarisha utendaji kazi na utekelezaji wa majukumu katika Wizara yetu ya Katiba na Sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nimefarijika sana kwa kuchangiwa mawazo na Waheshimiwa Wabunge wengi namna hii. Hii inaonyesha ni jinsi gani Waheshimiwa Wabunge walivyo tayari kutoa michango yao mizuri ya kimawazo katika kuendeleza sekta hii muhimu ya sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, michango ambayo Waheshimiwa Wabunge wameitoa ni mingi, na ni vigumu kuweza kutoa maelezo ya kujibu kila moja ya hoja zilizotolewa. Naomba nitamke tu kwamba michango yote iliyotolewa tunaithamini sana na nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge tutaifanyia kazi kikamilifu. Kama ilivyo

kawaida yetu tutaandaa majibu ya hoja zote kwa kina na tutawasambazia Waheshimiwa Wabunge kablasha lenye majibu yote hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kujibu nitaanza na hoja za jumla ambazo msingi na chimbuko la malalamiko mengi ya wananchi yaliyoelezwa humu Bungeni na Waheshimiwa Wabunge wameyachangia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ni yenyе kuzingatia misingi ya uhuru, haki, undugu, demokrasia na amani ili hayo yafikiwe kuzingatia utawala wa sheria ni suala muhimu na lisiloepukika. Kila mtawala na kila kiongozi anatakiwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa katika utendaji na utekelezaji wa majukumu yake. Wizara ya Katiba na Sheria muda wote tumekuwa tukifanya kila linalowezekana kuiwezesha Serikali katika ujumla wake kutekeleza na kuimarisha Utawala wa Sheria kwa kutambua kuwa huo ndiyo msingi wa uhuru, haki, demokrasia na amani ya kudumu katika jamii yetu. Misingi hiyo ndiyo msingi wa maendeleo ya kiuchumi pia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nguzo kuu ya utawala wa sheria ni uhuru wa Mahakama, sheria na taratibu na kanuni mbalimbali inabidi kutafsiriwa na Mahakama iliyo uhuru. Mahakama ni lazima isimamie sheria pasipo hofu wala woga.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya Bajeti nilieleza jinsi ambavyo uhuru wa Mahakama unavyotekeliza bila ya kuingiliwa na mhimili wa utendaji, naahidi kwamba hali hiyo itaendeleza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la uhuru wa kifedha pamoja na maslahi ya kimishahara na marupurupu mengine kwa viongozi na watumishi wa Mahakama ni kweli kuwa kwa kipindi kirefu hili limekuwa tatizo. Tunayo matatizo makubwa sana kutoka na Bajeti isiyotosha iliyokuwa ikitolewa kwa Mahakama na sekta nyingine za Sheria. (*Makofi*)

Hata hivyo kama nilivyoeleza jana katika hotuba yangu ya Bajeti, Serikali kimsingi imekwishakubali kuanzishwa kwa Mfuko wa Mahakama ambao utasaidia sana katika kutatua baadhi ya matatizo yaliyokuwa yanatusibu katika eneo hili. Kadri uwezo wa Serikali inavyoongezeka, Serikali haitasita kuongeza maslahi hayo ambayo inatambua kwamba ni madogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na ushauri wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala na Msemaji wa Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge wengine ambao wameshauri kuwa Wizara yangu iongezewe Bajeti ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la Mahakama ya Katiba ambalo Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani katika Wizara hii amelizungumzia. Nikubaliane naye kuwa katika Ibara ya 125 ya Katiba inaelezwa kuwepo kwa Mahakama Maalum ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, mamlaka, muundo na utaratibu wa shughuli za Mahakama hiyo umeelezwa katika Ibara ya 126, 127, na 128 za Katiba hiyo. Imeelezwa kuwa kazi pekee

ya Mahakama hii ni kusikiliza na kutoa uamuvi wa usuluhishi juu ya suala lolote linalohusika na tafsiri ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano iwapo tafsiri hiyo au utekelezaji wake unabishaniwa kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa upande mmoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa upande mwingine. Katika kutekeleza kazi yake Mahakama Maalum haitakiwi kuchunguza au kubadilisha uamuvi ulitolewa na Mahakama ya Rufaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pale upande wowote wa Muungano unapotaka suala lolote lenye utata wa tafsiri ya Katiba lishughulikiwe na Mahakama hii basi nusu ya wajumbe wa kuunda Mahakama hii watateuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano na nusu nyingine watateuliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kwa msingi huo na kama ilivyoelezwa na Ibara ya 128 ya Katiba Mahakama Maalum ya Katiba itafanya vikao vyake wakati ule tu inapokuwa na shauri la kusikiliza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hadi sasa hakujajitokeza suala lolote ambalo linahitaji kushughulikiwa na Mahakama Maalum ya Katiba, hivyo Mahakama hiyo hajawahi kuundwa au kufanya kikao chochote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe ufanuzi zaidi kuhusu masuala yanayopaswa kushughulikiwa na Mahakama Maalum ya Katiba huibuka mara chache mno na iwapo shauri lolote linalohitaji kuamuliwa na Mahakama hiyo litaibuka hakutakuwa na tatizo hilo kuhusu kuitishwa kwa Mahakama hii. Hivyo basi, hata sasa haipo sababu ya kufanya Mahakama Maalum ya Katiba iwe ya kudumu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kila nchi inao mfumo wake wa kushughulikia mambo yake. Kwa mfano, katika baadhi ya nchi masuala yanayohusu sheria na vitendo vinavyopingana na Katiba pia hushughulikiwa na chombo kinachoitwa Mahakama ya Katiba. Kwa upande wa nchi yetu kwa mujibu wa Sheria ya *Basic Rights and Duties Enforcement Act* ya mwaka 1994, masuala ya namna hiyo hushughulikiwa na Mahakama Kuu kwa utaratibu maalum wa kuwa na Majaji watatu. Masuala hayo hayo hayashughulikiwi na Mahakama Maalum ya Katiba. Hivyo, kutokuwa na Mahakama Maalum ya Katiba hakufanyi watu kukosa haki ya kufuatilia masuala ya haki zao za Katiba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu adhabu ya kifo uzoefu nchini na hata nje ya nchi umeonyesha kuwa mjadala kuhusu suala hili haukuanza leo na kwa kweli wala hautarajii mjadala huu kuhusu adhabu hii utaisha hivi karibuni, kwa mfano nchini Uingereza ambao adhabu ya kifo ilishafutwa, wapo watu ambao bado wanaibua hoja hii. Hali ni hivyo hivyo Afrika ya Kusini ambao maoni ya kuirejesha adhabu hiyo kuibuka mara kwa mara. Ni kwa msingi huo basi suala hili tulilipeleka katika Tume ya Kurekebisha Sheria ili lihusishe maoni ya wananchi walio wengi. Tume imeniarifu kwamba wanatafuta muda tu wa kuja kunikabidhi taarifa yao, wako tayari. Tukishaipata taarifa hiyo Serikali itayatafakari na hatutazingatia maoni hayo ya wananchi kabla ya kufikia uamuvi wowote. Naomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa jumla tuwe na subira kabla uamuvi wa kudumu haujafikiwa kuhusu suala hili la adhabu ya kifo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mgombea binafsi, tuliwahi kutoa tamko kwamba shauri husika lilikuwa bado liko Mahakamani. Kwa bahati mbaya Mahakama

ya Rufaa ilifuta rufaa ya Serikali kwa misingi kwamba ilikuwa na upungufu wa kisheria kutokana na rufaa hiyo kuwasilishwa Mahakama ya Rufaa ikiwa imeambatanishwa na *decree* iliyowekwa sahihi tarehe tofauti na tarehe ya hukumu ya Mahakama, kwa *technicality* ile rufaa yetu ikatupwa nje. Baada ya uamuzi huo wa kulifuta shauri Serikali imewasilisha maombi ya kuanzisha mchakato wa kukata rufaa tena, maombi haya yanatarajiwa kusikilizwa hivi karibuni. Lakini labda pengine nieleze sababu za msingi kwa nini Serikali bado inasisitiza kuendelea na rufaa katika Mahakama ya Rufaa. (*Makofi*)

Kimsingi hoja iliyopo iwapo Mahakama Kuu ilikuwa na mamlaka ya kisheria ya kuweza kutengua vifungu vya Katiba ambayo ndiyo sheria mama iliyounda pia hiyo Mahakama yenyewe. Hatuendi pale kusema tunamtaka au hatumtaki mgombea binafsi hapana, tunataka uamuzi utelewe na Mahakama ya juu ya nchi yetu. Je, Mahakama Kuu inayo madaraka ya kufuta leo au kesho vifungu viwili, vitatu, vinne vya Katiba ya nchi hii, Katiba ambayo iliunda hiyo Mahakama yenyewe na kwa kufanya hivyo je, kesho wakiamua kuifuta Katiba nzima wana uwezo huo? Ndio tunataka Mahakama ijitamke kwamba tunao uwezo huu au hatuna. Lakini suala la mgombea binafsi wala si mgombea binafsi awepo au asiwepo sio msingi wa rufaa yetu. Kwa hiyo, hoja yetu ya msingi ndiyo hiyo na tunakusudia kukata rufaa ili tupate mwelekeo wa sheria ukoje katika jambo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuongea kuhusu suala la mikataba. Imeulizwa ni lini Muswada utapitishwa na Bunge hili kulipa Bunge uwezo wa kupitia mikataba inayoandaliwa na Serikali. Suala la mikataba nimeshawahi kulzungumza lakini suala la mikataba hususan ile ya kibiashara kuwasilishwa Bungeni ili ijadiliwe na kuptishwa italeta mgongano katika mgawanyo wa majukumu ya mihimili mitatu ya dola. Ukiondona mikataba ya kuridhia iliyoanishwa katika ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya nchi mikataba ya kibiashara iko chini ya utendaji wa Serikali. Mikataba ya kibiashara ina sheria, taratibu na kanuni zake ambazo mojawapo ni suala la *confidentiality*. Hata hivyo Bunge linayo Mamlaka ya Kikatiba ya kuihoji Serikali kuhusu jambo lolote linalotokana na utendaji wake ikiwemo mikataba hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoleza katika hotuba yangu ya Bajeti mikataba huandaliwa na wataalamu mbalimbali ndani ya Serikali wakiwemo wanasheria, wachumi, wahandisi, wahasibu, wataalamu wa masuala ya kodi na kada nyingine kutoka sehemu mbalimbali kulingana na mahitaji ya mkataba. Mkakati uliopo kwa sasa ni wa kutoa mafunzo kwa vitendo kwa Mawakili wa Serikali pamoja na wataalamu wa kada nyingine kusaidia kujenga na kuimariswa uwezo wa wataalam wetu hao katika eneo la kujadili, kuandaa mikataba na kufuatilia utekelezaji wake. Mafunzo ya namna hiyo yataimarisha uwezo wa Serikali kwa ujumla na yatasaidia kuondoa dhana na kasoro hizi za kudhani kwamba ni ofisi moja tu ya Mwanasheria Mkuu ndiyo inayohusika au inayoandaa mikataba mibovu. Pia katika kuongeza ufanisi Wizara ya Katiba na Sheria inashauriana na Ofisi ya Rais Utumishi ili kuona uwezekano wa kuunda kitengo ndani ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ambacho kitashughulikia mikataba peke yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyazungumzia haya masuala ya jumla sasa napenda nijielekeze katika baadhi ya masuala mengine mbalimbali yafuatayo, kwanza lipo suala majengo ya Mahakama ambalo limezungumziwa na Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge wengi waliopata fursa ya kuchangia. Ni kweli kabisa kuwa upo uhaba mkubwa sana wa majengo ya Mahakama hasa Mahakama za Mwanzo Waheshimiwa Wabunge wengi wameomba kujengewa Mahakama sehemu zao. Serikali inapenda kujenga Mahakama katika maeneo yote yasiyo na majengo au yenyé majengo mabovu. Tatizo letu kwa kweli limekuwa ni ufinyu wa Bajeti na hili la ufinyu wa Bajeti karibu Wabunge wote wamelizungumzia kwamba Wizara ya Katiba na Sheria inapewa Bajeti ndogo labda ingefaa iongezwe. (*Makofi*)

Lakini hata hivyo shughuli za ujenzi tumekuwa tunazitekeleza kwa awamu kwa kadri tutakavyokuwa tunapata fedha. Lakini kwa msingi huo basi kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu ya Bajeti kuwa mkakati unaofanywa ni kuwaomba wananchi kushiriki kikamilifu kusaidia kujenga Mahakama za Mwanzo. Uongozi wa Mahakama na Wizara unapanga kukutana na Wakuu wa Mikoa, Wilaya na Wakurugenzi Watendaji wa Miji na Wilaya na kuihusisha wa Ofisi ya Waziri Mkuu kuzungumzia utaratibu mzuri wa kutekeleza mkakati huu. (*Makofi*)

Napenda niwashukuru wananchi wa mikoa ya Ruvuma na Rukwa na kwingineko ambao wamehamasisha wananchi kujitolea katika ujenzi wa majengo ya Mahakama. Ni imani yangu kwamba tutakapopitisha utaratibu huu wa Mahakama za Mwanzo kujengwa na Halmashauri basi itatuchukua muda mfupi sana kuwa na Mahakama ambazo zitatosheleza nchi nzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijaribu kuangalia hoja *specific* moja moja kama zilivyoletwa. Nimelizungumzia suala la mabadiliko ya Katiba lakini suala hili nataka niseme lililetwa limezungumziwa hapa na watu wengi sana. Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Fred Tungu, Mheshimiwa Salum Hemed Khamis, Mheshimiwa Kabwe Zitto, hawa wote wamelizungumzia suala hili wakitaka mabadiliko ya Katiba kukidhi hali ya sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini niseme tu kimsingi mabadiliko ya Katiba au tuseme kuandika Katiba mpya kunatakiwa kuwepo na sababu ya msingi sana ya kufanya hivyo. Mwaka 1961 tulipopata Uhuru kabla ya hapo tulikuwa tunatumia Katiba ya Uingereza, kwa hiyo tulipopata Uhuru tukatunga Katiba yetu ya mwaka 1961. Hili ni jambo kubwa nchi inajitawala, inatoka kwenye mikono ya nchi nyingine inataku kuwa huru kwa hiyo, lazima tuwe na Katiba yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 1962 tulifanya mabadiliko makubwa mengine tulipopata Jamhuri tukaandika Katiba nyingine sasa ni *Republic*. Katika ya mwaka 1977 ilikuwa ije baada ya Muungano lakini kipindi kile kikawa kirefu sana mpaka mwaka 1977 baada ya nchi mbili kuungana tukaunda Katiba ya mwaka 1977. Mabadiliko ya 14 ya Katiba yamefanywa baada ya ujio wa vyama vingi, haya ni *milestones* katika nchi

yetu, unapoandika historia haya ndiyo unayaweka, sasa tunasubiri tupate sababu ya msingi ya kuleta Katiba mpya. Mabadiliko ya Katiba hayakatazwi, tunaruhusiwa kufanya mabadiliko ya Katiba wakati wowote tunapoona kuna jambo hili au lile yanafaa kubadilishwa, tunabdalisha, lakini kuandika Katiba mpya tunapashwa tuwe na sababu kubwa sana ya msingi, bado mpaka sasa sababu hiyo haijapatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna hoja nyingine imetolewa kuhusu *RITA*. *RITA* ni wakala inayoshughulika na uandikishaji wa vifo, mirathi, ndoa, vizazi na kadhalika. Wabunge wengi wamesifia sana. Wameisifu *RITA* na inafanya kazi nzuri na mimi nataka niwashukuru sana kwa pongezi zao kwa kweli *RITA* imebadilika sana kutoka iliyokuwa inaitwa *Administrator General's Office* mpaka kuja kuwa *RITA* mabadiliko ni makubwa. Sasa hivi *RITA* wana uwezo mkubwa wa kuweza kuweka rekodi za matukio ya maisha ya binadamu kuanzia kuzaliwa mpaka kufa na sasa hivi wanaziweka kwenye kompyuta. Mradi mkubwa unaanza wa kujaribu ku-introduce hii kompyuta nchi nzima. Tumeanza mradi huu kwa kufanya majaribio na Wilaya ya Temeke na mpaka sasa mambo yanakwenda vizuri. Kwa hiyo, tunataka kuanza na Wilaya zote za Dar es Salaam halafu tutakwenda mikoa yote. Kwa hiyo, napokea pongezi hizo zilizotolewa na Kamati, zimetolewa pia na Wabunge kadhaa ambao wamezungumzia jambo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, labda nikiwa hapa nizungumzie lingine la jumla ambalo nililiacha makusudi nikasema niliseme mwisho, lakini nimepata wazo labda niliseme sasa, kwa sababu kwenye hotuba yangu ya Bajeti nililizungumzia mwanzo kabisa Mahakama ya Kadhi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, mjadala wa jana na leo umetoa *input* kubwa sana katika jambo hili la Mahakama ya Kadhi. Nataka niwahakikishie kwamba Serikali imesikiliza maoni yote, tumeyasikiliza maoni yote yaliyotolewa na tumesoma *mood* iliyopo na tumeona kwamba hatujakosea kuamua kwa makini sana katika kulishughulikia jambo hili. Bado tunaamua Serikali itakuwa makini sana kuliangalia jambo hili kabla haijatoa uamuzi. *Mood* ya humu ndani, mliokuwepo mmeiona na hawa ni watu hamfiki 200. Sasa tunapoizungumzia nchi nzima lazima Serikali kwa kweli iwe makini sana. Kwa hiyo, tunawaombeni muda, tumepewa ripoti ya kitaalamu iliyotolewa na Tume ya Kurekebisha Sheria tunayo, mtupe muda tuisome, tuitafakari halafu Serikali itakuja na msimamo ambao utazingatia *interests* za Watanzania wote kwa ujumla, hayo ndiyo nitakayoweza kusema kuhusu Mahakama hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nirudi kwenye mengine madogo madogo. Limezungumzwa suala hapa na mtoa hoja dada yangu Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbii, wakati akitoa hoja ya Kambi ya Upinzani kuhusu uenezaji wa matumizi ya TEKNOHAMA au teknolojia hii ya *ICT* katika Mahakama zetu. (*Makofi*)

Mimi nataka nikubaliane na Wabunge wengine wote waliozungumzia jambo hili. Ni kweli mpaka sasa Mahakimu wetu na Majaji wetu bado wanajipinda kuandika na kalamu sisi wenyewe mimi binafsi linanifiedhehesha jambo hili naona kwa kweli ni la kizamani sana tumepitwa na wakati, lakini pia tumechukua hatua mbalimbali ili kujaribu kurekebisha hali hii. Sasa hivi tumekwishaweka mitambo hiyo katika Mahakama yetu ya Rufaa pale na tunaweka pale katika Mahakama Kuu, hivi ninavyozungumza Majaji

wanafundishwa jinsi ya kutumia mitambo hiyo. Ni mitambo ambayo Jaji anakaa pale kama alivyokaa Mheshimiwa Spika ana *laptop* yake kwa hiyo, yanayosemwa yanaandikwa, kwa hiyo, anayasoma. Yanasemwa lakini yanajiandika na kwa wale *Advocate* huku na Serikali na wenyewe wanakuwa navyo pia. (*Makofî*)

Kwa hiyo, ni mitambo ambayo inahitaji kwa kweli wajifunze kuitumia. Mnafahamu sisi mambo haya ya kompyuta bado kidogo tuko nyuma lakini tukishayamudu tu basi yataanza kutumika mara moja, tunaanza na Mahakama ya Rufaa, Mahakama Kuu halafu tutakwenda kwenye Mahakama Kuu zote. (*Makofî*)

Kwa hiyo, tumeliona hilo kwamba kwa kweli tuko nyuma na tunahitaji kubadilika na tumeanza kuchukua hatua za kubadilika. Wenyewe tuna kitu tunaita *Judiciary ICT Road Map* mpango ambaa umegawanya katika sehemu tatu na unabainisha nini kifanyike awamu kwa awamu, kwa sasa Mahakama imeshaanza kutumia teknolojia hiyo kurekodi ushahidi katika Mahakama ya Biashara. Mahakama ya Biashara wenzetu walitangulia, wale wamekwenda vizuri kwa sababu nafikiri sijui kwa sababu wanashughulika na biashara lakini wamekwenda vizuri na ndiyo maana hata ukiangalia taarifa zangu za ufanisi katika Mahakama, Mahakama hii inaanua asilimia 80 ya kesi inazopokea. Kwa hiyo, matumizi ya *ICT* katika Mahakama hii yamesaidia sana na mimi nataka kuamini kwamba tutakapofika katika Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa basi tuta-*improve* zaidi katika umalizwaji wa kesi zetu haraka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, suala la mgombea binafsi nimelisema nafikiri halina mgogoro. Kulikuwa na suala limesemwa kuhusu marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ili usimamiwe na Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Hili lilisemwa na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, alisema kwa nini chaguzi za Serikali za Mitaa zinasimamiwa na TAMISEMI na kwa nini zisisimamiwe na Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba ushauri huu tumeupokea na tayari tunaufanya kazi, tuliletewa mapendekezo na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa hiyo, tunayafanya kazi *positively* na tuko katika hatua nzuri sana hivi sasa. (*Makofî*)

Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary na Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya walizungumzia kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwamba ina upungufu. Sisi tunaamini kwamba Sekretarieti ile inatekeleza vizuri usimamizi wa sheria hii, lakini kwa vile suala hili sasa wanadhani lina upungufu na ninayo taarifa kwamba kuna Kamati moja ya Bunge ikiongozwa na Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala wanaliangalia hili na pia Tume ya Kurekebisha Sheria itaiangalia sheria hii, kwa hiyo, nafikiri mapendekezo yatakayoletwa yataweza kuondoa haya mapungufu yaliyopo, ila nitawaomba tu Waheshimiwa Wabunge hasa Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya na Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary kama wataweza kutupa *input* yao ni nini hasa wanaona kingefaa au kina upungufu gani ili tuweze kulifanya kazi vizuri suala hili tutakapoleta mapendekezo au mabadiliko ya sheria tuwe tumekidhi haja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwenye Mahakama. Suala la maslahi ya Majaji na Mahakimu na watumishi wa Mahakama kuwa finyu hivyo kutoa ushawishi wa

kupokea rushwa, hili limezungumziwa sana na Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Rajab Hamad Juma na Mheshimiwa Mohamed Missanga. Nataka kusema tu kwamba maslahi ya Majaji sasa hivi yanashughulikiwa chini ya sheria yao mpya ambayo mmeipitisha hapa na mapendekezo yanatolewa na yametolewa sasa hivi kuboresha maslahi yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mahakimu na wafanyakazi wengine wa Mahakama yanashughulikiwa chini ya Tume ya Ntukamazina ambayo ripoti yake imekwishatolewa. Lakini hata hivyo nasema ushauri huu tumeupokea na tutaufanyia kazi. Kwa sababu ni kweli mishahara ya Mahakimu, mishahara ya Makarani ni midogo na katika hali ya uchumi ilivyokuwa ngumu sasa inaweza kuwa ni kivutio kimojawapo cha kupokea rushwa. Posho za washauri wa Mahakama ni ndogo hili limesemwa na watu wengi sana. Wanasema posho ni ndogo na kweli posho ni ndogo hizi shilingi 1,500/= ni ndogo kwa hiyo, ushauri huu tunaupokea ila mnajua hali yetu ya kiuchumi hasa Bajeti yetu ilivyo ndogo lakini hata hivyo ni ushauri amba tunaupokea na naomba niseme tutajaribu kuufanya kazi kadri tutakavyoweza kuboresha posho hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala la ujenzi wa nyumba za Mahakimu, kuna suala la usafiri wa Mahakimu na kuna ujenzi wa Mahakama za Mwanzo. Sasa hili la ujenzi wa nyumba za Mahakimu, hili kama nilivyosema tunajaribu kuwasiliana na Ofisi ya Waziri Mkuu ili tuweze kuliweka katika utaratibu ule wa *D by D* tuna hakika tutafanikiwa. (*Makofi*)

Kwanza ukizingatia sasa hivi majengo mengi ya Mahakama toka mwanzo hata kabla ya uhuru wa Mahakama hizi za Mwanzo yalikuwa ni majengo ya Halmashauri. Hata sasa majengo mengi ya Mahakama za Mwanzo ni majengo ya Halmashauri. Kwa hiyo, tunachofanya kwa kweli ni kurudisha tu utaratibu ule wa Halmashauri kujenga hizi Mahakama ili sisi tuweze kutoa wale watu wa kufanya kazi pale. Tunachokusudia kufanya ni kuwapa ramani maalum ambazo zitafanya Mahakama hizi zifanane na tutajaribu kuwaomba kwamba kila inapowezekana lazima pajengwe na nyumba ya Hakimu ambayo angalau basi iwekwe *solar*. Nalisema hili makusudi kwa sababu huko tunakokwenda tunakusudia kupeleka Mahakimu wa Mwanzo amba ni *graduates*. Sasa tutaanza programu hiyo kwa kuwapeleka katika *urbarn centres*, kisha kidogo kidogo tutawapeleka mpaka Mahakama zote za Mwanzo zitakuwa zinaendeshwa na Mahakimu amba wana digrii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninachosema ni kwamba kuanzia hapo tutakapotoa uamuza huo *entry point* ya *gradutes* katika Idara ya Mahakama ni *Primary Court*, atapanda from *Primary Court* atakwenda, atakwenda mpaka atakuwa Jaji. Hiyo ndiyo nia yetu na huo ndio mpango amba tunadhani tukifanya hivyo haya matatizo hatuna Mahakimu yatakwisha, kwa sababu sasa hivi tunatoa wanasheria wengi sana. Juzi pale ofisini kwangu walitangaza nafasi nane za *State Attorney* tulipata *application* zaidi ya 500 kwa nafasi nane tu, zaidi ya 500. Sasa hawa tunao na tuna *faculty* kumi katika nchi hizi ambazo zinatoa hawa watu wanasheria. Kwa hiyo, nina hakika tukiwawekea utaratibu mzuri tu kwamba hii ni kazi ila tu unaanzia hapa na mshahara wako ni huo wa *graduate*

lakini ni *Primary Court Magistrate* utapanda na nafikiri tutaweza kumudu na kuondoa matatizo haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, usafiri wa Mahakimu. Kwa sasa lengo ni kwa kila Wilaya kuwa na gari na tayari katika Wilaya 53 tumeshazipelekea magari. Magari haya Wilayani yanasaidia kufanya ukaguzi wa Mahakama za Mwanzo, pia yanasaidia kuwasafirisha wale Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ambao inabidi wahame kutoka kituo kimoja kwenda kusikiliza sehemu nyingine ambayo haina Hakimu. Ndiyo maana ya usafiri huu na nia yetu ni kufanya hivyo. Sasa hivi katika Mahakama za Mwanzo tunajaribu kugawa pikipiki kwa Mahakimu hao. Sasa nimepata maombi mengi sana ya Wabunge hapa Mheshimiwa Richard Ndassa anataka pikipiki, Mheshimiwa wa Mbozi anataka pikipiki, sasa ninachoweza kusema kwamba tutazingatia maombi hayo wakati tunafanya mgao huu wa pikipiki hizi 100. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini tunajua kwamba mpaka sasa kuna Mahakimu karibu 40 wamekwishakopeshwa pikipiki. Wakati niko kwenye jambo hili nataka nitamke kwamba nimepokea malalamiko kutoka kwa Mahakimu wa Arusha ameniletea Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa kwamba kuna Mahakimu ambao waliambiwa wanakopeshwa pikipiki wamekuwa wanakatwa mikopo hiyo lakini hizo pikipiki mpaka leo hawajazona. Sasa nataka nimhakikishie Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa kwamba hilo ni jambo kwamba nitalifuatilia ni bahati mbaya kwamba amenikabidhi wakati naingia humu ndani sasa hivi. Lakini ni jambo lazima tulifuatilie na nataka nimwagize *Registrar Court of Appeal* alitafutie ufumbuzi jambo hili kama kweli watu wamekopeshwa halafu hawajapata maana yake nini, lazima wapewe pikipiki zao haraka iwezekanavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia aliomba tumjengee Mahakama za Mwanzo Rufiji. Mheshimiwa Mtulia kwa mwaka huu wa fedha kulingana na Bajeti Mahakama za Mwanzo za Ngorongo na Mkongo zimo katika orodha ambazo zile zitajengwa na ile ya Utete itajengwa chini ya mradi wa maboresho ya sekta ya sheria, kwa hiyo, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia sijui ulijua lakini ombi lako lina majibu mazuri, nayo hizi Mahakama tukijenga, tutajenga pia na nyumba za Mahakimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala la upungufu wa Mahakimu ambalo nimeshajibu maswali mengi sana ya Bunge kuhusu suala hili. Ni jambo la kweli hatuna na ufumbuzi wake ndio huu tunaoujaribu kuuleta tuajiri *graduates* tuwapeleke kwenye hizi Mahakama za Mwanzo, hakuna njia nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, chuo chetu cha Lushoto kimekuwa kinatoa watu ambao wana *diploma* na hapa nataka kukiri kwamba tulivyokiwazia chuo kile kilikuwa ni kuzalisha Mahakimu. Tukaanza baadaye kutoa watu wa *diploma* sasa mtu wa *diploma* anawenza kuwa Hakimu lakini si lazima awe Hakimu. Sasa wenzenzu wale wanapata *diploma* zao pale inakuwa ni ngazi ya kuendelea Chuo Kikuu, hawakuja tena kuwa Mahakimu. Ni vizuri tunawahitaji watu wa *diploma* wawe Makarani, Ma-Legal Assistants lakini tunahitaji Mahakimu zaidi. Kwa hiyo, tumeona njia bora labda ni kutumia *graduates* waje kuwa Mahakimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Hakimu wa kuhudumia Mahakama ya Wilaya ya Ileje kwa sababu sasa inahudumiwa na yule Hakimu aliyoko Mbozi, ni kweli Mahakama ya Ileje haina Hakimu, lakini tunampeleka yule Hakimu kutoka Mbozi kwenda kuhudumia Wilaya hiyo, ila nataka nimuahidi Mheshimiwa Mbunge wa Ileje kwamba tunaajiri Mahakimu 40 katika mwaka huu wa fedha, tukishakamilisha ajira hiyo tutahakikisha kwamba mmoja wao anakwenda kuwa Hakimu katika Wilaya hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Godfrey Zambi na yeye pia alisema hakuna Mahakimu Mbozi. Tunaratajia kuajiri Mahakimu 70 wa Wilaya Mahakama za Mwanzo katika mwaka huu wa fedha, baada ya kuajiri nataka nimuahidi Mheshimiwa Godfrey Zambi tutampeleke Hakimu, siwezi kusema Mahakimu lakini Hakimu angalau mmoja. Niseme kwa ujumla kwamba suala hili la ukosefu wa Mahakimu hasa Mahakimu katika Mahakama za Mwanzo ni kubwa kwetu. Maombi ya Waheshimiwa Wabunge ni mengi kweli kuhusu Mahakimu. Tutajitahidi kadri tutakavyoweza ili tuweze kumaliza tatizo hili sio ndani ya mwaka huu wa fedha lakini kwa kadri uwezo wetu utakavyoruhusu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, ameomba kupata taarifa juu ya kesi ya mwanamke kule Zanzibar, Pemba Kaskazini, Wilaya ya Wete kwamba kuna taarifa ambazo hajazithibitisha kwamba kuna kesi ilionekana kuendeshwa kwa kisiasa, sasa alikuwa anasema hana uhakika, anaomba Waziri afutatilie. Ni bahati mbaya kwamba Wizara yangu haina *jurisdiction* kule, hatuwezi sisi kuzidhibiti Mahakama za Pemba au Zanzibar, kwa hiyo, ninachowenza kumshauri Mheshimiwa Mbunge labda kama anaona pengine maonevu basi haki za binadamu zinakuwa zinakiukwa alipeleke kwenye Tume ya Haki za Binadamu ambayo inayo *jurisdiction* Pemba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Gideon Cheyo, alizungumza kuhusu mgongano wa mashauri ya ardhi kati ya Mahakama za Mwanzo na Mahakama ya Ardhi. Kwa hiyo, Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wanatumia sheria mpya zinazohusu mfumo mpya wa kushughulikia migogoro ya ardhi. Ninachowenza kumweleza Mheshimiwa Cheyo ni kwamba kuanzia mwezi Oktoba, 2003 Mahakama za Mwanzo haziruhusiwi kushughulika na kesi za ardhi, zinashughulika na zile kesi ambazo zimewafikia wao kabla na kufikia mwezi Oktoba, 2003 baada ya hapo zinatakiwa kesi hizi ziende kwenye Mabaraza kama inavyostahili hii sheria. Kwa hiyo, kama unaendelea na kesi hizo zitakuwa ni zile ambazo ziliuka kabla ya Oktoba, 2003 lakini labda nichukue nafasi hii pia kuwaomba Mahakimu wazingatie sheria, wasipokee kesi za ardhi katika Mahakama za Mwanzo si mahali pake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala la malimbikizo ya malipo ya washauri wa Mahakama kwamba malimbikizo haya yamekuwa makubwa na sasa yamekuwa ni kero kwa nini washauri hawa hawalipwi kwa wakati. Hili liliulizwa na Mheshimiwa Dr. Omar Mzeru Nibuka. Malipo ya ushauri wa Mahakama hulipwa kufuatana na taratibu za fedha kuitia Hazina Ndogo. Aidha, hufanyika pia kwa kuzingatia Bajeti iliyoindhinishwa ingawa pia tunakubali kwamba haikidhi ndiyo maana kuna mrundikano huo. Pia Mheshimiwa Dr. Nibukau alikuwa ameomba kwamba uwekwe utaratibu wa kuchagua washauri wa Mahakama kwa taaluma zao badala ya kuutumia umaarufu wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, utaratibu na sifa za uteuzi wa washauri wa Mahakama umewekwa na Sheria na Mamlaka ya uteuzi ni Serikali za Mitaa kwa mujibu wa sheria ambayo ni Sheria ya Mahakama za Mahakimu ya mwaka 1984. Kimsingi hawa washauri wa Mahakama historia hizi Mahakama za Mwanzo zilikuwa zinaitwa zamani *native courts*. Zilikuwa zikitumiwa na Waafrika hasa zilikuwa zinashughulika na sheria za kimila. Ndiyo maana Hakimu akikaa pale inabidi ake na wazee wa sehemu ile ili wamshauri kuhusu mila za pale. Walikuwa wanazijua kwa hiyo, sifa yao kubwa ilikuwa ni kuzijua zile mila za sehemu ile na ndiyo maana wakawa wanachaguliwa. Kwa sasa utaratibu unapaswa kuwa ni huo huo ingawa unaweza ukasema mbona Dar es Salaam kuna mila gani pale. Pia *nature* ya kesi sasa hivi imebadilika, kesi zinazotoka pale mijini ni kutukanana, kupigana, na vitu kama hivyo wakati hasa nia ilikuwa ni zile ambazo zinahusu *customs* kama ndoa, urithi, mali na vitu kama hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Omar Nibuka, ameuliza kwamba je, utaratibu wa kuwapatia watumishi nafasi za masomo ukoje? Nasema tu kwamba watumishi wote wanahaki na uhuru wa kuomba nafasi za masomo kulingana na sifa walizonazo. Masomo hayo yapo ya muda mfupi na ya muda mrefu. Kila mtumishi anayo nafasi sawa sawa na wengine kuomba nafasi ya kusoma. Tumejitahidi sana kusomesha wafanyakazi wetu wa hii idara ya Mahakama kwa kadri ambavyo Bajeti yetu imekuwa ikituhusu. Lakini Bajeti yetu si kubwa na hatukuweza kuwasomesha kadri ambavyo tungependa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa ameuliza mpango mkakati wenyewe ratiba kamili wa kuwatekelezea Waheshimiwa Majaji na Mahakimu mahitaji ya vyombo vyaya kisasa vyaya kurekodia kesi kwa mfano *Hansard*. (*Makofi*)

Kama nilivyoeleza tumeshaanza utaratibu huo na pamoja na vifaa vyaya kurekodi Mahakama imeanza kuweka mfumo wa uendeshaji wa mashauri na utunzaji wa kumbukumbu kwa kutumia kompyuta yaani *electronic case management system*. Mfumo huu unalenga kutunza kumbukumbu kwa njia ya mtandao na kuwezesha wenyewe mashauri kupata taarifa za mashauri yao kwa njia ya mtandao. Mfumo huu unawezesha utayarishaji wa orodha ya mashauri ya kusikiliza kesi kwa njia ya mtandao. Mfumo huu tayari unatumika katika Mahakama ya Biashara kama nilivyosema, Mahakama ya Kazi na utawekwa katika Mahakama Kuu ya Dar es Salaam ambapo umeshawekwa na sasa hivi wanafundishwa wale watumiaji wa mitambo hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Gosbert Blandes aliomba kuanzishwa kwa tovuti ya Mahakama. Mahakama tayari ina mpango wa kuanzisha tovuti itakayo julikana ya www.judicially.go.tz hata hivyo Mahakama za Biashara, Kazi na Chuo cha Utumishi wa Mahakama Lushoto tayari zinazo tovuti zake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa amesema Wilaya ya Karatu tangu inaanzishwa haina Mahakama ya Wilaya wala Hakimu wa Wilaya, anauliza ni lini Wilaya ya Karatu itapata Mahakama ya Wilaya, jengo jipya la Mahakama ya Mwanzo ambalo lipo kwenye hatua ya kukamilika kutumika kama Mahakama ya Wilaya kuteuliwa Hakimu wa Karatu.

Ni kweli Wilaya ya Karatu haina Mahakama ya Wilaya wala Hakimu kwa sasa hivi. Mahakama ya Monduli ndiyo inahudumia pia Wilaya ya Karatu. Mpango uliopo ni Mahakama ya Mwanzo kuhamia kwenye jengo jipya. Jengo lililokuwa likitumika na Mahakama ya Mwanzo litakarabatiwa na kutumika kwa muda kama Mahakama ya Wilaya wakati taratibu za ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Karatu zikiendelea katika siku za usoni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuteuliwa kwa Hakimu wa Wilaya, ombi la kumteua Hakimu wa Wilaya ya Karatu litazingatiwa sambamba na kuajiriwa Mahakimu hao 40 ambao nimewataja ndani ya Bajeti ya mwaka huu. Kwa hiyo, tutegemee kupata Hakimu ndani ya Bajeti ya mwaka huu. Hili la upungufu Mheshimiwa Fred Tungu amelisema kwamba Wilaya ya Kishapu ina upungufu wa Mahakimu na majengo ya Mahakama yanayohitaji ukarabati. Wilaya ya Kishapu ina Mahakama za Mwanzo kumi na moja na ina Mahakimu sita. Hali hii ina unafuu mkubwa ukilinganisha na Wilaya nyingine nchini ambazo zina upungufu wa Mahakimu mkubwa zaidi. Hata hivyo nasema tutapeleka Mahakimu zaidi kadri hali itakavyoruhusu ili kukidhi mahitaji ya kishapu. Tutaangalia katika Bajeti yetu na ile ya mradi tuone kama tunaweza kujenga majengo ya Mahakama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, alizungumzia pia kuhusu Mahakimu wengi kukaa sehemu moja kwa muda mrefu. Ni kweli ingawa kwenye Bajeti yangu nimejaribu kueleza kwamba tumehamisha wengi wa Mahakama za mwanzo, tumehamisha kama 87 na zaidi ya mia katika Mahakama za Wilaya lakini bado pengine hatujafikia kuhamisha katika Mahakama zote. Tunazo Mahakama 1,105 za Mwanzo, kwa hiyo, hatujafikia, tumehamisha wachache lakini tunajitahidi. Lakini uhamisho wa mtu ni pesa nyingi. Kwa hiyo, kama kule Kishapu basi kuna Hakimu kakaa sana tutakuja tuangalie tuone jinsi gani tunaweza tukatafuta pesa ya kumhamisha Hakimu huyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Ameir amesema tunaomba Mahakimu na Majaji wawe waadilifu uwezo waliopewa uwe dhamana kubwa kwao binafsi, duniani na akhera tuendako. Mimi naukubali ushauri huu na tunaupokea kwa mikono miwili. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge wengi wamempungeza Mheshimiwa Rais kwa kuteua Majaji wengi lakini pia wengi wanawake. Naomba kwa niaba yake nipokee pongezi hizo, ni jambo zuri lakini hawa hawakuteuliwa kwa sababu tu ni wanawake, wameteuliwa kwa sababu tu wanaweza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, upo ucheleweshaji wa mashauri ya migogoro ya ardhi. Huyu ni Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mbunge wa Kalenga ambaye amesema pia kwamba Mahakama ya Ardhi, Hakimu mmoja anahudumia Wilaya sita, kumekuwa na ucheleweshaji wa kesi na kusababisha ucheleweshaji mkubwa. Tunakiri kuwepo kwa tatizo hili ni kutokana na uchache wa Waheshimiwa Majaji hawa ambao tunao watano tu katika hii Mahakama ya Ardhi nchi nzima. Sasa tunajaribu kushauriana na Mheshimiwa Jaji Mkuu tuone uwezekano wa kuteua Jaji mmoja katika kila zone awe anashughulikia kesi hizo za ardhi tu kwa sababu kesi hizi ni nyingi na kwa utaratibu huu tunaweza tusizimalize. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tukikubaliana naye aseme kwamba kama vile Dodoma kuna Majaji wawili au watatu basi mmoja huyu aelekezwe kuwa wewe utashughukia kesi za ardhi. Hili likifanyika nina hakika tutaweza kupunguza wingi wa kesi hizi na usumbufu ule wa kuondoka kutoka mbali kufuata Mahakama kwenye vituo hivyo vya Mahakama Kuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Mahakama Kuu Singida. Hili la Mheshimiwa Diana Chilolo. Mheshimiwa Chilolo amesema kwamba Singida tayari wameshapata kiwanja, wameshakusanya nguvu, wako tayari kujenga, amenitangulia tu kusema, ninataka nimwambie kwamba katika mipango yetu chini ya *Legal Sector Reform Programme* tunakusudia kujenga Mahakama Kuu Singida na tutakachomuomba Mheshimiwa Diana Chilolo aendelee kuwahamasisha wananchi wake ili tutakapokuja basi wawe tayari kutupokea vizuri ili tujenge Mahakama hiyo. Nazungumza katika mwaka huu wa fedha. Kwa hiyo, baada ya kukueleza hayo sikutegemei kama na wewe utasimama leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa suala la adhabu zinazotolewa Mahakamani kwa kufanya rejea kwenye hukumu za nyuma au za nchi nyingine kwa mfano Urusi. Hili limetolewa na dada yangu Mheshimiwa Maria Hewa, alisema kwa nini tunatumia kutoa adhabu kwa sababu ilishawahidi kutolewa Urusi. Wizi wa kuku basi kwa sababu Urusi alifungwa miaka sita na hapa tuna mfunga miaka sita.

SSasa utaratibu huu wa kujaribu kulinganisha na wenzetu wanafanya nini haupo sana kwenye adhabu, upo sana kwenye kujua je, ni kosa au si kosa. Lakini adhabu zinatungwa na Bunge hili na zimekuwa siku zote zinatungwa na Bunge hili. Tunachofanya pale tunapojaribu kusema kwamba jambo hili hatujawahi kuliamua hapa kwetu. Hivi ni kosa kweli kufanya hivi, tunatizama Uingereza, India sina hakika kama tumewahi kutizama za Urusi. Mimi katika kusoma kwangu Sheria na *ku-practice* bado sijakumbuka kama tuna-*quote precedent* za Urusi labda akina Mheshimiwa Nimrod Mkono wanaweza wakatuambia labda kwenye mambo ya biashara wanatizama hizo. Lakini kinachotizamwa sana ni je, hili ni kosa au si kosa. Katika kosa hili wenzetu walilitazamaje. Lakini adhabu zinawekwa na Sheria zetu za adhabu na tunazo za kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Misungwi, hapa Mheshimiwa Jacob Shibili kwanza amelalamika idadi ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo kwanza hawatoshi na ubovu wa Mahakama ya Mwanzo Inonelwa na Mbalikwa na kwamba Wilaya ipo tayari kutoa eneo la kujenga Mahakama ya Wilaya. Sasa mimi nasema ni kweli kwamba Wilaya ya Misungwi haina Hakimu wa Wilaya na kwa sasa inahudumiwa na Hakimu wa Kwimba. Hata hivyo tunategemea kuajiri Mahakimu wa Wilaya 72 na nataka nimuahidi Mheshimiwa Jacob Shibili kwamba tutampelekea Hakimu mara tu tutakapowaajiri hawa 72. (*Makofi*)

Kuhusu ubovu wa Mahakama ya Mwanzo ya pale Inonelwa na Mbalikwa ni kweli kwamba Mahakama hiyo ni mbovu na Serikali inayo lengo la kuijenga. Sasa hivi tatizo

letu ni hiyo Bajeti yetu haijaka vizuri lakini nataka kumuahidi kwamba tutajitahidi kuongeza Bajeti hii na mara Bajeti yetu ikitengemaa basi tutajitahidi kujenga Mahakama hiyo ya Inonelwa na Mbalikwa. Lakini nimuombe Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakapopitisha mpango huu wa *D by D* basi akae kwenye Halmashauri yake na waweke kipaumbele cha kujenga Mahakama hizi sisi tutamletea Mahakimu wa kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Joel Bendera analalamika kuhusu Mahakama ya *Old Korogwe* haijafunguliwa nini matatizo? Mahakama hiyo haijafunguliwa kutokana na kukosa samani. Samani za Mahakama hiyo zitapatikana katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mariam Kasembe dada yangu analalamika kwamba kuna ucheleweshaji sana wa upatikanaji wa fedha za mirathi. Ni kweli, nataka nikubali kwa sababu mimi mwenyewe nimeshughulikia na kuna malalamiko mengi sana ya pesa za mirathi. Lakini hali hii inatokana na ule mchakato wenyewe na taratibu zinazohusu kupatikana mirathi hii. Inabidi watu wakae kikao cha familia, wachague msimamizi wa mirathi, atangazwe kwenye gazeti zaidi ya siku 21 baada ya hapo ndiyo ana *log* Mahakamani na kule kuna *procedures* zake. Hili ni kweli kuna ucheleweshaji, lakini hii ni kutokana na taratibu na taratibu hizi hazina nia mbaya na nia yake ni kuhakikisha kwamba yule anayekuja kudai mirathi anastahili kufanya hivyo na ndiyo maana inachukua muda mrefu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumeambiwa hapa Chuo cha Lushoto kina Bajeti ndogo kifikiriwe kupanuliwa ili kumaliza uhaba wa matatizo wa Mahakimu. Hili limeletwa na Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Shally Raymond na wengine. Ni kweli Bajeti hii ni ndogo na Wabunge mmegundua Bajeti ya Idara nzima ya Mahakama kwa kweli ni ndogo lakini tunajitahidi. Sasa hivi kinachoendelea tunajaribu kukopa kwa *GEPF* kama Serikali itatupa *guarantee* basi chuo kile kitakopa kitapanua majengo yale na tunawenza kudahili wanafunzi wengi zaidi na hili ni jambo linaloendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Hassan Kigwalilo anasema vitendea kazi katika Mahakama ni vibovu, tupate kompyuta kwa ajili ya Mahakama. Huyu ni Mbunge wa Liwale na hili limesemwa pia na dada yangu Mheshimiwa Mariam Kasembe. Majaji wote kwa sasa wana vyombo vyta usafiri kasoro wale ambao wameteuliwa mwezi Mei na hawa nao tunawapatia magari hivi karibuni. Majaji kama sehemu ya jamii wamekuwa wanatembelea sehemu mbalimbali za nchi kwa ajili ya kuendesha mashauri nje ya vituo vyao vyta kazi. (*Makofi*)

Vile vile majaji wamekuwa wanajumuika kwenye shughuli kadhaa za kijamii na kutoa miadhara inayohusu utoaji haki hapa nchini. Wataendelea kufanya hivyo kadri hali ya fedha inavyowaruhusu maana wanaposafiri pia wanatumia fedha. Majaji Wafawidhi pia wamekuwa wakitembelea sehemu mbalimbali za kanda wanazoongoza kwa ajili ya ukaguzi na kusikiliza malalamiko ya wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunapokea pongezi za Mheshimiwa Hassan Kigwalilo kwa Mahakama nzuri ya Liwale tunashukuru. Mheshimiwa Hassan Kigwalilo vile vile

alizungumzia kuhusu gari la Mahakama. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Hassan Kigwalilo kwamba gari hilo litapelekwa mara moja na tayari hivi ninavyosema dereva amekwisheshatikana na amekwisheshawesa pesa za mafuta ili aanze safari ya kwenda Liwale kupeleka gari hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu rushwa Mahakamani. Wananchi wapewe elimu na ushauri kwamba si kweli Mahakimu wanakula rushwa. Mimi nafikiri tunaupokea ushauri huo na tuufanyie kazi. Suala la rushwa, mimi nafikiri tunaupokea ushauri huo na tuufanyie kazi. Suala la rushwa ni suala mtambuka na kila mahali unapopita nchini hapa unazungumza rushwa, rushwa lakinisa Mahakamani. Tunalifanya kazi, tunatoa elimu, tunaweka matangazo kila mahali na tunajitahidi kadri tunavyoweza kupambana na jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed aliuliza taasisi au viongozi wanapuuza maamuzi ya Mahakama na je, Jaji Mkuu hawezi kuititia uamuza wa Mahakama na wahusika waliokataa kuchukuliwa hatua. Sasa utekelezaji wa hukumu ni suala la Kimahakama na si la kiutawala hivyo si rahisi kwa Jaji Mkuu kuingilia. Hata hivyo Sheria inazitaka Mahakama husika zile zilizotoa amri kuhakikisha kwamba hukumu zake zinatekelezwa. Sasa kama kuna watu ambao wamempelekea malalamiko na bado wanalamika kwamba hukumu zao hazijatekelezwa kinachotakiwa kufanywa ni wao kurudi pale Mahakamani na kuitaka Mahakama ichukue hatua kuhakikisha kwamba hiso hukumu zao walizozitoa zinatekelezwa. Lakini Jaji Mkuu kwa kweli hawezi. (*Makofi*)

Pia alizungumza kwamba pamoja na ongezeko la Majaji bado msongamano wa kesi upo. Nasema pamoja na ongezeko la Majaji bado hawakidhi na hawatoshi, hata hivyo walioongezeka wameanza kazi juzi, *impact* yake labda tutaiona baada ya muda kidogo. Tuvute subira mimi nafikiri haiwezekani tukaongeza Majaji 30 halafu kusitonee chochote; nina uhakika kitatokea kitu. Tujipe muda tutafanya tena tutapima na tutaangalia nini kinaendelea katika Mahakama yetu. Pia katika kusikiliza kesi kama Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed anavyofahamu, kuna vyombo vingi, kuna upelelezi. Kwa hiyo, lazima upelelezi ukamilike ndiyo kesi iendeshwe. Sasa unawenza ukakuta upelelezi umechukua muda mrefu, kesi inakaa, upelelezi haujakamilika. Kwa hiyo, Mahakamani pale kesi ipo inatajwa tu. Kwa hiyo, kunaonekana kuna mrundikano lakini si kwa sababu Hakimu au Jaji hataki kusikiliza, kwa sababu kesi haijakamilika haijaletwa mbele yake, ndiyo maana katika progamu yetu ya *civilianization* huku kutenganisha upelelezi na uendesha mashtaka pia katika mradi huu wa *Legal Sector Reform Programme* tumewafundisha wapelelezi zaidi ya 180 mpaka sasa na tutaendelea kutoa mafunzo na vifaa vikiwemo *mobile cameras* 50 na pikipiki na vitu vingi ili upelelezi ukamilike haraka, kesi ziende Mahakamani zimalizike upesi na wenye haki zao wapate haki zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Said Nkumba amelalamika sana, anasema Sikunge kuna Hakimu mmoja tu wa Mahakama ya Mwanzo. Ninavyofahamu Wilaya ya Sikunge ina Mahakama tano inajumuisha ile Mahakama ile ya Kitunda, Ipili, Sikunge Mjini, Igigwa na Chabutwa. Ni kweli Mheshimiwa ana tatizo la Mahakimu na tunesema kwamba tunaajiri

Mahakimu na katika hao tunaowaaajiri basi tunafikiria ndugu yetu pale ili wananchi wake wapate haki kwa wakati unaostahili.

Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi alizungumzia kuhusu Wilaya mpya ya Rarya kwamba haina Mahakama ya Wilaya. Mheshimiwa anaomba kuanzisha Mahakama ya Wilaya kwa kutumia majengo ya muda. Wilaya ya Rarya ina Mahakama za Mwanzo nne tu ambazo ni za miaka ya 1970 iliyopita na ni chakavu. Wilaya ya Rarya inahitaji zaidi ya Mahakama nne kwani ina Kata 21 zisizo na Mahakama. Ni kweli Rarya haina Mahakama ya Wilaya, Serikali ina mpango wa kujenga majengo kwa ajili ya Mahakama za Wilaya tatizo ni Bajeti. Lakini jinsi Bajeti yetu itakavyoturuhusu tutajenga Mahakama za Wilaya. Ila nimuombe kwa zile Mahakama za Mwanzo basi washauriane na Halmashauri wafanye utaratibu sisi tutawapatia ramani wajenge Mahakama na watakapojenga tutahakikisha wanapatiwa Hakimu mara moja. Tuna mpango huo ambao kama nilivyoeleza kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu ambao nina hakika Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi atatutia moyo na atawahamasisha wananchi pale kwake ili waweze kushiriki katika ujenzi wa Mahakama hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Richard Ndassa yeche anasema usafiri kwa Mahakimu, Hakimu anayehudumia Nyambiti, Nyamikoma, Ngula na Mahakama ya Kolomije, huyu ni mmoja tu na hana usafiri anaomba katika zile pikipiki mia basi ombi lake lizingatiwe. Nataka kumwambia Ndugu yangu Mheshimiwa Richard Ndassa kwamba ombi lako la kupatiwa pikipiki tatalizingatia wakati tunagawa hizo pikipiki 100 zitakazokuja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Balozi Abdi Mshangama anasema hakuna Mahakama ya Mwanzo kwa kila tarafa kule kwake. Sera ya Serikali ni kuwa na Mahakama kwa kila tarafa na kuendelea hadi ngazi ya Kata. Kwa kuzingatia wingi wa wananchi na umbali kati ya Mahakama moja na nyingine lengo hili litafikiwa kufuatana na uwezo wa Bajeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli maombi ninayo mengi na ninaushauri mwingi sana kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na nataka niseme tu kwamba ushauri huu wote tumeupokea na Wabunge nataka niwahakikishie kwa wale walioomba Mahakama ninao Wakurugenzi wangu wa Mahakama za Mwanzo na za Wilaya; nataka kabla hawajaondoka basi waweze kukutana nao kama inawezekana ili wapeleke maombi yao moja kwa moja kwao, maana hivi ninavyosema mimi pengine Waheshimiwa Wabunge wanasema nazungumza tu hapa. Lakini watendaji hawa wapo na mimi ninaweza nikafacilitate ili waonane nao wazungumze kuhusu jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, najua sikufanya kazi ya kujibu hoja zote za Waheshimiwa Wabunge waliochangia lakini hoja zipo nyingi kama nilivyoahidi tutaziandika kila Mbunge aliyetoea hoja yake tutampelekea majibu yanayostahili. Naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru Wabunge wote waliochangia hoja yangu. Mmenipa heshima kubwa kwa kuwa na *interest* tu na Wizara yangu na kunipa ushauri huu na naomba niwaahidi kwamba nitaenda kuutekeleza kwa kadri ya nguvu zangu zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa ufanuzi wa utulivu kabisa, ingekuwa ni Mahakamani na mimi kama ningejaliwa kuwa Jaji basi ningesema kwa kweli ulivyowasilisha ni kitaalam sana na inapendeza kabisa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyopo mbele yetu ni ya kupitisha Makadirio ya Matumizi ya fedha ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2008/2009. Imewasilishwa na imeungwa mkono na kwa utaratibu wetu inahitimishwa baada ya kupitia hatua ya mafungu. Kwa hiyo, nitamwita Katibu kwa hatua hiyo. (*Makofi*)

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama

Kifungu 1001 *Administration and General* Sh. 571,311,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

SPIKA: Wale mnaodhani kunu mshahara wa Waziri hapa hakuna. (*Makofi/Kicheko*)

Kifungu 1002 *Finance and Account* Sh. 25,400,000/=

Kifungu 1003 *Procurement Management Unit* Sh. 21,700,000/=

Kifungu 1004 *Internal Audit Unit* Sh. 17,300,000/=

Kifungu 1005 *Recruitment, Appointment and*

Conf. Sh. 41,170,000/=

Kifungu 1006 *Ethics and Discipline* Sh. 26,150,000/=

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Kifungu 1001 *Administration and HR*

Management Unit Sh. 1,322,119,000/=

Kifungu 1002 *Finance and Account* Sh. 142,361,800/=

Kifungu 1003 *Planning Division* Sh. 230,570,600/=

Kifungu 1004 *Internal Audit Unit* Sh. 61,041,700/=

Kifungu 1005 *Info, Edu and Comm Unit* Sh. 81,240,200/=

Kifungu 1006 *Legal Registry Unit*Sh.118,242,900/=
Kifungu 1007 *Procurement Management Unit*Sh.77,406,600/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1008 *Research and Library Service Unit*...Sh. 258,242,900/=

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye *Sub-vote 260200 Education Material Supplies and Services*. Kwa ujumla wake kifungu hiki ndicho kinacholeta utata kwamba *Attorney General Office* haina Maktaba ya kuwawezesha Mawakili wa Serikali kuweza kufanya utafiti wa kina juu ya mambo mbalimbali kuhusu kazi zao. Nilikuwa naomba ufanuzi juu ya mikakati ya kuboresha eneo hilo ili liweze kukidhi mahitaji ya utafiti wa Mawakili wa Serikali.

MWENYEKITI: Swali lako linahusu kifungu ambacho tumeshakipitisha 1008 ndiyo *Research and Library Service Unit*. Sasa tupo kwenye *Management Information*. Samahani kifungu ndiyo hiki hiki. Mheshimiwa Waziri ufanuzi.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nimpongeze Mheshimiwa Juma Kaboyonga kwa swali lake na kuonyesha kwamba anajua matatizo yetu ya Maktaba yetu pale na vitabu katika ofisi zetu za Kanda kwa kweli pesa hizi si nyingi za kutosha kama alivyosema. Lakini tumetizama na kuona hizi ndizo tunazoweza kuweka hapa ili tununue vitabu hivi pale Dar es Salaam na katika Ofisi zetu za Kanda kila mahali. Hatuna zaidi na hii ndiyo Bajeti tuliyonayo. (*Makofii*)

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiasi naafiki. Lakini nataka Mheshimiwa Waziri anisaidie kufanua kwa nini angalau wasingekwenda kwenye *internet* kwa sababu utaratibu wa sasa hivi si kununua vitabu, mambo sasa yapo kwenye *internet*. Tukiweka *internet* kwa fedha hizi labda tunaweza kufanya vizuri zaidi kuliko kufikiria vitabu, vitabu, vitabu. (*Makofii*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana naye kwa kiasi, lakini kama unavyofahamu, tukienda mahakamani unabeba vitabu, lazima uende navyo. Kwa hiyo, haya ni muhimu. *Internet* pia tunayo pale ofisini na Wanasheria wetu wanatumia kufanya utafiti wa kutosha.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif.1009 – <i>Management Information System Unit</i> ...	Sh.108,242,900
Kif.2002 – <i>Public Prosecution Division</i> ...	Sh.1,919,930,500
Kif.2003 – <i>Legislative Division</i> ...	Sh.603,207,400
Kif.2004 – <i>Zonal Office – Arusha</i> ...	Sh.270,718,400
Kif.2005 – <i>Zonal Office – Dodoma</i> ...	Sh.207,435,400
Kif.2006 – <i>Zonal Office – Dar es Salaam</i> ...	Sh.387,445,800

Kif.2007 – <i>Zonal Office – Iringa</i>	Sh.192,496,300
Kif.2008 – <i>Zonal Office – Moshi</i>	Sh.200,791,200
Kif.2009 – <i>Zonal Office – Kagera</i>	Sh.154,917,400
Kif.2010 – <i>Zonal Office – Mbeya</i>	Sh.208,067,400
Kif. 2011 – <i>Zonal Office – Mtwara</i>	Sh.227,570,300
Kif.2012 – <i>Zonal Office – Mwanza</i>	Sh.337,493,900
Kif.2013 – <i>Zonal Office – Ruvuma</i>	Sh.184,050,300
Kif.2014 – <i>Zonal Office – Sumbawanga</i>	Sh.173,756,300
Kif.2015 – <i>Zonal Office – Tabora</i>	Sh.300,470,600
Kif.2016 – <i>Zonal Office – Tanga</i>	Sh.216,668,900
Kif.3001 – <i>Civil and International Law Division</i>	Sh.658,357,800
Kif.4001 – <i>Constitutional Affairs & Human Rights</i>	Sh.509,501,500

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 40 – Mahakama

Kif. 1001 – <i>Administration and General</i>	Sh.7,077,688,000
Kif. 2001 – <i>High Court</i>	Sh.788,242,000
Kif. 2002 – <i>Court Of Appeal</i> Dar es Salaam	Sh.851,245,000
Kif. 2003 – <i>Arusha Zone</i>	Sh.1,110,871,000
Kif. 2004 – <i>Dar es Salaam Zone</i>	Sh.2,601,613,000
Kif. 2005 – <i>Dodoma Zone</i>	Sh.1,042,788,000
Kif. 2006 – <i>Mbeya Zone</i>	Sh.1,944,756,000
Kif. 2007 – <i>Mtwara Zone</i>	Sh.808,770,000
Kif. 2008 – <i>Mwanza Zone</i>	Sh.1,445,687,000
Kif. 2009 – <i>Tabora Zone</i>	Sh.1,764,070,000
Kif. 2010 – <i>Tanga Zone</i>	Sh.629,541,000
Kif. 2011 – <i>Primary Courts</i>	Sh.6,121,865,000
Kif. 2012 – <i>District Courts</i>	Sh.4,977,123,000
Kif. 2013 – <i>Kagera Zone</i>	Sh.879,391,000
Kif. 2014 – <i>Ruvuma Zone</i>	Sh.403,599,000
Kif. 2015 – <i>Moshi Zone</i>	Sh.963,848,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

Kif. 1001 – <i>Administration and General</i>	Sh.1,572,927,200
Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts</i>	Sh.92,258,700
Kif. 1004 – <i>Legal Services</i>	Sh.177,067,000
Kif. 2001 – <i>Administrative Justice</i>	Sh.328,656,800

Kif. 2002 – *Human Rights*... Sh.223,607,400
Kif. 2003 – *Research and Documentation*... Sh.141,069,2000
Kif. 2004 – *Public Education and Training*... Sh.198,206,000
Kif. 3001 – *Zanzibar Office*... Sh.140,075,700

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria

Kif. 1001 – *Administration and General*... Sh.1,256,234,000

(*Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 60 – Mahakama ya Kazi

Kif. 1001 – *Administration and General*... Sh.900,689,600
Kif. 2001 – *Arusha Zone*... Sh.39,838,200
Kif. 2002 – *Dar es Salaam Zone*... Sh.176,123,200

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 64 – Mahakama ya Biashara

Kif. 1001 – *Administration and General*... Sh.1,137,512,000

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki sehemu ya kwanza, 250100; kiasi kilichopitishwa mwaka jana kilikuwa shilingi milioni 157.3, mwaka huu Wizara inaomba au *Court* hii inaomba shilingi milioni 139.8, wakati tunajua kwamba, mahitaji ya matumizi ya *Court* hii yanazidi kuongezeka; kwa nini hiki kiwango kilichopangwa kimepungua? Naomba ufanuzi.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama hii kwa sasa ina Majaji amba ni watatu. Kabla ya hapo walikuwapo wengi zaidi. Mahakama hii hasa ukiangalia ile inayofuata *PE*, wameweza kujiingizia pesa nyingi sana, kwa hiyo, wana *retention* ambayo wanatumia hasa kwenye *PE*. Mwaka jana walikuwa hawana nyingi, mwaka huu tumepunguza kutoka kwa Serikali, tunabakiza kwao wenywewe.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu – 90 – Mahakama ya Ardhi

Kif. 1001 – *Administration and General* Sh.1,138,289,000

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria

Kif. 1001 – Administration and General... Sh.3,652,026,500

MWENYEKITI: Tunarudi sasa ule ukurasa wa 140. Niwatahadharishe tu kwamba, tumepitia Mahakama za Mwanzo, Mahakama za Wilaya; *Votes* zote hizo hamkusema chochote. Ukisimama juu ya mshahara wa Waziri sasa, kuulizia yale tuliyokwishapitisha ni kinyume cha utaratibu. Ndiyo ilivyo, maana mambo ya Mahakama tumeyapitisha, sasa una suala lipi tena, ndiyo hilo litakuja hapa kwenye sera. Haya tuendelee sasa. (*Kicheko*)

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, nipate ufanuzi mdogo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumze kuhusu matumizi ya sheria. Kule mikoani hasa katika ngazi ya vijiji, tarafa na kata kuna matatizo makubwa ya tafsiri ya sheria za nchi. Kwa mfano, katika ujenzi wa shule na zahanati, wananchi wanachangishwa hela tuseme shilingi 10,000 au zaidi; wengine wanalipa na wengine hawalipi kwa sababu ya uwezo. Wengine wanakimbia majumba yao kujificha kwenye mapori au milimani huko kwa kuogopa kukamatwa. Wanakamatwa, wanawekwa vizuizini, wanafunguliwa mashitaka na wanafungwa Magerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri Serikali ndiyo yenyenye wajibu wa kujenga shule na zahanati, baada ya kukusanya kodi za wananchi. Vile vile si dhambi wananchi kuchangia katika ujenzi wa shule na zahanati watakapoelimishwa na wakaelewa. Sasa hii tafsiri kwamba, yule ambaye halipi akamatwe na kufikishwa mahakamani, wakati wajibu mkubwa ni wa Serikali; kwa nini inakuwa hivyo?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Hemed kama ifuatavyo:-

Hakuna sheria iliyotungwa na Bunge hili inayomlazimisha mtu kuchanga. Sehemu mbalimbali kunaweza kuwa na *by-laws* zimebekwa na Halmashauri katika kudhibiti michango hii na mara nyingi wale Watendaji wa vijiji huwa wanapelekwa mafunzo ya jinsi ya kuzitekeleza sheria hizi. Kuna Chuo chao hapa Hombolo wanafundishwa. Kwa hiyo, wanatakiwa watekeleze masuala hayo kwa kuzingatia sheria. Kabla michango haijaanza kukusanya, wananchi wanapewa taarifa, wanapewa mafunzo, wanapewa maelezo halafu ndio michango inakusanya. Kwa hiyo, Sheria iliyotungwa na Bunge hili kwa kweli hakuna, lakini zipo sheria ndogo ndogo za Halmashauri, ambazo zinakidhi kwa haja hiyo ya ukusanyaji wa michango ya wananchi.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri kwamba, hakuna sheria inayomlazimisha mtu kuchangia lakini haya mambo yanafanyika na yanajulikana. Watu wanashindwa kulipa kwa sababu ya uwezo, maana shilingi 10,000 vijijini ni hela kubwa sana. Mimi ninayo mifano mingi tu, watu wanakwenda kujificha kwenye milima juu kukimbia kukamatwa na kupelekwa magerezani na kufunguliwa mashtaka. Sasa kama hili linafanyika na sheria hakuna, sijui Wizara yake inachukua hatua gani ili kulikomesha?

MWENYEKITI: Nadhani hukumsikiliza vizuri Mheshimiwa Waziri. Katika nchi chini ya Katiba, tuna sheria na sheria ndogo. Sasa zinazotumika huko vijijini na hata katika kata za mijini ni sheria ndogo zinazopitishwa na Serikali za Mitaa, hizo nazo ni sheria na ndiyo wanazozitumia. (*Makofî*)

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nataka nzungumzie kuhusu Mahakama Maalum ya Katiba. Katika majumuisho yake, Mheshimiwa Waziri anasema, haijawahi kuundwa na kwa sababu hakuna jambo kubwa ambalo limeweza kutokezea, likasababisha kuundwa Mahakama ya Katiba, pia inaenda sambamba na maandiko ya Katiba mpya.

Mimi ninavyofahamu, kuna migogoro mingi ambayo inatokana na tafsiri ya Katiba na kwa maana hiyo, katika kumbukumbu ni kwamba, kwa mfano, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imewahi kuunda kamati 12 kwa ajili ya migogoro ya Katiba, ambayo inahusiana siku hizi tunaipa jina Kero za Muungano. Katika kamati 12 hizo, haijapatikana suluhu. Vile vile Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano, imeunda Kamati na Tume saba, kwa mfano, kuna Kamati ya Mheshimiwa Mtei, kuna Tume ya Mheshimiwa Nyalali, Kamati ya Shellukindo, Kamati ya Mheshimiwa Bomani, Kamati ya Shellukindo Namba Mbili, Kamati ya Mambo ya Muungano baina ya SMZ na SMT, Kamati ya *Harmonization*, Kamati ya Masuala ya Simu na yote hayo haujapatikana ufumbuzi maalum.

Vile vile kuna matatizo ya vyama vya siasa au Muundo wa Katiba katika vyama vya siasa. Hii migogoro ya Muungano sasa hivi imeshadumu kwa miaka 44. Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Ibara ya 126 inasema na naomba ninukuu: “Kazi pekee ya Mahakama Maalum ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ni kusikiliza shauri lililotolewa mbele yake, kutoa uamuzi wa usuluhishi juu ya suala lolote linalohusika na tafsiri ya Katiba iwapo tafsiri hiyo au utekelezaji wake umebainishwa kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Mheshimiwa Waziri atufafanulie ni jambo gani kubwa ambalo analijua yeye halijatokezea, ukiacha hayo yote ambayo yametokezea kwa muda wa miaka 44 na hayajapata ufumbuzi hata iwe leo hakuna haja ya kuunda Mahakama ya Katiba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, hivi karibuni tumesikia Naibu Waziri Kiongozi au Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, alivyopingana na kauli ya Waziri Mkuu hapa. Je, bado hakuna haja ya kuunda Mahakama ya Katiba? Naomba ufanuzi.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa ufanuzi Mheshimiwa Mnyaa kwa masuala aliyouliza. Mimi nianze kwa *ku-quote* kifungu hicho hicho cha 126 cha Katiba. Kinasema hivi: “Kazi pekee ya Mahakama Maalum ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ni kusikiliza shauri lililotolewa mbele yake, kutoa uamuzi wa usuluhishi juu ya suala lolote linalohusika na tafsiri ya Katiba hii iwapo tafsiri hiyo au utekelezaji wake unabishaniwa kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, kungeweza kukawa na vifungu vingi tu vya Katiba ambavyo havimpendezi mtu, hakipendezi kikundi fulani cha watu, lakini havibishaniwi baina ya Serikali zetu mbili hizi. Mimi sijawahi kusikia mabishano yaliyowahi kutokea baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Zanzibar kuhusu tafsiri ya ibara yoyote ya Katiba. Ndiyo maana nikasema kwamba, hii bado haijawahi kutokea.

Kilichotokea ni kwamba, kuna vifungu vya Katiba ambavyo watu ama vikundi vya watu hawavikubali. Katika hali ya namna hiyo, wanakwenda katika Mahakama Kuu, inaundwa *Column* ya Majaji watatu, wanasikiliza. Mheshimiwa Mtikila, amefanya hivyo mara nyingi tu kuhusu masuala haya haya ya Katiba na amepata maamuzi. (*Makofi*)

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tu ufanuzi mdogo kwa Mheshimiwa Waziri. Katika mchango wangu wa maandishi, nilikuwa nimeomba ufanuzi kuhusu matatizo yaliyojitokeza kuhusiana na *Law School of Tanzania*. Nina hakika Waziri labda hakuweza kunijibu kwa sababu ya muda, lakini akitusaidia itatusaidia kwa sababu yametokea mambo kadhaa hapa.

La kwanza, hawa vijana ambao wanamaliza Chuo Kikuu sasa, kwa mujibu wa sheria iliyopo wanatakiwa kwenda *Law School* kabla hawajapata nafasi ya kuajiriwa popote. Kwa mujibu wa sheria hiyo, hawawezi kuajiriwa kwa sababu mafunzo yao si kamili mpaka wamepitia kwenye *Law School*. Sasa kwa maana hiyo, inakuwa ni vigumu mtu aliyemaliza kupata ajira.

Tatizo la pili lilojitokeza ni kwamba, hata pale wanapotakiwa kwenda *Law School of Tanzania*, wanatakiwa wajilipie na gharama hizi ni kubwa na kwa sehemu nyingi ni kati ya shilingi milioni moja na milioni moja na nusu. Sasa kwa vijana wetu wengi hasa waliotoka tu Chuoni, hawana fedha hizo. Kwa bahati mbaya, sheria iliyopo haiwatambui kama wale wanaokuwa na haki ya kupata mkopo kutoka kwenye Bodi ya Mikopo. Je, Serikali sasa inasaidiae ili hawa vijana ambao kwa bahati mbaya hawawezi kupata ajira; *Law School* haina uwezo wa kupokea wanafunzi wengi kwa mara moja na wale wanaoweza kupokelewa hawana uwezo wa kwenda kulipa hiyo fedha kwa ajili ya

kujilipia ada; tunaweza kuwasaidia namna gani kundokana na hili pingamizi linalotokana na sheria iliyotungwa na Bunge letu? Naomba ufanuzi.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli matatizo anayoyazungumza Mheshimiwa Mbunge yametokea. Tulipounda hii sheria kulikuwa na kipengele ambacho kilisema wanafunzi wanaokwenda *Law School* hawataweza kupata mikopo, kwa sababu wanapata *Post Graduate Diploma* na Bodi ya Mikopo haitoi mikopo kwa wanaosomea *Post Graduate Diploma*. Kwa hiyo, tumefikia uamuzi kwamba, basi pengine ni jina tu maana kwanza, ile si *Post Graduate* kwa maana ya *Post Graduate*; ni mafunzo ya vitendo, haiwezi ikawa *Post Graduate* na watu wa *NACTE* walitushauri hivyo kwamba, hii haiwezi kuwa *Post Graduate* ikatambulika kama ni *Post Graduate Diploma*.

Kwa hiyo, katika Waraka wa Sheria ambao tutauleta kabla Bunge hili halijaisha, tutaibadilisha hiyo na itawaruhusu hawa vijana waweze kupewa mikopo na Bodi ya Mikopo. Kwa sasa, kwa wale ambao wapo, Serikali imekwishatoa fedha maalum Wizarani kwangu ili tuweze kuwapa na tunaanza kuwapa pesa hizo wiki hii, yaani kati ya leo, kesho na kuendelea, watakuwa wanapokea ili waweze kulipa zile ada na kujikimu maisha yao pale shulenii. (*Makofî*)

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika michango yangu ya maandishi, pamoja na mambo mengine, niligusia suala la Jengo la Mahakama ya Tabora kwamba limehemewa. Kwanza, si jengo ambalo lilikuwa limejengwa kwa ajili ya shughuli za kimahakama. Kwa hiyo, ninaomba ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa sikusikia akitamka nini kitafanyika Tabora; naomba anisaidie nijue Serikali inafikiria nini kuhusu ujenzi wa jengo jipya la Mhakama ya Kanda ya Magharibi? Naomba ufanuzi.

MWENYEKITI: Huwezi kuupata kwa sababu Mahakama ya Tabora ipo kwenye Fungu la 40 na nafasi hiyo ilipotokea hukusimama. Kwa hiyo, ingawa Tabora inanihusu, samahani sana tunaendelea.

(*Hapa Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga alisimama*)

MWENYEKITI: Hii ni *ruling* ya Spika, nakuomba ukae chini. (*Makofî*)

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971. Sheria hii ni ya siku nyingi na imepitwa na wakati na tumekuwa tukiuliza maswali hapa Bungeni. Japo Mheshimiwa Waziri alizungumzia kidogo kwenye hotuba yake, lakini kwa taarifa zilizopo pia katika *Law Reform Commission* wameishapitia na kutoa mapendekezo. Mimi nataka tu Mheshimiwa Waziri, atueleze ni lini Sheria hii italetwa hapa Bungeni, kwa sababu imepitwa na wakati na inawakandamiza zaidi watoto na akina mama? Naomba maelezo. (*Makofî*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa ufanuzi Mheshimiwa Lucy Owenya, kuhusu Sheria ya Ndoa. Sheria hii ya Ndoa ilitungwa mwaka 1971, baada ya mwaka 1969 kufanywa *White Paper* ambayo ilikusanya maoni ya wadau wote. Mwaka 1969 Jaji Spray, aliendesha *White Paper* hiyo na ikazaa Sheria hii ya Mwaka 1971. Ndoa kama unavyofahamu; ni mhimili mkuu sana wa jamii na ni mhimili muhimu. Walipofika mwaka 1971, yaliyomo ndani ya Sheria ile ndiyo ilikuwa muafaka. Sasa hivi miaka zaidi ya 30 imepita, kweli sheria hii inahitaji kutazamwa upya.

Serikali imeamua kuanzia mwaka huu wa fedha na tayari tumeshatengeneza hadidu rejea za kuendesha *White Paper* nchini. Jambo hili si dogo ni zito. Kwa hiyo, tunaendesha *White Paper* mwaka huu, tukikamiklisha tutatunga sheria mpya au tutaibadilisha hii iliyopo sasa. (*Makofi*)

MHE. BENADETHA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia humu Bungeni, nilizungumzia sheria zinazokinzana kama Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 na Sheria ya Maji ya mwaka 2002 na nikataku kujua ni lini zitarekebishwa ili kuondoa utata uliopo. Vilevile nilizungumzia juu ya sheria za mirathi ambazo zipo tatu; zote zinatumika lakini zinaendelea kumkandamiza mwanamke na mtoto wa kike; sheria ambayo inaruhusu mtoto wa miaka 15 kuolewa na ile sheria ambayo inamfanya msichana afukuzwe akipata mimba wakati tumeona kwamba watu wanaowapa mimba hawachukuliwi hatua.

Kwa kuwa mchakato umekuwa wa siku nyingi na watu wanazidi kuumia, watoto wa kike wanabakwa kila siku; ni lini Sheria italetwa hapa Bungeni na ningependa kupewa specific time kwa sababu wanaposema wanaendelea ni mpaka lini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mushashu, sasa unataka ufanuzi kwenye sheria zote? Nadhani ni vizuri ukamrahisishia Waziri ili tuelewe naye aweze kujibu.

MHE. BENADETHA K. MSHASHU: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia nilizungumzia sheria zote zinazokinzana na zile zinazombagua na kumnyanyasa mtoto wa kike. Kwa hiyo, ningependa kupata ufanuzi kwenye sheria zote.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufanuzi hasa kuhusu kile kinachoonekana mgongano wa sheria za maji na sheria za mazingira kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati natoa hoja katika Bunge lako Tukufu, nililitaarifu Bunge kwamba, mwaka huu tunatarajia kuleta Bungeni Muswada wa Sheria mbili; Sheria ya Rasilimali za Maji na Sheria za Matumizi ya Maji. Katika hilo, tutazingatia kwamba sheria hizi hazikinzani na sheria nyingine zozote za nchi na hazikinzani na sheria za mazingira. Ninamshukuru Mheshimiwa Mbunge kwamba, yeze vilevile ni Naibu Mwenyekiti wa Bodi ya Bonde letu la Ziwa Victoria.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba nitoe ufanuzi kwa hoja ya Sheria ya Mirathi na Ndoa, maana hii *age of marriage* ya miaka 15 ipo katika Sheria yetu ya Ndoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, kuhusu Sheria ya Ndoa; *White Paper* yetu itajumuisha pia Sheria ya Mirathi na Urithi na Sheria ya Ndoa. *White Paper* ni utaratibu mrefu ambao tunaenda kwa wananchi. Sheria ya Mirathi na Urithi imekaa siku nyingi na zipo nyingine nyingi. Mambo yanayohusu mila na imani za dini na mambo yanayohusu taratibu nyingine za Serikali, huwezi ukayachukua kwa haraka. Ndiyo maana tukasema hapana, tusikae tukaamua; twende kwa wananchi. Kama nilivyoukueleza, mwaka 1969 walikubaliana kwamba, kuolewa iwe miaka 15, jamii yetu hii ilikubali hivyo, ndiyo ikatungwa sheria. Kwa hiyo, kama inaona miaka 15 ni kidogo, basi twende miaka 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka kukueleza kwamba, siku moja nilikaa na watu wasiozidi 30 wenye akili sana, nikawaambia Sheria ya Ndoa tuibadilishe iwe miaka 18; nilipata ubishi wa ajabu, sikuamini maneno niliyoambiwa pale, nikasema labda twende kwa wananchi watupe mawazo yao.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Wakati nachangia kwa maandishi na pia kwa kuzungumza hapa Bungeni, nilizungumzia suala la Wananchi wa Kijiji cha Kisigiri Kata ya Ilolo, Wilaya ya Shinyanga Vijijini, ambao wametengwa tangu mwezi wa tano, kwa sababu ya kuhoji matumizi na mapato ya kijiji. Wananchi hawa wamekatazwa kwenda kokote, hawaruhusiwi kupata huduma nje ya kijiji na wakifiwa wanazika wenyewe. Wamepewa masharti ili waondolewe kwenye kizuizi wanatakiwa watoe ng'ombe 20 au mbuzi 100!

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale ambao wameweza kutoa wametolewa kizuizini, wengine bado mpaka sasa hivi wanaendelea kuteseka. *Details* zote ninazo na hata majina ya viongozi walioendesha kikao hicho na kutoa maagizo hayo ninayo. Naomba kujua Serikali inasemaje kuhusiana na wananchi hawa? Naomba ufanuzi.

MWENYEKITI: Sasa umekaa nayo ya nini, maana yake ingekuwa vizuri uipe Serikali ifanye kazi kama una majina hayo?

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, majina pia nimeyaandika kwenye maandishi Mheshimiwa Waziri anayo.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimjibu Mheshimiwa Magdalena Sakaya kama ifuatavyo:-

Tunamshukuru kwa taarifa hiyo, lakini namwaarifu tu kwamba, sheria ya kuweka watu kizuizini haitekelezwi namna hiyo. Hata pale ilipokuwepo ilikuwa haitekelezwi hivyo. Tunastaajabu kwamba, kuna watu wanaoweza kuweka wenzao kizuizini na

kuwapa masharti! Tutashukuru sana kama tutapata hayo majina na *data* za kesi hiyo zote tuzifuatilie.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuomba ufanuzi kwa Mheshimiwa Waziri. Nilipokuwa nikichangia kwa maandishi, nilichangia pamoja na maeneo mengine, eneo nyeti la kulipatia ufumbuzi suala la Mahakama ya Kadhi. Nilipochangia nilibainisha kwamba, hakuna ubishi kwamba, Waislamu Quran Tukufu inawapa au inawataka mambo yao yahukumiwe kupidia kwenye kitabu. Nilisema pia hakuna ubishi kwamba, Quran hiyo hiyo inaweka bayana au kutambua kuwepo kwa watu wa imani hiyo na watu wa imani nyingine kwamba, sisi na dini yetu na ninyi na dini yenu; *lakum dinikum waliyadini*. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliweka bayana katika mchango wangu kwamba, hakuna ubishi kwa kuwa wewe na mimi na dini yangu mimi niliye Mlutheri ninapata maamrisho yanayonitaka vilevile kama wewe unavyoamrishwa kwa imani ile kupata hukumu yako kupidia kwenye Quran kwamba, nendeni ulimwenguni mkayafanye mataifa yote kuwa wanafunzi wangu na kuwabatiza katika jina la Mungu Baba, Mwana na Roho Mtakatifu na tazama mimi nipo pamoja nanyi hadi ukamilifu wa dahari. Ninaagizwa mimi niliye Mkristo nifanye hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ibada zote hizo ambazo hazibishaniwi nilishauri kwamba, kwa kuwa hili lipo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ibara ya 19(2), linabaki kwamba ni suala la ibada ambalo linashughulikiwa na taasisi zenyewe. Je, Serikali haioni kwamba ili kuepuka kuingia kwenye mgogoro pengine katika suala la kuelekea kulipatia ufumbuzi suala hili la Kadhi ambalo linahusu watu wa imani moja, suala hili sasa lielekezwe tu kwamba hata kuanzia kesho, Waislamu wakakutane hata mbele ya Mufti na BAKWATA na wengine wote wakatafakari wenyewe waanzishe yao, lakini isiletwe ndani ya Bunge hili ambalo linatawaliwa na Katiba hii ambayo pengine ukiendelea kulijadili hapa litahitaji kubadilishwa kwa Katiba ya nchi na pengine litaanza kuleta mzozo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kupata maoni ya Serikali kwamba ni kwa nini hasa wasiwaachie washughulike nalo, wahukumiane wanavyoona wao na isiingie huku wala isiingie Serikalini; Serikali inapata kigugumizi gani kujiiondoa *completely* kwenye jambo hili na kuwaacha waendelee wao kama Wakatoliki wanavyoendelea na ya kwao na sisi Walutheri tunavyoendelea na ya kwetu? Nataka maelezo ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, katika mchango wangu wakati fulani nilipokuwa nikichangia Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, nilijaribu kutafakari juu ya kinga inayotolewa na sheria ya kufanya suala la akaunti ya mtu kuwa ni siri yake yeye na benki. Nilisema sheria ile haiweki bayana juu ya akaunti zile zinazohisiwa kuwa na fedha au harufu ya fedha chafu. Nikataka Serikali itupe maelezo kwamba, inaonaje kulitafakari jambo hili maana mimi nilipendekeza pengine iletwe katika hati ya dharura kubadilisha sheria ili zile fedha chafu ambazo zinawekewa kinga hata zile akaunti zenyewe, ziondolewe kinga sasa isiendelee kuwa ya faragha ibaki kuwa ya wazi na ili

kusaidia vita dhidi ya ubadhirifu wa mali ya umma. Nilikuwa nafikiri ni vizuri nikajua *position* ya Serikali katika hili.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufanuzi kwa maswali mawili ya Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Ole-Sendeka, akubali maneno niliyoyasema wakati nahitimisha hoja yangu kwamba, nimesikia Serikali imezisikia hoja zote zilizotolewa leo humu ndani, pamoja na ya kwake aliyokuwa ameiandika. Serikali itatafakari na itakapotoa uamuzi wake, itatoa uamuzi huo kwa kuzingatia hoja zote hizi zilizotolewa na Wabunge na wengine na mapendekezo ya Tume ya kurekebisha Sheria. Naomba akubali kwamba, tutachukua hatua hiyo na kama nilivyosema, mara uamuzi huo utakapotolewa basi utaletwa na wananchi wataufahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu akaunti ya fedha zinazosemekana ni chafu au zilizotokana na njia ambazo siyo halali ni kwamba, tunayo sheria inayoitwa *The Anti-Money Laundering*. Sheria hii inairuhusu Serikali kuzikagua hata kuzikamata akaunti hizo za pesa zinazohisiwa kuwa ni chafu, kuzichunguza, kuzikagua na kuzikamata na kuzifunga. Serikali ina madaraka hayo na hata hii sheria yetu mpya ya *PCCB* inaweza kutumika kufanya kazi hiyo.

MWENYEKIDI: Basi mfanye sasa inakuwa... (*Kicheko*)

MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi katika mchango wangu wa maandishi, nilitaka kujuwa watumishi wa mahakama wanapostaafu huwa hawapati mafao yao; kwa mfano, kuna mtumishi mmoja anaitwa Aloyce V. Toyi, aliystaaafu tarehe 30 Disemba, 1998 Kigoma Vijijini. Ilibidi nichukue hati zake nikazileta kwa Mheshimiwa Mary Nagu wakati akiwa Wizara hiyo tangu mwaka 2007, lakini mpaka leo hajapata kitu na yule mzee hawezitumbea ni wa kushinda ndani. Sasa hivi ana miaka 11 hajapata mafao yake; je, Serikali mnasemaje?

MWENYEKIDI: Tueleze alikuwa anafanya kazi gani katika mahakama?

MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA: Alikuwa ni mbeba mafaili. (*Kicheko*)

MWENYEKIDI: Sidhani kama kuna kada ya namna hii, yaani Mhudumu?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa ufanuzi uliouomba kwa Mheshimiwa Mbunge umenisaidia kuelewa tatizo linaweza likawa liko wapi. Hawa Wahudumu wapo katika kitu kinachoitwa *operation service*, siyo *permanent and pensionable*. Malipo yao yanatoka *NSSF* na wanachangia *NSSF*; kwa hiyo, wanapostaafu wanaidai *NSSF* wanalipwa hawadai Serikalini. Kama angekuwa ni mtumishi ambaye yupo katika zile *term za permanent and pensionable*, basi angelipwa na Serikali kama inavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda alileté kwangu, mimi nataka nimuhidi ndani ya miezi miwili tutakuwa tumempa jibu la kulimaliza jambo hilo.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi jioni hii. *The right of justice* ni haki ya kila Mtanzania na kwamba, maeneo ya Jimbo langu la Tandahimba haki hii inakosekana kwa sababu watu hulazimika kutembea umbali wa zaidi ya kilomita 100 kwenda Mtwara au Newala kutafuta haki hiyo, kwa sababu tunakosa mahakama, lakini Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba ...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Njwayo, hebu kaa kwanza. Waheshimiwa Wabunge, nilitoa mwongozo hapa kwamba, tutazame haya mafungu. Huyu anaanza tena kwenye Fungu la 40, tulikwisha lipitisha; kwa hiyo, kama unashida ya mahakama haiwezekani sasa labda ukija kwenye Kitabu cha Nne kama itahusu masuala ya maendeleo. Kwa Kitabu cha Pili tumekwishafunga, kwa hiyo tunaendelea

MHE. ATHUMANI S. JANGUO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niombe ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kuhusu Mahakama ya Kadhi. Nimemuelewa vizuri sana na tunashukuru kwamba, Serikali sasa hivi inashughulikia, lakini kwa kuzingatia kama alivyosema mwenyewe katika hotuba yake, suala hili limeanza tangu mwaka 1958; ni miaka 50 sasa. Je, anaweza kutuambia sasa itachukua muda gani katika kusubiri maamuzi ya Serikali ama kuja na tamshi au kuleta hoja hapa Bungeni kwa ajili ya kulishughulikia suala hili?

MWENYEKITI: Kabla hajajibu, labda tuelewe tu kwa ninyi wenzetu mnaolifahamu vizuri; kinachodaiwa hapa ni nini; ni mahakama itakayoundwa na Serikali au ni kitu gani hebu tuwe wazi tujaribu kupata jibu?

MHE. ATHUMANI S. JANGUO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumechangia kwa muda mrefu na katika mchango wangu wote wa kimaandishi, pamoja na wa kuchangia hapa Bungeni, nimeeleza hata *predecessor* wako; hatua alizozichukua kuunda Kamati mara tatu zikilishughulikia suala hili na kwenda katika nchi mbalimbali ambapo Mahakama ya Kadhi ipo ili kuweza kuona ni namna gani kero hii inaweza kushughulikiwa. Sasa leo Mheshimiwa Spika unauliza tunachodai ni nini; nitashindwa kujibu!

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tuelewane vizuri tu, hakuna haja ya jazba ya kiasi hicho. Tunachohitaji hapa dai lenyewe ni nini hasa; ni kwamba Bunge hili litunge sheria itakayoletwa kwa Muswada wa Serikali ili ianzishwe Mahakama ya Kadhi itakayoshughulikia sehemu moja ya jamii; ndiyo hoja hiyo? Sasa ukiniambia juu ya aliyenitangulia ni mambo mapya ni lazima tuelewane.

MHE. ATHUMANI S. JANGUO: Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia. Waislamu wanadai kuwapo Mahakama ya Kadhi ili masuala ambayo yapo chini ya *Personal Laws*; mimi siyo *learned friend* wewe mwenyewe najua ni *learned friend*;

ambayo hivi sasa yanaamuriwa na watu ambao hawajui yanayoagizwa katika Kitabu cha Waislamu; ambayo ni maagizo ya Mwenyezi Mungu, yaweze kuamuriwa kwa mujibu ya dini yao. Anayeweza kufanya hivyo, siyo Muislamu yejote tu, mimi siwezi lakini ni mtu ambaye amesomea *Islamic Law*, ambaye anaweza akatoa maamuzi yanayoendana na yale ambayo yapo katika dini. Ndiyo linaloombwa.

Kwa bahati nzuri, nashukuru kwamba, Chama cha Mapinduzi kimelitambua hili na katika Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2005; jana nimenukuu ibara ya 99 na ibara ya 108; wameliona hilo na wakasema lishughulikiwe ili liweze kumalizika.

MWENYEKITI: Lakini ilani inasema litafutiwe ufumbuzi, halisemi kwamba iundwe mara moja. Sasa mimi nadhani alichosema Mheshimiwa Waziri, jamani limekwenda kwenye Tume; suala la Kadhi ni muhimu sana kwani linagusa imani ya watu, tulichukue katika mkondo ambao Serikali inalishughulikia hivi sasa. Taarifa ya Tume ndiyo ameipata mwaka huu na kutokana na mjadala mtalionna ni gumu na lina utata. Kwa hiyo, pengine mimi ningeshauri kwa hali zote kwamba, tuliachie kwenye mkondo huo.

Katika vikao vijavyo, tuulize hatua zinazoendelea katika utekelezaji, kwa sababu kwa hatua za leo ya mwisho kabisa ndiyo hii ya Mheshimiwa Waziri kusema kwamba, Taarifa ya Tume ya Kurekebisha Sheria ambayo ilitembea nchi nzima, imefikisha mapendekezo yake Serikalini. Ahadi ya Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ni kwamba italetwa Bungeni. Mimi nadhani katika hatua hiyo sasa, kinachohitajika mwezi wa kumi na moja ni kuuliza *progress report*, mwezi Januari tuulize na mwezi wa nne nina hakika tutapata jibu.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima zote, Mzee Janguo ameshalieza na wewe umelieleza, basi naomba yazingatiwe yale ambayo wewe na Mheshimiwa Janguo mmeiyasema.

MHE. EMMANUEL J. LUAHULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi hii. Wakati nachangia kwa kuzungumza, niliongelea suala la Sungusungu na hasa nikaeleza Sungusungu ndiyo walinzi wakuu katika maeneo yetu kando ya ziwa, pamoja na maeneo ya Mkoa wa Tabora na sehemu nyingine ambapo imeanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sungusungu hawa wamekuwa wakifanya kazi hasa kwa upande wa Wilaya yangu, wamefanya kazi kwa hisani ya Viongozi Wakuu katika Wilaya ile kuwalea na kuwalinda. Nataka kujua kwamba, hawa Sungusungu wanalindwa na nini, kwa sababu tukiwaacha tu wakashindwa kufanya kazi zao; uhalifu na ujambazi utaongezeka sana hasa katika maeneo yangu katika Wilaya ya Bukombe?

Ninaomba ufanuzi hawa Sungusungu wanalindwa na sheria gani, kwa sababu mwaka 2006 katika bajeti hii ililetu mgogoro; aliye kuwa Waziri Mkuu akasema, Sungusungu waliofungwa walete taarifa zao likaishia pale. Nataka ufanuzi.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Luhahula kwamba, Bunge lako Tukufu bado halijaitungia sheria. Sasa hivi hawa wanaitwa walini wa jadi, wanatumika kulingana na sheria za jadi za sehemu walizopo. Labda kama Mheshimiwa Mbunge, anatushauri tuwatungie sheria; tutazingatia ushauri huo kuona ni jinsi gani tunaweza tukalinda zile shughuli zao. Hawa ni walini wa jadi na wanafanya kazi kwa kuzingatia taratibu za kijadi za sehemu walizopo.

MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri. Aliyoyaeleza ni sawa lakini nilichotaka kujua ni kwamba, hawa Sungusungu wakati mwininge wanapofanya kazi zao, anatokea mhalifu ambaye pengine wamemkamata na sisi kikwetu kuna siku ambayo wanasesma ni ya kutawazwa, wanawatambua wahalifu ndani ya kijiji kile.

Wakishawatambua pengine labda wanapeana faini, ndiyo nataka kulieleza kidogo labda atoe elfu ishirini au ngapi, wanakimbia kwenda polisi na polisi wanakuja kumkamata Sungusungu na kumuweka ndani. Matokeo yake, hawa wahalifu wanaendelea kutamba kwamba, sisi hamtuwezi kwa sababu hakuna sheria yoyote inayowalinda.

Ninachotaka kujua ni kwamba, japokuwa hawajatungiwa sheria; je, kwa nini usiwepo Waraka mahususi kwenye Serikali za Mitaa, unaohusu ulinzi shirkishi unaosemwa na *IGP* Mwema ili waweze kutambulika katika ulinzi shirkishi. Naomba maelezo.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, kuna sheria ambayo inatambua Sungusungu - Sheria ya *People's Militia*. Kwa hiyo, wakati wakifanya kazi zao wanatambuliwa kwamba ni Polisi.

MWENYEKIDI: Unaona mambo hayo, sasa hii naona itolewe elimu zaidi ili katika maeneo yanayohusika, waweze kuelewa miiko yake na kadhalika.

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nimezungumzia mambo mengi, mojawapo lilikuwa ni kuhusiana na kupandishwa vyeo kwa watumishi wa Wizara ya Sheria, hasa Mawakili wa Serikali. Nimezungumza kwamba, wapo Mawakili wa Serikali wamekaa ofisini zaidi ya miaka mitano, ambapo kisheria wanatakiwa wawe wameshapandishwa vyeo, lakini mpaka sasa hivi hawajapandishwa.

Mheshimiwa Waziri, wakati ana-*windup* hakuweza kulizungumzia vizuri. Mimi nilitaka atuhakikishie kwamba, wale ambao wamekaa zaidi ya miaka mitano na wanaendelea kupokea mishahara kama mtu aliyeanza mwaka huu; je, Serikali inasemaje na inalishughulikia vipi hili kwa haraka sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nilizungumzia kuhusiana na mafao ya Mawakili wa Serikali, hasa mishahara yao ni mibovu, midogo na inayokatisha tama. Mheshimiwa Waziri, alijaribu kulizungumzia kwa ujumla sana. Mimi nataka kujua ni lini Mheshimiwa Waziri ataleta sheria mahususi, inayozungumzia maslahi na mafao ya Mawakili wa Serikali?

MWENYEKITI: Nikuelewe vizuri, unataka kusema Mawakili watungiwe sheria yao ya maslahi; mbona hatuna sheria za maslahi?

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yangu ni kwamba, utaratibu wa maslahi wa Mawakili wa Serikali, kama ambavyo tumepitisha sheria ya maslahi ya Majaji.

MWENYEKITI: Sasa huo ni mhimili.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi kwa hoja mbili za Mheshimiwa Blandes kama ifuatavyo:-

Kuchelewa kwa watu kupandishwa vyeo, kunaweza kukatokana na sababu nydingi si *automatic* kwamba, ukishafikisha miaka kadhaa basi unapanda. Lipo suala la utendaji kazi, kuna watu wanakupima utendaji wako ukoje, ukishapata sifa za kutosha unapanda cheo. Kama wapo watumishi ambao wamefanya kazi vizuri na hawajapandishwa vyeo, nataka nichukue nafasi hii kuwataka Maafisa Utumishi, wazingatie wajibu wao na kuwapandisha vyeo maafisa wote wanaostahili kwa wakati wanapostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafao ya wanasheria yapo katika utaratibu wa kawaida wa mafao ya utumishi wa serikali. Kwa hiyo, suala la kutunga sheria rasmi kwa ajili ya mafao ya utumishi ya Mawakili wa Serikali peke yao, kwa kweli tutakuwa hatujafikiria. Wazo limekuja tunalipokea, tutaona kama uwezekano huo utakuwepo tutafanya hivyo, lakini tunalipokea kama wazo.

MHE. OMAR M. NIBUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina swal na wala sihitaji ufanuzi wa Mheshimiwa Waziri, isipokuwa wakati akijibu hoja za Wabunge jinsi alivyokuwa amezungumzia suala langu, nilijua kwamba hakunielewa. Hii ni kwa sababu wakati nikiingia kuzungumzia hilo jambo, kengele ilikuwa imelia ilibidi nikae chini nikiwa sijamalizia sentensi. Kwa hiyo, jinsi alivyojibu imeonekana kwamba ina utata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka kuzungumzia suala la Wazee wa Baraza kwamba, wanachaguliwa kutoptana na umaarufu wao siyo kwa taaluma zao. Kwa maana hiyo ni kwamba, watakapokuwa wamechaguliwa, basi angalau wawe wanapewa semina za mara kwa mara ili waweze kujua sheria kidogo. Waziri alipokuwa amejibu inaonekana kama vile mimi sitaki wale wasiokuwa na taaluma wachukuliwe. Kitu ambacho kinawenza kikaleta matatizo kwa wazee wakaona labda mimi sihitaji waweze kuchaguliwa kwenye mahakama. Nilitaka niiweke sawa hiyo ili isiletu utata na kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sawa katika *Hansard*.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Dr. Mzeru, ulikuwa ni mkondo wa hatari sana huo kwa Mbunge mwenye Jimbo. Sasa napenda niwathibitishie Watanzania wote na hasa wa Morogoro Mjini kwamba, Mheshimiwa Dr. Mzeru alichosema siyo kwamba, wazee wa hekima na busara wasichaguliwe kuwa Wazee wa Mabaraza hapana; alichosema yeye ni kwamba, pamoja na hayo yote, itazamiwe pia namna ya kuwajenga kitaaluma ili wawe bora zaidi.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif.1002 - <i>Finance and Accounts</i>	Sh. 564,118,000
Kif.1003 - <i>Policy and Information Services</i>	Sh. 770,684,000
Kif 1004 - <i>Internal Audit Unit</i>	Sh.213179,000
Kif.1005 - <i>Info Education and Communication Unit</i> ...	Sh. 196,969,800
Kif.1006 - <i>Procurement Management Unit</i>	Sh. 218,535,900

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1007 – <i>Management Information System Unit</i> ...	Sh. 567,693,000
Kif. 2001 – <i>Administrator General</i>	Sh. 0
Kif. 2002 – <i>Public Prosecution</i>	Sh. 0
Kif. 2003 – <i>Legislative Drafting</i>	Sh. 0
Kif. 2004 – <i>Public Legal Services Division</i>	Sh. 242,778,800
Kif. 2005 – <i>Legal Reform Unit</i>	Sh. 424,154,000
Kif. 3001 – <i>Civil and International Affairs</i>	Sh. 0
Kif. 4001 – <i>Constitutional Affairs</i>	Sh. 0

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Kif. 1003 – <i>Planning Division</i>	Sh. 1,500,000,000
Kif. 2002 – <i>Public Prosecution Division</i>	Sh. 1,637,250,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 40 – Mahakama

Kif. 1001 – <i>Administration and General</i>	Sh. 3,710,613,400
--	-------------------

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 – *High Court* Sh. 1,934,370,000

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, bila shaka hapa ndiyo penyewe; kuhusiana na tatizo langu la jengo la Mahakama Tabora. Nataka tu Mheshimiwa Waziri, anipe ufanuzi; je, katika kiasi hiki tunachotaka kukipitisha sasa hivi Tabora imo?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe ufanuzi Mheshimiwa Kaboyonga kwamba, katika hizi fedha karibu shilingi bilioni mbili hizi ni kwa ajili ya kurekebisha majengo yakiwemo majengo ya Tabora. *(Makofi)N*

Kif. 2002 – *Court of Appeal Dar es Salaam* Sh. 1,647,000,000

Kif. 2911 – *Primary Courts* Sh. 2,846,390,600

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2012 – *District Courts* Sh. 530,000,000

MHE. JUMA A. NJWAYO: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa tena nafasi. Labda nitangulie kuomba radhi kama nilili-bore Bunge lako. Kwa kweli kwangu mimi haki ya kupata haki ya kisheria (*the right of justice*) ni suala la kikatiba na pana; kwa hiyo ni sehemu ya sera. Lakini tuyaache, kwa sababu tumefika kwenye kifungu kingine ambacho nadhani hoja yangu inasimama.

Kama nilivytangulia kusema, haki hii inakosekana kwa watu wa Tandahimba, kwa sababu wanatakiwa kuifuata huduma hii ya kupata haki ya kisheria mbali sana. Sisi kama Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba, tulitoa jengo lililokuwa linatumika kabla ya jengo jipya la Halmashauri ili Mahakama iifanye kuwa Mahakama ya Wilaya na tulimwita *Zonal Judge* wa Kanda ya Mtwara akaja akaliangalia; ni mwaka sasa. Nikiangalia haya mafungu, hakuna hata panapotajwa jambo lolote pale na kwamba, wananchi bado wanahitaji msaada huu. Nilikuwa nafikiri ni wakati wa Waziri, *Learned Brother*, kusema kitu kidogo kwenye jambo hili. Ahsante.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kupokea mchango wa Mheshimiwa Njwayo na kumuahidi kwamba, tutafuatilia ili tuone uwezekano wa kutumia jengo hilo alilolitaja kuwa Mahakama ya Wilaya, kama litakidhi basi naweza kumhakikishia kwamba, tutaifanya Mahakama mara moja. Nimuahidi pia kwamba, nitakuja mimi mwenyewe na wataalam tuone kama linafaa basi tutalitumia kama anavyoomba tulitumie.

MWENYEKITI: Kabla sijampa nafasi Mheshimiwa Janguo, naomba nitumie mamlaka yangu chini ya Kanuni 104(1), kuongeza muda usiozidi nusu saa. Sasa zimebaki dakika kumi tuweze kumaliza shughuli za Kamati ya Matumizi.

MHE. ATHUMANI S. JANGUO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi tena nipate ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

Katika mchango wangu wa hapa Bungeni na kimaandishi, nilimueleza Mheshimiwa Waziri kwamba, Kisarawe hakuna kabisa jengo la Mahakama wakati kwingine kote wanazungumzia majengo mabovu. Mahakama ya Wilaya imehifadhiwa katika Ofisi ya DC na Mahakama moja ya Kwanza imehifadhiwa katika Ofisi ya DC licha ya kwamba, hata Ofisi ya Polisi imehifadhiwa katika Ofisi ya DC.

Mheshimiwa Waziri katika kujibu najua kashindwa kusema yote, lakini basi awaambie watu wa Kisarawe, Wilaya hii ambayo ndiyo mzee kuliko zote, ina miaka 102; kuwa haina hata jengo la Mahakama kwa kweli inakuwa ni matatizo.

Hata hivyo, Hakimu mwenyewe aliyekuwepo amestaafu, hakujakuwa na Hakimu mwingine. Hatuna jengo wala hatuna Hakimu; je, Serikali inafanya nini?

MWENYEKITI: Looo! Pole sana Mheshimiwa Janguo, hali mbaya sana hiyo. (*Kicheko*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema kwamba, nimesikia kilio cha Mheshimiwa Janguo, aliyekuwa Mwenyekitki wetu kabla.

Nami nashangaa kweli kama hali iko hivyo, basi naomba atuvumilie katika kipindi kifupi kijacho tutakuja kuangalia hali halisi, tuone ni jinsi gani tunaweza kupunguza au kuondoa tatizo hilo lililopo Kisarawe. Kwa kweli siyo jambo zuri kwa Wilaya kongwe kama hiyo, kuwa katika hali kama hiyo.

Tutakuja kuangalia na labda chini ya Mradi wetu wa Maboresho ya Sekta ya Sheria, basi tunaweza kufanya kitu ndani ya mwaka huu.

MWENYEKITI: Ahsante.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 2013 – Kagera Zone Sh. 0

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yyote*)

Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria

Kif. 1001 – *Administration and General* Sh. 0
Kif. 1003 – *Policy and Information* Sh. 17,522,326,600
Kif. 4001 – *Constitutional Affairs* Sh. 0

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

Kif. 1001 – *Administration and General* Sh. 100,000,000
Kif. 1004 – *Legal Affairs* Sh. 1,251,000,000

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

59 – Tume ya Kurekebisha Sheria

Kif. 1001 – *Administration and General* Sh. 572,636,000

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 60 – Mahakama ya Kazi

Kif. 1001 – *Administration and General* Sh. 0

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 64 – Mahakama ya Biashara

Kif. 1001 – *Administration and General* Sh. 368,375,000

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 90 – Mahakama ya Ardhi

Kif. 1001 – *Administration and General* Sh. 96,000,000

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilirudia*)

T A A R I F A

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2008/2009, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko yoyote. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, makadirio hayo sasa yakubaliwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria*
kwa mwaka 2008/2009 yalipitishwa na Bunge)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nawatakia mafanikio katika utekelezaji na kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba, kesho tutaanza Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ambayo itaendelea hadi Jumatatu kwa sababu ni ya siku mbili; kwa hiyo, tuijandae.

Lingine, kesho saa 7.30 mchana naomba Kamati ya Uongozi na Tume ya Huduma za Bunge tukutane pale katika Ukumbi wangu, kuna masuala muhimu sana ya kupanga shughuli zetu zilizosalia pamoja na ugeni mbalimbali ambao tutaupata wiki ijayo na pia baadhi ya Miswada na hoja nyingine binafsi. Inabidi tupange vizuri ili tuone tutamaliza viyi.

Kwa hiyo, nawaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi kwa ajili ya ratiba, lakini pia Tume kwa mambo mengine kama *CDF* na kadhalika, tuweze kukutana saa 7.30 kesho mchana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo, sasa nilahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 01.45 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,*
Tarehe 15 Agosti, 2008 Saa Tatu Asubuhi)

